

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Ishirini na Nne - Tarehe 13 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Usajili wa Makandarasi kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 31 Desemba, 2002 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Contractors Registration Board for the Year Ended 31<sup>st</sup> December, 2002*).

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Utalii Tanzania (*TTB*) kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2003 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Tourist Board (TTB) for Year Ended 30<sup>th</sup> June, 2003*).

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna Mawaziri wawili ambao wana majukumu mengine asubuhi hii, kwa hiyo, nitawapa wao nafasi kwanza wajibu maswali yao, nao ni Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Waziri wa Elimu na Utamaduni. Kwa hiyo, namwita mwuliza swali Na.229, Mheshimiwa Paul Makolo.

Na. 229

**Mpango wa Kuchimba Malambo**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeweka utaratibu wa kuchimba malambo ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji katika maeneo ya ufugaji:-

- (a) Je, katika Jimbo la Kishapu ni Vijiji gani vinafaidika na mpango huo?
- (b) Je, ni nini gharama ya uchimbaji wa malambo hayo?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Wizara yangu imeweka utaratibu wa kuchangia juhudi za wananchi katika suala la upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo, ambapo Wizara huchangia asilimia 50 ya gharama ya lambo linalokisiwa kuwa ni shilingi milioni sita, Halmashauri asilimia 30 na wafugaji wenyewe asilimia 20.

Jitihada hizi zinalenga kuvuna maji ya mvua, kupunguza mwendo mrefu unaotumiwa na mifugo kufuata maji na hivyo kuongeza uzalishaji, kupunguza kasi ya uhamaji ovyo ovyo wa wafugaji na mifugo yao na pia kupunguza usambazaji wa magonjwa ya mifugo. Hii pia ni njia ya kuendeleza nyanda za malisho ambapo baada ya kupata maji ni rahisi kuwa na mipango mizuri ya matumizi ya malisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Tangu mwaka wa fedha wa 2001/2002, Wizara yangu imechangia ujenzi au ukarabati wa malambo katika Vijiji saba vya Jimbo la Kishapu. Vijiji hivyo ni Kabila, Mipa na Ikonokelo, ambavyo vimechimbiwa malambo mapya, Mwamadulu na Miyuguyu ambavyo malambo yake yamefanyiwa ukarabati na kukamilika na Vijiji vya Mwamagembe na Sekeididi ambavyo malambo yake yatachimbwa mwaka huu wa 2004. *(Makofi)*

(b) Gharama ya malambo yote saba ni Shilingi milioni 42. Mchango wa Wizara yangu asilimia 50 ni Shilingi milioni 21, yaani Shilingi milioni tatu kwa kila lambo. Wafugaji walitegemewa kuchangia asilimia 20 sawa na Sh.1,800,000/= kwa kila lambo na Halmashauri ya Wilaya asilimia 30 sawa na Sh.1,800,000/= kwa kila lambo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzipongeza Wilaya za Shinyanga na Kishapu kwa kazi hiyo nzuri waliyoifanya na kuziomba Halmashauri nyingine zinazotekeleza mpango huu, kuiga mfano huo na kuhamasisha jamii katika suala zima la kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa fedha zilizotolewa mwaka 2003 na

Serikali zilikuwa hazijafika Kishapu, Mheshimiwa Waziri anaweza akaeleza ni sababu gani ambazo zimechelewesha fedha hizi zisifike mpaka sasa?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, fedha zilichelewa kutoka Hazina na baada ya kutoka Hazina tumehakikisha zimepelekwa, kama hazijafika ziko njiani na kabla ya Bunge hili kumaliza mkutano wake huu, nitakuthibitishia kwamba zimefika na tarehe waliyopokea kule Shinyanga. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami nina swali dogo la nyongeza. Mwaka 2003 Wizara iliahidi kuchimba malambo katika Wilaya ya Mvomero katika maeneo yenye wafugaji likiwemo eneo la Kambala, Kibati na Melela. Je, nini mipango ya Wizara hiyo katika maeneo ambayo tayari wananchi walishaelezwa? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Suleiman Sadiq kwamba, tuliahidi kufanya hivyo, tumefanya hivyo katika baadhi ya Wilaya na katika Bajeti hii tutafanya vile vile katika baadhi ya Wilaya ikiwemo Wilaya ya Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Na.230

### **Maji Katika Mji wa Geita**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali mara kwa mara inakiri kuwa maji ya visima sio salama kwa matumizi ya binadamu katika Ukanda wote wa Ziwa Victoria kutokana na kemikali zilizopo ardhini:-

(a) Je, Serikali ina mpango upi madhubuti wa kuupatia Mji wa Geita maji safi na salama?

(b) Je, Serikali haioni aibu kusafirisha maji umbali wa Kilometa 320 na kuacha Mji wa Geita ambao upo umbali wa kilometa 24 tu?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mbina, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, baadhi ya maeneo katika Ukanda wa Ziwa Victoria hayana vyanzo vizuri vya maji chini ya ardhi kutokana na maji kutokuwa na ubora unaoridhisha. Hata hivyo, yapo maeneo mengi vile vile katika ukanda huo yanayonufaika kwa kutumia maji chini ya ardhi. Kwa mfano, kati ya mwaka

2002 na 2004, jumla ya visima virefu 25 na vifupi 225 vilichimbwa katika Wilaya ya Geita na vina maji yenye ubora wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Geita wenye wakazi wapatao zaidi ya 50,000 unapata huduma wa maji kutoka kwenye visima 11 vilivyochimbwa katika maeneo ya Mji huo. Hata hivyo, visima vilivyochimbwa havitoshelezi mahitaji ya maji na utafiti wa maji chini ya ardhi haujaonesha mafanikio makubwa kutokana na uhaba wa maji chini ya ardhi katika Mji huo. Chanzo kingine kinachohudumia Mji wa Geita ni chemichemi zilioko katika mlima wa Kagera ambazo zina uwezo wa kuhudumia wakazi wapatao 4,000 kwa siku.

Kwa ujumla, vyanzo vilivyopo vinaweza kutoa maji kiasi cha mita za ujazo 280 kwa siku, ambazo hazitoshelezi mahitaji ya wakazi wa Mji wa Geita, ambayo ni mita za ujazo 2,500 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utafiti ambao umefanyika wa kutafuta vyanzo vya maji kwa Mji wa Geita, umebaini kuwa chanzo cha maji cha kuaminika kwa ajili ya Mji wa Geita ni maji ya Ziwa Victoria. Hivyo, ili kuupatia Mji wa Geita maji safi na salama ni wazi maji yatachukuliwa kutoka Ziwa Victoria. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara imetoa jumla ya Shilingi milioni 5.0 kwa ajili ya kupima na kusanifu mradi huo. Fedha hizi zimetumwa kwenye Halmshauri ya Wilaya ya Geita mwezi Juni, 2004. Kwa mwaka ujao wa fedha 2004/2005, kiasi cha Shilingi milioni 5.0 kimetengwa ili kukamilisha kazi za upimaji na usanifu wa mradi huu.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi mkubwa unaotekelezwa sasa hivi kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria ni ule utakaopeleka maji hayo katika Miji ya Shinyanga na Kahama pamoja na Vijiji 54. Urefu wa bomba kuu la kusafirisha maji unakadiriwa kuwa kilometa 196. Utekelezaji wa mradi huu unagharamiwa na fedha zetu wenyewe.

Kwa hali hiyo, Serikali inaona fahari kutekeleza mradi kama huu. Nia ya Serikali ni kuendelea kuyatumia maji ya Ziwa Victoria kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhudumia Mji wa Geita na Miji mingine inayozunguka Ziwa hili. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa inaonesha kwamba, Mji wa Geita hautapata maji kwa takriban miaka miwili inayokuja kama alivyosema Waziri. Je, Serikali inasema nini angalau wananchi wa Geita kutokana na uzalishaji wa zao la Taifa la dhahabu linalotoka pale wakapewa upendeleo angalau maji kama mrabaha, Serikali inasemaje? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Ernest Mabina kwamba, tutahakikisha kabla ya mwaka 2005, Mji wa Geita umepata maji. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musalika nilikuona, sio yule wa Malawi. *(Kicheko)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la maji Geita ni kubwa na kwa kuwa Serikali huko nyuma ilikuwa na mipango, mikakati, matumaini na ilikuwa inachelewa kuleta maji kama inavyochelewa kuhamia Dodoma na kwa kuwa Waziri ameshasema kabla ya mwaka 2005 maji yatakuwepo, napenda nitoe shukrani. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haya, shukrani zimefika. Tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni. Mheshimiwa Bernard Membe. *(Kicheko)*

Na. 231

### **Tathmini ya Mpango wa MEMEM**

**MHE. BERNARD K. MEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeshughulikia mpango wa ujenzi wa Shule za Msingi vizuri na sasa inajiandaa kuingia kwenye awamu ya pili ya mpango wa ujenzi na uimarishaji wa Shule za Sekondari na kwa kuamini kwamba tathmini ya mpango wa MEMEM imekwishafanywa ili matatizo kadhaa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wake yasijirudie tena:-

(a) Je, Serikali imejifunza nini kuhusu moyo wa wananchi wa kujitolea?

(b) Je, ni Maafisa wangapi wa Elimu wa Wilaya walihusika na vitendo vya ubadhirifu na wizi wa fedha za umma na ni hatua gani zimechukuliwa?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, Mbunge wa Mtama, lenye sehemu (a) na (b), naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tathmini ya MEMEM ilifanyika mwezi Oktoba, 2003 kwa kuwahusisha wadau wote wa Elimu toka ngazi za Taifa, Mkoa, Halmashauri, pamoja na Wahisani. Mkoa mitatu ya Arusha, Lindi na Singida ilitembelewa na timu kamilifu ya Wataalam ili kujionea hali halisi ya utekelezaji wa MEMEM.

Aidha, Serikali kupitia Kampuni ya *Deloitte and Touche* ikishirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hufanya ukaguzi wa mahesabu ya fedha katika Halmashauri zote. Zoezi la ukaguzi wa hesabu za fedha za MEMEM kwa nchi nzima linafanyika na litaendelea kufanyika kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge wa Mtama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na mpango wa MEM tumejifunza kuwa moyo wa kujitolea na utaratibu shirikishi ni muhimu sana katika kufanikisha utekelezaji. Maeneo mengi ambayo wananchi walihamasika na kushiriki kikamilifu katika kujitolea nguvu kazi, vifaa na fedha, majengo mengi mazuri yamejengwa. Kwa mfano, mwaka wa kwanza wa mpango (2002), malengo ya ujenzi yalikuwa kujenga madarasa 14,000 lakini kwa kutumia nguvukazi za wananchi na jamii, Serikali imefanikiwa kujenga madarasa 17,000 ambalo ni ongezeko la madarasa 3,000.

(b) Mheshimiwa Spika, fedha nyingi za ruzuku ya maendeleo ambazo ni za ujenzi zimekuwa zikipelekwa Shuleni, hivyo wanaohusika na usimamizi pamoja na ununuzi wa vifaa vya ujenzi ni Wajumbe wa Kamati za Shule na Walimu Wakuu kama Makatibu wa Kamati hizo. Hivyo, kwenye maeneo ambayo Kamati ya Shule wameshiriki katika kubaini ubadhirifu, waliohusika wamepelekwa Mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake. Kwa rekodi za Wizara yangu, Afisa Elimu wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Mkurugenzi wake, wametenguliwa nyadhifa zao pamoja na kusimamishwa kazi kutokana na ubadhirifu katika matumizi ya fedha za Serikali za MEM. Pia Afisa Elimu wa Halmashauri ya Lindi Vijijiji amesimamishwa kazi na amefikishwa Mahakamani. *(Makofi)*

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kumshukuru Waziri kwa kujibu ya kipengele (a) ingawa hakuwashukuru wananchi kwa moyo wa kujitolea, kwa niaba yake napenda kuwashukuru wananchi wote wa Tanzania kwa moyo wa kujitolea waliouonyesha. *(Kicheko)*

Baada ya hilo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Maafisa wa Elimu waliohusika na ubadhirifu wa fedha wengi wao wameachwa bila kuondolewa nyadhifa zao na badala yake wamepelekwa tu Mahakamani. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba namna moja ya kudhibiti fedha za Umma ni kuwawajibisha viongozi hawa kwa kuwaondoa nyadhifa zao bila kusubiri kuwapeleka Mahakamani na suala la Mahakama liwe baadaye? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa Viongozi hawa pia wameshirikiana na viongozi wenzao na watu wengine katika kula fedha hizo, Waziri atakubaliana na mimi kwamba, katika tathmini na uchunguzi unaofanywa, Serikali haina budi kuwawajibisha pia wale wote ambao wameshirikiana na watu hawa katika kula fedha hizo pamoja na viongozi wao kwenye Halmashauri zao wakiwemo na Waganga wa Kienyeji wanaowatumia? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza suala la kuwashukuru wananchi, nilitoa shukrani na pongezi kwa wananchi kwa uzito kabisa

katika hotuba yangu ya Bajeti. Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Membe naye kwa kuunga mkono. *(Makofi)*

Kuhusu Maafisa Elimu ambao amesema baadhi yao wamepelekwa Mahakamani lakini hawajasimamishwa kazi, mimi nitafurahi sana kupata orodha ya Afisa Elimu yeyote ambaye amepolekwa Mahakamani na hajasimamishwa kazi ili nitoe maagizo kwamba, asimamishwe kazi mara moja. Kwa sababu ni utaratibu kabisa, kama mtu amekwishafunguliwa mashtaka na kesi iko Mahakamani, kwa kweli hawezi kuendelea kuwa kazini mpaka suala lake la Kimahakama liwe limemalizika. Kwa hiyo, hapo naomba tusaiane tu kupeana taarifa. *(Makofi)*

Swali ambalo linaoana na la pili, kama wako wengine ambao wanajulikana wamehusika na ubadhirifu na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa, kwa kweli napenda niseme kwamba, Wizara na Mawaziri na Viongozi wa Serikali wa Kitaifa, sio rahisi kujua linalotokea kila mahali. Kwa hiyo, ni Wajibu wa ngazi zote za Uongozi, ngazi za Wilaya husika kuhakikisha kwamba, wanaohusika na ubadhirifu wanachukuliwa hatua zinazostahili, kufanya uchunguzi unaohitajika, kuwaripoti Polisi, kufanya uchunguzi ili waweze kuchukuliwa hatua.

Lingine kwamba wapo viongozi wengine ambao wameshirikiana na Maafisa Elimu kula fedha hizo, mimi napenda kutoa wito kwamba, tusiwe waoga kumfichua yeyote anayefanya maovu hata kama ana madaraka ya namna gani. Haiwezekani ukawa mwizi halafu ukafichama kwenye koti la madaraka ya uongozi uliopewa. Mimi nafikiri hii, yeyote anayehusika, taarifa zitolewe aweze kuchukuliwa hatua inayostahili. Hata huyo Mganga wa kienyeji kama anajulikana amehusika katika wizi, mwizi ni mwizi hata akiwa ni Mganga wa Kienyeji, kama amehusika katika wizi na ushahidi upo, achukuliwe hatua kama mtu mwingine. Lakini kama ni mtumishi au kiongozi ambaye amekwenda kwa Mganga kutaka asaidiwe na uganga wake, hapo inakuwa vigumu kumhusisha huyo mwenye uganga kwenye mashtaka kwa sababu aliyekwenda ni huyu mnayemtumumu. Tujitahidi kupata ushahidi na kuchukua hatua zinazohitajika. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa mpango wa MEM/MMES huwezesha kupatikana kwa madarasa mengi mazuri katika Shule zetu za Msingi, lakini katika Shule hizo ukifika unakuta madarasa mawili mazuri na madarasa mengi ya zamani yamechakaa yanahitaji ukarabati. Sasa je, Serikali inaandaa mpango gani au ina mpango gani wa kukarabati madarasa ya zamani ambayo yamechakaa sana? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, hali hii anayoizungumzia Mheshimiwa Mbunge ipo. Tatizo moja ambalo tumelipata ni lile nililolizungumza katika hotuba yangu ya bajeti katika kifungu kile cha matatizo maalum. Nimesema kwamba, Halmashauri nyingi wamechelewa kutoa taarifa za matumizi ya fedha zilizotolewa awamu ya kwanza na awamu ya pili na matokeo ni kwamba, Dola milioni 50 ambazo ni sawa sawa na Shilingi bilioni 50 za kutoka Benki ya Dunia ambazo ni za mkupuo wa tatu, zimechelewa kutolewa kwa sababu ya taarifa zilizochelewa. Hizo fedha zililenga zije zisaidie kukamilisha majengo haya yaliyobakia.

Kwa hiyo, napenda nirudie kutoa wito kwa Halmashauri chache kabisa ambazo zimebakia na nimetoa maagizo niletewe orodha hiyo chache ambayo inatuchelewesha mpaka sasa ili zile fedha za awamu ya tatu ambazo zinafanana kiasi na zile za awamu ya kwanza na awamu ya pili ili tusonge mbele tuweze kukamilisha majengo chini ya mpango huu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kufafanua kwa mara nyingine tena kwamba, mpango huu wa MEM ni kwa ajili ya majengo yote ya shule. Bado ziko Wilaya wanadhani ni kwa ajili ya madarasa, ni majengo yote ya shule, madarasa, nyumba za walimu, Ofisi, majengo ya maliwato au vyoo, wengine wanapenda kutumia neno hilo, yote yana-*qualify*. Anayepanga kwamba mwaka huu tufanye majengo yapi ni Wilaya husika sio Wizara. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane katika jambo hili. (*Makofi*)

Na. 232

### ***Fumigation* katika Sekondari Musoma**

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA (k.n.y. MHE. IBRAHIMU W. MARWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya unyunyizaji dawa (*fumigation*) katika Shule za Sekondari Mara (Musoma), Musoma Ufundi, Tarime - Kilimo zilizoko Mkoani Mara; na kwa kuwa kazi hizo zilifanyika kienyeji bila kufuata utaratibu kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ununuzi wa Vifaa na Huduma; na kwa kuwa ushahidi upo na unaonyesha kuwa kazi hiyo alipewa mtu mmoja kwa maslahi ya viongozi fulani fulani bila kufuata taratibu za zabuni:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitumika kwa kazi ya *fumigation* kwenye Shule hizo za Mara, Musoma Ufundi na Tarime na Kampuni iliyopewa kazi hiyo ilikuwa na Ofisi wapi na uzoefu wa siku ngapi kwenye kazi hiyo?

(b) Kwa kuwa Sheria ya Ununuzi wa Vifaa na Huduma ya Mwaka 2001 imetamka wazi kuhusu adhabu dhidi ya mtumishi yeyote atakayekiuka sheria hiyo. Je, ni hatua zipi za kinidhamu na za kisheria zilizochukuliwa dhidi ya Maafisa waliohusika na ukiukwaji wa sheria hiyo iliyopitishwa na Bunge?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Wankanga Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la unyunyizaji dawa, yaani *fumigation*, katika Shule za Sekondari za Tarime, Mara na Musoma Ufundi lilitolewa maelezo na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, wakati akijibu hoja za Waheshimiwa



Wabunge, waliochangia hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma hapo tarehe 6 Julai, 2004 katika Bunge hili.

Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa uchunguzi wa jambo hili unaendelea na kazi hiyo amepewa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili kusudi akishirikiana na Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Polisi, wachunguze kama kuna rushwa kuhusiana na suala zima la unyunyiziaji dawa katika hizo Shule za Sekondari.

Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge kuwa tsubiri matokeo ya uchunguzi wa timu hiyo ambayo naamini atapewa kama Serikali ilivyoahidi hapa Bungeni.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, inaeleweka kabisa kwamba, ubadhirifu ulipokuwa unataka kufanyika, Serikali ilielezwa mapema kabisa na sasa ni takriban mwaka mmoja. Kwa nini hatua hazijachukuliwa mpaka leo? Ni sheria imevunjwa hapo, lakini mpaka sasa ni mwaka mzima, kwa nini sheria hazijachukuliwa? (*Makofi*)

Pili, wanaozembea kuchukua hatua hizo za kisheria, kwa nini Serikali haijawachukulia nao hatua? (*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Dr. James Wanyancha kwamba, mimi kama Waziri wa Elimu na Utamaduni, mara nilipoletewa taarifa hiyo, nilikabidhi kwa vyombo husika kwa sababu tunavyo vyombo vyenye ufundi unaohitajika kufanya mambo haya.

Nakiri kwamba, ni siku nyingi na imechukua muda mrefu, lakini maadam tumeahidi, mimi naomba sana tsubiri, uchunguzi utakapofanywa utatujulisha pia kama ni uzembeaji katika kuchukua hatua nao umekuwa wapi.

Hayo maswali yote tutaulizana na taarifa kamili kama Serikali ilivyoahidi itatolewa na nina hakika itakuwa na hatua ambazo zitakuwa zimechukuliwa kwa yeyote aliyechelewesha uchunguzi wa jambo hili.

Na.226

### **Utengenezaji wa Barabara kwa Nguvu za Wananchi - Mbozi**

**MHE. EDSON M. HALINGA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Mbozi waliamua kuchonga barabara kwa kutumia zana za kawaida kama vile majembe, sururu, makarai na kadhalika kwa njia ya kujitegemea:-

(a) Je, Serikali inaonaje kama ikijenga madaraja kwenye barabara hizo kama hatua ya kuunga mkono nguvu za wananchi hao ili kuzifanya barabara hizo ziweze kupitika kwa nyakati zote?

(b) Je, Serikali inaweza kufuatilia uchongaji huo wa barabara unaofanywa na wananchi wa Wilaya ya Mbozi ambao hauhitaji vyombo vya gharama kama greda ili uwe mfano wa kuigwa kwa nchi nzima?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kutoa mashine ndogo za kushindilia zinazosukumwa kwa mkono au trekta kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ili kuziimarisha barabara hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edson Mbeyale Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi inatekeleza Mradi wa Usafiri na Uchukuzi Vijijini, yaani *Village Travel and Transport Programme*, ambao ulianza Mei, 1999 chini ya uhisani wa Serikali ya Norway kwa lengo la kujenga uwezo wa wananchi Vijijini, katika kutengeneza barabara na njia zao kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi, yaani *Labour Based* na kujenga uwezo wa Halmashauri katika matumizi ya teknolojia hiyo inapohitajika.

Halmashauri nyingine zinazotekeleza mpango huu ni Iramba, Muheza, Iringa, Rufiji, Masasi na Morogoro. Katika Wilaya ya Mbozi mradi huu ni wa majaribio, yaani *Pilot Project*, sawa na sehemu nyingine nilizozitaja. Wilayani Mbozi mradi huu unatekelezwa katika Vijiji vya awali 20 vya majaribio vilivyo katika Kata nne za Ruanda, Mlangali, Chitete na Msagano zilizomo katika Tarafa ya Iyula na Msagano.

Kutokana na kwamba mradi huu ulilenga zaidi maeneo ya majaribio ni Vijiji vichache tu viliweza kusaidiwa uwekaji wa kalvati. Pamoja na hayo Serikali ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya hii, sasa inajenga daraja katika Kijiji cha Myovizi na ilikwishakamilisha daraja lingine katika Kijiji cha Namhonga. Hizi ni jitihada za Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri na tutaendelea kusaidiana kuhakikisha madaraja yanajengwa. Halmashauri ya Wilaya itaendelea kuvisaidia Vijiji katika ngazi zake mbalimbali za utengenezaji wa maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi huu wa ulimaji barabara unatekelezwa na wadau mbalimbali ambao ni wananchi, Serikali na Wahisani. Ofisi yangu inafuatilia kwa karibu sana utengenezaji wa barabara za Vijijini chini ya mpango huu na ni azma ya Serikali kutaka kupanua uzoefu wa mbinu sahihi kutoka katika maeneo ya utekelezaji wa majaribio ili iweze kutumika katika maeneo mengine ndani ya Wilaya husika na Wilaya nyingine katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu kuanza kumpongeza sana Mheshimiwa Halinga pamoja na wananchi wa Mbozi, kwa kutekeleza Mradi huu katika hali ya kuridhisha sana. *(Makofi)*

Katika mwaka huu wa 2004/2005, Ofisi yangu imepanga kueneza mpango huu katika Halmashauri nyingine zipatazo 35 endapo Wahisani watauafiki mpango huu kwa asilimia 100. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hizi ili ziweze kuwa imara zinatakiwa kushindiliwa vizuri kwa kutumia teknolojia ya kisasa na rahisi kama vile mashine ndogo za kushindilia zinazosukumwa kwa mkono. Kutokana na uwezo mdogo kifedha kwa sasa Halmashauri inaweza tu kutoa vifaa vidogo vidogo ambavyo vinafaa kwa ajili ya kazi hizo.

Ofisi yangu itaendelea kuwasiliana na Wahisani wa Mradi kuona uwezekano wa kuwasaidia kupata vifaa kama vile *flowed roller*, *Hard roller* pamoja na trekta kwa ajili ya kazi za matengenezo ya barabara hizi.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nataka nimwulize Waziri kama anaelewa kwamba, magreda sasa hayapatikani kutokana na gharama kubwa ya mashine hizo. Lakini Katibu Mkuu wake alipotembelea Mbozi alijionea mwenyewe na akawashukuru sana wananchi sasa hivi wana moyo sana kwa kutegemea agizo alilolifanya. Je, Serikali itakuwa tayari kwenda kuwatuma Wataalam wakathibitisha kazi hii kuwa kweli ni ya kisasa na yenye kufaa?

Pili, Serikali kwa nini isiwe na utaratibu wa kuongeza fedha katika maeneo haya ambayo yamethibitisha kuwa ni kazi kazi nzuri ili kuwapa moyo na kuifanya kazi hii iwe ya Kitaifa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kutuma wataalam kwenda kuona kazi nzuri inayofanywa, nafikiri ni jambo zuri tu, nitamwomba Katibu Mkuu aende akaone hali hiyo kwa lengo kwa kweli pengine la kutaka kujua utaalim waliotumia wananchi hao, moyo waliotumia ili tuweze kusambaza katika maeneo mengine.

Kuhusu swali la pili la uwezekano wa kuongeza fedha ili kuchangia katika juhudi za wananchi. Ndiyo maana nimesema tunaendelea kukamilisha mazungumzo na Wahisani mbalimbali juu ya mpango huu kwa lengo kwanza la kuongeza lakini vile vile kuboresha yale maeneo ambayo tayari mpango huu unaendelea. Ni matumaini yangu kwamba, tutakapofikia muafaka, nina hakika hii rai ya Mheshimiwa Edson Halinga, inaweza vile vile ikazingatiwa.

Na. 227

**Barabara ya Msangamweru hadi Mkwajuni**

**MHE. PAUL E. Ntwina** aliuliza:-

Kwa kuwa lipo tatizo la ubovu wa barabara toka Kijiji cha Msangamweru/Mjele, Chang'ombe, Mnadani, Iwombwe (Ilasiro), Kanga hadi Mkwajuni na kwa kuwa licha ya matengenezo ya mara kwa mara ya maeneo korofi katika barabara hiyo, sasa imeharibika sana.

Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka za kurekebisha maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbalizi-Mkwajuni hadi Makongolosi yenye urefu wa kilomita 117.8 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na wakala wa barabara. Barabara hii imejengwa kwa kiwango cha changarawe na ni kiungo muhimu sana kati ya Makao Makuu ya Wilaya ya Chunya na Makao Makuu ya Mkoa wa Mbeya kwa kupitia vijiji vya Msangamwere, Mjele, Chang'ombe Mnadani, Viombwene na Kanga, ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inapita kwenye Bonde la Ziwa Rukwa ambapo ardhi yake ni kichanga. Hali hiyo inasababisha kuharibika mara kwa mara kwa barabara hiyo kutokana ufinyu na uharibifu wa tabaka la chini. Hata hivyo, barabara hii imekuwa ikipata matengenezo ya mara kwa mara ya maeneo korofi ili ipitike bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua zinazostahili kwa kutenga fedha kulingana na upatikanaji wake ili kufanya matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo mengine katika barabara hiyo. Kwa mwaka wa 2003/2004, barabara hiyo ilifanyiwa matengenezo ya sehemu korofi kwa Sh.70,000,000/=, matengenezo ya kila siku kwa Sh.22,000,000/= na matengenezo ya dharura kwa Sh.18,588,000/=. Matengenezo hayo yanaifanya barabara iwe katika hali nzuri kiasi cha kutosha na hivyo kuiwezesha kupitika kwa sehemu kubwa ya kipindi cha mwaka. Hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali, ubora wa barabara hii huharibika baada ya muda mfupi wa matengenezo. Sababu hizo ni pamoja na kusombwa na mvua wakati wa masika, barabara kutumiwa na magari makubwa na vile vile uharibifu unaotokana na mifugo kupitishwa katika barabara hiyo. Serikali itaendelea kufanya matengenezo mengine katika mwaka wa fedha huu wa 2004/2005. Naomba tu Mheshimiwa Mbunge, aendeele kushirikiana na Serikali ili kuhakikisha kwamba, barabara inafanyiwa matengenezo kwa manufaa ya wananchi.

**MHE. PAUL E. Ntwina:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Waziri amekiri kuwa ile barabara ina mchanga na hata haitengenezwi mara nyingi inapoharibika; na kwa kuwa yapo maeneo nchini ambayo yapo sawa na eneo lile la Jimbo langu; na kwa kuwa Msangamweru/Mjele katika awamu iliyopita walijenga lami kilomita 10 na eneo hilo linapitika vizuri; je,

Serikali inaweza kuangalia uwezekano wa kujenga barabara hii kwa lami, *cement* au *solid stabilizing chemicals* ambazo wanajenga katika maeneo mengine?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ni ngumu sana kwa matengenezo na *TANROADS* wanajitahidi kweli kweli. Hapo sehemu ambapo imejengwa lami ni kwa sababu palikuwa hapapitiki kabisa. Kwa hiyo, wanajitahidi kutengeneza vipande kwa vipande ili barabara hii ikamilike kwa uhakika na tunategemea kuitengeneza hii barabara kwa kiwango cha changarawe ya hali ya juu ili unyevunyevu wake uishe barabara ipitike mwaka mzima. Tunajitahidi.

Na. 228

### **Picha zinazoonyesha Mauaji ya Halaiki ya Rwanda**

**MHE. DR. CHRISTANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa maelezo yanayotolewa pamoja na picha zinazoonyesha mauaji ya halaiki huko Rwanda ni kuwa, masalia ya miili ya watu waliouawa yamewekwa wazi kama ukumbusho wa maafa hayo ya kinyama:-

(a) Je, kuendelea kuwaonyesha watu hao waliouawa katika hali hiyo hakuwezi kuendeleza hisia na baadaye kuja kuleta maafa mengine ya kulipiza kisasa kwa vizazi vijavyo?

(b) Kutokana na uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na Rwanda, je, Serikali yetu haiwezi kuishauri Serikali ya Rwanda kwamba masalia ya watu hao yazikwe katika eneo moja au katika maeneo yatakayokubalika kwa ajili ya kuwakumbuka kuliko ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mauaji ya halaiki ya Rwanda ya mwaka 1994, hayawezi kusahaulika kwa urahisi kwa sababu waliohusika kwa maana ya kuua na ndugu wa walioathirika, kwa maana ya kuuliwa pamoja na wenye vilema, bado wako hai kwa hivi sasa. Mauaji hayo ya halaiki yaligusa makabila yote makuu ya Rwanda. Wahutu na Watutsi na kila kabila linakumbuka mauaji hayo kwa namna yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Rwanda imeamua kujenga makumbusho ya mauaji haya ya halaiki katika kila mkoa kwa nia ya kuwakumbuka na kuwaombea wale waliopoteza maisha yao, kuwaonesha kumbukumbu wale walionusurika pamoja na waliofanya vitendo hivyo na wakati huo huo kuwa onyo kwa vizazi vya hivi sasa na vya

siku za usoni kuhusu uovu wa uhasama wa kikabila na kwamba mauaji hayo ni dosari kubwa katika historia ya Rwanda.

Nia ya Serikali ni kufukua makaburi ya halaiki yanayofahamika na yatakayofahamika au kugundulika siku za usoni na kufanya mazishi au hifadhi ya mabaki yatayopatikana katika makaburi au maeneo rasmi.

Sambamba na jitihada za Serikali za kuweka makumbusho hayo au makaburi rasmi ya waliouawa wakati wa mauaji ya 1994, Serikali hiyo inafanya jitihada vile vile kuwahimiza wananchi wasamehe bila ya kusahau kile kilichotokea mwaka 1994. Kwa maana hiyo, mabaki au makaburi hayo ni makumbusho, funzo na onyo na ni historia isiyoweza kufutika.

Hata hivyo, wapo baadhi ya Wanyarwanda, hasa wa kabila la Watutsi, ambao wanaonekana kutoitikia vyema wito wa kusameheana. Watutsi hao wanaojiita, waathirika wameunda vyama vya kutetea madai yao, kama vile chama cha *AVEGA* na *IBUKA*. Vyama hivyo, inaaminiwa, vina sauti kubwa kwa Serikali na hivyo kuwepo walakini katika zoezi zima la kuhifadhi mabaki ya waliouawa mwaka 1994.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na udugu na uhusiano mzuri uliopo kati ya Rwanda na Tanzania, ushauri wa aina yoyote kuhusu namna ya kuhifadhi mabaki ya wale waliokufa katika mauaji ya 1994, hautakuwa wa maana kwa kuwa shughuli za namna ya kuhifadhi mabaki hayo zimekuwa zikiendelea kwa muda mrefu, zimekuwa zikiboreshwa kila wakati na zimetungiwa sheria. Nia ya Serikali ya Rwanda licha ya udhaifu unaoweza kuonekana katika utekelezaji wa zoezi hilo ni kuona kwamba, zoezi zima linafanikiwa kwa malengo niliyoelezea hapo awali.

Aidha, katika kujenga makumbusho hayo, Serikali ya Rwanda imegharimika kwa hali na mali na hata wakati mwingine kuomba misaada kutoka nje kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo. Kila kiongozi au mgeni rasmi yeyote aliyetembelea Rwanda amekuwa akipelekwa katika moja ya maeneo yaliko hifadhiwa mabaki ya waliouawa mwaka wa 1994 kwa ajili ya kuona na kutoa mchango wa kuendeleza kuyajenga maeneo hayo. Hata Waziri Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, alipotembelea Rwanda mwaka 2000 alipelekwa kwenye eneo la Gikongoro ambako alitoa mchango wa dola 1,000. Hivyo, sio rahisi kuishauri Rwanda kufanya vinginevyo.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kutokana na jibu la Mheshimiwa Waziri kwamba, kuna vyama vya Kitutsi ambavyo vina uhusiano wa karibu na Serikali na kwa namna moja au nyingine vimekuwa vikifanya kazi kama ya kuchochea hali hiyo. Je, Waziri atakubaliana nami kwamba, kuendelea kuonyesha mafuvu ya watu waliokufa kunaongeza kisaikolojia hisia za mtengamano? (*Makofi*)

Pili, je, si kweli kisaikolojia kwamba hii pia inaweza ikatafsiriwa kwamba Mamlaka fulani yangependa mambo kama haya yatumike ili kuendelea kutisha baadhi ya jamii katika umoja huo wa Wanyarwanda? (*Makofi*)

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Ninajua unataka kueleza kwamba jambo hili liko Mahakamani. Siyo hivyo?

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Sivyo Mheshimiwa Spika. Mwongozo wa Spika. Ninaohitaji ni kwamba, kwa vile Jamhuri ya Rwanda ni nchi huru, kwa lugha ya kigeni ni *Sovereign*, je, Bunge hili lina uwezo wa kujadili mambo ya ndani ya nchi huru? (*Makofi*)

**SPIKA:** Nani anajua jibu la hilo? Linahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Spika, ili litoke jibu la usahihi. Lakini kwa sasa hivi naweza kusema kwamba, kwa kuwa swali hili linaulizwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na kazi ya Wizara hiyo ni mashirikiano na nchi nyingine, ndiyo maana lilikubaliwa liingie kwenye *Order Paper*. (*Makofi*)

Lakini Mheshimiwa Marmo, ana wasi wasi kwamba pengine kuna kasoro, basi nittoa mwongozo baadaye nikishalifanyia kazi vizuri. Lakini kwa sasa hivi, linaruhusiwa liendelee. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoelezea katika jibu langu la msingi, nia ya Serikali ya Rwanda si kuendeleza chuki na uhasama, nia yao ni kwamba jambo hili lisisahaulike lakini lisameheke. Hiyo ndiyo nia yao. Kwa maana hiyo basi, sioni kwamba ikiwa itaendelea na msimamo huo wa kutochochea uhasama na ikiwa wakati huo huo inashikilia kuendeleza mshikamano mwema na hata sasa hivi inakataza haitaki suala la Muhutu na Mtutsi lakini inataka Unyarwanda. Wananchi wa Rwanda tu ndiyo lengo lao. Ikiwa itaendelea hivyo, sioni hata kidogo kisaikolojia au vinginevyo kwamba, juhudi hizo zitazidi kuchochea uhasama.

Hata hivyo, hivyo vyama nilivyovielezea vya *AVEGA* na *IBUKA*, pamoja na kwamba vyama vingine vipo vya Wahutu, lengo lao si kuchochea uhasama, wala ulipizaji kisasi, kwa sababu tunavyosikia vyama hivi vimeanzishwa kwa kiwango kikubwa na wajane wa wale waliouawa, ili kusaidia watoto yatima ambao sasa hivi ndiyo wamekuwa wanalea ndugu zao ili kusaidia wenye vilema, ili kusaidia kupatikana ushahidi kwa wale ambao wanajulikana wamefanya vitendo hivi ili kuzuia vitendo hivi visitokee tena siku za usoni. (*Makofi*)

Na. 233

### **Mawasiliano ya Reli-Mpanda**

**MHE. MARGARETH J. BWANA** aliuliza:-

Kwa kuwa eneo la Mkoa wa Rukwa ni kubwa na hakuna usafiri wa ndege wa uhakika na hata barabara zake si nzuri:-

(a) Je, isingekuwa vyema kwa Serikali kuunganisha reli ya Mpanda kupitia Sumbawanga hadi Tunduma ili usafirishaji wa bidhaa na abiria uwe rahisi?

(b) Je, kuna hasara yoyote ya kiuchumi kama reli hiyo itajengwa na gharama za ujenzi zinaweza kufikia kiasi gani?

(c) Kama uwezekano wa kujenga reli hiyo upo je, ujenzi huo utanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth J. Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Napenda nikubaliane na ushauri wa Mheshimiwa Margareth Bwana na pia niunganishe na mawazo yaliyotolewa na Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Waheshimiwa Wabunge wengine, wakati wakijadili bajeti ya Wizara hii.

Sisi tunauona umuhimu wa kuwa na reli toka Tunduma hadi Kasanga kupitia Sumbawanga na hatimaye kuiendeleza toka Sumbawanga hadi Mpanda kwa lengo la kusaidia na kuboresha usafirishaji kwa Kanda hii, reli hii pia itafungua eneo hili na nchi kufaidika kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, reli hiyo itafungua Mkoa wa Rukwa, Nyanda za Juu Kusini mpaka Congo (*DRC*) na njia mbadala kwa jirani zetu wa Burundi. Itaweza kutuunganisha Mbeya na Burundi na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa mbalimbali mfano saruji toka Kiwanda cha Saruji Mbeya na bidhaa nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika mpango kamambe wa kuendeleza reli, ipo nia ya kuweka reli hiyo katika mpango huo na tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya *feasibility study*. (*Makofi*)

Nia ya Serikali ni kuwaondoshea wananchi wake kero mbalimbali na kuwarahisishia usafirishaji na uchukuzi kama inavyoendelea kufanya kwa kuzindua barabara na madaraja nchini kote na kama wanavyofanya Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Makamu wa Rais.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Waziri na pia swali la msingi ni kutatua matatizo ya usafiri katika maeneo mbalimbali. Kwa kuwa sasa kwenye Reli ya Kati ...

**SPIKA:** Reli ya Kati ni swali jipya hilo, tunaendelea. (*Kicheko*)



**Matengenezo ya Mwandiga - Manyovu**

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Mwandiga - Manyovu inafanyiwa ukarabati na Makandarasi watatu na kwa kuwa *workmanship* ya makandarasi hao imetofautiana sana na mmoja kati ya hao ana vyombo vya kisasa:-

(a) Je, kwa nini mkandarasi huyo mwenye vifaa vya kisasa asingepewa kazi ya ujenzi wa barabara hiyo kuliko wale wanaotumia zana zisizo za kisasa?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kusitisha kazi inayofanywa na wale wakandarasi wasio na zana za kisasa na ambao wamejenga barabara finyu na haiwezi kuruhusu magari mawili kupishana kwa urahisi?

(c) Kwa kuwa ziko nyumba nyingi zimewekewa alama ya X kama vile majengo ya Kanisa la Anglikana Musagara, Munanila na Kibwigwa, Shule za msingi za Musagara, Mukigo, Kalinzi na Kiganza pamoja na nyumba nyingi za watu binafsi ina maana gani hasa ikitiliwa maanani kuwa baadhi ya majengo hayo yamekuwa yakitumika kwa zaidi ya miaka sitini na baadhi ya majengo yako mbali na barabara husika na kwamba, Serikali itakuwa tayari kuambatana nami kwenda kuona ujenzi wa barabara hiyo pamoja na majengo yanayotarajiwa kuvunjwa yenye alama ya X na jisni inavyogusa hata nyumba zilizo kwenye umbali wa zaidi ya hatua kumi na tano?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwandiga - Manyovu kwa sasa inafanyiwa matengenezo ya aina tatu tofauti chini ya mikataba tofauti kwenye sehemu tofauti.

Mkataba wa kwanza ni wa matengenezo ya kawaida (*Routine Maintenance*) kati ya Mwandiga na Mkongoro yenye urefu wa kilometa 23.5 yanayofanywa na Mkandarasi *Western Engineering*. Kazi zinazohusika kwenye mkataba huu ni kusawazisha umbo la barabara (*Light Grading*), kuchimba mifereji, kufukia mashimo na kusafisha makalvati. Majembe na koleo ni nyenzo muhimu kwa aina hii ya kazi.

Mkataba wa pili ni wa matengenezo ya sehemu korofi kati ya Kijiji cha Mkingo na Mnamila yenye urefu wa kilometa 54.5 yanayofanywa na Mkandarasi *Kalyango Construction*. Kazi zinazohusika kwenye eneo hili ni kuchonga barabara (*reshaping*), kumwaga changarawe sehemu mbalimbali na kusafisha mifereji na makalvati kwa kutumia greda, magari (*tipers*), majembe ya mkono, makoleo na sululu.

Mkataba wa tatu ni wa matengenezo maalum (*Backlog Maintenance*) kati ya Mkongolo na mpakani mwa Tanzania na Burundi ukiondoa kilometa 5.5 kati ya Mkingo na Mnanila yanayofanywa na Mkandarasi *CICO* kutoka China. Kazi hii inafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), pamoja na Serikali ya Tanzania chini ya mradi wa kuimarisha miundombinu ya barabara zilizoathiriwa na mvua za *El-Nino* (*El-nino Infrastructure Repairs*). Mradi huu ni mkubwa kuliko ile niliyoitaja awali na zabuni yake ilishindaniwa Kimataifa, hivyo Mkandarasi husika ameleta vifaa na mashine bora zaidi kuliko wenzake ambao kiwango cha kazi ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika miradi hii yote mitatu, zana za mikono kama majembe, sululu na makoleo, hutumika kwa kazi zinazohitaji nyenzo hizo kama vile kusafisha na kuchimba mifereji, kusafisha makalvati na kufukia mashimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilonsi Mporogomyi, lenye sehemu tatu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mkandarasi *CICO* mwenye vifaa vya kisasa asingeweza kupewa kazi zote za miradi mitatu kwa kuwa zile zabuni mbili zilipotangazwa hakushiriki kwenye ushindani wa zabuni hizo, hivyo walipewa Makandarasi walioshindania na kushinda kwa kutumia vigezo vya zabuni husika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haiwezi kusitisha mkataba unaoendelea kwa kigezo cha kuwepo mkandarasi mwingine bora zaidi kwenye eneo la jirani na kazi. Serikali inaweza kusitisha mkataba kama Mkandarasi amekiuka misingi ya mkataba au ameshindwa kutekeleza kazi za mkataba, kama tulivyofanya kwa *Mkandarasi Kalyango Construction* aliyeshindwa kutekeleza na kukamilisha kazi za mkataba wa matengenezo ya sehemu korofi nilizozitaja hapo awali. Kazi hizi sasa zitakamilishwa na wakala wa Barabara Mkoa wa Kigoma.

Aidha, sehemu inayoonekana kuwa barabara ni finyu kati ya Mwandiga na Mkonogoro, hii ni kwamba barabara ilikutwa ikiwa hivyo na mkataba wa matengenezo ya kawaida katika sehemu hiyo hauna kipengele cha kuipanua.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Wizara yangu kupitia wakala wa Barabara (*TANROADS*), imekuwa ikitekeleza Sheria ya Barabara Na. 167 ya mwaka 1969 inayotaka kuachwa wazi kwa eneo la barabara la futi 75 (meta 22.5), kila upande toka katikati ya barabara. Tunakiri kuwa ni maeneo mengi yaliyoguswa na zoezi hili yakiwemo yaliyoainishwa na Mheshimiwa Mbunge.

Naomba kusesitiza kuwa eneo la hifadhi ya barabara linatakiwa kuachwa wazi kwa shughuli maalum za maendeleo ya barabara husika.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoielezwa kwenye taarifa ya Waziri iliyotolewa kwenye vyombo vya habari Jumamosi tarehe 22 Mei, 2004 kuwa nyumba hizo hazitabomolewa kwa sasa hadi eneo hilo litakapohitajika baada ya fedha za kujenga

barabara husika kwa kiwango cha lami kupatikana. Hata hivyo, ni vema wenye nyumba wakachukua tahadhari sasa badala ya kungojea hadi wakati huo. Alama za X zilizowekwa zifutwe.

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba niulize maswali yafuatayo: Kwa kuwa nia ya Serikali yetu ni njema ya kujenga barabara zilizo nzuri na zinazoweza kuwasaidia wananchi kufanya kazi vyema; na kwa kuwa hii jitihada imekuwa ikiendelea; je, si vyema Serikali sasa ikatambua kwamba barabara inapokuwa finyu inasababisha ajali za aina mbalimbali kama vile nivyo taja katika swali langu la msingi?

Pili, kwa kuwa barabara ya Mwandiga - Manyovu sasa inajengea kwa *otta seal* na kwa kuwa sasa Serikali katika majibu yake katika vipengele vingi vya maswali mengi yaliyoulizwa ndani ya Bunge imekuwa ikikubali kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuzingatia kwa umuhimu wa uchumi wa jiografia na barabara hii ni muhimu sana kufungua uchumi na nchi jirani ya Burundi. Je, si vyema sasa barabara hii badala ya kujengwa kwa *otta seal* ikajengwa kwa barabara ya lami ili magari mazito ya NHCR yaweze kupita kwa urahisi na kwa magari mazito yanayopeleka bidhaa kwenda Burundi na sehemu nyingine yaweze kupita sehemu hizo? Ahsante Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba barabara finyu huwa moja ya sababu ya ajali. Lakini barabara hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja, hatukuwa na mpango wa kuipanua na mkataba haukuwa na mpango wa kuipanua kwa hiyo, hapa alikuwa analalamikiwa mkandarasi. Haikuwa inalalamikiwa barabara na mimi nilijibu kwamba, mkandarasi hakuwa na mkataba wa kupanua barabara hiyo. Ufinyu wa barabara tunaujua.

Pili, kwa sasa tunatengeneza barabara hiyo ya Mwandiga - Manyovu kwa kiwango cha *otta seal* na Mheshimiwa Mbunge angependa tutengeneze kwa lami. *Otta seal* ni aina ya lami, inategemea tu ni aina hiyo ya lami unaitia kwa kiwango gani. Mfano mzuri Waheshimiwa Wabunge ni kuangalia kutoka hapa kuelekea Mnadani, ile barabara ni ya *otta seal* na ni nzuri na inaweza kudumu. Ni rahisi na kwa nchi yetu tunaweza kutumia lami ile na tukafika mbali kwa kiwango cha lami cha barabara ya *regional roads* na ndiyo maana tunaifanyia majaribio na kuiona. Sasa hivi kiwango hiki cha lami kiko kwenye majaribio katika Tanzania. (*Makofi*)

Na. 235

### **Ustawi na Maendeleo ya Barabara**

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya *The Highway Ordinance Cap. 167* ya mwaka 1969 inaelekea kuwa kikwazo kikubwa kwa ustawi na maendeleo ya barabara hapa nchini:-

(a) Je, sheria hiyo itarekebishwa lini?

(b) Je, Serikali haioni kwamba Halmashauri za Wilaya baada ya kupnguziwa mapato yake hazina uwezo wa kuzihudumia barabara hizo?

(c) Je, Serikali imezitembelea barabara zilizopendekezwa kupandishwa hadhi na Bodi ya barabara ya Mkoa wa Shinyanga mwaka 2002?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Enock Kipole, Mbunge wa Jimbo la Msalala, lenye sehemu (a), (b), na (c) napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Barabara ya *The Highway Ordinance Cap. 167* ya mwaka 1969, inayoendelea kutumika hadi sasa, imejidhihirisha kuwa na mapungufu kwa ustawi na maendeleo ya sekta ya barabara katika baadhi ya maeneo yake mbalimbali. Mapungufu haya yamebainika kutokana na mageuzi (*reforms*) mbalimbali ambayo yamefanyika katika sekta ya barabara tangu mwaka 1998.

Mageuzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya barabara ni pamoja na kuanzishwa kwa Sheria ya Mfuko wa Barabara na Bodi yake mnamo mwaka 1998, kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara (*TANROADS*) mwaka 2000 na mabadiliko ya majukumu ya Wizara yangu ambapo sasa inashughulikia masuala ya Sera na Ufuatiliaji. Lengo la mageuzi haya ni kukidhi mahitaji ya mikakati ya utekelezaji wa mabadiliko ya miundo ya kijamii na kiuchumi (*Social and Economic Restructuring*) iliyoanzishwa mwaka 1987 na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2000 - 2025.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel E. Kipole, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya barabara, hivi sasa inaandaa Muswada wa Sheria ya Barabara (*Roads Act, Bill*) ambao unatarajiwa kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu hapo baadaye. Muswada huo utazingatia kuondolewa kwa vikwazo vinavyokwamisha ustawi na maendeleo ya sekta ya barabara.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Barabara ya Mwaka 1998 (*The Roads Toll (Amendment) Act No.2, 1998*), Halmashauri zote za Wilaya, Miji na Manispaa zimekuwa zikipata ruzuku ya fedha kutoka Mfuko huu kwa ajili ya matengenezo ya barabara zake.

Aidha, Halmashauri nyingi zimekuwa hazichangii fedha kuhudumia barabara zake kutoka vyanzo vyake vya mapato nje ya fedha za Mfuko wa Barabara. Hivyo, hatua ya Serikali ya kupunguza mapato ya Halmashauri kutoka vyanzo vyake haitaathiri uwezo uliopo wa kuhudumia barabara zake kutoka vyanzo vyake ya mapato nje ya fedha za Mfuko wa Barabara. Hata hivyo, napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kuwa,

fedha za Mfuko wa Barabara hazitoshi kukidhi mahitaji ya ukarabati na matengenezo ya barabara zote. Hivyo, ingekuwa ni vyema kwa sasa Halmashauri nazo zingeanza utaratibu wa kutenga kiasi cha fedha kutoka ruzuku zinazopata kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya nyongeza ya fedha za kuhudumia barabara hizi.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haijatembelea barabara zilizopendekezwa kupandishwa hadhi na Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Shinyanga mwaka 2002. Kwa mantiki hiyo, ili kutotumia fedha mara mbili kwa kazi ile ile, barabara zote nchini zilizopo sasa na zile mpya zinazopendekezwa, zitakaguliwa kuona ni barabara zipi zinakidhi vigezo vinavyohitajika katika kupanda ngazi ama hadhi ya Barabara Kuu, Barabara za Mkoa, Barabara za Vijiji na Njia Kuu ili ziingizwe kwenye Sheria mpya ya Barabara kama nilivyosema katika jibu la sehemu (a).

Mheshimiwa Spika, napenda kuongeza kwa kusema kwamba, kupendekeza kwa Mkoa sio kwamba barabara hizo zimekubaliwa kupanda au kuteremka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Kipole ameridhika, nashukuru na muda wa maswali umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, kuna matangazo mawili ya Vikao vya Kamati. Kwanza, ni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mgana Msindai, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane leo tarehe 13 Julai, 2004 saa tano asubuhi chumba Na.133, ghorofa ya kwanza.

Kikao cha pili ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake, anawakumbusha Wajumbe wa Kamati yake kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 13 Julai, 2004 saa tano asubuhi chumba Na.428.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper*, Katibu.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii iliyowasilishwa mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, ninaanza kwa kumpongeza kwa dhati kabisa, Askari wa Mwanvuli wa Wizara hii, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Tunaridhika na utendaji wao wa kazi na tunaona *seriousness* wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba, wanaboresha masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kuwapongeza wale wote wanaomsaidia Mheshimiwa Waziri, ambao ni Katibu Mkuu, Ndugu Adadi, Mkurugenzi Mkuu wa Makosa ya Jinai, Ndugu Mwasasu, Ndugu Tibaigana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Makamanda wote wa Mikoa bila kumsahau Kamanda wangu wa Mkoa wa Rukwa, Ndugu Mkwama, pamoja na Makamanda wote wa Wilaya zote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuzungumzia hotuba hii, nina maeneo machache sana ambayo napenda niyazungumzie kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika Wizara hii. Kwanza kabisa, napenda nizungumzie juu ya suala la vitendea kazi kwa Ofisi zote za Makamanda wa Mikoa na Wilaya. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema kwamba, kuna magari ambayo yatatolewa na kusambazwa katika Wilaya na Mikoa, naomba magari hayo yasiishie katika maeneo ya Wilaya peke yake, yangefika mpaka kwenye Vituo vya Polisi vilivyoko mpakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano Kituo cha Karema, Ikola, Kasanga, Mtowisa, Kipili, Kapungu, Manyovu, Kalya, Ilagala, Sirari, Mugumu na kadhalika. Vituo hivyo mara kwa mara vimekuwa vikipambana na wahalifu wanaotoka nchi jirani. Mkoa wa Rukwa hususan maeneo niliyoyataja ya Karema na Ikola ni miongoni mwa maeneo ambayo kila wakati tumekuwa tukipambana na suala la watekaji kutoka nchi jirani ambao wamekuwa wakiwateka wananchi wetu, wakiwaibia nyavu zao, wakiwapeleka nchi jirani, wakifanya mauaji na vitendo mbalimbali ambavyo kwa kweli vinatishia amani katika maeneo hayo. Wananchi wetu wamefika mahali wakajikuta wanaogopa hata kulala kwenye nyumba zao inapofika jioni wanalazimika kwenda kulala porini kutokana na kuhofia usalama wao. Lakini ninalipongeza Jeshi la Polisi pamoja na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, wamefika mahali wakadhibiti hali hiyo vizuri sana na sasa hivi wananchi wetu wanalala vizuri kwenye nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wakati watakapokuwa wanatoa vifaa vya usafiri katika maeneo haya niliyoyataja wahakikishe kwamba, vituo vyote vya Polisi vilivyoko mpakani ambavyo vimekuwa vikipambana mara kwa mara na majambazi ambayo ni watekaji, wanapata nyezo za uhakika za usafiri. Huwezi kumtegemea Polisi atembee kwa miguu kilomita 50 kutoka kwenye kituo kwenda eneo la uhalifu, hana usafiri wa gari wala pikipiki akapambane na majambazi kule itakuwa ni ngumu sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe vile vituo vilivyoko mpakani nilivyovitaja, vipewe nyezo za usafiri ili iweze kuwa ni rahisi zaidi kwa wao kuweza kupambana na maharamia ambayo yamekuwa yakijitokeza katika maeneo hayo mara kwa mara. *(Makofi)*

Nina orodha ya matukio hapa na nitamkabidhi kama *reference* ili aweze kuyafanyia kazi kwa tarehe, matukio ya utekaji yaliyotokea katika eneo la Karema na Ikola na aina ya wizi uliofanyika katika maeneo hayo na vitu vilivyotekwa. Nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri baada ya hotuba yangu hii ili aweze kushirikiana na watendaji wake waweze kuona namna gani wanavyoweza kuirekebisha hali hii.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni ile ahadi waliyoitoa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake. Kuna kituo cha Polisi cha Ikola na Karema kilichojengwa kwa nguvu za wananchi na Mheshimiwa Waziri tangu mwaka 2003 alinahidi watahakikisha kwamba, wanamalizia hatua iliyobaki na mimi na Mbunge wa Jimbo linalohusika, Mheshimiwa Sumri, tukawaeleza wananchi wale kwamba, Mheshimiwa Waziri ameshatoa ahadi ya kuja kumalizia ujenzi wa kituo chenu cha Ikola na Karema. Sisi kule tulishazungumza kwamba, Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba, atakuja kumalizia kituo hiki. Nataka nifahamu Mheshimiwa Waziri anatamka nini, wananchi wale watapata lini hiyo fedha kwa ajili ya kumalizia kazi iliyobaki ili vituo hivyo viweze kuanza kufanya kazi mara moja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo tumekuwa tukizungumza kwa muda mrefu kuhusu kupatiwa boti kwa ajili ya kufanya doria katika ukanda wa Ziwa Tanganyika ili iwe ni rahisi zaidi kufanya mapambano na wale warahamia wanaotoka nchi jirani kwa mfano, Congo lakini mpaka sasa hivi hatujapata jibu lolote na vitendo hivi vya ujambazi na utekaji vimekuwa vikiendelea kila wakati. Nataka Mheshimiwa Waziri atueleze ni lini tutapata boti katika maeneo hayo ili iweze kuwa ni rahisi zaidi kwa Maaskari wetu wale kuweza kupambana na wahalifu hawa?

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nizungumzie suala la kuboresha makazi ya Maaskari wetu. Nianzie kwanza na jengo la Makao Makuu ya *Traffic* pale Dar es Salaam. Lile jengo linatia aibu. Jengo lile liko kando kando ya barabara ambayo Viongozi wetu Wakuu na wageni mbalimbali wanaokuja hapa nchini ndio barabara wanayopita. Wanapopita wanakuta kuna jengo zuri sana la *NSSF* linapendeza na linavutia hata kwa kuangalia, wanapotoka pale mbele tu kidogo wanakutana na jengo moja chafu la Makao Makuu ya *Traffic*, halipendezi hata kwa kuangalia. Wafanyakazi wake ni wazuri, wasafi, wanapendeza sana na zile nguo zao nyeupe lakini lile jengo kwa kweli ni jengo ambalo linawavunja heshima na ni jengo ambalo linaweza kufanyiwa tu ukarabati hata kwa kupakwa rangi. Ninaomba wakatafute hata mifuko ya nilu pale *RTC*, inauzwa pale nje au mifuko ya chokaa waweze kulipaka rangi jengo lile. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Makamba, amekuwa akijitahidi kuhamasisha wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam kufanya usafi wa majengo yao ikiwa ni pamoja na kuyapaka rangi. Hicho kitu kimekuwa kikifanyika sana, sasa nashangaa yeye ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama sijui kwa nini lile jengo hakuliona. Tunaomba na kushauri kwamba, kwa kweli tunaomba jengo lile lipakwe rangi ili liweze kuwa katika hali ambayo inavutia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba pia ifanyike jitihada ya makusudi ya kuhakikisha kwamba, nyumba za askari zinafanyiwa ukarabati. Pale nyuma tu kuna maghorofa yako pale, maghorofa yale nadhani tangu yamejengwa hayajawahi kupakwa hata rangi lakini ukiyapitia pia nadhani na yenyewe yanachangia katika kuambukiza maradhi mbalimbali. Mabomba ya maji machafu yameharibika maji yanatoka ovyo, kwa ujumla mfumo wa maji machafu pale unatakiwa ufanyiwe ukarabati na watoto wanachezea mle mle kwenye yale maji. Kuna mabomba yalishaharibika siku nyingi

yanamwaga maji saa zote. Ninaomba vitu kama hivi vifanyiwe ukarabati. Kwa hiyo, watakapokuwa wanashughulikia suala la kupaka rangi majengo yale, waende sambamba pia na upakaji wa rangi wa zile nyumba za Maaskari wetu wa Polisi kule Sumbawanga na zenyewe zinahitaji kupakwa rangi, haziko katika hali nzuri hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie mapendekezo kadhaa ambayo ninaona ni muhimu tuyazungumzie katika bajeti hii. Ukifika pale *Kilwa Road* utakuta kuna magari chungu nzima yamepaki pale na inasemekana kwamba, magari yale yako pale muda mrefu kutokana na ukosefu wa *spare*, ni msaada wa magari waliyopata kutoka nje. Sasa yale magari yatakaa pale mpaka lini? Ninapenda kushauri kama imefikia mahali magari yale yameshindikana kufanyiwa matengenezo ni heri basi magari yale yakapigwa mnada ile pesa itakayopatikana kutokana na magari yale itafanya kazi nyingine ya kuboresha shughuli za Polisi. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pendekezo langu la pili ni kuhusu kutoshughulikiwa kwa mirathi ya watumishi mbalimbali wa Jeshi hili la Polisi wanapofariki. Ninakubaliana na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, nami nimekuwa nikifuatilia suala la mirathi ya ndugu yangu huu mwaka wa 12 sasa tangu amefariki. Mirathi ile mpaka leo haijashughulikiwa wala hatujui hatma yake ni kitu gani wakati *supporting document* zote zilishawasilishwa Wizarani, kuna nini huko?

Kwa nini wasiige mfano wa Jeshi la Magereza wao wanafanya vizuri sana katika eneo hili kwa nini kule Polisi inachukua zaidi ya miaka 10 kufuatilia mirathi ya mtu?

Huyu aliyefariki kama ile hela ndio inayotegemewa kwa ajili ya kuwasomesha watoto wake, watawezaje kusoma katika mazingira ya namna hii? Naomba hili nalo wajirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la upandishaji wa vyeo katika Jeshi la Polisi ni tatizo, unamkuta mtu anakaa miaka 20 katika nafasi moja hana 'V' hata moja kwenye bega lake, ana miaka 20 anatumikia Jeshi la Polisi, hivi *system* ya upandishaji vyeo katika Jeshi la Polisi ukoje? Unatia mashaka na inabidi kwa kweli ifike mahali ifuatiliwe kule kuna nini. Mtu atakaaje kwenye cheo kimoja miaka 20 hajapandishwa cheo hata kimoja, maana yake ni nini hii, kuna tatizo gani hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo na kuisitiza tu kwamba, vituo vyote vya Polisi vilivyoko mpakani vipewe usafiri, vipewe magari, Karema, Ikola, Kasanga, Mtowisa, Kipili, Kapungu, Manyovu, Kalya, Ilagala, Sirari, Mugumu na kadhalika, ili iwe rahisi kwa wafanyakazi hawa kutekeleza vyema majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante. *(Makofi)*



**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, pili, natangulia kabisa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Vile vile napenda Serikali ione kwamba, watu wote wanaofanya kazi vizuri tuna haki sisi Wabunge kuwapongeza na wale ambao hawafanyi vizuri tutanyamaza au kuwalaumu kwa wazi bila kuwaonea haya kwa sababu hii ni moja ya kazi yetu hapa Bungeni sio kuoneana haya. Kwa hiyo, tunawapongeza hawa wenzetu wawili wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianzie na suala la rushwa katika Jeshi la Polisi. Mimi ni miongoni mwa watu wanaofanya utafiti kabla ya kusema maneno. Mimi nataka niseme kwa dhati ya moyo wangu, ukichukua idadi ya Polisi Tanzania ambayo sitaisema ukachukua na kazi kubwa wanayoifanya nchini Tanzania, napenda tuwapongeze kwamba, kwa kweli kama ukipima kwa kiwango cha rushwa wote wangukuwa wala rushwa, nchi ingevurugika vibaya sana. Naomba tusiwalaumu Polisi kwa kosa la mtu mmoja. Juzi Mheshimiwa Waziri mwenyewe alitueleza hapa Askari wangapi wamechukuliwa hatua waliofanya ovyo. Napenda kusema tulipongeze Jeshi la Polisi kwa kiwango kikubwa, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binadamu wana tabia ya kulaumu bila kusifu. Juzi hapa fedha zimeibiwa kule Moshi kama Polisi wetu wangukuwa ovyo, wala rushwa, wangeweze kukamata fedha zile, isingeweze kana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata juzi lilitokea tatizo pale kwa mke wa Mheshimiwa John Malecela, wale wahalifu wote 12 walikamatwa aliyewakamata ni nani, ni Polisi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu mimi siku zote natumia takwimu. Someni katika kitabu hiki cha taarifa muone ile sehemu inayozungumzia habari ya rushwa. Kule Mkoani kwetu kuna *dash* ni kwa sababu Polisi wa kule wanafanya kazi nzuri na napenda nimpongeze *Regional Police Commander* wa Mkoa wangu, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Mkoa ule. Naomba tutambue kazi nzuri inayofanywa na Jeshi letu. Sisi tunaotembea katika nchi jirani tuna kipimo cha kulinganisha kati ya Jeshi letu na Majeshi ya watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, napenda nizungumzie jambo lingine, nchi yetu ilishaingia kwenye mkataba wa kupokea wakimbizi lakini madhara ambayo yametokana na wakimbizi kwa nchi yetu ni makubwa sana. Kwa mfano, ukifika Mikoa ya Kigoma na Kagera, uharibifu wa mazingira ni mkubwa sana katika maeneo waliyohamia wakimbizi. Sasa hii ni hasara kwa nchi, ukishaharibu mazingira kuyarudisha kama alivyounda Mwenyezi Mungu ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yetu itafute wataalam wafanye hesabu wakadirie uharibifu ili ukishajulikana uende ukazungumzwe kwenye Umoja wa Mataifa kwenye chombo kinachohusika kwa sababu tunaumia bure. Haiwezekani tukapokea wakimbizi tukiishi nao na uharibifu ukatokea tukaachwa hivi hivi, kwa nini tupate hasara? Hili ni jambo ambalo ni *very serious*, naomba Serikali yetu ifanye tathmini na mje mtueleze kama kweli Umoja wa Mataifa unakataa kutufidia kwa sababu hatuwezi kukubali hasara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tunabeba mzigo hata huu uhalifu unaofanywa na baadhi ya wakimbizi unatokana na njaa. Waafrika wakimbizi wanalipwa na *UNHCR* posho ya kuwagharamia kuishi dola senti 16 lakini Wazungu kule kwao ambao ni wakimbizi wanalipiwa dola mbili. Sasa huu ni ubaguzi, Wazungu wanatunyanyasa sisi Waafrika, eeh ni unyanyasaji. Binadamu wote ni sawa na Umoja wa Mataifa ni kwa ajili ya watu wote, kwa nini Umoja wa Mataifa unakubali Wazungu walipwe dola mbili Waafrika walipwe senti 16? Sasa ni chombo gani hiki hakifuati haki? Naomba Serikali ipige kelele juu ya jambo hili kwa sababu hili ndilo linatuletea matatizo na wakimbizi wengine wanaanza kufanya mambo ya ovyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakimbizi wanaishi maisha ya ovyo kweli, mwaka 2003, Wizara yenyewe wanajua kuna wakati fedha za kulisha wakimbizi zilikuwa hakuna na chakula kilikuwa hakuna ikawa matatizo makubwa sana. Sasa jambo hili tunataka vile vile litafutiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda Serikali itazame, tuliwahi kufanya makosa ya historia. Kule Kigoma wakimbizi walipokuja wale wa miaka ya kwanza, waliingizwa ndani ya vijiji vya wananchi, wamo ndani ya vijiji vya wananchi. Kwa hiyo, inapotokea matatizo kati ya nchi yetu na nchi jirani, sisi tunapata lawama za bure kwa sababu majirani wanadhani sisi tunafundisha uhalifu kutoka katika nchi yetu lakini sio kweli, hatufundishi hao ila ni kweli kwamba, kwa sababu hao wameishi katika vijiji wameoleana na Watanzania na inakuwa kazi ngumu kweli hata suala la kutoa uraia au kutokutoa uraia inakuwa ngumu. Kwa hiyo, ninachopendekeza hapa ni kwamba, Serikali iache kuweka wakimbizi pembeni ya nchi tuwalete katikati ya nchi, waleteni Dodoma, mnawaweka pembeni wanatuletea migogoro. Kila inapotokea ugomvi na jirani wanasema wanafundishwa kuja kutupiga tuwaletee katikati ya nchi, katikati ya nchi hii ni Dodoma. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulisema hapa na Mheshimiwa Margareth Bwana amelisema na jambo hili tusilipuuze, tatizo la mpaka wetu Tanzania na nchi jirani ni kubwa kwa maana ya uhalifu wa upande wa pili. Kule Congo hata sasa kui-*manage* nchi ya Congo ni kazi kubwa sana, ni ngumu mno. Mimi nimeishi kule mpakani nimefika mara nyingi kule nilipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na Kigoma, Serikali ya Kinshasa wala hawajui kinachoendelea *Lake Tanganyika* huku mpakani mwetu na wao, hawana habari kwa hiyo tunaumia sana sisi Tanzania kwa sababu ya uhalifu unaofanyika kule.

Lakini sisi ndio wenye eneo kubwa la *Lake Tanganyika* wa pili ni Congo, hatuna vyombo vya kufanyia kazi, Polisi hawana *speed boat* kama alivyosema Mheshimiwa mwenzangu, hata Mkuu wetu wa Mkoa wa Rukwa na Kigoma havezi kutembelea kwa ufanisi wananchi wa mipakani mle kwa sababu hana vyombo vya kutembelea. Hivi kweli Serikali inashindwa kununua meli ndogo ya kuwawezesha *RCs* kufanya kazi, wangeweza kununua *boat* za kisasa hata moja wakawa wanachangia *RCs* wetu wanapanda mitumbwi, *RC* anasafiri kwa mtumbwi, Polisi wanakwenda kwa mitumbwi kukagua usalama inawezekanaje, leo karne ya 21 Polisi aende kwa mtumbwi kukagua usalama, inawezekanaje, ni kichekesho! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tufikirie *priority*, usalama wa nchi ni *priority number one*. Katika itikadi za ulinzi na usalama, usalama wa nchi yangu kwanza. Kwa hiyo, naomba tufikirie jambo hili, tupeni fedha zinunue boti nzuri kwa ajili ya utawala na *speed boat* kwa ajili ya ulinzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulisema hapa ni kuhusu mambo madogo madogo ambayo ni kero. Kule Rukwa kuna mchezo ambao sio mzuri. Mtu akihukumwa na Mahakama ya Mwanzo yule aliyemshtaki mwizi au mhalifu anaambiwa na Polisi atoe hela ampe Askari ndio Askari ampeleke mfungwa *escort* Magereza Sumbawanga. Sasa inawezekanaje? Mimi nimekwenda kushtaki, kesi imehukumwa mhalifu amepatikana ana kesi ya kwenda kufungwa, inawezekanaje sasa mimi ndio nitoe hela kumpa Askari kumpeleka mfungwa wao kule Sumbawanga? Jambo hili tunao ushahidi na nina rekodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile niliwahi kueleza hapa na Waziri akasema watafanya uchunguzi, leo nataka tupate maelezo Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Sheria, kule Rukwa katika vijiji ambako kwanza hakuna rumande zilizojengwa na Serikali lakini watu wakifanya makosa Hakimumu na wale Polisi kule wanamuweka mtu rumande halafu wanawaambia ndugu zake wawe wanalipa Sh.3,000/= kila siku za kumgharamia pale. Sasa inakuwa kama hoteli, rumande inakuwa hoteli, inawezekanaje? Tena sio rumande ni *vi-lockup* vya ovyo tu ambavyo ni ukiukaji wa haki za binadamu. Naomba nalo hilo tupate maelezo maana nilishalisema siku nyingi wakaahidi watachunguza, naomba leo nipate jibu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo napenda kulisema hapa ni kuwa Magereza katika nchi yetu Tanzania ilikuwa ni shule ya kila mtu kwenda kujifunza namna ya kuendeleza kilimo, ilikuwa chuo cha mafunzo. Nchi zote jirani za Afrika wamekuwa wakija kujifunza kwetu namna Magereza yanavyofanya kazi leo ukifika katika maeneo ambayo Serikali iliwaomba wananchi tukatoa kuwapa mashamba ya Magereza sasa yamekuwa majani, kilimo kimekufa. Songwe ilikuwa inaongoza walipata zawadi mara kadhaa ya kilimo kizuri, Gereza la Mollo kule ninakotoka na mimi nikiwa Mbunge ndio nilipepetea Serikali wakaja kujenga Gereza kwa madhumuni ya kilimo, sasa yote haya sasa hakuna kilimo.

Hawa Wafungwa wanakaa bure kwa nini mnataka hawa Wafungwa wakae bure mwende mkawagharamie tena maana zamani walishaanza kujitegemea! Bajeti ya Serikali

kulisha Magereza ilishuka sana kwa sababu walikuwa wanajilisha wenyewe sasa Serikali inazungumzia kujitegemea mnakubali tena kubeba mzigo, mimi naona kama kichekesho kidogo, wale wanafanya kazi wenyewe.

Kwa Gereza la Mollo lilikwishakuwa ni kampuni iliyokuwa inaitwa *Corporation Sole*, kuna wakati walikopwa na Makao Makuu ya Magereza fedha zaidi ya shilingi milioni 70, kwa hiyo, wakashuka kufanya kazi. Wanakwenda kulima kwa mkono hawawezi kununua tena trekta mpya ili waendeleze kilimo. Kwa hiyo, natoa wito kwamba, suala la Magereza kujitegemea katika Tanzania tulirudishe kama tulivyoanza wakati wa Azimio la Arusha kwa sababu wanakaa bure hawa wafungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba kurudia tena kusema kwamba, naunga mkono hoja ya Serikali na nawapongeza wote wanaofanya kazi katika Wizara hii. (*Makofi*)

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu. Pili, kama ilivyo ada na kawaida, namwomba Mbunge aliyetutoka hivi karibuni, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mwenyezi Mungu amlaze mahali anapostahili.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako ni jumba lenye heshima kubwa sana ambapo si mahali wala si uwanja wa kuchezea ... au rucha roho. Ni mahali pa kutoa maelekezo kwa Serikali yetu, mapendekezo, ushauri na kadhalika. Kama mtu hana la kusema ni afadhali anyamaze.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Ngoja amalize kusema ndiyo utaomba mwongozo wa Spika. Endelea Mheshimiwa Karim.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Spika, kama mtu hana la kusema ni afadhali anyamaze. Si vizuri hata kidogo kumzungumza mtu ambaye katika Bunge hili hayumo. Huyu ni kiongozi wa watu, je, ingekuwa kiongozi huyu ni mimi nikasimama na nikamtaja kama alivyomtaja, nikasema labda Mheshimiwa Mangula, nikaendeleza yale ambayo aliyoyazungumza, ingependeza? Hii si tabia nzuri, tuheshimu viongozi wa wenzetu ili na wetu waheshimiwe. Uchokozi si mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jana tulipokea ujumbe humu ndani ya Bunge kwamba, mwaka 2005 lazima CCM itashinda na itashinda kwa vyovyote vile, vyovyote iwayo. Hivyo na sisi tunasema kwamba, haiwezekani. CCM itashinda lakini itashinda kwa uamuzi wa wananchi kupitia uchaguzi huru, wa sheria na haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vinginevyo *Walahi, Billahi, Tallahi* na sisi twasema tena kwamba, hakuna njia, utumie vikosi vya ulinzi, ujanja au ghiliba, yote hayo sasa hivi hayatafanya kazi na kama ni ukimbizi tutakwenda pamoja na kama ni kuuawa hatutakufa peke yetu sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia kuhusu kuoja na kuolewa katika Jeshi la Polisi. Kwa kweli Sheria hii imepitwa na wakati, kwamba askari baada ya kuajiriwa ni lazima atimize miaka mitatu ndiyo aoe au aolewe. Naomba kwamba, vijana wetu mara wakishamaliza mafunzo yao na kujiunga na Jeshi letu, waruhusiwe kuoja na kuolewa ili kujikinga na janga ambalo lipo mbele yetu la UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wetu alipiga marufuku kwamba, watu wa CUF huwafundisha vijana wao judo na kareti. Lengo letu ni kulinda viongozi wetu pamoja na mali zetu na Chama. Sisi tumekubali hilo na tulidhani kwamba, amesema hilo kwa nia nzuri. Tumejifunza Bukoba kwa kushambuliwa msafara wa Mwenyekiti wetu Profesa Ibrahim Lipumba. Suala hili hatukulipenda na tuna uhakika kwamba limefanywa na CCM ...

**MBUNGE FULANI:** Siyo kweli.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Kwa sababu aliyefanya ni Diwani wa CCM, ndiye aliyetayarisha kundi la vijana kufanya uharamia huo. Je, CCM mmetukopesha tulipe? Lakini Mheshimiwa Waziri kutuzuia kuandaa vijana wetu kulinda viongozi wetu sisi tumekubali lakini ukijua huu, huu huujuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna habari ya ajira ya vijana wetu hawa wa Jeshi la Polisi. Hali ya umaskini wetu umewafanya vijana wetu wadumae, kwa hiyo, naomba hii sheria ya kusema kwamba askari ni lazima afikie futi tano na nchi kumi na moja ndiyo awe askari, nafasi hii itachukuliwa na Wasukuma peke yao maana yake ndiyo waliopanda kidogo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aipitie tena sheria hii kwa sababu ya hali yetu ya kiuchumi, vijana wetu wamedumaa, kwa hiyo, kigezo ambacho ningomba kitumike ni elimu yao na uwezo wao wa kufanya kazi. Lakini hili la urefu tungeliacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majengo ya Polisi ya Wilaya yangu ya Mkoani ni mabovu. Kuna kituo cha Kengeja, Mtambile na hicho cha Mkoani. Majengo haya kwa kweli hayakuwa ni ya Polisi, ni majengo ambayo yalirithiwa tu kutoka kwa wakoloni, kwa kweli mapaa yanavuja, askari hawana mahali pa kukaa. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapofanya safari ya kwenda Pemba aje katika Wilaya yangu ya Mkoani atazame majengo yetu yalivyo. Wakati wa mvua askari hawana pa kukaa. Mwisho wanakaa katika majumba mabovu, ukiingia kwenye Ofisi ya OCD haifanani kabisa kwa sababu majengo hayo hayakutayarishwa kwamba ni kambi au ni ofisi kwa ajili ya Polisi.

Mheshimiwa Spika, juzi Zanzibar kulikuwa na maandamano. Maandamano ambayo yalikuwa ni halali, yaliruhusiwa na askari walikuwa wakiyalinda na tunawashukuru sana askari kwa kazi hiyo. Maandamano yalikuja zake mpaka kufikia Ofisi Kuu ya CCM. Pale kulikuwa na kijana mmoja mkereketwa wa CCM akataka kutoa gari lake kwenye uzio wa ofisi kuu na kuingia barabarani wakati maandamano yanaendelea.

**WABUNGE FULANI:** Si kweli.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Aaskari wakamzuia kijana yule wakamwambia bwana usitoe gari lako. Kwa sababu ya ukereketwa wake na kwa sababu ya kiburi chake alilingiza gari barabarani, waandamanaji wangepanya nini, awagonge au tusubiri mpaka awakanyage? Vijana wakamzuia. Sasa walipomzuia, yaliyotokea ndiyo hayo. Walimpa kisago kidogo. Sasa yale maandamano yakaendelea, usiku askari polisi wakapewa agizo, wakashindilia bastola zao mfukoni na mabomu yao ya machozi wakatembea Vijijini kuwasaka vijana wa *CUF*.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kwa taarifa yako, vijana saba wapo ndani. Naiomba CCM, naiomba tena, iacheni hii nchi iwe ni kimbilio la watu ambao nchi zao hazina amani. Tunaomba vijana hawa watolewe mara moja. Kosa lao lilikuwa nini? Aliyetia gari barabarani baada ya kukatazwa na Polisi au wale waliomzuia asiumize watu barabarani wakati wa maandamano?

Mheshimiwa Spika, gazeti la jana la Nipashe lilieleza kwamba, Mzee asema amechoka. Lakini tuliochoka ni sisi zaidi ambao tulitwikwa mzungu mwaka 1995, ukatuliwa na muafaka. Tukatikwa mzungu mwaka 2000, ukatuliwa na muafaka. Hatutakubali tena kutwikwa mzungu mwingine mwaka 2005. Nasi tumechoka, hatukubali, tupo tayari, hatuogopi, ila tunaheshimu sheria na Katiba ya nchi yetu hii. Endapo sheria na Katiba itapindwa kwa makusudi kwa kutumia Jeshi la Polisi hatukubali na hatukubali maana askari ni binadamu kama sisi, bunduki ni chuma tu na gereza ni nyumba. Kufa tumezoea, kinachosikitisha ni yule ambaye anayedhani ataishi hapa milele. (*Makofi*)

Tuinamishe nyuso chini kidogo, tuwakumbuke wapenzi wetu Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, kama tungeshauriwa tunganema abaki miaka ishirini zaidi. Yuko wapi maskini katuacha mayatima, Dr. Omar Ali Juma, yuko wapi? Hao ndio ninaowasikitikia kwamba watu labda wanafikiria kwamba wataishi hapa milele.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi ni zuri kweli kweli na tunalipongeza na hii bajeti tungependa iwasaidie wao na sisi hatukukataa wao kuongezewa bajeti, iwasaidie askari hawana nyumba, wakienda likizo hawana huduma, askari hawana chochote hata sare hawana, wangesaidiwa hilo kwanza. Lakini kununua silaha kwa kupambana na raia wake sio suluhisho, nguvu ya umma haiwezwi na Askari Polisi. Tunamwomba sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, ni mtu safi sana, awarekebishe viongozi wake ambao hawaitakii mema nchi yetu hii. Kama kuna kiongozi anasimama hadharani na akasema kwamba, Mkuu wa Wilaya hakikisha kwamba CCM imeshinda katika uchaguzi huu na maneno haya anamwambia Mkuu wa Wilaya ambaye vyombo vyote vya ulinzi ni vyake, tunachotarajia ni kwamba, Mkuu wa Wilaya hata kubali kukosa kazi, atakaa pamoja na *OCD* wapange uharamia. Je, hiyo ni haki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakitokea watu ambao watapinga mtasemaje? Mtajibu nini kwa Mwenyezi Mungu? Asikubali Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kupotezwa

na kuharibiwa na kuchafuliwa, yeye ni mtu safi sana. Kama huo si uhuni ni kitu gani? Asikubali hata kidogo .

Waziri Mkuu juzi katoa kauli hapa kuwaambia Wakuu wa Wilaya ambao hawatahakikisha kwamba Wilaya yake njaa imeshindwa, ina maana atashindwa kuondoa njaa katika Wilaya yake, atamfukuza kazi. Hiyo ndiyo kauli ya kiungwana na ndiyo amri ambayo inatakiwa aipeleke kwa kiongozi wake ambaye yuko chini yake.

Lakini kauli hii ya kusema kwamba, Chama cha CCM lazima kishinde, hii ilikuwa ni kauli ya kumwambia Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, si Mkuu wa Wilaya ambaye ni Mkuu wa dola Wilayani, ni Gavana wa Wilaya ambaye vyombo vyote vipo chini yake.

Mheshimiwa Spika, sisi tukizungumza tunasema kwa ushahidi. Tunakuombeni muiache nchi hii iwe makimbilio ya watu ambao nchi zao hazina amani. Vinginevyo mtakuja kutukumbuka tukiwa kwenye mashimo yale ya Mwanza kule Geita yanayochokolewa dhahabu, tutaingia mle sote na itakuwa hajulikani nani anamkimbia nani. Yakianza Kigoma yatamalizikia Kigoma. Kwa hiyo, naomba sana na namwomba Waziri, pia *IGP* atakapokuja, kiongozi wa siasa hata Waziri wake, ajue kwamba Waziri wake ni Katibu Mwenezi wa CCM, atakachompelekea akitie katika mizani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Haroub Said Masoud, uliyetaka kuomba mwongozo endelea sasa.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, naomba kupata mwongozo wa Kiti chako. Msemaji aliyekaa punde hivi alizungumza vizuri kwamba, Bunge si mahali pa masihara, mzaha na aliyasema yaliyomkera, lakini nadhani Bunge lako limedhalilishwa kiasi ambacho nikikutajia tafsiri ya maneno aliyosema, basi utaingiwa na kiwewe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ametamka kitu, jana pamechezwa ... hapa. Natoa tafsiri ya ... kwa sisi Wanzibari ni mchezo au ni ngoma inayochezwa na mashoga wakiwa uchi, wanakaa na mabwana zao. Sasa kama lugha hiyo unairuhusu basi mimi nilitaka mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Spika hakujua maana ya ... ndiyo maana hakuona kwamba neno hilo lina athari kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Kwa hiyo, tutalifuta kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

*(Neno hilo lilifutwa kwenye Hansard kwa maagizo ya Spika)*

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, nami pia napenda nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuzungumza katika kuchangia

hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Kwa kuwa si mara yangu ya kwanza kuchangia, nilishatoa pole na pongezi kwa watu wote waliostahili.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijatoa mchango wangu, kwa kuwa kitu hicho nilikisahau pale nilipochangia katika Wizara ya Ujenzi, ningependa kumshukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Kisiwa chote cha Pemba na Wazanzibari kwa ujumla, Mheshimiwa Rais Mkapa kwa msaada wake, alipokwenda kufungua nyumba za Polisi kule Pemba, kwa kutembelea shule yetu ya sekondari pale ya Fidel Castro, akajionea mwenyewe hali ilivyo. Kutokana na uchakavu wa shule hiyo kama alivyotangulia kusema mwenzangu hapa kwamba, Mheshimiwa Benjamin Mkapa ni mtu safi, mwenye imani, Mwenyezi Mungu alimzidishia imani hapo akatoa msaada wa shilingi milioni kumi kuboresha hali ya shule hiyo na namshukuru kwa kusema ukweli kwamba, amezitembelea shule nyingi sana za sekondari katika Tanzania hii na nje ya Tanzania, lakini hakupata kuona shule ambayo ipo katika hali mbaya sana ikapita ile ya Fidel Castro na akazidisha kwa kusema kwamba, shule iliyoko katika mazingira kama hayo angeweza kupasi angalau mtoto mmoja. Lakini kwa sababu wanapasi zaidi ya mtoto mmoja akaona kwamba, kwa kweli kazi ya ziada inafanywa na walimu na wanafunzi wa hapo. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wote wa Pemba ambao watoto wao wanasoma hapo, ningependa sana kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa ukarimu wake huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kusema kwamba, tofauti na wanavyofikiria watu wengine kwamba, labda Vyama vya Upinzani au *particularly* Chama cha CUF, ambacho ndiyo Chama changu, kina ugomvi na uhasama na Jeshi la Polisi. Si kweli kabisa, ningependa nikisemee kabisa Chama changu kwamba, si kweli. Chama changu hakina ugomvi na jeshi lolote, hakina ugomvi na Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi, Usalama wa Taifa wala kikosi chochote cha ulinzi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hususan kuhusu Jeshi la Polisi, Chama changu kinatambua kabisa kabisa na kuthamini mchango na umuhimu wa kuwepo kwa Jeshi hili kwa sababu Chama changu kinaamini kwamba, katika jamii kuna watu kama alivyoeleza Mbunge mmoja jana hapa, wa makundi tofauti. Kuna watu wazuri, wabaya, wahalifu, wa kawaida na majambazi. Sasa kwa kuwa Chama hiki kina wanajamii, kiko katika jamii ambapo jamii isingependa kwa kweli kukerwa na kubanwa na waovu hao na kwa sababu Chama changu kinaelewa kwamba jamii yenyewe isingeweza kuepukana na adha za waovu hao, basi bila shaka tungeamini kwamba, kuwepo kwa Jeshi la Polisi kungesaidia sana kutusaidia tukapumzika. Hatuna matatizo na Jeshi la Polisi. Tunawatakia kila la kheri katika kutenda kazi zao isipokuwa tunasema tu kwamba, wawe waadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni Jeshi muhimu sana, lina kazi ya kulinda raia na mali zao, lina majukumu mazito na kuhakikisha kwamba, sisi hatuna ugomvi na hawa, mimi katika hotuba yangu ya mwaka 2003 nilichangia pia na kwa kweli nilipiga kelele sana kama Mheshimiwa Waziri atakumbuka, kwamba Jeshi la Polisi pamoja na ugumu wa kazi yao na mazingira magumu waliyonayo katika kutekeleza kazi zao ukilinganisha kazi yao, majukumu yao na majukumu ya vikosi vingine vya ulinzi na usalama, ukiangalia mapato yao kwa kweli tunaweza kusema kwamba, jeshi hili linapunjwa sana kimaslahi kwa sababu inaonekana kwamba, hawana nyumba za kuishi kama inavyoelezwa hapo.



Mbunge mmoja alisema hapa kwamba, katika nyumba wanazoishi, *partition* baina ya nyumba moja na nyingine ni shuka. Hiyo ni hali dhaifu ambayo kwa kweli kila mmoja anaweza kuielewa, lakini ndiyo inayowakabili na haimfurahishi mtu yeyote kwa sababu hii inafanya mtu afikiri kwamba, mtu kujiunga na jeshi hili anakuwa dhalili kiasi gani pamoja na umuhimu wake. Kwa hiyo, tungeomba kwa kweli Serikali isitie pamba kwenye masikio, isikilize matatizo yanayoelezwa na Wabunge hapa kuhusu matatizo yanayolikabili Jeshi la Polisi na iyatatue.

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayolikabili Jeshi la Polisi yameelezwa na ni mengi. Kwanza, tunasema kwamba, hawana usafiri wa kwenda hata katika vituo vyao vya kazi. Unamkuta Askari Polisi anatembea kwa miguu, amebeba bunduki au anakwenda kazini na baiskeli pia amebeba bunduki. Hebu tuyaangalie mazingira kama haya jamani, binadamu ni binadamu, kwa mfano, amebeba bunduki, amekosewa akapondwa au kukanyagwa na gari, hiki ni kitu ambacho mara nyingi kinamtia mtu hasira. Sasa yakitokea mazingira kama hayo, amekasirika na ana bunduki mkononi itakuwaje? Anaweza kufyatua, akifyatua ile, matokeo yatakuwa ni mabaya. Kwa hiyo, mimi nadhani tungeishauri Serikali hasa hasa wale askari wanaokwenda malindoni na bunduki begani, likaonekana kama hili ni tatizo wakapelekwa kwa usafiri maalum.

Mheshimiwa Spika, halafu Wabunge wengi wamepiga kelele hapa kwamba, Askari Polisi hawapandishwi vyeo. Mimi nilikuwa nazungumza nao kabla ya kuja hapa kwa kweli wengi wao ndio kilio chao hicho. Mmoja ananiambia mimi nipo katika jeshi hili huu ni mwaka wa kumi na tano na kama unavyoona mabega yangu ni matupu, hakuna chochote, miaka kumi na tano! Lakini tatizo siyo hilo tu, wanasema kwamba, hata hao wanaopandishwa vyeo baada ya kurudi masomoni wanakaa muda mrefu hawalipwi kulingana na vyeo vyao vipya.

Mheshimiwa Spika, pale Chake Chake kuna mfano mmoja, kuna askari mmoja marehemu pale alikuwa anaitwa Nahoda Uffi. Huyu amekufa akiwa na cheo cha Sajini Meja, miaka tisa imepita toka ameondoka kwenye Usajini akaenda kwenye Usajini Meja, lakini amefariki akiwa bado hajalipwa tofauti ya mishahara kutoka Usajini mpaka Usajini Meja, miaka tisa! Sasa tunaweza kujiuliza jamani hivi hii mishahara inayotokana na ngazi tofauti za hawa maaskari ni haki yao au ni bahashishi tu kwa sababu kama ni bahashishi mtu anaweza kupewa wakati wowote, lakini kama ni haki yao kwa nini inacheleweshwa kiasi hiki?

Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri mambo kama haya kwa kweli ayarekebishe kwa sababu kama tunavyosema kwamba, Jeshi la Polisi ni muhimu na ikiwa kuna mapungufu makubwa kama haya yanawavunja moyo na wakati mwingine ndiyo yanayowasukuma kuingia katika hayo mambo ambayo tunasema kwamba sio mazuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu suala la *passport*. Mwaka 2003 pia nilisema hapa kwamba, *passport* inampa mtu uhuru wa kwenda anakotaka kihalali lakini zinabanwa sana katika kutolewa kwake lakini hakuna marekebisho yoyote kwa kweli

yaliyofanywa mpaka sasa. Nadhani Tanzania nzima hii pamoja na ukubwa wake ni vituo viwili tu vinavyotoa *passport*.

Kwa upande wa Zanzibar zinatolewa Unguja Mjini pale na kwa upande wa Tanzania Bara sehemu yote hii, Mkoa mmoja wa Tanzania Bara ni mkubwa kuliko Visiwa vyote viwili vya Unguja na Pemba na pamoja na hivyo ni kwamba *passport* zinatolewa Dar es Salaam peke yake kwa mujibu wa ufahamu wangu.

Sasa hebu na tuangalie, mtu anayetoka Kigoma, Mwanza au Mtwara anaifuata *passport* Dar es Salaam, jamani huu si usumbufu kweli kweli?

Mheshimiwa Spika, kwa nini kila Ofisi ya Uhamiaji ya Mkoa isiwe ni kituo cha kutolea *passport*. Kuna tatizo gani? Ikiwa sisi wenyewe tunasema kwamba, mtu ana uhuru wa kwenda anapotaka basi kwa nini kila Mkoa usiwe na kituo cha kutolea *passport*?

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilisema hapa kwamba, sisi *CUF* hatuna tatizo kabisa na Jeshi la Polisi na katika hilo nataka kunukuu maneno aliyozungumza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake: “Aidha, hatua maalum zitachukuliwa kuliwezesha Jeshi la Polisi kujiandaa kwa ajili ya kutekeleza na kufanikisha vyema majukumu yake katika kuhakikisha usalama wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.”

Sisi hatuna matatizo na hili, isipokuwa utekelezaji tu wa hili ndiyo tuna mashaka nalo. Kwa sababu ni kweli kwamba, katika uchaguzi wanasiasa kila mmoja anavutia kwake. Kauli zimetolewa hapa kwamba, iwe isiwe lazima CCM washinde. Imetolewa kauli hapa kwamba, kwa vyovyote CCM haiwezi kuondoka kwenye madaraka.

Sasa hapo ni wazi kwamba, nguvu, hila, zitatumika na sisi Wapinzani lazima tuhakikishe kwamba, tunatumia nguvu kupingana na nguvu zitakazowahakikishia watu kukaa kwenye madaraka. Sasa tunachomba Polisi jamani na vyombo vingine vya ulinzi vimetolewa rasmi katika siasa, tulikuwa na Mkoa mzima wa Majeshi lakini sasa hatuna. Vimetolewa katika siasa, tunawaomba watuachie wanasiasa tupambane sisi kwa sisi wasiingize mkono wao. (*Makofi*)

Vyama hivi ni Vyama vya wazalendo, hakuna mgeni aliyeunda chama hiki, kila mmoja ameruhusiwa kuunda Chama na maana yake ni kwamba, anaruhusiwa kutawala nchi hii, ndiyo maana yake. Sasa unaposema kwamba, CCM itakaa daima hamkubali Wapinzani kushinda huko ni kutangaza vita.

Sasa kama ni kutangaza vita basi mimi ningeshauri vita hivi vipiganwe kati ya vyama na vyama. Tusingefurahi hata siku moja kuona chombo chochote kile cha kiulinzi kinashiriki kuvuruga uchaguzi. Sisi *CUF* tunasema kwamba, lilopita basi si ndwele tugange lijayo. Muungwana ndiyo maneno yake hayo.

Tulishuhudia kule Pemba Polisi kwa maelekezo mabaya walichukua masanduku kwa mtutu wa bunduki katika uchaguzi wa mwaka 2000 wakayapeleka katika Ofisi za Wakuu Wilaya. Yaliyotokea ndiyo hayo yaliyotokea na yakazaa na kuzaa watu wakafariki kwenye maandamano Januari, 21, nchi hii ikazalisha wakimbizi, ni matatizo yaliyosababishwa na Polisi kuingilia ushindani wa kisiasa. Sasa ningeomba kwa kweli Jeshi la Polisi liwe safi, lituachie sisi wanasiasa tupambane kila mmoja avune alichokipanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nategemea tutapata mabadiliko ya kutosha katika uchaguzi wetu wa mwaka 2005, kwa maslahi ya Watanzania na kwa maslahi ya kila anayeitakia mema nchi hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. KHAMIS ALI SALEH:** Mheshimiwa Spika, shukrani nyingi sana. Nilikuwa na hamu nayo sana ndiyo maana nikawa namna hii. Unajua *I was eager to get this chance*. Kwanza, ni masikitiko, mnajua mwalimu ni mtu maskini sana katika Tanzania hii, nasema labda katika ulimwengu wote hata England mwalimu ni mtu maskini. Leo mwalimu kapata *chance* moja ya urithi wa kaka yake, kapata urithi wa ardhi au kiwanja cha kujenga nyumba, urithi maana hana umiliki wa kuweza kumiliki yeye, kwa kweli mwalimu ni mtu maskini. Kwa kweli hata sanda anachangiwa, naomba mkubali suala hilo, kama yupo mtu amekuwa mwalimu hata sanda anaweza kuchangiwa, mwalimu ni mtu maskini sana. Hilo tujue kabisa.

Leo mwalimu huyu kapata *chance* ya urithi wa kaka yake kafariki kawahi kupata kiwanja hicho. Leo mwalimu kajitayarisha Baraza la Mji limempa *chance* ana *right* ya kupata kiwanja hiki na ana *right* ya kujenga katika kiwanja hiki. Leo kajenga maskini kafika katika *course* ya nne katumia *one and half millions* katika kujenga kwenye kiwanja hiki, leo kaambiwa hii sehemu ni ya Polisi na *before hand it was not the property of Police*, ilitokezea tu vipi kajenga mwalimu huyu maskini ya Mungu kadunduliza fedha zake mpaka kajenga bahati nzuri mpaka kafika *four courses*, ni jambo kubwa sana kwa mwalimu. Mwalimu ni maskini kabisa katika ulimwengu huu hata England, *I tell you*. Hiyo mtambue. Mimi nilikuwa mwalimu najua hiyo hali. Nafahamu sasa mwalimu huyu kaambiwa abomoe nyumba yake ni eneo la Polisi, *how comes*, ameshajenga mwenyewe kajiwekea fedha zake, yeye na mke wake amefanikiwa kujenga nyumba hiyo mpaka kafika *four courses* kaambiwa abomoe!

Mheshimiwa Spika, *this is a property of Police, how comes na before hand it was not like that*. Jamani kaambiwa abomoe na kafika kuwekwa ndani kwa sababu hakubomoa. Hii imetokezea Wete Pemba ni sehemu ambayo kabla ilikuwa si *property* ya Polisi lakini ilitokezea tu *emergence* kama hii ni *property* ya polisi, yeye karithi kwa kaka yake. Baraza la Mji limempa habari kwamba, ana *right* ya kujenga akajenga *four courses* kafika, mwalimu ni maskini anachangiwa sanda nakwambia hivyo lazima *to believe* hii *situation*, wengi wetu sisi tulikuwa walimu. Sasa huyu bwana kaambiwa akajenge, kajenga Baraza la Mji limemruhusu kisha baada ya muda kaambiwa abomoe na akakataa kubomoa katiwa ndani *one day* kwa sababu ya kukataa kubomoa. *Then* imebidi abomoe amebomoa. Mwalimu ni maskini kaamua kubomoa au labda imebomolewa na

Polisi wenyewe, jamani katumia milioni moja na nusu mwalimu anaipata wapi hiyo ya kujengea nyumba nyingine kabomolewa.

Kwa hiyo, hili suala ningemba huyu mwalimu kwa kweli aangaliwe vizuri *at least* alipwe *one and half millions* jamani, mwalimu ni mtu maskini *I tell you. I was a teacher before hand, I tell you* abomoe nyumba mwalimu maskini ya Mungu, maskini wa Macca tunamwita kwa jina lingine abomoe *four courses*. Kwa hiyo, tuangalie hiyo hali. Kwa hiyo, naomba huyu mwalimu *at least* alipwe fedha zake. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni masikitiko kwamba, yuko Askari kastaafu kazi baada ya muda maskini Mwenyezi Mungu kajalia ahadi yake imefika kafariki. Sasa hivi watoto wake wanataabika wanataka riziki zao *at least* wafutie machozi, baba yao kafariki walipwe fedha zao jamani. Jamani mimi nimewahi kumpa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi barua na *documents* zote kuhusu suala hili, lakini baada ya hapo hakuna lililotekelezwa mpaka sasa hivi. Askari huyo kafariki watoto wake wanataabika wanasoma, wanataka chakula, wanataka fedha za *uniform* na wanataka vitu vingi tu. Jamani tulifikirie hili suala Askari maskini wa Macca hana fedha hata za sanda. Askari kafariki watu wake wanataka angalau wapate chakula, wapate fedha za *uniform*, wapate fedha za kulipa ada na mambo mengi tu, lakini Askari huyu hana alilolipata.

Mheshimiwa Spika, lingine tunaamini kwamba, Askari ni chombo muhimu sana katika ulimwengu, nafahamu labda haitwi kama mtu kafa kiahadi tu haitwi lakini ukianguka mti Polisi anaitwa, kauliwa mtu mwrite Polisi, mambo kama hayo. Sasa huyu Polisi ana jukumu kubwa sana katika ulimwengu huu nafikiri hatujui lakini kwa kweli ana jukumu kubwa sana kabisa, nafahamu ana jukumu zito kabisa lazima tumwangelie. Lakini Askari leo kapata nafasi ya kwenda kusoma Moshi na kafanikiwa kafaulu vizuri sana mitihani yake, ame-*qualify* sehemu nyingi sana, kwenye *Police Duties* kapata *marks* nzuri, kwenye *Leadership* kapata *marks* nzuri, *Criminal Laws* kapata *marks* nzuri, *Traffic Investigation* kapata *marks* nzuri, *Criminal Investigation* kapata *marks* nzuri, *Criminal Procedures* kapata *marks* nzuri na *Law of Evidence* kapata *marks* nzuri.

Polisi huyo, *not* mwalimu, *his conduct was good, his academic ability was good*, sasa huyu mtu haki zake, kaacha watoto wake akaenda kusoma Moshi anarudi *at least* apate kitu kinachostahili, *he should get status*, bega lake lina nyota lakini jikoni hakuna kitu. Jikoni hakuna kitu, *status* kubwa, ana nyota nzuri sana begani, *but in the kitchen there is nothing*. Polisi jamani ni lini atafikiriwa huyo. *I know the man well*, huyo ni *D2734 PC* Bakari Khamis Kombo, Polisi Kaskazini Pemba. Kamaliza masomo tarehe 9 Novemba, 2001 mpaka mwaka 2004 hana chochote, bega lake lina nyota nyingi, *this man is important* lakini hakuna kitu. Jamani lini atafikiriwa kijana huyu? *I talk about Police*. Lini atafikiriwa kijana huyu leo mpaka mwaka 2004 hana chochote.

Kwa hiyo, naomba hili suala Mheshimiwa Waziri wa Mambo Ndani ya Nchi alifuatilie, nakumbuka ni mwalimu wangu ndiyo maana namwita mwalimu mara nyingi. Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri ni Mwalimu, *he taught me*, anafahamu. Kwa hiyo, hili suala alitazame jamani.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la Kariakoo, *I mean is market place and others market places* katika *region* zingine. Ni kwamba Kariakoo ni mahali mtu anakwenda kununua chakula na kununua bidhaa zote. Lakini leo unakwenda pale kidogo unaporwa simu yako mwenyewe umeinunua na una saa unaporwa. Sasa unaporwa vile, unateguliwa hivi, hakuna mtu anayekusaidia, Polisi anapita pale, Mgambo anapita pale, *you need a police to help you for that* hakuna, Polisi anakwenda, *how comes*, mgambo anakwenda, mimi ninauliwa hapa jamani mnaniona ehee *what is there*. Kuna nini baina ya Polisi na huyu anayepora, labda kuna kitu ndani yake! Ningeomba mlione hili suala, Kariakoo unakwenda kununua chakula, leo unaporwa pale watu wanaona wote hawathubutu kukusaidia na Polisi anapita hivi anakwenda zake, nakuhitaji uje unisaidie leo unakwenda tu, mgambo jamani unaniona nauliwa hivi, *how comes* Kariakoo na nchi hii imejitawala.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la *FFU* Finya, nashukuru Mheshimiwa Waziri kalizungumza hili suala kwamba, sasa anaendeleza majengo katika bajeti hii. Lakini kuna matatizo ile sehemu ya Polisi *before hand* ilikuwa hakuna Polisi ile. Pale kulikuwa na njia watu wanapita, Polisi pale kuna njia kabla ya yale majengo, watu walikuwa wanapita pale kwenda mashambani, wanafunzi wanatoka kwenye kijiji fulani kwenda mashuleni, lakini baada ya kujengwa Polisi pale wamezuiwa njia. Hadi inafikia wanazunguka maili moja na nusu nafikiri hadi kufika shuleni kwa wanafunzi na wakulima wanapata tabu sana. Hii njia ilikuwepo kabla.

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wanaomba kwamba hii njia jamani iwepo hata kama kuna Polisi wanapita kama kawaida leo hii vipi wanapewa masafa makubwa wanafunzi wanachelewa hata kufika shuleni wanafika si kwa wakati. Suala hili nafikiri niliwahi kumpa Naibu Waziri sijui *how far it has been resolved, I don't know*, lakini nilimpa suala hili kwamba wananchi wanapata tabu, wanatoka mbali kisha pale wanapata masafa makubwa sana, wanafunzi wakitoka kijiji fulani wanapita pale inabidi wageuze njia na kwenda sehemu mbalimbali hata wakifika shule wanachelewa.

Kwa hiyo, tunaomba *at least* hii njia iwepo, nafikiri hawana madhara yoyote na wako mbali na ile sehemu ambayo njia ipo, inapitika bila matatizo yoyote ya kuharibu hali ya Polisi ilivyo, haidhuru sasa hivi na majengo yanakwenda kuongezwa pale nafikiri, lakini wapewe njia wapite ili wanafunzi wafike shuleni mapema, tunaomba hilo.

Mheshimiwa Spika, mimi nafsi yangu napata tabu sana kule wananchi wananiambia jamani mwalimu mbona hujaomba kuhusu suala hili, nawaambia nimeomba nimelipeleka kimaandishi, nimewahi kuzungumza kuwa *at least* mpewe ile njia ili muweze kufika shuleni kwa wakati na wakulima wapite katika njia ile bila tabu yoyote lakini *still* nafikiri, *no solution has been obtained so far*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri pamoja na majengo ambayo yataweza kuendelea pale, naomba wapewe njia wananchi wasipate masafa ya kutembea mbali kabla ya kufika kwenye mashamba yao na wanafunzi wasitembee mbali kabla ya kufika shuleni.

Nawashukuru sana *FFU* wa Finya, *they are very disciplined* lakini *problem* ni hii, wapewe njia hawa wakulima wanapokwenda kwenye mashamba yao na wanafunzi wanapokwenda shule, wapewe nafasi ya kupita katika njia rahisi ili wafike shuleni bila ya kuchelewa. Hii ni kuonyesha kwamba hatuna matatizo sisi Wapinzani, tunaipongeza sana bajeti hii, tunataka waongezewe Polisi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi ya awali kabisa, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niwe mchangiaji mmojawapo katika bajeti hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, nitumie pia nafasi hii kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Katibu Mkuu, *IGP*, Makamishna wote na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii nzuri, yenye mtazamo wa kuimarisha ulinzi wa raia na mali zao.

Baada ya kusema hivyo, naomba nitamke kabla sijafika mbali kwamba, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nitumie nafasi hii kuwapongeza Makamanda ambao wanajitahidi kwa kiasi kikubwa kuhakikisha ulinzi wa Mikoa yao unaimarishwa nikianza na Mkoa niliopo sasa hivi, Afande Gumbu apongezwe. Kwa kweli Mkoa wa Dodoma sasa hivi ni shwari na ninapata kifua cha kuzungumza kwamba, CCM itaendelea kupeta tu kwa sababu mifano hai tunayo. Nikisogea Morogoro ni shwari na *RPC* ni bomba. Nikienda Pwani safi, nikisogea Dar es Salaam mambo shwari, nenda Kilimanjaro, nenda Arusha hata Zanzibar mambo ni shwari tu. CCM itaendelea kushika madaraka tu. Wengine mnasumbuka mkiweza jisalimisheni si nyumbani njooni tu, tutawapokea, tufanye kazi pamoja ya kuleta amani katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo Mikoa hiyo tu hata nyumbani nilikotoka hali siyo mbaya sana. Mkoa wa Singida ulianza kutetereka kidogo kwa sababu *RPC* alikuwa anaumwa kwa muda mrefu, namwombea kwa Mwenyezi Mungu aendeleo kumpa uzima ili aweze kushika nafasi yake na kuchemka kama alivyozoea. Labda nitumie nafasi hii niombe Serikali impe msaidizi hodari ambaye atachemka kama yeye anavyochemka ili kuhakikisha kwamba, haya mapungufu madogo madogo yanayojitokeza yanatokomezwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, *RPCs* ni wengi tu wanaofanya vizuri bila kuwasahau wanawake wenzangu, yuko dada yangu *RPC* wa Tanga, Mtwara huko wanawake wanafanya kazi nzuri sana. Niombe Serikali iendeleo kuwatambua akinamama na kuwaongeza madarakani, uwezo wanao. Tuna mfano hai hapa tunaye *OCD* Jamila ni mwanamke lakini Mji ni shwari. Yuko mwanamke nje pale ni mdogo tu, Meja Mary, anaongoza magari yetu, Meja Mary akikosekana siku moja tu magari yanayumba pale. Dada wa watu anafanya kazi barabara, basi niombe Serikali hii iwe

na utaratibu wa kuwapongeza na kuwapa tuzo wale wanaofanya vizuri ili kuwatia moyo. Utaratibu huo wa kuwapongeza udumishwe iwe ni pamoja na kuwapeleka masomoni watu wakapandishwe vyeo maana wenzetu *promotion* zao zinahitaji kusoma, wapatiwe nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kuchangia bajeti hii kama ifuatavyo: Nikianza na vigezo vya kwenda kujiunga na Jeshi la Polisi, naishukuru sana Serikali imekuwa na utaratibu mzuri kila baada ya miezi sita vijana wetu wanaenda kuchukua mafunzo ya Jeshi la Polisi. Sasa idadi inayokwenda kule ni wachache, vijana wetu wengi wanabaki mitaani ndiyo mwanzo wa kuwa na wazururaji, ama mwanzo wa kuwa na majambazi. Tuongeze idadi ya kupeleka vijana wetu kwenye mafunzo ya Jeshi la Polisi ni nafasi ambayo inaweza ikachukua vijana wetu. Vilevile vigezo vinavyotumika kwenda katika Jeshi la Polisi vingine vimepitwa na wakati vifanyiwe marekebisho.

Hili suala la urefu mimi sioni kama ni kigezo kizuri, hivi kijana mfupi ana tatizo gani kama ni silaha kuishika anaweza, kama ni busara kichwani zipo, vigezo hivi naomba vipunguzwe na habari ya kusema kwamba mpaka kijana afaulu apate *division three*, hivi *division four* ina tatizo gani? Kijana ana upeo mzuri kabisa wa kuelewa mambo. Tuongeze vigezo ambavyo vitawaruhusu vijana wengi kujiunga na Jeshi la Polisi na Majeshi mengine ya Magereza na kadhalika. Naomba na *division four* itambuliwe ili vijana wengi waweze kujiunga na mafunzo haya ili kupunguza vijana wanaozurura ovyo mitaani bila kazi kwa sababu sifa wanazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, nitumie pia nafasi hii kuongea suala zima la ujambazi. Naipongeza Serikali kwa kweli imepunguza kwa kiasi kikubwa wimbi la ujambazi, tunasikia Kilimanjaro wamekamatwa, sijui Dar es Salaam wamekamatwa, sijui wapi wamekamatwa, kwa kweli kazi nzuri inafanyika. Lakini bado wapo, hivi tuna sababu gani ya kushindwa kutokomeza hawa majambazi hapa nchini wote waishe. Inawezekana adhabu wanazopata ni ndogo, mimi naiomba Serikali hao majambazi wakikamatwa sasa hivi wauliwe, maliza hapo hapo, hawana sababu ya kuishi hawa. Mbona wenyewe wanapovamia kwenye nyumba za watu wanawaua unakuta wanamuua baba mwenye nyumba, wanaua mama na wanaua watoto. Kwa hiyo, mimi nadhani hata sisi tuna haja ya kubadilisha vipengele vingine vya kuwahukumu hawa watu.

Nina hakika tukifanya hivyo, tutakuwa tumetokomeza suala la majambazi. Majambazi wana mtandao kweli kweli, aliyeko Kilimanjaro unakuta anawasiliana na wa Tabora, sasa tuhakikishe mtandao wao tunaufuatilia na tunauharibu kabisa.

Mheshimiwa Spika, tukifuatilia mtandao wao tutakuwa tumewavunja nguvu na ndani ya kupambana na ujambazi tuhakikishe kwamba, Serikali yetu inakuwa na silaha zinazotosheleza na zenyewe uwezo wa kupambana na silaha wanazotumia hao majambazi. Majambazi wa leo si wa jana, wana silaha za hali ya juu na zenye uwezo mkubwa.

Kwa hiyo, ni vizuri na sisi tukawa na silaha zenye uwezo wa kupambana na majambazi hao na siyo silaha tu, pamoja na magari. Wilaya zetu zina gari moja, gari hilo OCD anaongozana na msafara wa Waziri Mkuu, kwenye Kituo hakuna gari, je, likitokea lolote huko nyuma watafanya nini?

Mpaka aende ajinadi kwa Mkuu wa Wilaya, ajinadi kwa Mkurugenzi kuomba gari, hao majambazi watakuwa bado wanasubiri tu. Ninaomba kila Wilaya ipewe angalau magari mawili ili waweze kupambana na majambazi wanaojitokeza wakati gari moja labda OCD amesafiri nalo. Nina hakika tukifanya haya tutakuwa tumesaidia kwa kiasi kikubwa kuleta ulinzi wa amani katika Wilaya zetu na Mikoa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba niongee habari ya madawa ya kulevya. Kweli Serikali inapambana sana na madawa ya kulevya, bangi na vinginevyo, lakini bado yapo mambo haya na inawezekana hata sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge hapa tunafahamu watendaji, tutumieni tutawaelekeza kwamba nyumba ile pale nenda utapata. Tutumieni tutawaambia, yanawaumiza vijana wetu, vijana tunawazaa wana akili nzuri, lakini wameshakuwa wajinga tu wanazurura ovyo, wanalewa ovyo, wanavuta bangi ovyo, kwa sababu zipo zinaingia na zinapatikana. Nawapongeza waliochoma bangi huko Musoma, hongera zao.

Tuulizeni tuwaambie hivyo vitu vinapatikana wapi tutawaonyesha na mkiwapeleka Mahakamani basi wafungwe wakae huko hata miaka 30 wakirudi huku mradi umekufa. Sasa mvuta bangi au muuza unga anaingia Magereza leo na anatoka.

Mheshimiwa Spika, nimelindwa sawasawa muda wangu kweli, naona napelekwa puta? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, niongelee suala la nyumba za Askari. Niliongea hapa tukajibizana na kaka yangu Mheshimiwa Capt. John Chiligati kwamba, nyumba za Askari hadhi yake ni ndogo, hazina maadili. Sasa tuwe na mkakati wa kudumu. Tuambiwe hapa kwamba mwaka huu tunajenga nyumba za Askari, Singida tutajenga nyumba kadhaa na mikoa mingine kadhaa, zenye hadhi ya kumudu familia zetu. Familia za watoto wa kiume na wa kike wapate heshima yao. Mtasababisha watu hawa waanze kuoana sababu wanalala wote. Singida pale nyumba zimepitiwa na barabara zimebomolewa. Sasa ni wakati muafaka kutafuta maeneo makubwa ili muanze kujenga nyumba za kudumu za askari.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo vile vile maaskari hawa wawezesheni wakistaafu wataelekea wapi. Hawana nyumba hawa, mishahara haitoshi, wakopesheni vifaa vya ujenzi wajenge nyumba zao ili waking'atuka wawe na mahali pa kuelekea. Wanakuwa wanatangatanga tu wanapostaafu mpaka tunawahurumia kwa sababu maandalizi ni duni ya kustaafu kwao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, niongelee juu ya suala la rushwa. Rushwa kwa kweli Serikali inajitahidi kuitokomeza lakini bado ipo. Hii ni kwa sababu maaskari hawa hawajashiba, mtoto ukimlisha akashiba kudowea kwa jirani haendi.



Mishahara yao midogo, ongezeni mishahara yao. Nina hakika mkiwashibisha hawa, hivi vishawishi vitapungua. Wapeni marupurupu yao. Nashukuru sasa hivi wanalipwa madai yao mbalimbali yaliyosalia. Basi nadhani leo ni wakati muafaka wa kutamka kwamba, mpaka mwezi fulani malipo yatakuwa yameisha kama mlivyofanya kwa Walimu. Nina hakika maaskari watafurahi nchi nzima na watafanyakazi zao barabara.

Niongelee suala la Uhamiaji. Nashukuru *PCB* sasa hivi ina huduma mpaka Wilayani. Ninaomba basi na Uhamiaji huduma zao zifike mpaka Wilayani na ikiwezekana habari za kupata pasipoti iishie Mkoani. Hii habari ya mlolongo mpaka Wizarani mpaka wapi, mtu unachukua miezi miwili, mitatu, mpaka sita. Mtu ana *scholarship* yake ya kwenda nje mpaka anachelewa. Mtu ana biashara yake ya kwenda nje mpaka biashara inachacha.

Ukiritimba wa kupata pasipoti umekuwa ni mkubwa tena tunawa-*over work* watu wa Makao Makuu. Wanakuwa na kazi kubwa kumbe huduma hii tungeipeleka mikoani tungekuwa tunawanusuru watu wa Makao Makuu. Ukienda Uhamiaji Makao Makuu unakuta utitiri wa watu, tatizo ni pasipoti. Pelekeni huduma Wilayani na Mikoani kupunguza karaha kwa wananchi. Nilisema juzi hapa watu wanavyofuatilia fuatilia mambo Dar es Salaam watagongwa na magari kule, hawajui matumizi ya taa. Pelekeni huduma mahali watu walipo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niongelee habari za ajali barabarani. Ajali zinaendelea kupatikana siku hadi siku. Jana basi la Tashrif limeanguka huko Manyoni limeua watu kwa ajili ya mwendo mkali. Hivi suala la vidhibiti mwendo liliishia wapi, mbona magari yanakimbia mno? Huu mradi ulikuwa mradi gani ambao unaishia mbugani? Nina hakika magari hayana vidhibiti mwendo vilishatolewa kama sio kuondolewa vimelegezwa. Ninaiomba Serikali ihakiki magari hayo yote upya kuwanusuru wananchi. Wananchi wetu hata Bima za Ajali hawana, wanakufa kama ng'ombe amekufa, hata haki zao zinapotea. Magari yanakimbia kupita kiasi. Nina hakika kungekuwa na vidhibiti mwendo hadi leo, *speed* hizo zisingekuwapo. Kwa hiyo, ninaamini Serikali itakuwa imelisikia hili, itafuatilia magari yanakimbia mno.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la Zimamoto. Nashukuru kwamba, Jeshi la Polisi kuna askari wa Zimamoto, lakini hawana vitendeakazi wapo tu. Mikoja yetu haina magari ya zima moto, Singida kiliungua kituo cha stendi kiliteketea tunaangalia hivi hivi kwa macho. Nyumba za watu zimeungua zinamalizika hivi hivi tunaziangalia. Magari ya Zimamoto hakuna. Tuhakikishe tunakuwa na mikakati yenye kuwasaidia watendaji kufanya kazi zao kikamilifu. Hatutanusuru mali za wananchi, mali za Serikali katika suala zima la moto kama hatutakuwa na vitendeakazi hasa mikoani. Nashukuru Dar es Salaam sasa hivi wana mikakati, wananunua sasa hivi magari ya Zimamoto Manispaa zote karibu za Dar es Salaam basi na mikoani, hii mambo ni mikakati tu jamani. Nina hakika Serikali mkijiwekea mikakati yenu mtatekeleza. Waziri wa Fedha, alituambia hapa kwamba yeye ni mtaalamu mzuri kabisa wa kutafuta fedha na kweli Waziri anajitahidi. Pelekeni bajeti inayolingana na mahitaji yenu, Serikali ione yenyewe jinsi ya kusaidia. Msipeleke bajeti kwa kujinyimanyima mambo mengine mtashindwa kutekeleza tutawalaumu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Napenda niseme kwamba, kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, ninawapa pole sana ndugu zetu wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa kufiwa na ndugu yetu Mheshimiwa Marehemu Yete Sintemule Mwalyego na tunamwomba kwa Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ni nzito sana Kitaifa kwa sababu Wizara ya Mambo ya Ndani imebeba mambo mazito katika Katiba ya Nchi. Katiba ya Nchi imebeba mambo makubwa mawili, nayo ni haki na wajibu kwa mtu mmoja mmoja na kwa vyombo vyetu vinavyoshirikiana kumfanyia kazi mwananchi ambaye kazi yake ni kuiweka dola kwenye madaraka ili iweze kumtendea haki na iweze kumsaidia katika maendeleo yake. Sasa napenda niseme kwamba, ni wajibu wetu Watanzania kuwapa haki zao wenzetu wanaofanya kwenye vyombo vya dola. Wawe ni Polisi, Askari Magezea, Wanajeshi na wengineo katika vyombo hivyo ni vyema tukazingatia wakati wote kuwapa haki yao. Haki ya wenzetu kwenye vyombo vya dola ni haki ile ile ya msingi kwamba, lazima wapate chakula, lazima wapate malazi, mahali pa kupumzika na lazima wapate haki ya elimu na mafunzo, vinginevyo wanakuwa hawawezi kuendelea kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, rai yangu ni pamoja na rai ya wenzangu wengine kwamba, umefika wakati wa kumaliza tatizo la malazi kwa Askari Polisi wetu nchi nzima. Sasa naomba tulimalize hilo. Nilikuwa naomba Wizara na Serikali kwa ujumla, ituambie ina mkakati gani wa kumaliza tatizo lenye aibu kubwa la namna tunavyowalaza Askari Polisi wetu. Jana wenzangu wamezungumzia juu ya nyumba zilizo na mapazia kwa kugawanya vyumba na kwamba ukieleza malazi ya Polisi wetu maeneo mbalimbali ya nchi bado unakuta tuna vijumba ambavyo hatustahili kuwalaza Askari Polisi wetu katika maeneo ya namna hiyo, ni kuwanyima haki na kuwaondolea haki ya msingi walitakiwa kwa kweli watupeleke kwenye Tume ya Haki za Binadamu.

Mimi ninaomba Wizara na Serikali kwa ujumla, iweke mkakati pamoja na kwamba, sisi Wabunge tumeshinikiza kwa kweli Serikali ikaongeze bajeti ya Wizara hii ili vyombo vyetu vya dola viweze kufanya kazi katika maeneo mbalimbali yawe ni maeneo ya vifaa na sasa suala la malazi naona hili limebakia sugu. Mimi naomba Waziri atuambie vizuri mkakati walionao wa kumaliza kabisa tatizo la malazi ya ovyo ya askari wetu nchi nzima. Hatuwezi kuendelea na hali hii katika Karne ya 21. Kwa maana nyingine nilitegemea kwamba, tungeletewa hapa Bungeni utafiti unaoonyesha ni namna gani tunaweza tukaanza kujenga nyumba kwa ajili ya Polisi wetu nchi nzima zenye heshima kama ambavyo tunajenga nyumba 300 hapa Dodoma za wafanyakazi wa Serikali na nyumba nyingine zinajengwa Dar es Salaam, kwa nini tusingetumia hata fedha hizo tukabadili kabisa sura hii ya makazi ya Polisi wetu nchini, ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili mimi nitaling'ang'ania ili leo mpaka nielezwe vizuri kwamba, tuna mpango gani hasa wa kwenda karne ya 21 kwa pamoja kwa sababu haki hii ni ya msingi kwa ndugu zetu. Kwa nini walale na watoto wao wakati watoto wao tayari wana matiti na wengine wanataka kuoa. Kwa nini? Kwa nini hali hii tusiiondoe tuweke mkakati gani tuambizane na Watanzania tunajua namna ya kuweka mikakati tunaweza tu. Tuweke *reform* ambayo inaweza kutupa moja ya mambo ya kuweka ni makazi ya heshima kwa Polisi wetu nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo napenda liambatane na suala la kutazama mfumo mzima wa mambo ya vyombo vyetu vya dola. Wenzangu wamezungumza kwamba, tuko kwenye karne ya 21, tuna vyombo ambavyo tunaweza tukavitumia leo katika ulinzi wa nchi yetu. Tuna ushirikiano mzuri wa Afrika Mashariki, tuna ushirikiano mzuri wa *SADC*, tuna ushirikiano mzuri wa nchi mbalimbali za Afrika ambapo tunakumbushwa kwamba bila amani na utulivu nchi haiwezi kuwa na maendeleo ya kweli. Sasa amani na utulivu ni pamoja na vyombo vya dola kufanya kazi kwa ufanisi. Polisi wawe na magari. Mimi najua tatizo la magari kwa Polisi wetu ni kubwa. Kwa nini tusiweke mkakati kwamba magari yawepo ya kutosheleza na tuweke mfumo ambao utahakikisha tuna magari mwaka hadi mwaka.

Mimi nakumbuka Wilayani kwangu Sengerema ninahangaika na magari hawana hata namna ya kuleta mahabusu kwenye Mahakama ambayo iko mbali, kilomita 11 inakuwa vigumu. Kwa hiyo, hatimaye mwananchi mmoja mmoja anapata matatizo ya kupata haki yake kwa sababu tumeshindwa kutoa vifaa ambavyo vinatakiwa vitumiwe na Polisi na vyombo vingine vya dola. Mimi nasema tulifanyie utafiti jambo hilo la namna ya kuweka *reform* kama ambavyo tumefanya katika maeneo mengine ya vyombo vya Serikali. *Reform* nzima itakayoendana na karne ya 21 na utoaji wa haki ili watu wawajibike ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hivyo nilikuwa nataka niombe kwamba, Polisi hawatoshi nchi hii na katika nchi nyingi unaweza ukakuta Polisi hawatoshi. Nchi nyingi za Afrika Polisi hawatoshi, lakini pale wanapopata nafasi ya kuwa na wenzao kama Sungusungu basi hao lazima wawape utaratibu wasaidiane nao ili katika upelelezi katika kushika majambazi timu yake iliyopita tumefanikiwa sana kuwatumia Sungusungu. Lakini ilifika mahali sijui ilitokea kitu gani, Sungusungu wamefifia wametoweka na mimi nafahamu kuna mifano ambayo walikuwa wanasema aah siku hizi tunabambikiziwa mambo ya ajabu kwa hiyo tunajitoa katika kufuatilia mambo ya uhalifu. Kwa hiyo, uhalifu wa miaka ya 1970 umerudi upya baada ya kuumaliza na kuupunguza miaka ya 1980 na 1990 sasa umerudi upya na Polisi hawatoshi na wananchi Watanzania tumeongezeka na ujanja, utapeli, wizi na ujambazi, umeongezeka pamoja na athari za wakimbizi. Sasa huwezi ukakwepa kuwatumia Watanzania wenzako ambao katika sehemu kadhaa za nchi unakuta wako wanaoitwa Sungusungu.

Hilo nilikuwa napenda nilizungumze kama kifungu cha (a) cha haki ambayo Polisi anastahili apewe kama mwananchi mwenzetu, kama chombo chetu cha dola cha kutusaidia sisi tufanye kazi kwa amani na utulivu. Sehemu ya pili ni ile ambayo inataja wajibu. Polisi nao tunawaomba wawajibike kwa suala moja kubwa kwamba wananchi

wanalalamika Vijijini wanabambikiziwa kesi. Mimi katika jimbo langu na Wilaya yangu nafahamu mifano kadhaa ambayo dhahiri mimi nimeifuatilia mpaka hata Ukerewe nimeifuatilia. Bahati nzuri mimi nimepata bahati ya kuwa Mkuu wa Mkoa Mwanza, pamoja na Ukerewe ikiwemo. Maeneo hayo ya kubambikiziwa kesi yapo ni ya kweli. Sasa Polisi wachache wenye tamaa wanawabambikizia kesi wananchi kwa tamaa ya rushwa. Katika maeneo ya wafugaji kama Mwanza, Shinyanga, Tabora, Mara na sehemu zingine watu wanabambikiziwa kesi ili kusudi watu wajipatie hiyo mifugo wauze watajirike. *Yarabi*, wananchi wanateseka kule kwa tamaa za Polisi wachache!

Mimi nafahamu mifano ambayo mwezi Januari, Februari, nimekagua Gereza la Kasungamile Wilaya ya Sengerema, nikawakuta watu wanaeleza dhahiri kwamba, inaonekana wamebambikiziwa sio wao waliofanya makosa. Sasa mtu anaweza akasema aah hilo ni suala la Mahakama kuweza kujua kama ni makosa au la. Lakini kuna *common sense* ambayo ingeweza kutumiwa na Polisi kwamba hivi ni kweli huyu tumemsingizia. Mbona mimi kuna mzee mmoja alisingiziwa na watu wa Vyama vya Upinzani kwamba huyo mzee wa CCM alihusika na kesi ya kuuu mtu. Tulipofuatilia tukakuta yule muuaji akasema kabisa pale pale gerezani aah sio huyu mzee ni mimi ndiye niliyefanya mambo hayo, kwa masikio yangu mwenyewe. Kwa hiyo, ni dhahiri kabla watu hawajapata njia ya kufika kwa *State Attorney* wakasema juu ya suala kama hilo utakuta mtu atateseka pale mahabusu atakosa haki yake na ataliwa mali kwa muda mrefu kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ninakotoka, kuna wananchi Vijijini hasa wale wanaonekana ni matajiri kidogo, kwa stadi za Vijijini wana ng'ombe na vitu vingine, hao wanabambikiziwa kesi ili kusudi ng'ombe waanze kuchukuliwa mmoja mmoja na hatimaye wanamalizika. Athari kubwa sasa ya suala hilo ni kwamba, kama mtu anafahamika Kijijini vizuri, anafanya shughuli zake za maendeleo vizuri, ni mfano wa kuigwa na wenzake akaja akabambikiziwa kesi akaanza kuendeshwa maana yake kwamba anapopata hofu anapochukuliwa kwenda mahabusu na mahabusu ndio unakwenda kukaa wala siku hazihesabiki. Anapochukuliwa huyu Kijiji kizima kinapata hofu kinaogopa hakifanyi tena mambo ya maendeleo. Huu ni utafiti wangu. Hakifanyi tena mambo ya maendeleo watu wanasema aah Mlekwa amechukuliwa nani tena atakuwa hapa, ataonyesha kifua chake. Maana amechukuliwa yule *opinion maker*. Yule Kiongozi wa kushauri na ameonyesha maendeleo, yeye ndio anakuwa mtu wa kuonewa.

Mheshimiwa Spika, mimi hilo jambo linaniuma sana na ninaomba kabisa wajibu wa Polisi wetu la kwanza liwe la kuambizana kwamba kama una tamaa ya rushwa basi tuambizane Kitaifa. Polisi tuwape mishahara tuwaongezee lakini hili tuhakikishe kwamba halitokei tena. Wako wananchi mahabusu wanateseka kweli na ndio maana napenda nipendekeze, pamoja na kuwaambia Polisi waache mtindo huo wa kubambikizia kesi watu, mimi naomba tuweke mfumo wa Mabaraza ya haki Wilayani ambayo kila wiki au wiki mbili yapitie kesi hizo ambazo zinasema Shija amefanya hivi au Maduhu amefanya hivi, tuzipitie kwa maana ya safu ya Viongozi ili tujue kwamba hii kesi ya kuku wala sio kesi, achana nayo na Wazee wa Baraza wa maeneo hayo, wanaowafahamu watu wanaotuhumiwa waweze kusema. Hilo mimi naliona ni jambo muhimu sana. Ukimkosesha haki mtu maana yake hata familia yake umeiua, maana yake hafanyi kazi

ya maendeleo, maana yake Taifa hili halizalishi kupitia kwake na wale wanaomfuata na hasa kama akiwa Kiongozi wa familia yake au Kiongozi kwenye eneo lake, maana yake unaua Taifa kisirisiri.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo napenda tuizingatie, pendekezo langu ni kwamba, tuwe na Mabaraza ya haki pale Wilayani. Mkuu wa Wilaya atakaa humo, wazee mashuhuri watatu labda na Idara ya Polisi itakuwemo na tutaweka safu nzuri pamoja na vyombo vingine vya madhehebu na kadhalika, tuweze kuanza kutenda haki na kupunguza idadi ya mahabusu ambao wanakaa katika Magereza na mahabusu kwa muda mrefu bila kupata haki yao. Suala hilo ni la msingi sana, kuna wananchi Vijijini wametuambia na sisi wenyewe tunajionea wanakosa haki wanashindwa kuzalisha na Taifa maana yake linakuwa halina tija kupitia vitendo vya namna hiyo.

Baada ya kusema hivyo, napenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi na kwa kweli namuunga mkono Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anazungumza naomba akumbuke nilimwandikia barua kuhusu matatizo ya Polisi na Magereza Sengerema. Barua hiyo alinijibu akasema kwamba, anaishughulikia. Sasa kama ni kuishughulikia leo nampa pesa aniambie Mheshimiwa Waziri kwamba analishughulikiaje tatizo hilo la Sengerema.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami nichangie hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu binadamu tuna tabia ya kusahau, mimi naomba nianzie kwa kuiunga mkono mia kwa mia na wala sina mushkeli wowote na hotuba hii na yote yaliyokuwemo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu, *IGP* na watendaji wote wa Jeshi hili. Kwanza, vile vile nimtakie kila la kheri jirani yangu hapa Mheshimiwa George Lubeleje katika mechi yake ya kesho anayopambana na Simba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa binadamu tujiulize tunakotoka, tulipo na tunapokwenda na hasa hata sisi Wabunge tunatakiwa tuangalie miaka 10 iliyopita tulikuwa wapi nchi yetu juu ya maendeleo. Lakini kwa vile leo tunazunguzia suala la Wizara ya Mambo ya Ndani, tujiulize wale Wabunge waliokuwa mwaka 1995 wamo ndani humu na wale waliokuwa hawamo tuangalie namna ya Jeshi hili lilivyokuwa mwaka 1995 na yale ambayo yameshafanikiwa hadi hivi sasa. Sasa binadamu tunatakiwa tukishayafikiria hayo, tutaweza kuboresha na kuweza kupata maendeleo katika nchi yetu.

Wizara hii ilikuwa katika Wizara duni kabisa na nadhani miaka si mingi iliyopita Waheshimiwa Wabunge hawa hawa tukiwemo sisi tulipiga kelele sana juu ya Jeshi hili tukampigia kelele sana *IGP* na tukamwona kama vile amekosea kwa sababu ya kusema

kwamba, bajeti yake ni ndogo na akiongezewa bajeti basi ahakikishe kwamba, atailinda nchi hii ipasavyo. Leo baadhi yetu tumeisikia hotuba iliyosomwa kwa niaba ya Upinzani. Leo baada ya mafanikio mazuri na baada ya Serikali kuongeza bajeti, tunailaumu Serikali kwa kuituhumu tuhuma ambazo sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana miaka miwili iliyopita ni kwa sababu Serikali imeanza kwenda mbio, imeanza kujiweza katika mapato yake na ndiyo maana Wizara ya Mambo ya Ndani ikasaidiwa. Hapa jana palizungumziwa suala la ujambazi. Mimi kwa kweli nilikuwa mnyonge sana kusikia Mheshimiwa Mbunge anayesoma hotuba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, anasema eti badala ya kuipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani au Jeshi la Polisi, anasema kwa sababu Kiongozi Mkuu wa Nchi akiwemo Mheshimiwa John Malecela, mkewe ndiyo amefikwa na maafa yale ndiyo askari wanafanya kazi yao vizuri. Si kweli. Nasema si kweli kwa sababu nina ushahidi wanyonge kuliko wanyonge wamevamiwa na majambazi na hatua waliyochukua Polisi hawa ni kubwa zaidi kuliko hiyo iliyochukuliwa kwa Mheshimiwa John Malecela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki tatu zilizopita majambazi walivamia duka la Simu za Mkononi Mtaa wa Uhuru, wakafunga barabara ya kuingia na kutokea eneo lile wakaiba simu zile. Kwanza, wenye duka wale ni vijana wetu wadogo wa kutoka Pemba ndio duka lao lile pale. Hawana Waziri, si Viongozi wa Chama cha CCM, si Kiongozi yeyote. Majambazi walitoweka wakakimbia wakaenda zao wakasalimika. Lakini Jeshi hilo hilo la Polisi ndiyo maana nikasema nimekuwa mnyonge sana kwa kutowapongeza Jeshi lile. Baada ya siku tatu Jeshi hilo hilo lilifanya uchunguzi wake likapambana na majambazi hao hao na baadhi yao wakauawa na baadhi yao wakatoroka.

Lakini sasa kwa sababu hatutaki kumpa mtu haki yake lakini miongoni mwa majambazi hao kwa sababu majambazi wote hao walikwenda pale walikuwa wanatoka Kisiwa cha pili cha Pemba, nasema hivi mmoja wao alitoroka akaenda Zanzibar, Mwera, Kijiji changu, Jimboni kwangu akajificha. Sasa niambie baada ya kuwasifu Mapolisi unawabughudhi. Baada ya siku nne kikosi cha askari 10 walitoka Dar es Salaam wakaenda kule wakamvamia wakamchukua wakamleta Dar es Salaam. Sasa duka lile la nani la Mheshimiwa John Malecela, Spika au Waziri wa Mambo ya Ndani? Ni jamaa wadogo kabisa wa Kipemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nawapongeza sana na tunapozungumza tujaribu kufanya utafiti, tuseme yale ya ukweli. Pale nyuma walikuwa hawawezi kufanya kwa sababu nyenzo walikuwa hawana. Magari kama tulivyosikia jana hapa, bado tuna kila wajibu kuwatetea kama yukimkunika Waziri wa Fedha ana haki kuwatafutia angalau kila mkoa, *Land Cruiser* moja na atuletee *mini-budget* hapa wakati wowote tutaipitisha sisi kwa Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuchangia nazungumzia suala la Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Kusini Unguja. Tangu nimeingia Bungeni hapa nilikuwa nikizungumzia suala hilo. Alipokuwa Mheshimiwa Muhammed Seif hapa ni Waziri nilimwambia bahati haikuwezekana kutokana na ufinyu wa bajeti. Nakumbuka mwaka

1997 nilipokwenda Uhamiaji pale ilikuwa Ofisi iko Mkoani nikaingia ndani mle sikukuta meza wala kiti, nikauliza jamaa wako wapi kumbe wako kwenye mwembe. Kama sikosei wakati ule alikuwepo Mkuu wa Uhamiaji wa Mkoa, alikuwa ana masharubu kama yangu mimi, akiitwa jina la masihara *Teacher*. Nikauliza mbona hivyo, akasema nyumba haikaliki. Nikapiga kelele hapa baadaye nashukuru sana Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja akatupatia angalau Ofisi ya kujishikiza.

Mheshimiwa Spika, ulipokuja pale Tunguu kuweka jiwe la msingi na ukatoa ahadi tarehe 25 Aprili, 2004 katika sherehe za siku ya Muungano tukalifungua jengo lile la Ofisi ya Bunge nikashtuka sana nikasema leo kazi ipo. Nikaonana na ndugu yangu Mheshimiwa Capt. John Chiligati nikamwambia sasa kuna mbio baina ya Naibu Waziri na Waziri wako na Mheshimiwa Spika, una uwezo gani sasa na wewe mwezi Aprili, 2005 jengo lile la Uhamiaji liweze kuhamiwa. Nashukuru ndugu yangu aliniahidi kwamba na yeye atakuwa yuko bega kwa bega na wewe ahakikishe kwamba, Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Kusini Unguja inafunguliwa katika sherehe za Muungano mwezi Aprili, 2005. Bahati nzuri nimefarijika sana kuona katika kitabu hiki kwamba, maelezo yamo mazuri sana. Kwa hiyo, mimi nampongeza sana na hasa namfagilia sana Mheshimiwa Capt. John Chiligati na naomba tuendelee kufagiliana mimi na yeye na Wazanzibari wote ili yeye arejee na mimi nirejee hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia sasa hivi ni suala la ukarabati na ujenzi wa majumba ya Askari Tanzania nzima. Tukitaka tusitake, Wizara ya Mambo ya Ndani imejitahidi na inaendelea kujitahidi.

Mheshimiwa Spika, lakini labda nieleze jambo moja kabla sijaelezea hilo. Kiasi cha miaka kumi iliyopita nilialikwa katika harusi na harusi hiyo ilikuwa kubwa sana. Kule Zanzibar tuna kwamba tabia siku ya harusi kunakuwa na sherehe kubwa, tunakwenda bwawani, bi harusi anavalishwa veli. Hiyo harusi niliyokwenda mimi bibi harusi alivalishwa veli thamani yake Sh.300,000/= . Sasa tulipokaa bibi harusi na bwana harusi wameishaingia kumbe yule bibi harusi hana viatu! Hiyo ni kwa sababu unapoingia ndani huwezi kuiona miguu yake. Nilipouliza ni kwa nini hana viatu, nikaambiwa kulikuwa hakuna pesa Sh.50,000/= ya kununua viatu. Nikasema hii Kasheshe sasa. Tumeweza kutoa Sh. 300,000/= lakini tukashindwa kununua viatu! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mfano wa hayo nimetoa kwa zile nyumba za Chake Chake za Mfikiwa, Wawi. Ni nyumba nzuri sana zimejengwa *in billions* zinang'aa, lakini hazina umeme na umeme *cost* yake haipindikii milioni 15. Nadhani Mheshimiwa Waziri afanye kila njia huyu bi harusi avalishwe viatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwepo pale Chake Chake kama Mkuu wa Kituo mwaka 1970. Nimetokea kule na ndiyo maana kila mara ninakusisitiza kwamba usinikoseshe nafasi katika Wizara hii, Polisi wananiuma kwa sababu na mimi nilikuwa ni Polisi. Nilipokuwa pale tulikuwa na tabia kwamba kila baada ya miezi fulani hivi Mkuu wa Kituo anafanya *inspection* katika majumba na *uniform* zao. Sasa kuna nyumba za

ghorofa pale Chake Chake, nilipokwenda juu kukagua, kwa sababu unaingia mpaka ndani, kwa bahati mbaya nikaagonga chupa hivi kumbe chupa ile ilikuwa na mkojo!

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu nyumba zile zilikuwa hazina vyoo chini wala juu mpaka uteremke chini uende masafa ya mita 20 ndiyo uende haja na yule Askari alikuwa ana maradhi ya kisukari, huchukua chupa yake juu kwani anaona tabu kuteremka na hasa siku za mvua anaweka mle. Nilimwonea huruma sana. Kuna nyumba ndogo mbili pale nikamhamisha siku ile ile nikamweka katika nyumba ndogo nikamwambia kaa huku.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeona tatizo lile, imewajengea nyumba Askari, tunapongeza sana na tunampongeza Mheshimiwa Faida Bakar naye kwa sababu kila wakati anamfuatilia Mheshimiwa Chiligati kuona kwamba umeme unawekwa katika nyumba zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingawa tunajenga majengo mapya bado iko haja majengo ya zamani kwa kila Kambi ya Polisi libakishwe jengo moja ili tuwaonyeshe wale ambao wanasema kwamba nchi hii hakuna maendeleo, iwe kama ni nyumba za historia, ili waone nyumba ya ghorofa haina choo juu wala chini. Sasa zile ni lazima zibakishwe zisivunjwe zote.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninaomba kuchangia ni umaliziaji wa nyumba ambazo ziko pale Tunguu. Nusu ya nyumba zile zimeishaanza kukarabatiwa na ziko safi kabisa. Sasa itakuwa ni kichekesho kwamba Ofisi ya Bunge inafunguliwa, Ofisi ya Uhamiaji ya Mkoa inafunguliwa, lakini nyumba za Askari Tunguu milango yake imewekwa makuti. Nimeona pesa nyingi sana zimo katika ukarabati wa nyumba za Askari, ningekuomba vile vile kwa udugu wetu na urafiki mtufikirie sana na nyumba zile zimalizwe kwa sababu pale patakuwa ni mahali patukufu pakubwa sana kwani *University* ya Zanzibar nayo inajengwa pale pale Tunguu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naomba Wizara ya Mambo ya Ndani ilifanye kadri iwezavyo ni kujenga Kituo cha Polisi Uguja Ukuu, Kaipwani. Nimefurahi kwa kituo kizuri na kwa kupatiwa gari, lakini tungeangalia katika fedha hizi zilizotengwa za nyumba za Askari angalau nyumba moja ikaanzishwa kujengwa pale akaweza kukaa Mkuu wa Kituo ili aepukane na masafa marefu ya safari zake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba Askari wanaokaa kwenye Kituo cha Polisi cha Mwera kiutendaji wako Mkoa wa Kusini. Kwa hiyo, nina kila wajibu kuwatetea nao vile vile, lakini kimakazi wako Jimbo la Mwera.

Baadhi ya nyumba zile za ghorofa mwenyewe Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wanaelewa kwamba zinavuja sana inaponyesha mvua. Pesa zinazohitajika pale siyo nyingi, ningeuomba afanye kadri awezavyo nayo atupangie mambo maalum ya fedha za ukarabati pale.



Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwapongeze Vingozi wote wa Polisi wa Mkoa yote ya Tanzania wakiwemo Mkoa wangu wa Kusini Unguja, Kaskazini Unguja, sisahau vile vile kwa sababu Mkoa wa Rukwa ulikuwa ni Mkoa ambao ulikuwa ukipambana na ujambazi, lakini sasa umetulia kutokana na ukakamavu wa Mkuu wa Polisi wa Mkoa ule. Lakini pia, tungeomba Wizara ikaangalia uwezekano wa kuweka vituo maalum katika mipaka mle kama Kalema na Ikulo ili viongeze ulinzi kutokana na wakimbizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nalizungumzia suala la wakimbizi kwa sababu zimebakia dakika zangu mbili, ni kwamba wakimbizi idadi yao imetajwa hapa. Idadi ya wakimbizi wote sasa hivi ni 627,264, lakini hivi karibuni mimi na Mheshimiwa Asha-Rose tulipotembelea katika baadhi ya makambi ya Kigoma tukakuta kila ukoo mmoja, kila mume na mke ni kama kuna mashindano ya kuzaliana.

Hakuna ukoo hata mmoja katika wakimbizi wale waliokuwa na idadi ya watoto wasiopungua 15. Hii ni hatari sana. Sijui Mheshimiwa Waziri atatuambia nini wakati wa majumuisho yake hapa kwa sababu ikiwa sasa hivi ni 627,264 na kwa mujibu wa tathmini tuliyoipata pale kila mwezi mmoja kambi moja wanazaliwa watoto 127. Nasema hili ni pigo sana kwa Mkoa wa Kigoma unaowaweka wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, sijui sheria inasemaje, lakini kama kuna njia ya busara ya kuwapa vidonge vya uzazi wa majira, basi nadhani hiyo ndiyo itakuwa *solution*. Kama si hivyo wataongezeka hadi wafike milioni kumi, kama kila mwezi kambi moja, wanazaa hivyo! Aaah, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni kuhusu habari ya Magereza yetu. Magereza yetu kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge wengine bado iko haja ya kuyaboresha na vile vile kutafuta njia ambazo baadhi ya nchi jirani hata za wenzetu wanafanya, kwa sababu mfungwa siyo maisha yote atakuwa mfungwa, kuna siku atatoka nje. Kuna baadhi ya Magereza ya nchi nyingine wafungwa wanasomeshwa kompyuta, wanacheza mpira na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya atafuatiwa na Mheshimiwa Awesu. Mheshimiwa Yahya, jitahidi usipigiwe kengele mbili. *(Kicheko)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, najua wapo wengi wanaoomba nafasi kama hii, ni nafasi adhimu kabisa. Kwa hiyo, nakushukuru sana.

Pili, niwashukuru watoa hotuba hii Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Uongozi wake wote kwa jumla kutokana na hotuba yao nzuri ya kuleta ufanisi mzuri katika utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilio changu bado kipo hasa katika uongozi wa juu kuhusu Jeshi la Polisi. Mara nyingi sisi kabla ya hapo tulijitawala kwa kuondoa baadhi ya matatizo na kuweza kujiamulia wenyewe kwa yale ambayo tunahisi yana maslahi katika nchi yetu. Kutokana na hali hiyo tuliona kwamba baadhi ya mambo ya kikoloni hayaoani na maadili yetu na ndiyo maana tukafikia kiwango hicho. La kusikitisha zaidi na mara nyingi kilio hiki nakileta hapa kwamba, kuna baadhi ya *PGO* ambazo zimepitwa na wakati, kwa hiyo tunawajibika kuziondoa. Lakini baada ya kuangalia niliona haziathiri kwa Viongozi, bali zinaathiri kwa wale Askari wa chini, ndiyo maana mpaka leo hatujatafuta ufumbuzi wa kuweza kufanikisha shughuli hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, niliwahi kuzungumza hapa katika Bunge lililopita kuhusu *PGO* namba 47 na 48. Hata ukiangalia namba 47 kuna kitu ambacho wamejenga tabaka, Kiongozi wa juu/Afisa mwaka mmoja anakwenda likizo kwa siku 28, lakini hazikuingizwa Jumamosi wala Jumapili, kitu ambacho ni kinyume na Askari wengine. Kwa hiyo, utamuona kwamba Askari huyu anapata siku 36 kwa mwaka. Ukimuangalia Askari wa kawaida miaka mitatu anapata siku 84, lakini yule Askari wa juu utaona anapata siku 108. Sasa suala kama hili linaleta malalamiko kwa Askari wetu na panajenga kitu kama tabaka sehemu ya juu na sehemu ya wale Askari wa chini.

Mheshimiwa Spika, ningeomba mambo kama haya, madogo madogo kama hivi tuweze kuyarekebisha na hasa ukiangalia huko nyuma baadhi ya mambo sheria nyingi hapa tunazopitisha hazitekelezwi. Tulipitisha hapa mwaka 1999 kuhusu umri wa kustaafu, lakini lilikuja jibu lingine kabisa kwa upande wa Polisi. Jeshi lina kazi nzito sana na liliweza kuongezewa japokuwa miaka miwili, lakini kwa Polisi haikufanyika hivyo na hii inatokana na uongozi wa juu wenye mamlaka. Sasa ni vizuri yale mambo ambayo tunaweza kuyafanikisha tuweze kuyafanikisha kwa haraka zaidi isipokuwa kinyume na hivyo tunawavunja moyo ndugu zetu Askari wa chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna sheria hii ya *PGO* namba 48. Wakati wa kikoloni kweli ndugu zetu walikuwa wanaajiri, wanaajiriwa na mara nyingi mambo yao yalikuwa wanaajiriwa kuwa wawe wa kiinua mgongo. Naweza kusema kwa wakati ule kwamba hawa watu hawakuweza kueleweshwa vizuri nini faida yake na nini hasara yake. Sasa wakati suala kama hili tumekwishalielewa nini hasara yake na nini faida yake kwa nini tusiweze kulirekebisha? Sheria ngapi zinakuja hapa tunatunga sisi na wala haitimii miaka miwili baada ya kuona tu kwamba hapa hapana ufanisi mbona tunazibadilisha katika Bunge hili hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa ndipo pananitia mashaka kwa uongozi wa juu kwamba hauwafikirii Askari wake wa chini. Hapa wanasifiwa tu wanafanya kazi, lakini kwa uzalendo wa nchi yao na siyo kimapato. Kwa hiyo, masuala kama haya madogo madogo ningeomba vile vile tuyarekebishe. Leo Askari anafanya kazi miaka 37, wakati Askari yule ni wa kiinua mgongo anapata Sh.1,040,000/=. Unamkuta Askari aliyekuwa *pensionable* anapata Sh.9,000,000/=. Watu wale wameingia pamoja, wamefanya kazi kwa pamoja na muda wote huo wamechukua. Hivyo, mtu huyu unamfikiria atafanya kazi vipi? Maisha yake yatakuwa vipi?

Mheshimiwa Spika, hapa juzi tumepitisha sheria baada ya kuona wastaafu waliochukua pesa zao kwa mkupuo hawafaidiki na tukapitisha sheria hiyo ili wafaidike. Huyu leo hata pesa za mwezi hazipati kwamba umeandama akachukue pesa yake, unafikiri ataishi vipi? Mambo kama haya yanavunja moyo na mimi nasema yanavunja moyo kwa sababu Viongozi wa juu hawayafikirii. Haya hayakuwagonga wao na nina mifano mizuri tu.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1996 niko katika Bunge hili, yako mambo pia yalijitokeza, lakini Askari wa chini pia wakaweza kunyimwa. Sasa leo ajabu kabisa kwamba kuna watu wanaajiriwa pale ni Askari wa kawaida tu wenye namba zile *PF*, lakini utaona kwamba wanapata mapato kuliko hawa ambao wametumikia miaka mingi sana na wamepitia katika vituko mbalimbali. Sasa watu kama hawa tunawajibika kuwafikiria. Hizi sheria zibadilishwe kwani huu siyo wakati wake, kama nchi hii tumesema tujitawale kwa nini tunafuata sheria za kikoloni na bado zile haziendani na wakati wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili, ndugu zetu hawa ndiyo wenzetu. Ndugu zetu wametumikia Taifa hili muda mrefu sana, *PGO* hizi nasema zibadilishwe huu siyo wakati wake, ili tuwaridhishe na ndugu zetu kwa yale matakwa ambayo yataleta ufanisi katika shughuli zao za kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu kituo cha Chwaka. Muda huu unaingia mwaka wa 19 tunaomba usafiri katika Kituo cha Chwaka. Hivi sasa katika Jimbo la Chwaka nimefurahi kwamba kwenye kitabu chako ukurasa wa 19 pale ulisema kwamba bila shaka gari litakuwepo, lakini hakuna uhakika kwamba tutafanikiwa au vipi. Miaka 19 tunaomba usafiri, Jimbo langu hivi sasa sehemu za pwani zina shughuli za utalii na mara nyingi yanatokea matukio mbalimbali na yanataka kufuatiliwa. Sasa bila ya kupata usafiri wa uhakika Askari hawawezi kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa hiyo, naomba kipindi hiki tusaidiwe gari katika Kituo cha Chwaka.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kituo cha Chwaka hakikujengwa kwamba hasa ni Kituo cha Polisi, ni kituo cha kurithi na hivi sasa kimezungukwa na nyumba za Kijiji, ina maana hapana siri hapo. Kwa hiyo, naomba wafanyiwe utaratibu ili kupatiwa kituo kipya na kiwanja wanacho pale njia ya kuenda Uroa. Nafikiri Mheshimiwa Waziri ni mwenyeji pale anaelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, gari hili litatumika kwa ushirikiano na Kituo cha Dunga. Kwa hiyo, tukifanikiwa gari hili haimanishi kwamba litakuwa Chwaka, ina maana litafika mpaka kule sehemu za Mchangani na litakuwa inafanya kazi kikawaida kwa matukio yote yatakayojitokeza. Kwa hiyo, ina maana pana umuhimu sana kwa gari hili kuweza kuhudumia vituo viwili na tunaweza kufanikiwa katika shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini hicho kituo chenyewe cha Dunga tulipata kwa msaada, lakini ukikiangalia sasa hivi hakina dari na kina nyufa. Kwa hiyo, tunahitaji msaada mkubwa ili kuweza kukirekebisha kituo hicho kiwe kizima. Wapo wanaomba

wajengewe upya, sisi hatutaki kujengewa upya, tunataka kufanyiwa ukarabati, hivyo ina maana hasara yake itakuwa ndogo na ni hatari usipoziba ufa utajenga ukuta. Mheshimiwa Waziri, ningomba tusifikie hatua hiyo ya kuweza kujenga ukuta katika kituo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa kama ulivyoniya ni kwamba sijagongewa kengele. Kwa hiyo, leo najua na ninaunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwa vile ni mara yangu ya pili kuchangia, sina haja tena ya kuwapa pole wale waliofiwa na walioumia. Naomba niendeleo tu moja kwa moja na haya niliyoyakusudia.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mheshimiwa *IGP* ( rafiki yangu Bwana Mahita) na Maafisa mbalimbali wa Jeshi la Polisi na Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kwa kusema kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu nawaomba wakati wa kuchangia tupunguze jazba kwa sababu ili uchangie vizuri ni vizuri upunguze jazba.

Mheshimiwa Spika, la pili, ningewaomba wenzangu tusiingilie mambo ya ndani ya Jeshi la Polisi, hebu tuwaache wenyewe wafanye kazi zao, tusiwapangie. Nafikiri kila mmoja akisimama hapa sijui Polisi wametayarishwa kwa CCM, sijui wamefanya nini, si vizuri. Polisi bwana hawaangalii CCM wala hawaangalii *CUF*. Polisi wanafanya kazi ya kulinda nchi tuwaachieni wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba, binafsi ninapingana sana na kauli hizi za baadhi ya Viongozi wenzetu kung'ang'ania kule Shimoni. CCM hatutakwenda kabisa! Tusing'ang'anie kusema tutakwenda Shimoni, mimi nafikiri si kauli nzuri. Kauli za kung'ang'ania Shimoni tungojeane kwenye majukwaa ya siasa, lakini tusing'ang'anie hapa kwenye Bunge, kila mmoja tutakwenda Shimoni, tutakwenda CCM, tutakwenda *CUF*. Sisi CCM hatutakwenda, mtakwenda peke yenu mlizoea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, nina kero nne naomba niziseme. Kwanza ni suala la gari la Polisi katika Wilaya ya Mkoani. Wilaya ya Mkoani ina Kituo cha Polisi Mkoani na Mkoani ndiyo Makao Makuu ya Wilaya, kuna Kituo cha Polisi Kengeja na kuna Kituo cha Polisi Mtambile. Sasa hakuna gari hapa, ninachosema pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 19 kuwa: “Kuna magari ya Polisi ya Wilaya 174 yatanunuliwa.” Lakini haikufanuliwa kuwa na Wilaya ya Mkoani itapata, inawezekana tukapata au inawezekana tukakosa.

Mheshimiwa Spika, hizi gari hata zikinunuliwa, unasikia kauli za wenzetu huko Zanzibar mara wengine tutafanya vurugu, hivi hawa Askari Polisi watafuatilia saa ngapi na hawana usafiri? Naiomba Serikali popote pale, lakini Wilaya ya Mkoani ipatiwe gari

la Polisi, ni hatari sana. Ipatiwe gari ya Polisi na tusingalie jiografia ndogo, hii Wilaya ya Mkoani kuna Kisiwa Panza, Chambani, Wambaa, Kiwani ni kubwa tu. Sasa kukaa pale hatuna gari ya Polisi ikitokea ngangari hapa Wananchi wanaweza wakapata matatizo kwa sababu Askari Polisi watakuwa hawana gari ya kufuatilia. Tunategemea gari ya Mkuu wa Wilaya tu peke yake pale.

**WABUNGE FULANI:** Na yako je?

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mimi gari yangu nitawaazima sina matatizo, lakini wataazima gari yangu mpaka saa ngapi! Kwa hiyo, naomba nikiondoka hapa Mheshimiwa Waziri basi hilo gari la Polisi la Wilaya ya Mkoani niondoke nalo, nikishuka pale naenda kulikabidhi mwenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda nizungumzie ni kuhusu fedha za uhamisho. Kuna Askari Polisi wengi wameshahama, wengine wanatokea Wete wamepelekwa Unguja, wengine wanatokea Unguja wamepelekwa Mkoani na wengine wametokea Mkoani wamepelekwa Mkokotoni, hawa wao kuja hapa Bungeni wakasema hawana ubavu kwa sababu sisi ndiyo Mabalozi wao, wametutuma. Kuna mwenzangu mmoja juzi alilia hapa akamlilia Diwani wake na Mbunge mmoja naye alilia akamlilia Askari wake, sasa mimi nalilia hawa Askari ambao hawajapata pesa zao za uhamisho.

**MBUNGE FULANI:** Lia tusikie. *(Kicheko)*

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Naomba Askari Polisi waliokuwa hawajapata fedha zao za uhamisho wapatiwe malipo yao mara moja. Hii naomba ifuatane na ile ya Walimu, mbona ile ya Walimu ilikwenda mara moja tu! Walimu waliambiwa mara moja pesa zao watapewa. Sasa naomba na hawa Askari Polisi ambao walikuwa hawajapata pesa za uhamisho na wao waingie katika mkondo huu wa kupata fedha za uhamisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, naomba nizungumzie kuhusu nyumba za Askari Polisi Mkoani. Nyumba za Askari Polisi Mkoani wanazoishi au wanazofanyia kazi ni mbovu. Sasa naomba nyumba ya Polisi ya *OCD* pale itengenezwe na ofisi itengenezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe rai kuhusu nyumba za kuishi Askari Mkoani. Mwenzangu alipiga kelele mpaka zile nyumba zikajengwa. Najua kujengwa kwa mpigo haiwezekani, hebu kila kipindi cha baada ya miezi sita tujenge nyumba moja tu ya familia mbili. Mtambile mjenge moja, Kengeja mjenge moja na Mkoani mjenge moja. Hata tukimaliza miaka mitano inayokuja au kipindi kitakachopita hicho itakuwa tayari tumeishamaliza kujenga nyumba za Askari. Hili ni ombi maalum.

Mheshimiwa Spika, kuna Askari wengine hivi ninavyokuambia wanakaa Chokocho na Kisiwa Panza wanafanya kazi Mkoani. Mtu atoke na baiskeli tangu Chokocho mpaka afike Mkoani anakimbilia kufanya kazi Kituo cha Polisi Mkoani, wewe

unafikiria atafika kazini saa ngapi? Sasa naomba nyumba za Askari Polisi zijengwe na kila mmoja afanye kazi kwa kujua kuwa anafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu wastaafu. Wastaafu wengi wana matatizo ya kupata fedha zao kwa wakati. Ninachokumbuka ni kuwa wastaafu wanalipwa kila baada ya miezi sita, sasa wamenituma nao hivyo hivyo.

Basi huo muda upunguzwe, badala ya miezi sita mtu alipwe kila baada ya miezi mitatu ili kupunguza hii bughudha. Kwa hiyo, naomba pesa za wastaafu badala ya kulipwa kila baada ya miezi sita walipwe miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu vyeo vya Polisi. Nina ushahidi hasa hata pale Mkoani Pemba kuna Askari sasa wana miaka 13 wana cheo cha koplo na ninajua si Mkoani tu ni sehemu chungu nzima. Basi vile vyeo vya koplo imefika wakati tena watu wamevizea hata mtoto anamuita baba yake aliyemzaa koplo.

**MBUNGE FULANI:** Eeenh!

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Koplo Suleiman, Koplo Makame, Koplo Simba, jina lake halijui tena ni koplo tu. Hebu tuondoe hii adha ya kuwa tuna mtu koplo tu, watafutieni maarifa mengine muwape vyeo vingine ili watoto wao wabadilisha majina badala ya kumuita baba fulani anamwita Baba Koplo. Naomba yaangaliwe vizuri sana masuala ya vyeo vya Polisi ili na wao wajisikie raha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nisije nikasahau, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FETEH SAAD MGANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi sina budi kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie machache katika hotuba hii. Napenda kukuhakikishia wewe pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba sitakuwa na mengi kwa sababu mimi ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na tulikaa tukaichambua sana na tulivyoipitisha kule tunangojea muhuri wenu tu hapa kwamba sasa ikubalike Kitaifa.

Kwa hiyo, nasema kwamba tulifanya kazi nzuri na ninawaombeni Waheshimiwa Wabunge muwe pamoja nasi kwa sababu mlituamini mkatupeleka kule tukakae tuingie ndani kabisa ya Wizara hii tuifanyie kazi na tumeifanyia kazi. Kwa hiyo, nawaombeni muipitishie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli kama ni Askari wa Mwamvuli basi ni Askari wa Mwamvuli kweli, wamefanya kazi zao na wameteremka mahali kunapo janga la mapambano, hawa hawakuteremka juu ya miti wakakwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenyewe ni watendaji wazuri na wao wenyewe pia wana watendaji wazuri na wanawasaidia kazi kuanzia Makamanda wote wa Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji na hata hao wapokezi pia wa wakimbizi wanafanya kazi nzuri maana kama na wao wangukuwa hawafanyi kazi nzuri kule tungeanza kupata malalamiko nchini na duniani kututangaza kwamba sisi tunawatesa wale watu ambao ni Wakimbizi.

Lakini wanawaweka vizuri na wanawahudumia vizuri. Kwa hiyo, ninawapongeza wote katika utendaji wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza ndugu zangu wa polisi kwa sababu polisi ndiyo wanaoweka amani, ndiyo wanaoleta utulivu wa taifa letu hili. Wana kazi ngumu sana ya kulinda usiku na mchana. Ukiwatazama haya maisha yao hukubali kama alivyolalamika Mheshimiwa Mbunge mmoja akilia mwalimu na mimi nalia polisi wana shida. Mishahara ni midogo hali zao ni duni. Kubwa liliopo ni kwamba polisi hawezi kukaa nyumbani yeye anapangwa katika Mkoa, katika Wilaya katika sehemu mbalimbali na huko anaambiwa akae miaka mitano aondoke aende mkoa mwingine au aende Wilaya nyingine. Sasa mtu huyu yeye kazi yake kuondoka hapa kwenda hapa kutuliza amani, kukaa hapa kwenda hapa kutuliza. Lakini tatizo lililopo ni kwamba pale anapostaafu kwa nini basi tunamchelewesha huyu kumpa haki zake? Huyu anaporudi nyumbani anakuwa mgeni anaanza maisha mapya hana bustani, hana chochote kule nyumbani. Anahamia na wanae anarudi nyumbani akiwa amestaafu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri askari anapostaafu ahangaike kupewa mafao yake haraka akaanze maisha mapya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nakuomba kupitia kwako kwa Mheshimiwa Waziri, hata kama atapewa hiyo posho yake, lakini kama haikutazamwa kutoka sasa hivi akasaidiwa kuongezewa mapema, ataondoka na yale aliyazungumza msemaji mmoja hapa alikaa kwa miaka 12 akapewa shilingi 45,000. Naomba hili lisitokee maana hawa ni watoto wetu, ni ndugu zetu, vijana wetu wako katika shida kubwa. Ni juzi tu kumetokea wizi mkubwa kule Moshi wamefanya kazi kubwa walikuwa hawa polisi hawapo lakini wametumia juhudi yao na elimu yao waliyopewa. Wametumia vyombo ambavyo tunavyolalamikia hapa waongezewe fedha kwa sababu wasingeweza kuwagundua wako wapi, wale lakini wametumia *intelligence* zao na huwezi kumtumia mtu bila kumwalia vizuri. Uwezo wao ni sisi kuwapa zana na kuwapa uwezo na kuwawezesha waweze kufanya kazi zao vizuri, hapo ndipo wanaweza kukamilisha kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda ningozee tu juu ya suala la ujenzi wa nyumba. Kweli waliyozungumza wenzangu hapa kwamba pale Zanzibar pana kambi moja ya Ziwani hiyo kwa kweli sote tumezaliwa tumeikuta pale ni ya tangu miaka na miaka. Ni kambi ya zamani, si hiyo tu hata Kambi ya Ng'ambo lakini ile ya ziwani ndiyo tunasema kama sehemu kubwa ya Makao Makuu pale. Lakini hali ya kambi hiyo, tunashukuru juhudi zinafanyika lakini haijaridhisha kulingana na hali ya majengo yalivyo ndani. Wenzangu walizungumza hapa wakasema kwamba majengo yale yawekwe kama historia, lakini kwa kweli hata hiyo historia haifai maana ni kama mbavu za mbwa. Ni historia lakini kweli historia kama ile? Kama ni historia kunajengwa kitu mfano wa historia wa kuonyesha kuwa walikuwa wanakaa humu. Lakini kwani tunampeleka mtalii gani katika vikosi, katika ulinzi, zivunjwe zijengwe nyumba za kileo. Nani unampeleka katika

kambi ya ulinzi? Katika kambi ya ulinzi hawezi kupelekwa mtalii, hawezi kupelekwa mtu kwenda kutafuta historia, historia itolewe katika vitabu kule zibaki kambi za walinzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilizungumza na Mheshimiwa Waziri na mimi nalia katika kambi yangu ya Buwini kituo kidogo tu hata milioni 20 tu zinaweza zikamaliza kila kitu pale, mimi nimesema muda mrefu sana katika Bajeti iliyopita na Waziri akaniahidi kwamba basi ataalingalia suala hili.

Mheshimiwa Waziri, mimi ni rafiki yangu sana, pamoja na Naibu wake na nisingependa kuzungumza haya hapa lakini inabidi nizungumze kwani bado naona zile hatua hazijachukuliwa. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, vijana wangu wale wana shida kubwa sana, kambi yangu ya Bumbwini ina shida kubwa sana ikinyesha mvua inabidi vijana waondoke ndani ya lile jengo, hawana usafiri, hawana vifaa vya mawasiliano. Halafu eneo lake Bumbwini ni kubwa wanalofanyia kazi, ni eneo kubwa sana la Bumbwini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana hili suala ulishughulikie. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, labda nimalizie kwa kusema kwamba umefika wakati sasa hivi tugeuze mfumo wetu wa majeshi yetu katika kupambana na majambazi. Hali ilivyo ya majambazi sasa wanajifanya wao ndiyo wanataka kutawala nchi, sisi hatuwezi kuacha nafasi hiyo hata siku moja. Nchi itatawaliwa kwa mujibu wa sheria na kanuni, kwa mujibu wa wananchi wenyewe, siyo kutawaliwa na majambazi. Majambazi leo wanaingia mahali mchana na kuiba, faa iishe hivi hivi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba sana tuimarisha vikosi vyetu na zaidi turudi vijijini kwa sababu vijijini tunao ulinzi wa jadi, tunao mgambo, kwa nini tunashindwa kuwatumia vizuri hawa? Tuwatumie vizuri. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, tuimarisha *intelligence* yetu itakayoweza kutupa habari ya kila wakati kuna nini kinachopatikana katika majimbo yetu. Tukiimarisha mambo haya nina uhakika kinachotokea chochote tutakipata kabla hakijatokea, kwa sababu usalama ni kinga siyo tiba. Sasa sisi tukipata taarifa mapema tunaweza tukakinga. Linapotokea jambo basi tumefeli mpaka likatokea jambo, kwa nini tunaacha na kufeli wakati Tanzania ni nchi kubwa, Tanzania ni walimu? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kuzungumzia juu ya magereza kwa ujumla. Katika ziara yetu tumetembelea magereza mengi tu. Lakini naomba tuwashukuru viongozi na tuishukuru Serikali, imejitahidi sana. Kwa kweli hali ya msongamano kweli upo lakini siyo kama ule tuliokuwa tunauzungumza katika miaka iliyopita huko nyuma. Mheshimiwa Rais kwa uwezo wake alionao karibu ametoa wafungwa, *parole* imesaidia. Niipongeze Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa ushauri wake iliyokuwa inatoa kila wakati kumshauri Waziri na kuishauri Wizara kusaidia kupunguza msongamano katika magereza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nakupongeza wewe na kuipongeza Wizara yako kwa kazi nzuri lakini tuongeze juhudi zaidi. (Makofi)



Mwisho kabisa ili na mimi nisipigiwe kengele nasema hivi tukizungumza CCM ishinde tunanuna? Hakuna kununa CCM itashinda na tutarudi humu ndani. Kazi iliyoko ni kushirikiana kufanya kazi vizuri na hiyo ndiyo sera ya CCM. Ina sera nzuri na itashinda na ninawahakikishieni kwa msaada wa Mwenyezi Mungu tutarudi. Baada ya kusema hayo narejea kusema tena naipongeza Bajeti ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja kwa mia ipite. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya mwisho mchana huu ili niweze kuchangia katika hoja hii kwa sababu yako mambo ya msingi ambayo kwa kweli ni vizuri yakawekwa sawa.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao kwa kweli wamenipongeza sana katika hotuba zao za Bajeti na mimi nazipokea pongezi hizo kwa mikono miwili. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuwasilisha hotuba hii ya Bajeti vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa nisemee kuhusu maeneo mawili tu ambayo ni polisi na magereza. Mimi kule kwangu sina wakimbizi. Wengi wamezungumza hapa kwamba polisi iimarishwe na katika ukurasa wa 10 na 11 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa kweli Bajeti, inaongezeka mwaka hadi mwaka na hili ni jambo la msingi sana. Mimi ningependa niungane na Waheshimiwa Wabunge, waliosema kwa kweli Bajeti ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ingeongezeka kama uwezo unaruhusu basi iongezwe kwa asilimia 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la msingi kwamba vitu vyote hivyo tunavyopitisha hapa vitekelezwe, vinategemea sana utulivu na amani katika nchi yetu. Huwezi ukasema unajenga barabara wakati watu wanapigana pale, huwezi ukasema unachimba bwawa la maji wakati watu wameuawa kwenye kijiji hicho watu 100. Huwezi ukasema unajenga zahanati wakati kuna matatizo ya kiusalama na utulivu katika eneo hilo. Kwa hiyo, mambo yote ya maendeleo ambayo tunazungumza hapa na kuyapa Bajeti kwa kweli yanahitaji ulinzi, utulivu na amani, usalama wa raia na mali zao. Hii ni kazi ya polisi. Sasa mimi nilikuwa nasema polisi tusingalie uwingi maana kilio cha Wabunge hapa ni kwamba polisi ni wachache, polisi wachache kwa utaratibu gani? Mimi nasema polisi hawa wangefundishwa kabisa, wapate mafunzo na wapate wito kwa sababu kila kazi ni wito. Hata kufanya biashara ni wito uwe *committed* na kazi yako. Hata kuwa Padri/Askofu/Shekhe ni wito. Hata kuwa Mbunge ni wito, hata kuwa Spika ni wito. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa mimi nafikiri siyo uwingi wa polisi, tuangalie mafunzo ya hawa polisi wetu, kweli wanafundishwa, wana maadili mazuri? Maana yake polisi lazima awe mkakamavu, awe mwepesi. Sasa wengine wamenenepa mno hamna hata mafunzo ya ukakamavu. Sasa unaambiwa kuna majambazi pale, kuna ku-*crow* sasa tumbo liko kama tani moja utalivutaje? Hawa polisi mimi nasema wafundishwe wapewe ukakamavu wakomae halafu wafundishwe maadili. Mimi najua wako wachache ambao hawana maadili ya kipolisi na wenyewe wachunguzwe waondolewe, wanaharibu sifa nzuri ya jeshi letu la polisi. Halafu vitendea kazi hili nalo ni la msingi kuwe na vitendea kazi vya kisasa. Kwa

sababu mambo ya rushwa, kubambikizwa kesi ni watu wasio na maadili, hawana wito. Wale wote waondolewe katika jeshi letu la polisi ili liweze kuheshimika. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, pia suala mishahara. Suala hili la mishahara na lenyewe liangaliwe. Huyu polisi wa kawaida anapokea sijui shilingi 70,000/= kwa mwezi, lakini mtu mzito kabisa polisi anapewa karibu mishahara milioni. Sasa hii tofauti inakwendaje atajisikiaje? Mtu anayefanya kazi kubwa na nzito ni hawa polisi wa kawaida. Zamani polisi hawa wa kawaida unamkuta yuko magerezani amejifanya mfungwa, leo huwezi kumtesa huyu polisi wa Tanzania, aende akajifanye mfungwa magerezani apigwe ngwara! Lakini zamani polisi walikuwa na wito, anakwenda anateseka mahali pagumu kabisa hamuwezi kujua. Au anakwenda kuishi kijijini kwenye *rural* kabisa hamuwezi kujua kumbe anapeleleza kuna majambazi, kuna mauaji na kadhalika, mtu unakuja unakamatwa kila kitu na anakuja anatoa ushahidi unanza kushangaa huyu si alikuwa mwanakijiji mwenzangu, kumbe alikuwa polisi. Leo hawa polisi wako wenye maadili hayo na wito huo? Hamna. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, halafu hili la kuteka nyara kwa kweli ni aibu katika nchi ina miaka zaidi ya 40 tangu 1961 tumejitawala kwa utulivu na amani tumesaidia hata nchi zingine kupata uhuru, leo sisi tunashindwa kujilinda wenyewe, watu wanatekwa nyara wanapoteza maisha, wanapoteza mali, wanafanyiwa vitendo vya aibu hatuna ulinzi. Tunaacha eneo lingine la nchi yetu litawaliwe na majambazi. Hii ni Burundi? hapana! Nchi hii hatuwezi tukaruhusu ikawa kama Burundi. Ukiwa Burundi unasindikizwa na askari mchana na mnaambiwa mharakisha kurudi kwa sababu saa 12 ni utawala wa waasi, kule wanaitwa waasi. Sasa na hii Tanzania ni hivyo kutoka Ramadi kwenda Bariadi ukifika Dutwa pale ulale. Sasa nilale kitanda kiko wapi? Nani ananilipia gesti? (Makofi/Kicheko)

Ukitoka Mwanza kwenda Shinyanga Misungwi pale ulale, mimi nasema kama kuna askari mnawapa kizuizi pale, muwape hela za kuwalaza kwenye gesti hawa wanaowaambia walale kwa sababu hatuwezi kufanya hivyo. Maana yake nini? Mimi naona ajabu, Bwana Mahita, vaa njuga sasa acha hiyo kombati tukapambana na hawa na sisi raia tuko tayari hatuwezi tukaacha eneo lingine litawaliwe na majambazi eti majambazi na hawa ni majambazi waoga kwanza. Kwa nini mchana wanapotea hatuwaoni? Jeshi letu la ulinzi lina kazi gani, hatuna vita kama tunakwenda kusaidia Jeshi la Umoja wa Mataifa kwa nini Umoja wa Kitanzania tuisaidiane hapa? Naomba sasa Serikali kwa ujumla wake ifanye *marshal inspection* ya majambazi. Tukifanya upembuzi yakinifu wa kujua majambazi hawa wako wapi na wana silaha gani na wote tuwaue, hatuwezi kuendelea kuchezewachezewa kienyeji. Maana yake hawa ni waoga kwanza. Sasa hili la kuteka nyara kwa kweli ni aibu sana. Mimi sitaki kabisa wanateka mabasi na kadhalika. Kwenda Mwanza ukifika Magu pale unakwenda Mwanza unatoka Bariadi au msindikizwe na *escort* hapana hii siyo Burundi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, pia huu uvamizi wa Ziwa Victoria hii Serikali inafanyaje hawa wako wapi hawa?

Mheshimiwa Spika, halafu jambo moja ambalo ningependa niliweke wazi la msingi kabisa juu ya vyanzo vya uhalifu ambavyo ameorodhesha Mheshimiwa Waziri amesema mambo mengi ushirikina, visasi, uchumi duni, utamaduni, sheria mbovu na kadhalika. Lakini kiko chanzo kingine cha siasa. Katika nchi yetu siasa tunataka kuifanya kama chanzo cha uhalifu.

Mheshimiwa Waziri ni shahidi tulikuwa naye Bariadi kwenye uchaguzi mdogo. Bila kuwa na askari wa kutosha ulikuwa umeandaliwa uhalifu wa hali ya juu. Wenzetu wamekodisha mabaunsa kutoka Dar es Salaam, wamejaa *fuso* wamekuja Bariadi na wamesambazwa kwenye vijiji walikuwa na maandalizi gani? Tunataka kugeuza siasa kama chanzo cha uhalifu katika nchi. Tunataka kupanda mbegu mbaya na hawa watu wanatoka Dar es Salaam, wanakwenda kuchonganisha watu vijijini baada ya uchaguzi wanaondoka hawa wanakijiji wanaachiwa ugomvi usioisha. Naomba jeshi hili kwa kweli liimarishwe hasa tunapokwenda katika Uchaguzi Mkuu. Pia watu wengine wanafanya kwa maslahi yao na Mheshimiwa Waziri, siku moja amezuiwa kwenda kwenye mkutano watu wanatoka pale na magari na bendera za chama hicho wanatafuta nini?

**MBUNGE FULANI:** Chama gani?

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Ahaa! Hii *UDP*, sijui *UDP* sijui nini huko!  
(*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi nasema upinzani siyo kuvunja sheria wewe kama ni mpinzani fuata sheria. Wewe kama ni CCM fuata sheria usijidai wewe ni CCM utalindwa na sheria hapana, usijidai wewe ni *CUF* au *UDP* basi uko nje ya uwezo wa sheria. Napenda kumpongeza sana Kamanda wa Polisi wangu wa Mkoa wa Shinyanga N dugu yangu Abdallah Msika kwa ukakamavu aliouonyesha Bariadi. Tulihitaji polisi akatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine alizungumza Mheshimiwa Mbunge mmoja na mimi naomba sana Bunge hili kweli lipewe heshima. Wako watu wanaropoka ropoka hapa. Mtu mmoja akasema eti mama mmoja alipigwa Mkoma akatolewa mimba yuko wapi ana ushahidi? Kabla Bunge hili la Bajeti halijaisha tunaomba huyu mtu athibitisha alete ushahidi huyo mama aliyepigwa na polisi ikatoka mimba. Ni nani na ushahidi wake ni nini? Eti huyo mtoto aliyekufa labda angekuwa Rais. Wewe unacheza, ulikuwa wapi wewe? Mtu anazungumza kama ametoka porini. Wewe unajua hata kijiji alichozaliwa huyo mama? Mambo ya siasa za wapi hapa? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba athibitisha alete vielelezo mambo ya kupanda panda siasa zisizo na utaratibu hizi unafika mahali tunashindwa kuelewa. Ndiyo maana wanasema wanasema Bajeti ya Uchaguzi. Lakini unaogopa polisi wa nini? Polisi inalinda usalama wako na mali zako basi. Wewe kama unatenda haki, siyo mkosefu unataka kuogopa polisi kwa sababu gani? Sasa wewe unataka kuwa polisi mwenyewe? Anayeogopa polisi ni mhalifu. Pia nimeona ukurasa wa 19 kuna magari yananunuliwa kweli Bariadi tuko wengi sana. Tuko watu zaidi ya 600,000. Sasa kuna maeneo mengine yana watu 50,000 unagawa magari sawa, sisi inabidi tupewe magari zaidi na

Mheshimiwa Ndassa na yeye anasema watu wengi apewe gari kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa kweli utakapokuwa unajumuisha haya mambo utupe magari ya kutosha Bariadi na Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia magereza, napendekeza kwamba magereza yawe nje ya mji. Sasa kwa mfano gereza liko Butimba Mjini, liko Ukonga Mjini, Keko Mjini tena katikati ya Jiji, hawa watu wanatakiwa kujitegemea walime wajilishe, huyu mtu mimi nikikatwa, mimi nalima nalisha familia wake na watoto sasa siwezi kujilisha mimi nikiwa gerezani kweli? Kwa hiyo, mimi nafikiri haya magereza yangewekwa ndani ya vijiji halafu wapewe vitendea kazi vya kilimo, ufundi miradi mbalimbali. Kwa mfano, hili gereza kama la Bariadi liko Mjini tumepewa pale mradi wa *UNDP*....

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Kengele ya ngapi?

**WABUNGE FULANI:** Ya pili.

**DANHI B. MAKANGA:** Ahaa! Sasa huu msongamano, naunga mkono hoja hii. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Dakika 10 zinaweza kukutosha Mheshimiwa Musalika kama umejiandaa vizuri.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya mwisho kuchangia hoja hii. Pamoja na ufinyu wa muda nitajitahidi kupangua mtiririko wangu wa mawazo kama nilivyokuwa nimepanga. Lakini kwanza kabisa niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza tu kwa baadhi ya mambo ambayo ni ulinzi na usalama wa raia na kwa kuwa suala hili, limezungumzwa na wasemaji wengi nitajielekeza sana kwenye maeneo ya sehemu ninazotoka kwa sababu ya hali halisi ya ujambazi katika Kanda ya Ziwa na hususani Wilaya ya Geita. Kama zilivyo sehemu nyingi silaha zimetapakaa sana na hususan katika Wilaya ya Geita. Wilaya ya Geita, Bukombe, Kahama, Biharamulo, Ngara na Wilaya za Kigoma zina miundombinu ambayo inafanya majambazi yaeneo huko au yazagae.

Kwa mfano katika Wilaya ya Geita kijiografia ina maeneo ya migodi ya Rwamungasa, migodi ya Nyarugusu, migodi ya Geita Mjini pamoja na maeneo mengi. Maeneo haya yanavutia watu wengi wakiwemo majambazi. Lakini pia kuna *centers* za biashara ambazo zimefumuka kufuatana na idadi kubwa ya wananchi walioko huko maeneo kama Kasamwa, maeneo kama Karumwa, maeneo kama Katoro, maeneo kama Ushiroombo, Masumve, Isaka, Kagongwa, Kakora, maeneo haya yana watu wengi sana na ni maficho ya majambazi. Lakini kuna mialo vile vile ya wavuvi kama vile Nkome na visiwa kama Maisome, Izumacheli pamoja na sehemu zingine yote haya ni miundombinu

ya majambazi. Lakini pia kuna misitu minene sana katika sehemu hizo ambayo ni maficho ya majambazi. Lakini pia Wilaya hizi zinapakana na maeneo ya wakimbizi au nchi ambazo ziko kwenye vita na Wilaya zingine zinakuwa na wakimbizi. Kwa hiyo, yote haya yanafanya sasa majambazi yapate miundo mbinu ya kuishi huko pamoja na kufanya kazi bila matatizo. Sasa matatizo yaliyopo kwa mfano Wilaya ya Geita ni makubwa sana. Nashukuru Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameitambua Wilaya ya Geita kwa tatizo la mauaji na unyang'anyi wa kutumia silaha uliotokea mwezi wa Tano mwaka huu kwamba Wilaya ya Geita, ina eneo kubwa sana ni zaidi ya kilometa za mraba 3200. Lakini pia miundombinu yaani barabara zake ni mbovu sana. Ofisi ya *OCD* ni ofisi ambayo ilikuwa na gari mbili mbovu sana na ziko kwenye mawe. Lakini pia ni gari ambazo haziwezi kufanyiwa *service* ni gari kwa siku moja inakwenda kilometa zaidi ya 500, lakini wakati gari inakwenda huko haina mafuta ya kutosha, haijafanyiwa *service*.

Kwa hiyo, *OCD* wa Geita kati ya watu waodaiwa na watu wenye visima vya mafuta pale Wilayani ilikuwa ni pamoja *OCD*. *OCD* inafikia mahala anapopata mgeni pale kwenye *counter* anauliza kwanza vijana ni nani, wakimwambia mzee kuna mgeni, anauliza ndiyo yule wa mafuta? Akiambiwa hapana ni Mheshimiwa Mbunge, basi anawambia mwambie aje kwa sababu ya kuogopa madeni waliyo nayo ya mafuta. Lakini kazi lazima ifanyike. Nataka kusema kwamba katika Bajeti hii Waziri amesema atanunua magari 174 katika magari haya tunaomba sana Wilaya ya Geita, yenye watu zaidi ya 700,000, yenye miundombinu ambayo inaweka majambazi tupatiwe magari mapya mawili bila kukosa, *OCD* apatiwe fedha ya kununua mafuta ya kutosha na kulipa madeni anakodaiwa. *OCD* apewe hela ya *service* kwa ajili ya kufanyia *service* magari haya.

Katika nchi hii ziko zaidi ya 130 na kwa mgao wa magari haya ukisema kila Wilaya uipe magari mawili mawili haziwezi kuenea. Sasa tukubaliane kwa hali halisi kuna Wilaya zingine ambazo zilivyokaa hazina matatizo makubwa sana ujambazi. Nasikia kule Pangani na Bagamoyo kule huwezi ukaiba na kufanye ujambazi kwa sababu utatumiwa vipande kuna watalaam wa vipande au majini. Sisi Geita hatuna utalaamu huo tunategemea polisi na magari haya. Kwa hiyo, tunaomba katika mgao huu lazima tupate magari mawili. Vijana tunao wanajituma sana. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana *OC' CID* yuko mwanaume mmoja kutoka Sumbawanga anaitwa Aloyce Oswald vijana wake wanampenda na wana ushirikiano. Yule *OC' CID* anakwenda kwenye tukio la ujambazi huo kuna mambo yake anayofanya lakini lazima wale wakamatwe. Sijui huwa anafanya nini. Kwa hiyo, namwomba sana *IGP, OC'CID*, asihamishwe Geita badala yake aongezewe nguvu hizi ili aweze kufanya kazi hizi ambazo tunazisema hapa. Kwa haraka kuhusu maslahi ya polisi na mimi niseme kama vile walimu tulivyokuwa tunaomba walipwe madai yao ya nyuma, malimbikizo ya uhamisho, likizo na mishahara mwaka jana tuliwaongezea Bajeti, lakimi malalamiko yapo hasa kwa askari wadogo, naona wakubwa wanalipana kwanza kwao, wale wadogo wa chini naomba sana Waziri umwambie *IGP* awaangalie wadogo, muwalipe hao pia ndiyo wenye matatizo makubwa, hasa wanaokaa vijijini huko. Pia, tatizo kubwa la polisi limeshasemwa na Waheshimiwa Wabunge, wengi sana kwamba kwa kweli nyumba za polisi hawa wadogo hasa wa *FFU* na hawa polisi wa general order ni matatizo. Nyumba ambayo tunasema ni full suit ndogo, lakini mtu akaa pale na familia yake. Chumba maana yake ni partion kama askari

ana uwezo anaweka pazia zito kama hana uwezo ndiyo anaweza shuka ambalo ni transparent inahitaji nidhamu ya juu sana hasa wakati wa kulala usiku. Nimewahi kusikia kwamba kulikuwa na tukio moja usiku wa manane watoto waliangua kilio kwenye nyumba moja ya askari simsemi hapa. Basi wakalia watoto wale wazazi wanashangaa mbona watoto wanalia kumbe wamesikia mama yao analia wakadhani anapigwa na baba, wakaanza kulia kumsaidia mama yao, baba yao akawa mkali akawatuliza wakalala. Sasa ndiyo hali inavyotokea inahitaji nidhamu ya juu sana kuishi kwenye nyumba hizi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wako askari ambao wako tayari kufyatua matofali ya kuchoma wao wenyewe lakini Serikali iwawezeshe vifaa kama tunavyofanya kwenye mpango wa MEM shule za msingi wapewe *cement* wapewe mabati wako tayari kujenga nyumba za gharama nafuu wakaishi. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri alete mkakati kama ilivyoshauriwa na Wabunge wengine atuletee mkakati kwamba tatizo la nyumba analimaliza vipi? Mbona shule za msingi walimu sasa tunamaliza, polisi tunafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie kuhusu *traffic*. Kwenye kikosi cha polisi kuna kitu kinaitwa *PGO* zamani walikuwa wanahamisha kila polisi baada ya miaka mitatu wanahamishia kikosi kingine. Lakini sasa hivi haiko hivyo. Sasa kikosi cha *traffic* ni kikosi cha neema, kikosi cha *FFU* ni kikosi cha balaa. Wakati polisi *traffic* anahangaika apate wapi kiwanja cha pili kujenga nyumba ya pili, mke wa *FFU* hawezi hata kupata hela kununulia mkaa wa kupikiea maharage.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mradi wa ujenzi wa jengo la mahabusu katika Mji wa Chunya. Kiwanja kilipatikana tangu mapema miaka ya 1990 lakini ujenzi haujaanza hadi leo. Kutoka Chunya hadi Mbeya ambako Mahabusu wanahifadhiwa ni kilometa 75. Sio rahisi kupata gari la kuchukua mahabusu na kuwafikisha Mahakamani Chunya.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nyumba za Polisi Chunya ulianza wakati Yohana Mapunda akiwa *RPC Mbeya*, lakini haujaendelea. Tunataka Chunya iingizwe kwenye *program* ya kujenga nyumba. Polisi Chunya wanaishi kwenye magofu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya haina Kituo cha Polisi kinachojitegemea. Wapo ndani ya jengo la Boma la Mkuu wa Wilaya na wamebanana sana. Tunaomba Kituo rasmi cha Polisi kijengwe Chunya.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limejitahidi sana kukabiliana na ukubwa wa ujambazi na matendo mengine maovu ambayo yamejitokeza katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kufikiria kujenga upya Kituo cha forodha mpakani mwa Tanzania na Zambia (Tunduma) jambo ambalo linaleta heshima kubwa kwa nchi yetu. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Makao Makuu ya Polisi Wilayani ni ya zamani mno yalitolewa kama zawadi kwa Serikali na yalitumika wakati wa manamba. Kwa hiyo Serikali havijawahi kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya. Tunaomba Serikali ifikirie kujenga majengo mapya yanayofanana na shughuli yenyewe.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1997 Waziri Mkuu aliweka jiwe la msingi ili kuanzisha Kituo kidogo cha Polisi katika Makao Makuu ya Tarafa ya Msangano, lakini bado hakijafunguliwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumeshaandika barua mara mbili Wizarani kuomba gari mpya kwa ajili ya Kituo cha Tunduma ili kuwawezesha Askari kupambana na uhalifu uliokithiri mpakani (ujambazi na magendo). Bado Tunaendelea kuomba gari lenye uhakika wa kutenda kazi hiyo kwani Kituo hakina gari hivi sasa.

Pamoja na yote haya, tunaipongeza Serikali kuifikiria sana Wilaya ya Mbozi katika Bajeti hii ya mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri katika kuhitimisha hoja yake jioni hii. Naendelea kuunga mkono hoja hii.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza sana Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Polisi nchini kwa kazi nzuri inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, ubora wa Jeshi la Polisi utategemea mipango ya mafunzo ya kisasa, uwezo wa matumizi ya vifaa vya kisasa na upatikanaji wa vifaa vyenyewe kwa kiwango cha kutosha, ujasiri wa Polisi wenyewe katika utekelezaji wa kazi zao na wajibu wao na motisha ya kutosha kuwezesha moyo wa uendeleu wa Polisi kufanya kazi zao hadi muda wao wa kustaafu.

Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri kwa mwaka 2004/2005 inagusa maeneo yote niliyodokeza hapo juu na ni matarajio yetu wote kwamba yatatekelezwa. Tatizo linalolikabili Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa mipango yake ni kukosa uwiano katika mgawanyo wa miradi ya maendeleo kati ya maeneo ikiwemo ngazi za Mkoa na Wilaya. Kwa mfano katika Wilaya ya Muheza hali ya majengo Makao Makuu ya Polisi Wilaya ni mbaya na hakuna hata mpango wa ukarabati. Ofisi ya Ardhi Wilaya ya Muheza

(Halmashauri) imetenga eneo la ardhi kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Polisi lakini mpango wa kuendeleza eneo hilo haupo.

Kituo kidogo cha Polisi kilichopo Amani zaidi ya kilometa 47 kutoka Makao Makuu ya Wilaya hakina Askari wa kutosha, nyumba hazitoshi, Kituo hakina usafiri hata wa pikipiki na hata chumba cha kuhifadhi silaha kilichojengwa na Wahisani wa Kampuni ya Chai Amani (*EUTCO*) hakitumiki. Eneo la Hifadhi ya Msitu wa Amani una Taasisi mbalimbali zaidi ya mashamba na viwanda vikubwa vya chai, Ofisi za hifadhi, Kituo cha Utafiti wa Malaria, eneo kubwa la idadi kubwa ya uchimbaji na biashara ya mauzo ya dhahabu. Kwa vigezo vyote hivyo na kuongezeka uhalifu ndani ya hifadhi ya misitu ya Amani na hasa biashara ya madini (dhahabu) ipo haja ya kuimarisha Kituo cha Polisi Amani.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri afahamu kwamba kutokana na mahusiano mazuri kati ya Viongozi wa Wilaya, Ofisi ya Mbunge na Wawekezaji Kampuni ya Chai, *East Usambara Tea Company (EUTCO)* wamekuwa tayari kutoa msaada wa kukarabati nyumba za Polisi Kituo cha Amani na misaada itakayohitajika ili kuinua uwezo wa ulinzi katika eneo la Amani. Ni vema Wizara ikatumia nafasi hii muhimu kukabiliana na hali ngumu ya Jeshi la Polisi Wilayani. Hali mbaya ya usafiri katika Kituo cha Amani imechangia sana kuvunjika kwa maadili ya baadhi ya Polisi wa Kituo hicho hasa katika kipindi cha uchimbaji wa dhahabu ambapo wahalifu wengi wanaovamia maeneo ya uchimbaji au kupora wanapofikishwa kituoni hapo kesi zao hazifiki popote na mali zote za ushahidi hazifiki Wilayani na kesi hazifunguliwi. Ni kwa uadilifu gani basi Polisi akamate mhalifu akiwa na gramu kadhaa za dhahabu ampeleke mhalifu huyo na mali zake kwa usafiri usioaminika, malori au mabasi ya kiraia, zaidi ya kilometa 47? Matokeo yake ni kuwaingiza Polisi hao katika vishawishi vya kushiriki katika biashara haramu ya dhahabu na kukiuka sheria na maadili ya Askari Polisi. Hivi kweli Wizara au Uongozi wa Jeshi la Polisi haujui kinachoendelea katika Kituo cha Polisi Amani? Tunasubiri hadi umma uliumbue Jeshi la Polisi kutokana na Askari wachache waovu?

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia tena haja ya kuwepo kwa uwiano katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Jeshi la Polisi na kuangalia vigezo muhimu vya kiuchumi vilivyoko katika baadhi ya Wilaya ili kuwalinda raia na mali zao vizuri na kwa msingi huo Wilaya ya Muheza ipewe nafasi katika mpango wa maendeleo ili kukarabati au kujenga upya Ofisi (Kituo cha Polisi) katika baadhi ya Wilaya, kuongeza usafiri (gari) na kukarabati Kituo cha Polisi Amani.

Mwisho, Jeshi la Magereza lipitie upya hoja zilizokwisha tolewa hapa Bungeni miaka miwili iliyopita kuhusu hali mbaya sana ya nyumba za Maofisa wa Jeshi hilo katika Kituo cha Gereza dogo la Kilulu- Muheza. Maofisa hao katika karne hii ni hali ya aibu sana. Kwa nini Jeshi hili halina mpango wa kuondoa hali hii mbaya kwa watumishi wake?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii.



**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru Mungu kwa kunipa uwezo wa kuchangia hoja hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii, pamoja na mashirikiano yao katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza sana Wizara kwa juhudi zake za kutaka kujenga mazingira mazuri kwa Askari wake, kwa kuwajengea majumba ya kuishi karibu nchi nzima pamoja na kwamba bado hayajakidhi haja, lakini ni hatua nzuri iliyofikiwa. Tunaomba tu Wizara izidi kuziona zile sehemu ambazo bado hazijapata huduma hii ya majumba, basi Wizara itupie jicho huko ili na wao wafaidike na hilo. Hili la ujenzi wa nyumba litapunguza ile kero ya Askari kuishi uraiani.

Mheshimiwa Spika, uhalifu nchini ni suala la kupewa kipaumbele sana ili kuifanya nchi kuwa salama kwani bila kuwa na usalama na amani hapana maendeleo yatakayopatikana kwani wananchi hawatakuwa na utulivu katika shughuli za kuleta maendeleo. Hivyo basi, lazima Wizara ipange mikakati ya makusudi ya kupambana na hali za aina zote ukiwemo ujambazi, unyang'anyi, unyanyasaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa Askari Polisi umekuwa unalalamikiwa sana nchini hasa katika Mikoa ya Zanzibar na hasa Pemba kwamba ajira inaelekezwa kwa wale tu Wana-CCM jambo ambalo sina hakika lakini ni uvunjaji wa Katiba maana uajiri ni haki ya kila mwananchi ila tu atimize sifa zinazohitajika katika ajira ile na sio kwa itikadi ya mtu. Kwa hiyo, tunapenda Mheshimiwa Waziri alitolee maelezo suala hili na hatimaye atoe agizo kwa vyombo vinavyohusika na uajiri wa Polisi nchini visiendeleo na uovu huo. Sio vibaya vyombo husika kushirikiana na Masheha kwa kule Zanzibar, bali kibaya ni kufanya ubaguzi katika kutoa haki.

Mheshimiwa Spika, mlundikano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza ni suala la kuangaliwa sana ili kuepusha madhara ambayo yanaweza kutokea. Hivyo ni jambo la msingi sana Wizara kuongeza majengo kwa ajili ya kutoa nafasi zaidi kwa wafungwa popote pale (wakati) hali ya fedha itakaporuhusu.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la bajeti kwa Vyombo vya Ulinzi limepokelewa kwa mitazamo tofauti karibu nchini kote. Lakini kwa sisi wengine tunadhani ni kwa ajili ya siasa zaidi kuliko kijamii au vinginevyo. Katika ukurasa wa 20 ndani ya kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii, Waziri Amesema, ninanukuu: "Aidha, hatua maalum zitachukuliwa kuliwezesha Jeshi la Polisi kujiandaa kwa hali ya kutekeleza na kufanikisha vyema majukumu yake katika kuhakikisha usalama wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005", mwisho wa kunukuu.

Hii inadhihirisha kwamba Serikali inajiandaa na vurugu na ni nani hasa aneyetarajiwa kuanzisha vurugu hii? Ni mtu tu wa kawaida ambaye atakwenda pale Kituoni kupiga kura au ni yule ambaye kwa uwezo wake anataka kufanya mambo

kinyume na sheria na akihojiwa kwa nini anafanya vile iwe ni chanzo cha vurugu katika uchaguzi? Hapa Waziri ni vyema atueleze maana na lengo la ibara hii.

Mheshimiwa Spika, katika miezi ya hivi karibuni kule Zanzibar palitokea milipuko ya mabomu na taarifa hiyo ikaenea duniani kote. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Muungano ilifanya uchunguzi wa kina wa jambo hili, sasa tunajiuliza mbona mpaka leo hii hayajatolewa maelezo juu ya jambo hili? Ni akina nani hao waliohusika na matendo hayo? Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo kuhusiana na hili. Atuambie ni hatua gani imechukuliwa dhidi ya watuhumiwa wa milipuko hiyo.

**MHE. MCHANDE S. MCHANDE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kupata kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Aidha, nachukua nafasi hii kuwapa pole wote waliopata misiba na wale waliopatwa na matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi sina mengi sana isipokuwa napenda nichukue fursa hii kumweleza Mheshimiwa Waziri kuhusu jengo la Kituo cha Polisi katika Jimbo langu la Konde.

Mheshimiwa Spika, jengo la Kituo cha Polisi Konde kilijengwa mnamo miaka ya hamsini. Kwa maana hiyo Kituo hicho sasa kinahitaji ukarabati wa hali ya juu. Namwomba Mheshimiwa Waziri aje katika Jimbo langu ili twende tukakague jengo la Kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi vigae vilivyoezekewa jengo hilo vimeanza kudondoka na ni hatari kwa Askari wanaoishi katika majengo hayo. Aidha, madirisha ya majengo hayo yamekuwa mabovu. Kubwa zaidi ni kuwa makaro ya vyoo yameziba na maji machafu yamezagaa nyuma ya majengo hayo ambayo huweza kusababisha maradhi ya mlipuko. Aidha, Askari wa Kituo hicho hawana vitendea kazi kama vile gari au pikipiki. Gari walilionalo ni bovu na haliwezi kukidhi haja hasa yanapotokea matokeo ya uhalifu wanashindwa kufuatilia vizuri. Kwa hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri ikiwezekana Kituo hicho kipatiwe gari lingine.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalopenda kusema ni kwamba nikiwa katika Jimbo la Konde palikuwa na Ofisi ya Uhamiaji lakini Ofisi hiyo iliamishwa mara moja sijui kwa nini. Naomba turejeshewe Ofisi hiyo.

Mwisho nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na yenye mwelekeo wa ufanisi wa kazi.

Mwisho kabisa naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake na namna alivyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, mimi katika Wizara hii nitazungumzia zaidi siasa kwenye Jeshi letu la Polisi. Wabunge wenzetu wa CCM kutoka Zanzibar wanapochangia huwa wana mdomo mrefu na kujigamba sana kwa kutegemea Jeshi letu la Polisi kwa kuwapatia ushindi kwani wanajua kuwa kwa kura za wananchi hawana ubavu huo, lakini wanaposimama husimama na hudiriki hata kutaja majina ya viongozi walioko mbali na Bunge na kusema eti hawaogopi. Sisi tunasema hakuna anayemwogopa mwenzake.

Mheshimiwa Spika, Waziri mwenyewe ni shahidi ya yote yaliyotokea kule Zanzibar kwa chaguzi zote mbili anazielewa zilivyokwenda kwa ule uchaguzi wa mwaka 1995 na huu wa 2000. Ushindi wao wa mwaka 1995 ni wakupika matokeo baada ya kuona wameshashindwa kura laki tatu, walikaa siku tano matokeo hayajatolewa, walichokifanya sote tunajua. Uchaguzi wa mwaka 2000 nao hivyo hivyo, baada ya kuona tayari wameshashindwa walianza hila zao na baadaye wakafanikiwa kuitisha Tume ya Uchaguzi Zanzibar nayo ikakubali kubatilisha uchaguzi wa Mkoa Mjini Magharibi na baadaye kuvuruga uchaguzi wote wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mimi namwuliza Waziri wa Mambo ya Ndani, uchaguzi umeharibika Mkoa wa Mjini Magharibi, zile kura za Majimbo ya Pemba na Mikoa mingine zilichukuliwa kwa mtutu wa bunduki na kupelekwa Wilayani kwa sababu gani kuwa sio wizi wa kura na baadaye zikalindwa na Polisi bila ya mawakala wa Vyama? Baada ya yote hayo ndiyo wakapatikana Wabunge wa uongo ndio hao wanaokaa wakapiga kelele za kujisifu.

Mheshimiwa Spika, sasa basi ninamshauri Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na Naibu wake ambaye ni rafiki yangu (Chiligati) mara hii waiombe Serikali yao itayarishe uchaguzi ulio huru na wa haki na wasithubutu kulitumia Jeshi la Polisi kwa kulipatia faida ya ushindi. Vinginevyo sisi *CUF* hatuko tayari tena kwa vyovyote vile kuibiwa kura kwa ghiliba, hadaa na udanganyifu. Hii tunasema kweli wala si uongo, Mheshimiwa Mapuri yeye ni Muislam na anakijua kiapo cha Kiislamu mimi namuapia Wallahi, Billahi na Tallah sasa sisi tushaamua roho zetu tayari lakini hatuwezi kuibiwa na watu kama sisi mara tatu, kwani tunaamini hakuna muafaka wa mara tatu. Uchaguzi ukiwa wa huru na wa haki sisi hatuna tatizo, mkishinda tutawapa mkono na tutatoa ushirikiano. Mheshimiwa Mapuri anazielewa zaidi kuliko Mheshimiwa Chiligati kwa sababu yeye siasa za Zanzibar hazijui naomba aniwie radhi. Vinginevyo wakilitumia Jeshi la Polisi kwa maslahi ya Chama yatakayokuja kutokea nyinyi ndio mtakaokuja kuulizwa kesho mbele ya haki.

Mwisho kabisa, napenda nizungumzie kuhusu Jeshi la Polisi Zanzibar mbona lina ubaguzi wa kutoa vyeo? Askari kutoka Pemba hawapandishwi vyeo kwa visingizio tu eti ni *CUF* mbona wanaojifanya CCM mnawapandisha vyeo mara kwa mara? Mheshimiwa Mapuri yeye anazielewa habari hii, mzizi huu wa fitina walianzisha wao na Serikali yake na Mheshimiwa Salmin Amour.

Mheshimiwa Spika, ikiwa hatukubali kushindwa na hatuwezi kutenda haki, basi tufuteni Vyama vingi tubakie na Chama kimoja lakini tusibaguane kwa kitu chetu sote. Nchi hii sote tuna haki ya kutawala, isiwe wengine hawana haki.

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Wasaidizi wao wote katika Wizara na Vyombo vilivyo chini ya Wizara hii kwa namna wanavyojitahidi kuendesha shughuli za Wizara hii ambazo ni nzito na nyeti. Tukitilia maanani ukweli kuwa uwezo wa kifedha sio wa kutosha kwa kweli Wizara hii ingefaa siku zote isifiwe badala ya kulaumiwa.

Hata hivyo naomba nami niungane na Wabunge wengine nieleze au nisisitize machache. Kwanza suala la Uhamiaji Zanzibar, watumishi wa uhamiaji Zanzibar wanaonekana kuathirika kutokana na ukweli kuwa wanalazimika kuwa watiifu kwa Serikali mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Watumishi hao wa uhamiaji hawana kosa kwa kuwa watiifu kwa Serikali zote mbili, maana Serikali hizo mbili zinatambuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Sasa ninachoomba ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuwasiliana na wenzake wa SMZ ili hali hiyo inayokabili Watumishi wa Uhamiaji Zanzibar kujikuta wanateseka kwa maamuzi ambayo hawana mamlaka nayo.

Huu mpango wa ujenzi wa nyumba za Polisi kwa Mikoa mingine haihusiki nao? Nauliza hivyo kwa sababu miaka nenda, miaka rudi mpango huu sijaona kuhusika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Katika Mkoa huo pale Mahonda, Wizara iliwahi kutenga ardhi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Polisi. Ni miaka mingi imepita hakuna nyumba iliyojengwa. Je, hivi kipimo cha Askari kujengewa majumba ni uhalifu kukithiri au watu kuuawa kama ilivyotokea Pemba? Nashauri kwa pesa hizo hizo kidogo na Mikoa mingine iangaliwe hata kama kwa nyumba moja kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuajiri Polisi nao naona unahitaji kuangaliwa kwa undani zaidi. Ingawa utaratibu wa hivi sasa unahakikisha kupata Askari kutoka pembe zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado kipo kilio cha upendeleo. Kuna maeneo kuwa kadri majina ya wanaoomba kazi yanavyopita katika mlolongo wa kuajiriwa kuanzia Wilayani bado yapo malalamiko ya upendeleo na hata rushwa. Hapa mimi naomba Waziri afafanue jambo hili kwa sababu kuna malalamiko mengi na wanaolalamikiwa ni wanasiasa.

La mwisho, naomba nisisitize juu ya usafiri katika chombo cha Polisi. Namna Polisi wanavyoomba *lift* mabarabarani ni jambo la kudhalilisha. Ufanisi wa Polisi unaathiriwa sana kutokana na tatizo hili la usafiri. Hivi sasa raia akitoa ripoti juu ya tukio lolote linalohitaji huduma ya Polisi ikiwa raia hana usafiri, huduma ya Polisi ama inachelewa sana kupatikana au haipatikani kabisa.

Kwa mfano kule Zanzibar madaraja mengi ni membamba. Inapotokea ajali ya magari na magari hayo yakaziba daraja huhitajika Polisi wa Usalama Barabarani kuja kufanya kazi yao (*COW*) ili daraja liweze kupitika. Hivi sasa hali kama hiyo ikitokea huwa bughudha kubwa kwa sababu ya kuchelewa kufika kwa Polisi wahusika na ucheleweshaji huo mara zote husabishwa na tatizo la usafiri. Angalau hawa Polisi wa Usalama Barabarani wahakikishiwe usafiri wa uhakika kwa kuwapatia vyombo bora vitakavyowafikisha wanapohitajika kwa haraka.

Namalizia kwa kuwapongeza tena kwa kazi nzuri na ngumu. Hizi rai za wanasiasa uchwara za kutaka muwaachie wafuasi wa vyama wapambane hazina nafasi. *Law and order must be maintained at all costs.*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri Mapuri, Naibu Waziri John Chiligati, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye kueleweka na takwimu nyingi ambazo husaidia uelewa wa hoja husika.

Mheshimiwa Spika, nachangia machache yafuatayo:-

Mwelekeo wa uhalifu ingawa hotuba imetoa matumaini mazuri, kwa upande wangu hali sio hivyo *provided that* vyanzo vya uhalifu havitadhibitiwa kwa mfano ujio wa wakimbizi nchini kwetu ambao wengine huja na silaha ovyo ovyo tu, vijana wetu wengi kutokuwa na shughuli za maana za uzalishaji mali hivyo kuweza kujikimu katika maisha, kuiga mitindo ya uhalifu wanayoiona kwenye *television* na kadhalika. Uhalifu nchini utaongezeka kama inavyoanza kujitokeza mwaka huu 2004. Hivyo nakubaliana na hatua zilizochukuliwa lakini nashauri masuala ya Jeshi la Mgambo uimarishwe zaidi katika Vijiji na Miji yetu ili jamii yote kwa ujumla iweze kujilinda na wahalifu hao kwa kuweza kujihami.

Pamoja na ushauri huu nilioutoa naomba utafutwe mkakati wa jinsi ya kuhakikisha kuwa Askari Polisi, Wanajeshi wanaoachishwa kazi kwa makosa mbalimbali wanadhibitiwa ili wasiwe chanzo cha uhalifu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri katika mazingira magumu ambayo taratibu Serikali ikiendelea kuongeza Bajeti naamini kuwa Polisi watafanya kazi nzuri zaidi. Hata hivyo kuna Askari kadhaa wa Usalama Barabarani ambao wanachafua sifa ya kazi nzuri ya Jeshi hili kwa ajili ya kudai rushwa kwa wenye Sekta ya Usafirishaji wa abiria, mizigo barabarani, wanadai rushwa kwa wasafirishaji wanaovunja sheria na kwa wale ambao hawavunji sheria mradi wapate fedha za ziada za kujengea majumba na kadhalika. Hili linatokea kwa sababu Askari hawa hawakosi kupata kosa kila wakisimamisha gari.

Lakini linalosikitisha ni pale wanapodai rushwa kwa wasafirishaji ambao wanatii sheria za nchi, halafu wao huwabambikiza makosa ili tu wapewe chochote na kuwapendelea wale wanaovunja sheria na kutoa rushwa kubwa *in advance*. Vitendo hivyo vipo na la msingi ni kutafuta mbinu za kudhibiti hawa Askari wachahe wanaoliaibisha Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kudhamiria kuboresha mazingira ya makazi ya Polisi na ukarabati wa mashua ya doria za Maziwa yetu Makuu ya Tanganyika, Nyasa na Victoria ambako ujambazi wa majini upo. Licha ya mashua, nasisitiza kuwa vitendea kazi vingine pia viongezwe. Baada ya kuandika haya, naunga mkono hoja.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake. Nasema hongera sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana *IGP* wetu ndugu Omari Mahita kwa kazi zake nzito na kusimamia Jeshi lote la Polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ikamilishe Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Meatu kwani mpaka sasa jengo liko usawa wa *Rental* bado tu kupauliwa. Aidha, *lines* ya Polisi nayo naishauri Serikali ikamilishe ili Askari waweze kupata mahali pa kuishi na kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, *IGP* Mpendwa Omari Mahita alifika Wilayani Meatu na kuahidi gari dogo katika Kituo cha Mjini Mwanhuzi miaka mitatu iliyopita. Naomba ahadi hiyo itekelezwe mwaka huu.

Aidha, ombi la *DC* Meatu limeishia wapi ambalo liliomba kubadilisha Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya ya Meatu Ndugu Issa Buregu *OC - CID*. Ni kero sana kwa wananchi wa Wilaya ya Meatu na Uongozi mzima wa Jeshi la Polisi Wilayani. Naiomba Serikali ilijali ombi la Mkuu wa Wilaya.

Pia, naiomba Serikali kuipa Wilaya magari mawili ambayo yatafanya kazi badala ya mabenzi mawili yaliyokuwepo miaka ya nyuma ambayo hivi sasa ni mabovu.

Askari walioko kwenye *OPP* kama vile Mwangudo, Makao, Paji, Longalonga na Bukundi wapewe posho kwa kuwa huwa wako nje ya Vituo vyao vya kazi.

Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Awali ya yote nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri inayofanywa japo katika mazingira yasiyoridhisha. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara yaani *IGP*, Mkurugenzi wa Uhamiaji, Kamishna wa Magereza na Mkuu wa Zimamoto kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mwenyezi Mungu awajalie dhamira hai na safi katika kutimiza majukumu yao kwa kuwatumikia watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nauelekeza mchango wangu katika mambo makuu matatu. Kwanza suala la ujambazi. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi, kwa mtazamo wangu bado Jeshi la Polisi linatumia mbinu na mikakati ya kizamani mno. Mifano iliyo wazi, hai na halisi ni uwajibikaji wa Jeshi la Polisi baada ya maafa kutokea. Naeleza kwa kifupi mifano yenyewe watu wanapovamiwa na kuuawa kama vile mabenzi yanapoibiwa *CRDB, NBC Moshi*. Hivyo nashauri kuwa Idara ya Upelelezi iimarishwe na ikiwezekana mafunzo yapatikane katika nchi zilizopiga hatua kubwa kwenye fani ya

Upelelezi. Vile vile, nashauri Jeshi la Polisi liimarisha mahusiano mema kati ya raia wema ili mawasiliano yafanyike kwa urahisi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, suala la wakimbizi limekuwa sugu katika maeneo yanayohifadhi wakimbizi, Biharamuko ikiwa ni mojawapo. Miaka yangu yote ya Ubunge ndiyo imekuwa agenda yangu. Nimekuwa nikieleza adha, usumbufu, mateso na mauaji ya wananchi wasiokuwa na hatia katika Kata ya Nyakahura bila mafanikio. Baada ya jitihada zote hizi kufanyika bila ya mabadiliko ilinilazimu kumwandikia barua Mheshimiwa Waziri yenye kujieleza yenyewe. Mheshimiwa Waziri anaifahamu!! Nayo mpaka sasa sijapata majibu. Jitihada zote hizo zimegonga ukuta. Kwa sasa nimebaki na mshangao. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Biharamulo kwa kushirikiana na wananchi wenye mapenzi mema (*well wishers*) wamejenga jengo la *Police Welfare Building* na kufikia kwenye *stage* ya kuezeka. Kutokana na kufikia hatua hii naomba nguvu za Wizara au mchango wa Wizara utolewe ili kuonyesha ushirikiano wa kuthamini nguvu zilizokwishachangwa. Chonde chonde naomba msaada huo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa ni vyema Serikali ingekuwa na mtazamo maalum kwa Jeshi la Polisi Zanzibar hasa kwa vile Zanzibar pia ni Makao Makuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kifungu cha *Plant Equipment and Machinery* kimetengewa kiasi cha Sh.10,050,000/= kwa mgawanyo wa miezi 12 sawa na Sh.837,00/= kwa mwezi. Fedha hizi ni kidogo sana kwa mwezi kwa kazi za matengenezo ya magari na vifaa vyote vya Jeshi la Polisi kwa Zanzibar nzima. Hivyo ni vyema Serikali ikazingatia kwa kutenga fedha zinazolingana na hali halisi.

Katika kifungu cha *fuel and Oil* zimetengwa Sh.211,000,000/= ambazo ni sawa na Sh. 58,611/= kwa siku au wastani wa lita 586,111. Kiwango hicho ni kidogo sana kwa kuweza kutosheleza Zanzibar nzima, hivyo ni vyema hili likazingatiwa kama tatizo hasa kwa mazingira ya kisiasa ya Zanzibar. Katika Jeshi la Polisi wapo wananchi walioajiriwa ambao sio Askari lakini wanatumika ndani ya Jeshi la Polisi. Watumishi hawa maslahi yao yanayumba lakini kwa mazingira ya kikazi ndani ya Jeshi inakuwa ni vigumu kufuatilia kwa viongozi wao kuulizia chochote kuhusu hali zao hivyo ni vyema matatizo yao yakapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Magereza mapya pamoja na kuwa hivi sasa lipo tatizo kubwa la msongamano wa wafungwa na mahabusu. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya matengenezo madogo madogo tu. Hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie ufafanuzi kuhusu mikakati ya Serikali katika kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHALIFA MOHAMMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Watendaji wao wote kwa jitihada kubwa ya kuiongoza Wizara hii ngumu.

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi kuchukua fursa hii angalau kwa uchache nichangie mawazo katika hoja hiyo. Napenda mchango wangu moja kwa moja nianze kuzungumzia kwa upande wa Jeshi la Polisi. Sote tunaelewa kwamba pamoja na ulinzi na usalama wa raia na mali zao, pia Polisi wana wajibu wa kupeleleza na kuwakamata watuhumiwa wa makosa ya jinai na kuwapeleka Mahakamani. Hoja yangu ni kwamba uzoefu unaonyesha kuwa watuhumiwa wengi wa makosa ya kawaida tu hushikwa na kupelekwa Kituoni, mara nyingine huwekwa Rumande kwa siku mbili hadi tatu na baadaye kupelekwa Mahakamani na huko mwendesha Mashataka humwomba Hakimu amrudishe mshitakiwa ndani kwa kisingizio kwamba ushahidi haujakamilika na akiwa nje ataharibu ushahidi. Sasa swali langu ni kwamba ni ushahidi wa asilimia ngapi ambao Askari anapaswa kuwa nao hadi kumwezesha kumshika mtuhumiwa kumweka ndani na kumpeleka Mahakamani?

Mheshimiwa Spika, nauliza hivyo kwa sababu kesi nyingi ambazo hufunguliwa na watuhumiwa kuteseka katika mfumo huo hatimaye kufutwa na Mahakama kwa kukosa ushahidi. Hali hiyo husababisha kuingia gharama katika Jeshi la Polisi na kuzidisha msongamano ndani ya jela zetu. Lakini pia watu kukosa imani na chombo chao hicho.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika hilo ni kwamba watuhumiwa wa makosa haya madogo madogo ya kawaida wafanyiwe uchunguzi wa kina kabla ya kushikwa hadi upatikane ushahidi wa kutosha wa kuweza kumtia hatiani mtuhumiwa ndio afunguliwe mashtaka. Ushahidi wa hayo ni watuhumiwa wengi hasa hawa wa makosa yanayoambatana na mambo ya siasa kusota Rumande kwa siku, wakitolewa na kupewa dhamana hubakia nenda rudi kwa siku nyingi Mahakamani. Mwisho ushahidi unakosekana na kesi hufutwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda nilitahadharishe ni uzoefu uliokubuhu wa kudumazwa kwa Askari wa Jeshi letu la Polisi, kutokufanya wajibu wao kwa kututumia taaluma, ujuzi na maadili ya kazi yao hasa ya upelelezi badala yake hufanya kazi kwa pressure za wanasisia na matakwa yao. Kila panapotokea uhalifu na hujuma mbalimbali, tayari Polisi wanahukumu kwamba hujuma hiyo imefanywa na aina ya watu (Wapinzani) hayo ni maarufu sana hasa Zanzibar. Mfano ni yale mabomu yaliyopigwa kule, moja kwa moja wamelengwa Wapinzani.

Jambo hili kwa maoni yangu ni hatari sana. Yaweza kutufikisha mahali pabaya mno badala ya Wapelelezi wetu kufanya kazi ya kutafuta ukweli na kuwashika wahalifu wa kweli, inabaki kuwahukumu watu kabla ya upelelezi kufanywa. Katika hali hii tunaomba sana, Wapelelezi wetu wapewe taaluma ya kutosha ili kuweza kufanya kazi zao kwa undani na hatima yake kushikwa wale wahalifu wa kweli.



Mheshimiwa Spika, kuhusu Magereza kama ilivyo katika ibara ya 37 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwamba jukumu la Jeshi la Magereza ni kuhifadhi wahalifu wa aina zote pamoja na kurekebisha tabia za wale waliohukumiwa vifungo.

Mheshimiwa Spika, ikiwa lengo la Magereza ni hilo, kwa kweli ni zuri mno, lakini kwa hali halisi Magereza yetu ni pahali pa mateso, manyanyaso, udhalilifu na mahali pa kukata tamaa. Hivyo watu watajifunza nini katika hayo zaidi ya usugu, chakula hakiridhishi, mahali pa kulala sio pa kibinadamu, watu wanasongamana chumba kidogo watu wengi, kuna utaratibu wafungwa kujisaidia ndani ya hicho chumba cha kulala wakati wa usiku.

Mheshimiwa Spika, katika hili naomba nishauri kwamba inatosha mtu akifungwa aukose ule uhuru wake wa kuchanganyika na jamii yake lakini haki nyingine zote za kibinadamu afanyiwe. Kwa hiyo, naomba Wizara ifikiriwe katika huo uwezo mdogo iliyonayo ijenge Magereza hatua kwa hatua yenye mahitaji yote, madirisha mengi na makubwa vyoo vya kutosha vyenye maji ya kutosha, yenye sehemu nyingi na kwa kiasi kikubwa wapunguzwe mahabusu ili Magereza yasiwe na msongamano.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kupata nafasi nichangie hoja hii.

Nawapongeza sana Waheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu wake Mheshimiwa Capt. Chiligati kwa kazi nzuri ya kuandaa hotuba hii. Vile vile naipongeza Menejimenti yake (Watendaji) chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu Bwana Bakari Mahiza.

Baada ya hapo naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kumpa pole Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapu kwa kazi nzuri na vile vile kama Rais pamoja na maumivu aliyonayo anaendelea kuiongoza vyema Serikali. Mwenyezi Mungu ampe ahueni na afya njema *inshallah*.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa inayofanywa ili kuhakikisha amani inaendelea katika nchi yetu. Pamoja na yote, bado tatizo la uvunjaji wa amani, tatizo la ujambazi na unyang'anyi bado ni kubwa na kuwafanya wananchi wakose amani. Lakini tatizo hili pia linachangiwa na uhaba wa vitendea kazi. Mheshimiwa Waziri ametueleza nia ya Serikali ya kuongeza usafiri. Tunaomba katika hilo asaidie sehemu zenye uhalifu mkubwa wapatiwe usafiri.

Mheshimiwa Spika, siku hizi ajali mbaya zimekuwa ni *fashion* na inaonekana kama kitu cha kawaida. Watu wanapoteza maisha na kutengeneza vilema kedekede. Sababu ya ajali nyingi ni kutokana na uendeshaji mbaya wa madereva kana kwamba hawana leseni. Hivi ni mikakati gani imewekwa ili kupunguza hali hii? Ni sahihi kila

siku watu wapoteze maisha na wakati huo huo madereva wanatoroka? Nani awajibike? Kwa nini kama ikidhihirika kosa ni la dereva na akatoroka, basi mwenye mali asiwajibishwe ili iwe fundisho la wao pia Waajiri, waajiri madereva waadilifu?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea kutueleza malengo yao ya mwaka 2004/2005 ikiwemo kumaliza viporo vya ukarabati wa majengo, Gereza la Handeni likiwemo. Nakumbuka mwaka jana fedha ilitengwa ili kumalizia ukarabati, lakini kazi hii bado. Sasa ni vyema kipindi hiki Gereza hili liishe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utendaji kazi mzuri katika hali ngumu, bado wanaishi katika mazingira magumu sana. Hawapandi vyeo, nyumba zao zinawadhililisha na kuwanyanyasa, mishahara ni tabu na usafiri hakuna. Iweje matokeo? Halafu tunawalaumu! Hebu Mheshimiwa Waziri atueleze ni mikakati gani ya muda mrefu imewekwa katika kuboresha hali hii? Tupate maelezo.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawapewi haki zao inapotokea wanakwenda kutoa ripoti Polisi, huwa wanapaswa kupewa msaada. Nakiri wanapatiwa huduma nzuri, lakini kwa kipindi kirefu nimekuwa nikiuliza, haki ya aliyejeruhiwa unapokwenda Polisi kupata *form* ya matibabu. Miaka miwili sasa imepata bado sijapata jibu kuhusu marekebisho ya *form* hii (PF.3) ambayo Bunge lako Tukufu iliahidi. Mbona kimya? Ningeomba kupatiwa maelezo hadi sasa hatua ikoje? Au tuendeleo kuwaacha wananchi kukosa hela zao hasa wanawake wanaobakwa na wengine kuambukizwa Ukimwi wakati wanapotakiwa kupokea vielelezo ili watendewa haki. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nakushukuru tena na nawapongeza Watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Mawaziri wake. Nawatakia kila la kheri na mwakani basi malengo haya yawe yametekelezwa. Kila la kheri, ahsante.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jengo la Uhamiaji Kigoma, mvua itakayonyesha mwezi wa Tisa italibomoa kwani ni bovu sana. Sijui kama kuna chochote kwa jengo hilo.

Pia kuna suala la doria kwa Mkoa wa Kigoma kwa wavuvi, bado wanachukuliwa mali zao wakati wa uvuvi ziwani. Wizi ni mkubwa sana na boti hakuna.

Mheshimiwa Spika, naomba kijana wangu ambaye amewekwa ndani katika Gereza la Tanga kwa tuhuma kwamba ni mkimbizi aachiwe huru kwani baba yake na mama yake ni wapigakura Kijijini kwangu. Yuko Gereza la Maweni kutoka Kigoma Wilaya ya Kigoma Kijiji cha Matiazo.

Mheshimiwa Spika, daftari la Wapiga kura ni ukombozi kwa Mkoa wa Kigoma ili kuondoa Urundi na Utanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Mkoa wa Kigoma upewe upendeleo wa Askari kwani uhalifu bado ni mkubwa sana. Viwango vya ulipaji kwa faini za magari Sh.20,000/= kwa kila kosa bado inatoa mwanya wa rushwa. *Operation* maalum ifanywe kutoa motisha kwa wale wanaotoa taarifa ya majambazi na pesa ijulikane kwa Polisi watakaofanya au kupambana na majambazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba; Je, Polisi anapouawa familia yake inalipwa nini? Je, mpaka sasa wamelipwa au tunawasahau? Ninaunga tena mkono hoja hii.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri na hotuba nzuri sana. Hongera kwake yeye binafsi, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Viongozi wote wa Wizara yake pamoja na wataalam wa aina zote.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwapongeza sana wafanyakazi wa Idara ya Polisi katika Jimbo langu. Maafisa hawa wanafanya kazi nzuri lakini kwa ugumu usio kifani na hatari kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Jimbo hili la Morogoro Kusini lipo mbali sana na Mji wa Morogoro ambapo ndiko kuliko Makao Makuu ya Wilaya ya Morogoro Vijijini. Kutoka Morogoro hadi Matombo ni umbali wa Kilometa 85. Hapa ndipo kilipo Kituo pekee cha Polisi. Kutoka Matombo hadi Kisaki Station ni Kilometa 80. Hapa pana Kituo cha Polisi cha *TAZARA*. Jimbo la Morogoro Kusini lina eneo la Mraba la *13,000 square kilometers*. Nusu ya Jimbo hili ni milima mikubwa ya Uluguru. Hakuna barabara kwa zaidi ya miaka 40 sasa. Jimbo hili lina wanyama wakali, wachimbaji wadogo wadogo wa madini ni wakorofi sana, wafugaji wa Kimasai, Wamang'ati na Wasukuma ambao wamehamia katika Jimbo hili wanagombana na kuuana baina yao wenyewe na wanawakera sana wenyeji, mapigano, mauaji na wizi wa mipango ni vitu vya kawaida. Pale ambapo panatokea vifo, basi si ajabu Daktari wa Uchunguzi wa sababu ya kifo afike baada ya siku nne hadi saba.

Katika eneo lote hili la Jimbo, Polisi wa Matombo wanalalamika kutembea kwa miguu huku wamebeba silaha moja au mbili. Kwa hali hii ya sasa hii ni hatari sana, hasa ukijua kuwa majambazi na wanyama wakali wapo wengi.

Mheshimiwa Waziri ninaomba Jimbo la Morogoro Kusini Polisi wapewe angalau gari moja la kuwasaidia katika kutenda kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwa hili.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makamanda wote wa Mkoa hasa wa Mkoa wa Dodoma pamoja na Askari wote wa nchi hii kwa kazi kubwa na nzuri ya ulinzi wa watu na mali zao. Kwa hili nawapongeza sana na ninawatia moyo waendeleo na kazi hiyo siku zote.

Mheshimiwa Spika, suala la ujambazi limepungua na hilo linaonekana wazi jinsi Polisi inavyofanya kazi. Narudia tena kumpongeza *RPC* wa Dodoma kwani sasa hivi tunalala usingizi. Vile vile, nampongeza *IGP* kwa kazi nzuri ya kusimamia hali ya usalama nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri katika mambo mbali mbali katika Wizara hii. Nashauri Serikali ijitahidi kujenga nyumba za Askari za kuishi ili kulinda heshima zao na kurekebisha hali ya malezi ya watoto wa Askari kwani hawatalelewa katika nidhamu inayostahili.

Pili, naishauri Serikali kwamba inapotokea Askari wamehamishwa ni vyema wakalipwa haki zao kabisa badala ya kutokuwapa. Hiyo ni uonevu watakuwa hawatendewi haki.

Tatu, inapotokea baadhi ya Askari wanakiuka maadili ya kazi zao ni vizuri wakachukuliwa hatua zinazostahili ili kulijengea heshima Jeshi la Polisi na nchi kwa ujumla. Vile vile, baadhi ya vitendo vya uhalifu vinavyotokea hasa wanapowakamata wahalifu ni vizuri kesi hizo zikapelekwa Mahakamni badala ya kuishia Polisi ili kuziba mwanya wa rushwa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Makamanda kwa kazi yao wanayoifanya na kukutana na Askari mara kwa mara. Naomba vikao hivyo vitumike kikamilifu na Askari kupewa nafasi ya kutoa mawazo yao ili kuboresha utendaji kazi. Vile vile kuwe na visanduku vya kutoa maoni ya wananchi na Askari na viwekwe kwenye kila Kituo cha Polisi na kwenye maelezo ya Ofisi ya Serikali na hatimaye maoni hayo yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe utaratibu wa mabasi yanayosafiri kutoka Vijijini na kwenda Makao Makuu ya Wilaya na Mkoa. Ni kwa nini mabasi haya yanaondoka usiku wa manane kwa maana ya saa 7.00 za usiku na kusababisha baadhi ya wasafiri kupanda na kushuka katika Vituo mbalimbali kabla ya kufika mwisho wa safari na wakati mwingine wasafiri hawa kukutana na wanyama wakali? Hivi huu ndio utaratibu wa mabasi ya Vijijini kutembea usiku? Naomba kupata jibu ili nisije nikaomba ufafanuzi wakati wa kupitisha Bajeti.

Naomba Serikali ijitahidi kufuta ujambazi ili kuondoa vizuizi vilivyopo katika maeneo mbalimbali kwani hata Askari wanaokaa katika maeneo hayo ni binadamu na ni hatari hata wao kuvamiwa na haina maana kabisa kwani wahalifu wanaweza wakapita mchana wakakaa porini na wakaendelea kuteka magari na bahati mbaya Askari walioko

kwenye Vituo hivyo ni wawili au watatu. Sasa hawa watasaidia nini wakati ujambazi unafanywa na kundi la watu na wenye silaha?

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza rushwa katika Jeshi la Polisi naomba Serikali iwaongeze mishahara Polisi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa shukurani nyingi kwa Bunge lako Tukufu kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kidogo. Nianze kuchangia kwa kulipongeza Jeshi la Polisi kwa juhudi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na timu yake yote.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kuhusu suala la ajali barabarani. Pamoja na jitihada kubwa za Jeshi letu la Polisi, nitazungumzia kuhusu ajali za mabasi.

Mheshimiwa Spika, ukipanda ndege lazima utaona kuna mlango wa dharura. Cha kushangaza kwenye mabasi yetu ya Tanzania hayana mlango wa dharura. Hivyo inapotokea ajali mlango ambao hutumika ni mmoja tu. Kwa hiyo watu wengi wanakufa kwa sababu ya kukanyagana wakati wa kutoka. Ushauri wangu ni kwamba ili kupunguza vifo lazima mabasi yote yawe na mlango wa dharura.

Mheshimiwa Spika, nichangie kidogo kuhusu kuzagaa kwa silaha. Naiomba Serikali itoe tamko la kwamba mtu yeyote ambaye anamiliki silaha bila kuwa na kibali asalimishe kwa viongozi ambao watateuliwa kuzipokea na atakeyesalimisha Serikali haitamchukulia hatua. Hii itasaidia sana kwani kuna mtu mmoja aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na alifanikiwa sana. Pia kuna *RPC* mmoja (Msika) aliwahi kutoa tamko kama hilo na matokeo yake yalionekana. Hivyo ninashauri hilo lifanyike.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa kuamua kufika Kilolo kuona na kusikia matatizo ya Gereza la Mgagao.

Hili ilinitia moyo sana kwamba kweli Serikali ipo. Leo tulifikiwa na mgeni, Mheshimiwa Rais wa Namibia na alichokufanya ni pamoja na kutembela sehemu ambazo aliwahi kuishi kama Mpigania uhuru. Amefika Mbeya na Dodoma na sehemu hizo zimetumika vizuri maana kuna Shule na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Mbeya na Dodoma wanaweza kugeuza sehemu hizo zikawa sehemu za vivutio vya utalii na histori nzuri.

Mheshimiwa Spika, hebu fikiria kama leo angefika Mheshimiwa Rais wa Namibia akaelezwa kuwa Vituo hivyo vimegeuzwa Vituo vya Kutolea Adhabu yaani Gereza, angejisikiaje?

Mheshimiwa Spika, sehemu ambayo ninapenda kuzungumzia ni Gereza la Mgagao - Kilolo. Ninaomba Serikali hii ibadili wazo lake la kufanya sehemu hiyo muhimu kuwa Gereza na ligeuzwe angalau kiwe hata Chuo cha Polisi au Magereza. Pale Mgagao kuna vyumba viwili muhimu ambavyo vinatunzwa kwa sababu chumba kimoja kilitumika kulala Mheshimiwa Nelson Mandela na kingine kilikuwa chumba cha Mheshimiwa Thabo Mbeki. Je, endapo Mheshimiwa mmojawapo ataamua kufika kama alivyofanya Mheshimiwa Rais wa Namibia tutampeleka Magereza? Na kwa kuwa ni muda mrefu alifungwa atajisikiaje?

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kuwasiliana na Ubalizi wa South Africa wameonyesha nia ya kutaka mimi niweze kuwasiliana na Mheshimiwa Nelson Mandela ili aweze kusaidia kwa jambo hili. Watakaopata elimu pale watasaidia kuijenga nchi yetu na sitegemei kama Gereza litasaidia chochote. Kumbuka kuwa wale wakimbizi waliacha watoto pale ambapo wangeparajika zaidi kupata elimu kwani walio wengi hawana wazazi (baba).

Mheshimiwa Spika, nichangie kidogo kuhusu Jeshi letu la Zimamoto. Leo tunategemea kuanza kutumia gesi toka Songosongo. Hivi tumejiandaaje? Ningependa kutoa mapendekezo yafuatayo:- kwamba tuanze kuangalia Ofisi ya Zimamoto kwani zinasikitisha sana tena sana. Ofisi zinazotumika hadi leo ni za kupanga, ni jambo la kushangaza sana. Bajeti ya Idara haitoshelezi majukumu yanayopunguza shughuli za utendaji likiwemo la Ukaguzi wa Tahadhari na Kinga ya Moto kwenye maeneo mbalimbali kwa nchi nzima hayatekelezeki ipasavyo kutokana na ufinyu wa bajeti. Ukiyaona magari ya Idara hii yalivyochakaa utashangaa na ni machache. Naomba Idara ya Zimamoto wapewe magari mazuri na ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, sehemu kilipo Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kwenye eneo la Kiwanja cha Ndege Dar es Salaam (*Old Terminal*) karibu na *VIP* hapastahili hata kidogo. Naishauri Serikali itafute sehemu nyingine. Hata sehemu ya mazoezi hakuna, maana wakati mwingine hutakiwa kuwasha moto kwa ajili ya mazoezi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Chuo ingetakiwa pawepo hata Mabweni.

Mheshimiwa Spika, ukiona magari mawili yaliyopo hapo Chuoni utashangaa. Hivyo lazima yapatikane magari ya Zimamoto ya kisasa. Hivyo ningeshauri kwamba Idara hii hasa Chuo cha Zimamoto kiongezewe bajeti ili kiweze kufanya kazi vizuri. Chuo hiki kina wanafunzi wachache na tuna upungufu wa wasomi, wengi wanatumia uzoefu tu.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kutoa ndege ambayo ipo kwa ajili ya kazi maalum ya kupambana na wakulima haramu wa bangi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya hii ya Kilolo ni mpya, kwa hiyo ningependa kutokana na umuhimu wa pekee Wilaya hii ipatiwe japo magari mawili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema atasaidia pale ambapo wananchi wameamua kujenga nyumba, Ofisi kwa ajili ya Polisi, pale Ilula tayari tumejenga tungeomba tupewe furniture na baadhi ya vitu vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Idara ya Uhamiaji kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya na pia uboreshaji wa Ofisi hii na ninajua kwa kuwa sasa wataanza kutumia vote yao, watafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waziri atakavyokuwa anajibu hoja za Wabunge anieleze wale wenzetu waliotuokoa Watanzania tusiteketee na moto pale Ubungo walipewa motisha gani?

Mheshimiwa Spika, ninaunga hoja hii mkono lakini nitataka ufafanuzi wa mambo haya, kwamba ni lini Kilolo tutapatiwa magari kwa ajili ya Polisi? Kuna Vituo mfano Polisi Mbuyuni, Polisi Ilula, Polisi Mtitu, Makao Makuu ya Wilaya Kilolo. Pili, nataka nijue motisha waliyopewa wale waliotuokoa na janga la moto pale Ubungo. Ahsante.

**MHE. SHAIKU AHMADA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Nami naungana na wenzangu kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza wewe kwa kuliongoza Bunge hili kwa ufanisi kabisa. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa hotuba yake tunayoichangia. Kwa hakika hotuba ni nzuri sana na kama itatumiwa vizuri italeti mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa naanza kuchangia hotuba hii kwa kuanza na kumwomba Mheshimiwa Waziri ili anisaidie Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Mwembe Makumbi kuna Vituo viwili ya Polisi. Kituo kimoja kiko sehemu inayoitwa Karakana na Kituo kingine kiko sehemu inayoitwa Maruhubi. Matatizo makubwa ya Kituo cha Karakana ni ukosefu wa umeme.

Kituo hicho hivi sasa kimezungukwa na majengo yenye umeme na kiko katikati ya majengo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kuweka umeme katika jengo hilo la Kituo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kituo kingine cha Maruhubi kina umeme lakini Kituo hicho hakina simu na kiko sehemu nyeti kabisa na kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kuweka simu kwenye Kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani katika ukurasa wa 19 kipengele cha namba ya Rome II kinachoelezea kuhusu ukarabati wa Mashua za Doria; katika ukarabati wa mashua hizo Zanzibar haikuhusishwa. *Port*

*Marine* ya Bandari ya Zanzibar kwa kiasi cha miaka kumi iliyopita bati zake zimeharibika na hazipo kabisa. Hivi sasa doria za Polisi kwenye Bandari ya Zanzibar na Vitongoji jirani hazifanyiki kutokana na upungufu huu.

Mheshimiwa Spika, vilevile wako Maaskari wa Jeshi la Polisi wanaishi mitaani kutokana na upungufu wa majengo ya kuishi Makambini. Maaskari hao wanajilipia kodi za nyumba walizokodi. Mheshimiwa Waziri angewafikiria wapiganaji wake ili awalipie kodi za nyumba kwani wanaishi nje ya Kambi kutokana na upungufu wa nyumba Makambini mwao.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo yote sina zaidi na ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Serikali kujenga Vituo vya Polisi na nyumba za kuishi Polisi hasa katika ngazi ya Wilaya. Ila wananchi wa Tanzania wameuamua kushirikiana na Serikali yao kujenga Vituo vya Polisi hata katika ngazi ya Wilaya. Wilaya ya Simanjiro haina Kituo cha Polisi na Serikali inajua sisi tunahudumiwa na *OCD* wa Arumeru au wa Kiteto, hao ni baba wa kambo ambao kwa bahati mbaya sina hakika kama wanapewa mafungu ya ziada ya kuhudumia Wilaya ya Simanjiro.

Mwaka 1998 Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipofanya ziara Wilaya ya Simanjiro aliahidi kwamba kuanzia bajeti ya 1998/1999 Serikali itajenga Kituo cha Polisi na nyumba za Polisi. Mpaka sasa Serikali haijatumia ahadi hiyo japo nimekuwa nikiikumbusha Serikali. Baada ya wananchi kungoja ahadi hiyo bila mafanikio, viongozi akiwepo Mbunge, wananchi, Halmashauri na Mashirika mbalimbali tumeamua kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ambacho kimefikia hatua ya kuridhisha. Hapa namshukuru *IGP* Mahita, Mkuu wa Jeshi la Polisi kwa kutupatia mifuko 100 ya saruji. Lakini nasikitika sana kutofikiriwa kwenye bajeti kumalizia Kituo au kujenga nyumba za Askari. Namwomba Mheshimiwa Waziri leo awajibu wananchi wa Simanjiro kwamba hatambui wala hatekelezi ahadi za Mheshimiwa Rais ili tuweze kuunda ujumbe maalum wa kupeleka majibu hayo kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni usalama ulivyo Mererani. Wananchi wa Mererani wamejenga Vituo viwili vya Polisi, nawapongeza sana. Pia naishukuru Serikali kwa kutupatia Askari Polisi. Kwa bahati mbaya sana pamekuwa na matukio ya watumishi wa *AFGEM* kuwashambulia watu kwa bunduki bila Serikali kuchukua hatua. Sheria yetu inasema hakuna aliye juu ya sheria na mtu asichukuwe sheria mkononi. Watumishi wa *AFGEM* wamekuwa wakichukua sheria mikononi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anijulishe hatua zilizochukuliwa na Serikali dhidi ya hao wanaochukua sheria mikononi. Au watumishi wa *AFGEM* wako juu ya sheria? Je, watumishi wa *AFGEM* wana ruksa ya kuchukua sheria mkononi?



**MHE. LEONARD N. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuchangia machache katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2004/2005 ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Hotuba hii ni nzuri na imemulika maeneo yote yanayogusa kazi na maisha ya Jeshi la Polisi nchini na Asasi zake kitaifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maeneo nitakayochunguza na kuomba mabadiliko ili kuboresha kazi na huduma za Wizara hii, nachukua nafasi hii kwanza kuunga mkono kwa dhati kazi nzuri ya Jeshi la Polisi, Magereza na Usalama inayojidhihirisha katika kulinda Taifa letu wakati wote. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Inspekta Jenerali wa Polisi na Wakuu wote wa Utawala wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Asasi zote zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo matatu ningependa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi anihakikishie kuwa yapo katika makisio ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2004/2005. Eneo la kwanza, ni kuhusu ujenzi wa ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba na Vituo vya Polisi katika Wilaya ya Iramba hususan nyumba za Polisi na Polisi Magereza Kiomboi, Bomani, Shelui na Misigiri (Kituo kipya muhimu kilichopo barabara kuu itokayo Dodoma- Singida kwenda Nzega - Shinyanga - Mwanza). Wananchi wamejitolea kwa hali na mali na sasa wanachoomba ni Serikali kusaidia haraka iwezekanavyo kutenga fungu la fedha za kutosha kwa ujenzi wa nyumba za Askari Polisi na familia zao.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 18 na 27 ibara ya 35/48 kuhusu Matarajio ya shughuli za Polisi katika mwaka 2004/2005 pameorodheshwa maeneo mbalimbali lakini Vituo na nyumba za Polisi vinavyoendelea kujengwa kwa nguvu za wananchi Kiomboi, Misigiri na Shelui Wilayani Iramba havikuorodheshwa hata kidogo.

Tatizo hili nimepata kuzungumza na kumjulisha kwa maandishi Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa heshima na taadhima ningependa Mheshimiwa Waziri atoe kauli na awahakikishie wananchi wa Wilaya ya Iramba kuwa nao wanastahili kuungwa mkono na Serikali katika kukamilisha shughuli hii mwaka 2004/2005. Kama Wilaya nyingine zimetengewa fedha kwa shughuli kama hizi kwa Jeshi la Polisi si Magereza, kwa nini Iramba itengwe pembeni?

Tatizo la pili ni kuhusu ufufuaji wa trekta linalotumika kwenye shamba la Magereza la Ushora, Wilaya ya Iramba. Shamba hili ni muhimu sana na linalisha na kutoa kipato cha fedha kwa Magereza yote yaliyopo Iramba. Trekta linalotumika limeharibika sasa yapata miaka minne. Mwaka 2001 nililifikisha suala hili kwa Mheshimiwa Naibu Waziri lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 32 Ibara 55(xi) “kuendeleza uzalishaji katika mashamba ya kilimo na mifugo kwa kuyapatia zana na pembejeo zinazotakiwa.”

Ningependa na nasisitiza kuwa Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi wa Iramba kuwa Shamba la Magereza la Ushora litakuwa mojawapo katika kukarabati, kufufua trekta ambalo limelala miaka mingi na pia kupatiwa zana nyingine muhimu

kuliwezesha Jeshi la Magereza, Wilaya ya Iramba kufufua, kupanua na kuimarisha shamba la kilimo la Ushora. Katika kifungu cha 44, 28 “Uimarishaji wa mashamba ya Magereza Makadirio Shs.500,000,000/=.”

Mheshimiwa Spika, tatizo la tatu, ambalo limeikumba Wilaya ya Iramba ni uduni wa vyombo vya usafiri (magari) ambavyo vinahitajika sana kwa Jeshi la Polisi na Magereza kuhudumia Wilaya pana kama ya Iramba. Jeshi la Polisi Wilaya ya Iramba linahitaji magari mawili zaidi na pia panahitajika kukarabati kwa hali ya juu magari yaliyopo sasa yanayotumika kwani hali ya magari hayo siyo ya kuridhisha.

Hata ikiwa uwezekano wa kupata gari mpya hautawezekana, wananchi wa Wilaya ya Iramba watahukuru sana hata ikiwa Wizara itatenga fedha kiasi cha kukarabati magari ambayo sasa yako katika hali mbaya kusudi yasaidie angalau kidogo kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri ya kusimamia na kuendesha vizuri sana shughuli za Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono makadirio ya bajeti 2004/2005 ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watalaam wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa mwaka wa fedha 2003/2004. Nawaomba waendeleze moyo huo wa kizalendo ili mwaka unaofuata wa 2004/2005 uwe wa mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo nataka kuchangia ni kuhusu mabomu na mambo ya kihuni yanayofanywa na baadhi ya wananchi huko Zanzibar. Kwa kweli jambo hili liko wazi kwani baadhi ya wanasiasa wapotofu wanahubiri hadharani mambo ambayo hayastahiki kuhubiriwa.

Kwa mfano kusema kwamba safari hii wakitaka wasitake CCM itashindwa kwenye uchaguzi ujao na mara zote kutokana na uzoefu uliopo CCM inaposhinda viongozi hao waliofilisika kisiasa huwaelezea wafuasi wao kwamba wamenyang’anywa kura na hatimaye suala hilo huzaa migogoro na umwagaji wa damu usiokuwa wa lazima.

Ushauri wangu ni kwamba, Wizara yako kwa kushirikiana na Msajili wa Vyama vya Siasa hapa nchini idhibiti hali hiyo haraka sana kabla ya kuleta madhara. Ingelikuwa vizuri zaidi mkawadhibiti hata viongozi hao wanaoleta siasa za uchochezi na kuwagawa wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kilio changu kingine ni kuhusu Kikosi cha Police - Marine. Nimepitia kwa makini hotuba ya Waziri na nimeona mashua saba za doria za Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa zitakarabatiwa. Hongera sana kwa hilo. Lakini kwa

upande wa Bahari ya Hindi sijaona ni namna gani Wizara imetoa umuhimu kwa mashua zilizoko kwenye bahari hiyo. Kwa hili, naomba nipate maelezo.

Mwisho kwa heshima kubwa naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia japo kwa maandishi hotuba hii muhimu sana ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ya Bajeti ya mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana yenye mwelekeo halisi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hakika, kama Bajeti hii itatumika kwa malengo yaliyokusudiwa adha na dhiki iliyoko kwenye Wizara hii itapungua kwa kiasi kikubwa. Atakayefanya ubadhirifu ashughulikiwe bila huruma.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza *recruitment* kwenda *CCP Moshi* watoke JKT peke yake. Mtindo wa kuokoteza watu wa Vijijini na Mitaani ukome kabisa. Tujenge uzalendo.

Pili, uhamisho ni wa lazima kwa Askari na ufanywe kwa Wilaya zinazopakana ili kuokoa gharama. Kwa mfano *Police Traffic* wa Himo wapelekwe Moshi Mjini, Himo - Mwanga, Mwanga - Same na kadhalika.

Tatu, wanamgambo wachanganywe na Polisi kwenye doria za mchana na usiku. Polisi mmoja kwa Wanamgambo watano hadi kumi, wizi utaisha tu. Hii izingatie zaidi Vijijini chini ya Afisa Mtendaji wa Kata. Kwa hiyo, Wanamgambo watatoka majumbani mwao na Polisi ni wale Polisi kata wenye nyumba za kuishi na Vituo vya Polisi Kata.

Nne, Polisi Mwendesha Mashitaka asichukue zaidi ya miezi sita kukamilisha upepelezi na mtuhumiwa kuhukumiwa. Hii itapunguza msongamano wa mahabusu Magerezani.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri na Watalaam wake wafuatilie sana *Hansards* za Bunge kuhusu maoni ya Wabunge ili Wizara iboreke.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED ALI SAID:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi.

Vile vile niwashukuru Wabunge wote. Pia natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na baba yao, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kwa kufiwa na jamaa zao.

Pia nawapa pole wale Waheshimiwa Wabunge, wote waliopata matatizo mbalimbali.

Sasa naanza kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwanza ninalishukuru sana Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri linayoifanya. Lakini kuna kasoro ndogo ndogo zinazojitokeza kama binadamu. Kuna baadhi ya askari wanaoshirikiana na majambazi katika kufanya vitendo vya uhalifu.

Mfano ni wizi wa pesa uliotokea hivi karibuni katika Benki moja kule Moshi ambapo baada ya uchunguzi wa kina Askari watano walihusika na kadhalika.

Hili ni tishio kubwa sana kwani wao ndio tunaowategemea kwa kulinda watu na mali zao. Ikiwa hali ni hiyo wananchi watakuwa na imani na Jeshi lao la Polisi? Naomba uchunguzi wa kina ufanyike na wale wanaopatikana na makosa hayo wafukuzwe na adhabu kali ifuate dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, si vizuri kuchanganya Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na Siasa kwani vyombo hivi si vya CCM wala Chama kingine chochote, hivi ni vyombo vinavyowatumikia wananchi wote kwa haki na usawa. Vinginevyo vyombo hivi vikitumiwa kwa njia za kiitikadi za kisiasa inaweza kuharibu amani ya nchi mara moja jambo ambalo amani ni jambo tunalojivunia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sisi Wapinzani tuna wasiwasi sana na tamko la Waziri wa Fedha katika bajeti yake mwaka huu, ukurasa wa 40. Anasema, kutokana na ongezeko la matukio ya ujambazi nchini, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu mwaka ujao na vitendo vingine vya uhalifu Bajeti ya mwaka 2004/2005 imeongeza mgao wa fedha kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wetu ni kuhusu suala la uchaguzi kuchanganywa na vitendo vya ujambazi na uhalifu. Kwa maana hiyo uchaguzi ni jumla ya vitendo vibaya. Tuna wasiwasi zisije zikatumika nguvu za ziada kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama ili kuvikandamiza Vyama vya Upinzani na kuilazimisha CCM ishinde, kwa sababu suala la uchaguzi ni jambo la kidemokrasia.

Pale Serikali inapotaka uchaguzi ufanyike vizuri, basi unafanyika vizuri bila matatizo yoyote.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji kwa utekelezaji mzuri wa majukumu waliyopewa na Taifa. Aidha, naunga mkono hotuba ya Bajeti ya Waziri kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika mambo yafuatayo:-

Katika bajeti ya mwaka 2003/2004 ilitazamiwa kwamba kutokana na hadhi ya Magereza watagawiwa matrekta likiwemo Gereza la Ibiri Ludewa kwa ajili ya kilimo lakini utekelezaji wake umechelewa sana. Aidha, nampongeza Mkuu wa Gereza la Ludewa kwa kuongeza uzalishaji wa zao la mahindi kila mwaka licha ya kuwa na vifaa duni vya kazi. Nawashauri kutekeleza ahadi iliyotolewa mwaka 2003/2004.

Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 Mheshimiwa Mbunge wa Ludewa aliomba majengo ya Kituo cha Polisi ambayo yalijengwa miaka ya sabini kule Manda - Ludewa, yanayoendelea kuharibika vibaya; Askari wanaoishi hapo mazingira yao ni mabaya kwa vile *system* ya maliwato zimeharibika; nyumba za kuishi zimepata *crack* kubwa; rangi zimefikia uchakavu wa hali ya juu kabisa; hivyo Wizara pamoja na upungufu wa fedha uliopo ingeandaa utaratibu wa nyumba hizo hatua kwa hatua.

Miongoni mwa Wilaya ambazo hazina Ofisi ya Polisi ya Wilaya ni Ludewa, licha ya Wilaya hiyo kuanza mwaka 1975, ingawa wananchi wameanza kuchangia ujenzi wake. Tunaomba kuungwa mkono na Wizara ili kukamilisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ni nzuri, uchambuzi wa kina umefanyika na inaeleweka, kutokana na hali hii naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Makamanda wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika mwaka 2003/2004 niliahidiwa mambo mawili.

Kwanza, ukarabati wa Kituo cha Polisi na nyumba 20 za Askari. Nyumba za Askari na Kituo cha Polisi Mbamba Bay ni ya zamani hazijafanyiwa ukarabati hata mara moja toka zijengwe na sasa zinavuja. Nilitegemea mwaka 2003/2004 hali ya kifedha haikuruhusu, pengine ningefikiriwa mwaka huu wa fedha wa 2004/2005. Ningeomba mwaka huu maombi yangu yangeingizwa katika Bajeti hii.

Pili, Kituo cha *Mbamba Bay* kinatakiwa kiwe na Askari 20 lakini waliopo ni 9. Mwaka jana niliahidiwa kuwa Askari wataongezwa lakini hakuna lililofanyika. Naomba tupewe mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Kituo hiki ni cha mpakani na kina kazi kubwa sana ya kusimamia usalama mpakani. Kinahudumia wageni toka Malawi na Msumbiji hivyo ingefaa sana kituo na nyumba za Askari zikakarabatiwa ili kilingane na kazi nzito wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, *Mbamba Bay* kuna Idara ya Uhamiaji na kwa bahati mbaya hakuna Ofisi na wafanyakazi ni wachache. Naishauri Wizara ijenge Ofisi ya Uhamiaji *Mbamba Bay* na iongeze wafanyakazi ili waweze kupambana na matatizo ya mpakani.

Mheshimiwa Spika kwa kuwa Hotuba ni nzuri mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi na mimi mwenyewe binafsi naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mia kwa mia.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika naomba kutoa wasiwasi wangu kuhusu utekelezaji wa Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, Wananchi wa Wilaya ya Mbozi wameshiriki kwa sehemu kubwa ujenzi wa gereza la Vwawa kwa kuchangia mabati na matofali. Sasa ni zaidi ya miaka mitatu Wizara imekuwa ikiahidi kumaliza jengo hili, lakini katika mpango huu hakuna maelezo yoyote. Ninaomba kupewa majibu ili niweze kuwapa moyo zaidi wananchi, hasa ni lini litakamilika ili kuwapunguzia usumbufu wa watuhumiwa kwa kushindwa kuwawezesha kuhudhuria kesi zao Mbozi kutoka Mbeya (Ruanda).

Pili, Mbozi ni Wilaya yenye matatizo ya usafiri kwa kujua kwamba Kamsamba iko kwa zaidi ya maili 100, Mkutano mpakani na Sumbawanga ni zaidi ya maili 90. Barabara vijijini si za kudumu hasa ukubwa wa mazingira yake kwani toka Wilayani hadi Iyula, Isansa (Magamba) mpakani na Chunya inaifanya Wilaya ishindwe kuwezesha huduma ili kukidhi mahitaji ya umma. Ipo haja ya Wilaya kupewa gari lenye kuweza kuhimili hali ya Wilaya. Naomba maelezo.

Tatu, Utendaji wa Polisi katika kuwahudumia wananchi unahitaji Ufuatiliaji kwani Askari wa ngazi za chini kwa vituo vya Mlowo, Vwawa, na Kamsamba vina manung'uniko makubwa sana kwa kudai rushwa kwa wana vijiji na kuzima kesi ama kuzichelewesha kuzifikisha Mahakamani. Mpelelezi wa Wilaya amekiri na kusema kuwa ameshindwa kufuatilia maana hana usafiri. Naomba Askari wasio waaminifu wasikae muda mrefu maana hali ya rushwa katika Wilaya hii ya mpakani ni kishawishi kikubwa.

Nne, Naomba Serikali iwe inawapa moyo wananchi wanaosaidia sana kuwanasa waharifu kama wachuna ngozi ambao hadi leo hakuna kinachoeleweka pamoja na kwamba wananchi walijitolea sana kuwafichua na kushiriki kuwakamata. Serikali itoe tamko ni hatua gani zinaendelea mpaka sasa ili kujenga imani na utulivu kwa wananchi.

Tano, Naomba Wizara izingatie sana kuwalipa maslahi Askari kama mirathi kwa familia zao wanapopatwa na vifo. Naomba suala la Cpt. Mwashinya Mbozi familia yake ilipwe, maana watoto wa marehemu wana hali mbaya sana. Sita, Mheshimiwa Spika, wananchi wako tayari kusaidia ujenzi wa Station ya Polisi ya Wilaya. Hali ya Kituo kilichopo ni kibovu na cha aibu, tena kipo barabarani. Hakionyeshi hadhi kwa wageni wapitao. Ili Msaada wa wananchi uweze kutolewa, Wizara ionyeshe shukrani kwa mchango uliotolewa kwa ujenzi wa gereza.

Mheshimiwa Spika, Naunga mkono kwa kujua kuwa Wizara itayatilia maanani maombi yangu na kuyatolea maamuzi.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, Naomba kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Omar Ramadhani Mapuri (Mb) hususan kwenye Idara yake, Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Spika, Naomba awali ya yote kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwenye Idara, Taasisi na Asasi zote zilizo chini ya Wizara yake kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii. Shukrani za pekee kwa Wizara kuwezesha Magereza ya Kilimo mawili Jimboni kwangu Kilombero, gereza la Idete na lile la Kiberege kwa kupatiwa matrekta mapya.

Mnamo tarehe 5 Julai, 2004, nilitembelea gereza la Idete, nilifurahishwa sana na hali ya chakula cha kutosha kinachotolewa kwa wafungwa pamoja na Uboreshaji wa vyoo gerezani hapo ambapo Mitondoo haitumiki tena, vyoo vya kuvuta vimejengwa chini ya Mkuu huyu mpya wa gereza hilo. Tofauti na hali ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Nikirejea kwenye hotuba ya Waziri Ibara ya 37 hadi ibara ya 47 kuanzia kurasa ya 21 hadi 27. Swala la Msongamano kwenye Magereza ulijitokeza pia Idete hususan kwenye kundi la Mahabusu. Jingine lililojitokeza ni kuwaweka Mahabusu *Juveniles* wawili wenye umri wa miaka 13 na 14 kwenye gereza hilo. Ombi langu ni kuomba Wizara ifanye kila linalowezekana la kuwatoa vijana wawili wale haraka iwezekanavyo kwenda kwenye Magereza na Mahakama Mbadala na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na Magereza yetu kuwa finyu kwa ongezeko la wafungwa kufuatana na ujenzi wa Magereza haya kufanya kazi wakati ule zilipojengwa, jibu siyo kulundika wafungwa kwenye ufinyu huo ila ni kujenga Magereza zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu ya uhaba wa fedha nchini swala ni kutumia raslimali hii kujenga uwezo wa upanuzi wa Magereza yetu. Raslimali yetu ni Wafungwa wenyewe kiasi cha 25,000 zaidi ya kiwango cha 22,000 kama kilivyojengwa na Wakoloni

Mheshimiwa Spika, Serikali imekabili hili kwa kiasi chake kwa kuanzisha Magereza ya Kilimo kama vile yale mawili ya Jimboni kwangu, gereza la Kilimo la Kiberege na lile la Idete.

Mheshimiwa Spika, Nashauri, kwa mtazamo wa Ibara ya 44 ya hotuba ya Waziri Mheshimiwa Mapuri, kwa upanuzi zaidi wa Kilimo cha kisasa kwa tija ili kuunda uwezo wa upanuzi wa Magereza. Hatua nyingine ni kupunguza idadi ya wafungwa wasio na umuhimu wa kuwepo magerezani kwa matumizi zaidi ya *Extra Mural Labour Law of 1967, for more productive activities*, kama vile ujenzi wa barabara, ujenzi wa Magereza mapya na kazi nyingine ambazo zinapasa zitumie fedha za Serikali. Wenye kupewa hukumu hizi wasiachiwe tu au kupewa kazi laini bali watumike kwenye kazi za maendeleo hususan kwenye sekta ya Magereza.

Mheshimiwa Spika, hali hii iendelezwe kuhusiana pia kwa wafungwa wa vifungu vifupi au waliobakiza kipindi kifupi, washirikishwe kwenye kazi za upanuzi na ujenzi wa Magereza mapya.

Mheshimiwa Spika, Usalama wa raia wa mali zake dhidi ya wafungwa hawa uzingatiwe kama alivyotahadharisha mwenyewe Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi hususan kwenye ibara ya 40 ukurasa Na. 23.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo yote, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. JANETH E. MASHELLE:** Mheshimiwa Spika, Kwanza kabisa nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kushughulikia Uhalifu nchini, pamoja na kulipongeza Jeshi la Polisi, napenda kuwashauri waendeleo na moyo huo huo wa kupambana na wahalifu hao kwani ujambazi ulikuwa umekithiri hapa nchini. Takwimu zinaonyesha uhalifu huo umepungua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kulipongeza Jeshi hilo ninapenda kuishauri Serikali ifanye utaratibu mzuri kuongeza vifaa katika Idara ya Zimamoto na Uokoaji ambayo uhaba huo wa vitendea kazi umesababisha uharibifu wa mali mbalimbali na matukio mbali mbali ambayo yametokea, vile vile upungufu wa Idadi ya Askari wa Zimamoto hasa wenye mafunzo ya juu ya Zimamoto na Uokoaji. Na pamoja na hayo ninaishauri Serikali kuongeza Vyuo vya Mafunzo hayo ya Zimamoto na Uokoaji kwani hata hivyo Chuo kipo lakini hakina majengo na eneo la kutosha la kufanyia mafunzo na vifaa vimechakaa na hakuna vifaa vya kutosha, vile vile Jeshi hilo liongezewe Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishauri Serikali Wakimbizi warejeshwe makwao na wale wahamiaji haramu katika Mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Naishauri Serikali kujenga nyumba za Askari Polisi Nchini kwani Askari wetu bado wanaishi katika mazingira magumu sana. Utakuta sehemu zingine bado wanaishi kwenye nyumba ambazo hazina hadhi ya kuishi Polisi wetu na wengine kwa ajili ya kukosa nyumba wanaishi kwenye mahema na familia zao na sehemu zingine nyumba zao utakuta bati juu na chini, sasa kipindi cha jua inakuwa matatizo hata usingizi hauji kwani moto unamuwakia hapa hapa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Serikali iimarishe Askari wa upelelezi ili kuondokana na ucheleweshaji na kesi kwani utakuta kesi nyingi hucheleweshwa kupata hukumu kwa sababu ya upungufu wa Askari wa upelelezi kuwa wachache na Ufuatiliaji wa kesi hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kurudisha mabaraza ya vijiji na Kata ili kupunguza msongamano wa kesi na kumaliza kesi kwa njia ya usuluhisho na kupunguza idadi ya kesi zinazofikishwa Mahakamani.



Mheshimiwa Spika, Naishauri Serikali kuwasaidia wale wafungwa wenye vifungu virefu wawe wanaandaliwa sehemu za kuishi wanaporudi vijijini. Wapewe zana za kufanyia kazi kwa sababu wanapokuwa gerezani kwa muda mrefu, hujifunza vitu vingi ambavyo vitawasaidia hata kwenye maisha yao hata watokapo. Hivyo ingekuwa vizuri zaidi wafungwa hao wangesaidiwa kwa kupewa zana mbalimbali za kuanzia maisha.

Mheshimiwa Spika Nawasilisha.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Aidha nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Inspekta Jenerali wa Polisi, Kamishna Mkuu wa Magezea, Wakuu wa Idara na Askari wote kwa kazi nzuri na ya ujasiri katika kuleta amani na usalama kwa raia wa nchi yetu, pamoja na kuwa kazi wanaifanya katika mazingira magumu na upungufu wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ya Waziri, naomba wakati wa Uchaguzi Mkuu 2005 Askari wapatiwe vifaa vya kutosha ili kuendelea kudhibiti usalama ili tuwe na uchaguzi wa amani. Kwa mara nyingine naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara yake kwa kazi nzuri waliyoifanya, naunga mkono Hoja hii asilimia 100.

Pamoja na kazi nzuri ya Waziri, naomba Serikali iwapatie Askari wa Iramba Mashariki gari la kufanyia kazi na gari hilo likae Nduguti siyo Kiomboi. Kituo cha Polisi Igugumo nao wapatiwe Umeme, maana umepita Mita tatu toka nyumba/ofisi ya Polisi. Naiomba Serikali iongeze Askari na vitendea kazi Iramba Mashariki, Ibagu, Nduguti na Igugumo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara yake, Polisi, na Watendakazi wote.

Mheshimiwa Spika, Napenda kuchangia hoja katika eneo la *Traffic*. Bado rushwa na dalili zote zinaonekana kwa hawa *Police Traffic*, naomba Serikali iendeele kusafisha eneo hili. Wamejaa katika barabara kuu wakisimamisha kila gari inayopita, zaidi ni kuomba rushwa ndogo ndogo waache. Gari ikitoka Dar es Salaam kwenda Tunduma itasimama mara ngapi njiani na atatoa rushwa mara ngapi?

Mheshimiwa Spika, Serikali ishughulikie suala la kufuta utozwaji fedha wahalifu wanaposafirishwa vijijini, mlalamikaji anapomfikisha mhalifu Polisi vijijini, Polisi husema hawana fungu la Kuwasafirisha Wahalifu hadi Wilayani, waliotendewa uhalifu ndiyo huombwa na Polisi kutoa fedha ya kuwasafirisha wahalifu hadi Wilayani, hii ni

kero, Mheshimiwa Spika, Serikali itoe maelezo kwani mkoani Rukwa Wilaya ya Sumbawanga limekuwa jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, Serikali iimarisha Usalama Mipakani, Mkoa wa Rukwa tuna Wakimbizi wengi, usalama wa Mkoa umepotea, uhalifu umeongezeka Ziwa Tanganyika na katika misitu inayotuzunguka, uporaji wa magari unaofanyika na majambazi, Wizara inachukua hatua gani? Tunaomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, serikali ina mipango gani ya kuwapatia vifaa Vituo vya Polisi mipakani hasa Kasesya, Mosi, Kasanga, Kipili, Kirando na Karema, hawana vifaa, *radio calls*, nyingine ni hafifu, magari hakuna, hata *OCD* wa Sumbawanga hana gari la uhakika, lini atapatiwa gari ili afanye kazi yake ipasavyo kwani eneo analosimamia ni kubwa mno Wizara inafanya nini mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, vituo vya Polisi vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi na kuahidiwa msaada na viongozi wa Polisi kama vile Mwimbi na Kasanga, wapewe msaada wa mabati ili ujenzi ukamilike, ahadi za viongozi zitekelezwe.

Mheshimiwa Spika, Polisi wanaokaa sehemu moja kwa muda mrefu wawe wanahamishwa ili wasizoe sehemu moja, hivyo kujiingiza katika uhalifu na kubambikizia watu kesi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Polisi waliojiandikisha kufanya kazi kwa mikataba na kulipwa *gratuity* wanapostaafu na kupata kiasi kidogo mno, ufanyike mpango, wakivuka miaka 12 basi wawe pensionable ili kuondoa malalamiko yao. Wale waliostaafu na kulipwa kiasi kidogo utafutwe utaratibu nao waingizwe katika pensheni kama ilivyofanyika kwa Wastaafu wengine ili nao wafaidi matunda ya kazi yao. Kero hiyo ipo kwa Polisi na Magereza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALI SHEHA MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naiunga mkono hoja hii, kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nami sina budi kuungana na Waheshimiwa wenzangu wote kwa kutoa pole kwa Familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete S. Mwalyego, pamoja na Waheshimiwa mbalimbali waliopata matatizo kadha wa kadha humu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende kwenye hoja hii, ni kwamba hapo nyuma niliuliza swali na kujibiwa na Serikali juu ya *Speed monitor* kule Zanzibar ya kwamba jambo hili kwanza lipelekwe kule Baraza la Wawakilishi Zanzibar ili lipewe baraka. Je! Mbona hadi sasa kimya! Kwani ajali za kijinga zinaendelea kutokea ingawa hakuna wa kuzuia ajali. Lakini hata hivyo pengine tukijitahidi jambo hili linaweza kupungua kidogo. Kwa hiyo, naomba tena ikiwezekana kifaa cha *speed monitor* na kiwepo ili ajali zipungue kwani madereva wetu wanaweza kujali kwa kiasi.

Mheshimiwa Spika, vile vile pia huko nyuma niliongea juu ya ujenzi wa *Barracks* pale Mahonda Mkoa Kaskazini - Unguja. Kwani tayari kiwanja kipo, pamoja na kuwepo ufinyu wa Bajeti ya Maendeleo kwenye Jeshi hili. Lakini mbona kwenye hotuba hii halikuzungumziwa hilo, mara nyingine naomba jambo hili liwekwe kwenye mpango. Kwani Mkoa Kaskazini - Unguja una Wilaya (2) A + B. Isitoshe una wakazi wengi, wakati mwingine hutokea upungufu wa maaskari wetu, hivyo kwa kuona kwangu, kikiwepo Kituo kikuu *barracks* inawezekana kusaidia. Hasa pakizingatiwa kuwa lile eneo Ukanda wa Pwani, Kiwengwa hadi Nungwi ni eneo la Utalii.

Wakati ambapo likitokea jambo linaweza kukabiliwa mara moja. Halafu ni mkoa wenye watu wengi sana hasa wakati wa Siasa za vyama vingi hapo 2005 yaani kwenye Uchaguzi Mkuu. Sakata za mambo ya Siasa hujitokeza tokeza, hivyo tukiwa na *barracks* - mahali kama pale Mahonda kukiwa na tatizo tunaweza kulikabili kwa urahisi kuliko kama tupige simu - mjini Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kero ya kusumbuana, naomba tu kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, wakati mwingine Mheshimiwa Mbunge anafikwa na tatizo, au kusumbuliwa na vijana wetu maaskari wa Polisi kuwa anashangaa tu. Kwani siku ya Jumatatu iliyopita tarehe siikumbuki. Baada tu ya kupinda toka kituo cha Polisi, Mahonda kuelekea mjini Zanzibar natokea Jimboni Mkwajuni, kama Saa 31/2 asubuhi, mbele walijitokeza vijana wetu wawili (2) maaskari Polisi, mmoja kavaa *uniform* nyeupe na mwingine kavaa kaki za kawaida. Mwenye kaki alisimamisha gari ambalo nimo mimi. Hapa nikamtaka dereva wangu kusikilizwa. Basi punde hapo yule Askari mwenye kaki alikuja juu na kupeana lugha ambazo si nzuri. Na mimi nikabaki kuangalia tu.

Bwana Polisi anadai kuwa lazima amshitaki dereva wangu na dereva wangu anamwuliza yule Polisi unanishitaki kwa kosa gani? Askari akamjibu: “Kwenye mpindo hukusimama”. Dereva: “kwani hukuniona kuwa nimesimama na kuashiria indiketa hiyo kama unavyoiona!” Lakini yule Polisi kashikilia tu, sasa mimi nilishangazwa na yule Polisi, anamuuliza mwenzake: “je! Nimshitaki kwa kosa gani huyu!” Mara yule Polisi akaja na karatasi yenye maandishi na kumpa yule dereva wangu na kuambiwa weka sahihi. Hapo dereva wangu alikataa, Polisi akaendelea kusema kesho uende Mahakamani Mfenisini asubuhi. Dereva wangu akamwambia Polisi wewe huoni huyu ni mzee wetu umeshamchelewesha Boti ya kusafiri Saa 4:00 asubuhi. Jambo ambalo ni kweli hilo lilitokea, na kulazimika kusafiri wakati mwingine.

Ingawa baadaye nilipokea simu toka kwa askari mwingine pale kituoni ya kwamba nimtake yule Dereva wangu asiende Mfenisini Mahakani kwani jambo hilo tayari limesharekebishwa. Lakini kwangu jambo lile lilikuwa ni kama usumbufu. Hivyo naomba kwa Mheshimiwa Waziri awatake wenzetu waelewe majukumu yetu.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii bila kigugumizi chochote kile.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utangulizi wangu huo, naomba mambo yafuatayo yashughulikiwe kupata ufumbuzi ili kuondoa kero zinazozuia utekelezaji kazi bora katika Wizara hii Wilayani Kondo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Gari la *OCD* Kondo limechoka sana na kwamba Wilaya ni kubwa kushindwa kufuatilia matukio ambayo hujitokeza kwenye Tarafa 8, Kata 35 na Vijiji zaidi ya 179. Na pia Wilaya ina matukio mengi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iifikirie Wilaya ya Kondo kupewa Gari jipya moja kati ya magari 174 yatakayonunuliwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, pili, Kituo cha Polisi Kidogo cha Tarafa ya Bereko kilichopo kilomita 67 toka Wilayani Kondo hakina usafiri wowote ule. Shughuli zinafanywa kwenye mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, tatu, nyumba anayoishi *OCD* Kondo ni chakavu sana kwa vile ni ya siku nyingi sana. Kwa hali ya sasa haina usalama wowote. Naomba na kushauri kwamba ifanyiwe ukarabati wa kiwango kikubwa ili iweze kuhimili kuishi watu humo ndani. Nne, Je Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kujenga nyumba mpya za Askari kila mwaka angalau chache kila Wilaya ili hatimaye kuondoa kabisa tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, tano, Kwa kuwa msitu wa Bosay hadi Araa Wilayani Babati na Kondo ni hatari sana kwa vile wasafiri wa magari huvamiwa na majambazi, kwa nini Serikali isianzishe utaratibu wa Askari kusindikiza magari kama wafanyavyo kati ya Zamahero na njia Panda ya Itiso (Chenene). Polisi waliopo Bereko (Kondo) na wale wa Babati wanaweza kufanya kazi hii. Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja hii. Kabla sijachangia napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii kwa umakini mkubwa. Kwa msingi huo pamoja na kuridhika na utekelezaji wa kazi za Wizara hii kwa kipindi cha 2003/2004 kwa hiyo naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa lengo la kuboresha naomba nichangie eneo la Uhamiaji haramu.

Wako wahamiaji wengi sana katika nchi yetu, wengine wamekuwa wahamiaji haramu kutokana na wazazi wao au hata babu zao. Lakini wengine wanaingia kinyemela hasa wale wanaoishi mipakani hasa ikizingatiwa kuwa mipaka yetu ni *porous*. Hatua ambazo Serikali inachukua hazitaweza kudhibiti hali hiyo kwa sababu tayari mfumo wa Serikali umevamiwa, na watu wenye mahusiano na wahamiaji hao haramu.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti hali hiyo watu wote waandikishwe na watahadharishwe kuwa atakayedanganya kuhusu uraia wake ataadhibiwa na kufukuzwa nchini. Lengo la kuandikisha wananchi wote ni kuzuia wahamiaji haramu wanya.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata ya Litembo, Maguu na Matiri Wilaya ya Mbinga wamejitolea kujenga vituo vya Polisi, kwa sasa wamekwama. Serikali itoe mchango wake ili kuongeza ari ya wananchi kuendelea na moyo wa kujitolea.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe mchango wangu kwa kuitaka Serikali ikarabati jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Wilaya, Mbinga ambalo linavuja na tayari lina nyufa.

**ME. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri, Katibu mkuu, Maofisa na Watumishi wote wa Wizara hii muhimu kwa usalama na umoja wa nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaiunga mkono Bajeti hii asilimia mia (100).

Mheshimiwa Spika, pia ninachukua fursa hii kuipongeza sana Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongeza fedha katika Bajeti ya vyombo vyetu vya ulinzi na Usalama nchini katika mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, serikali yetu imeongeza Bajeti ya vyombo hivi kwa sababu tatu kuu muhimu ambazo ziliaiinishwa katika Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuwa ni:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kutokana na kuongezeka kwa matukio ya ujambazi nchini.

Pili, ni Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ujao.

Tatu, ni kukabiliana na vitendo vingine vya uhalifu nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Serikali kuongeza bajeti hiyo ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, wapo baadhi ya Watanzania wanaona kuwa Serikali haikufanya sahihi kuongeza fedha katika bajeti ya vyombo hivi vya ulinzi na usalama kwa kuangalia upande mmoja wa Uchaguzi Mkuu ujao bila ya kuangalia haya maeneo mengine mawili muhimu kwa usalama na umoja wa Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la ongezeko la matukio ya uhalifu nchini pamoja na suala la kukabiliana na vitendo vingine vya uhalifu nchini ndiyo maeneo ya kuangaliwa juu ya ongezeko la bajeti ya vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, kama Watanzania, hatuna budi kuungana pamoja katika kujenga na kuimarisha usalama na umoja wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia ni kuwa kwa muda mrefu Jeshi la Polisi lilikabiliwa na tatizo sugu la ufinyu wa bajeti yake jambo lililoathiri utendaji wake wa kazi katika kukabiliana na Wimbi kubwa la uhalifu unaotumia teknolojia za kisasa. Pia Jeshi hili la Polisi lilikabiliwa na upungufu wa vitendea kazi, Ofisi na nyumba za kuishi Askari.

Mheshimiwa Spika, ni nani ambaye anapingana na hali hii ilivyokuwa kwa muda mrefu katika Jeshi letu la Polisi? Je hapa ufanisi ungepatikana vipi kukabiliana na Wimbi hili la uhalifu unaotokea nchini kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa wiki iliyopita kupitia vyombo vya habari nchini tumeona baadhi ya silaha zikichomwa moto pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunalazimika kuimarisha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama nchini ili kulinda usalama na umoja wa Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Jeshi la polisi ni kulinda na kusimamia usalama wa Raia na mali zao. Kwa hivyo Watanzania wote hatuna budi kuondoa tofauti zetu tutoe ushirikiano kwa Jeshi letu katika kuwafichua wahalifu wote hapa nchini kwa faida yetu sisi wenyewe na mali zetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nikinukuu vyombo vya habari vya hapa nchini, vilielezea juu ya wizi wa mamilioni ya fedha *NBC Moshi* kuwa Mkenya anaswa na mamilioni Nairobi.

Mheshimiwa Spika, Mkenya huyo aliyekamatwa akiwa nyumbani kwake, alikutwa na fedha T.Shs. milioni 170, K.Shs.171,000, Dola za Marekani 78,000. Pia alikwisha kununua gari ya kifahari, nyumba, kiwanja na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ambazo zilibiwa *NBC Moshi*, tunaelezwa kuwa kwa taarifa za awali zinaonyesha kuwa fedha zilizoibiwa kwenye tukio hilo ni nyingi sana. Kati ya fedha hizo nyingi ni za *BOT*.

Mheshimiwa Spika, *BOT* ni Benki yetu Kuu ya Tanzania ambayo ni mali ya Watanzania wote. *BOT* ikiwa inatumia Ofisi za *NBC Moshi* kuendesha shughuli zake za kifedha katika Mkoa wa Kilimajaro. Tunaelezwa kuwa wizi huo ni mkubwa zaidi katika Benki zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, wizi huu ambao watu kumi na tano (15) wanatuhumiwa kuvamia *NBC Moshi* wakati inakaribia kufungwa Saa 10:00 jioni inadhihirisha kuwa wahalifu kweli ni wazoefu, wenye mbinu na silaha za kisasa jambo ambalo linatulazimu kujenga Jeshi la Polisi lenye uwezo wa kukabiliana na uhalifu wa aina hii na mengineyo hapa nchini kuanzia sasa na siku zinazokuja.

Mheshimiwa Spika, tuangalie utaona wahalifu wa aina hii ni wazoefu na wenye kujua suala zima la uhalifu na faida wanayoweza kuipata Pindi wanapofanikiwa kufanya uhalifu wao huo. Huyu Mkenya aliyekamatwa inaelezwa kuwa ni Mkurugenzi wa

Kampuni moja nchini Kenya. Tujenge na tuimarishe Jeshi letu kwa faida ya nchi yetu na mali zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono asilimia kwa mia (100).

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote napenda nichukue nafasi hii maalum nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na amani nchini mwetu. Aidha nachukua fursa hii kumpa pole sana Katibu Mkuu wa CCM na Naibu wake wa Zanzibar kwa hasara waliopata kwa kuvunjwa gari la Mkuu wa Utawala CCM Kisiwandui na kuhimizwa kwa kujeruhiwa na wasiopenda amani ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Alhaji Amani Abeid Karume, kwa kuonyesha kukomaa kwake katika siasa ya fujo; Mungu atampa uwezo zaidi wa kuhimili vitendo vya kifisadi vinavyoandaliwa kwa lengo na nia ya kuchafua amani ya Zanzibar.

Baada ya kumpongeza Mheshimiwa Karume sasa nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Mbunge Omar Ramadhan Mapuri na Naibu wake Mheshimiwa Chiligati pamoja na Wasaidizi wao wote kwa kuandaa hotuba nzuri sana yenye kufahamika sana.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya hotuba hii ni kielelezo tosha cha kuonyesha kuwa Wizara hii inahusu mambo yanayowahusu wananchi katika uhai wao na mazingira yao na ndiyo sababu imechambua bila ya kuchelewa jambo kwa faida ya wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeridhika sana na juhudi ambazo zinachukuliwa na Wizara hii hasa kwa upande wa Jeshi la Polisi hususan kule Zanzibar kwa Mkoa Kaskazini Unguja. Naelewa fika kuwa wenzetu hawa wanafanya kazi katika hali ya mazingira magumu ya vifaa hafifu vya kazi, uchache wa vyombo vya usafiri, lakini bado kazi na juhudi zao zinaficha uchache wa zana hizo na wanafanya jeshi hili lionekane imara sana. Kwa niaba yao naomba nimpongeze sana Kamishna Mkuu Khalid Mwinzani na kuwapelekea pongezi Makamanda wake wa Mkoa. Wilaya za Kaskazini na vituo vyake vyote.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuendeleza ujenzi wa kambi ya *FFU* Finya Pemba pamoja na ujenzi wa Chuo cha Polisi ziwani na nyumba za wapiganaji wake kimekua kinaboresha mazingira mazuri kwa kuishi na kufanya kazi mahala pazuri. Hali hii inadhihirisha nia ya Serikali za CCM kuandaa mazingira ya kuwaweka Askari wake vyema. Aidha nichukue fursa hii nimpongeze sana Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo kule Zanzibar kwa namna ambavyo usafi wa mazingira unavyofanywa kuanzia mijini Unguja na Pemba na mashamba yote.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imeelezea kwa kina kizuri tena kwa ukweli kabisa juu ya uzuri na udhaifu wa utendaji wake jambo ambalo halitoi mwanya wa kuchangia

chochote. Kwa maana hiyo mimi ninaomba Serikali kwa mwaka ujao wa fedha imsaidie Mheshimiwa Waziri kumpatia fedha za kuweza kufanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Kuwapatia mashua au *Boat* ya doria kwa Polisi Marine pale Zanzibar.

Pili, Kufanya ukarabati kwa kituo kidogo cha Bumbwini kulingana na hadhi ya Jeshi la Polisi huko Zanzibar, kwa sasa kuanza ukarabati wa nyumba za Polisi Mkokotoni, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, suala la usafiri kwa Maafisa wa Polisi ni jambo ambalo nalipongeza sana ingawa hali si nzuri sana ila kwa wale wachache waliopatiwa hivyo vyombo, mfano gari bado wanapata shida ya matengenezo yake. Ni dhahiri kuwa hata hiyo mishahara yao haitoshi kukimu matengenezo yake na kwa ushauri wangu ninaona ni bora sasa kasma ya matengenezo ya magari sasa itiwe katika mishahara yao wakati wa kupatiwa magari hayo. Hili linaweza likawasaidia kuwapa uwezo wa kutengeneza gari zao tofauti na utaratibu wa sasa.

Mheshimiwa Spika, mimi sina pingamizi na Wizara hii na kwa niaba ya watu wa Kitope natamka kuunga mkono hoja hii na nawatakia utekelezaji imara zaidi. Shukrani.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia (100).

Mheshimiwa Spika, namkumbusha Mheshimiwa Waziri ombi langu la gari la Polisi Wilaya ya Bunda naomba mwaka huu tupewe gari jipya.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilishauri Polisi wasinunue gari aina ya *L/Rover 110* siyo madhubuti kulinganisha na *Toyota*. Nashauri Polisi wanunue *Land Cruiser Hard Top Pick ups* kama *Tanzania National Parts (TANAPA)*. Ulimwengu unabadilika nasi tubadilike. Naomba hili lizingatiwe, magari ni *Toyota*.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kwa kuongoza Wizara vema na kwa mafanikio makubwa. Mfano mwaka uliopita waliahidi kutoa *Vote* ya Uhamiaji na kweli wameteteleza. Nawapongeza sana na naomba waendeleo na juhudi hizo. Ahsante.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kuelezea Kituo cha Polisi Mangaka kilichopo ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu Wilaya Masasi. Kituo cha Polisi cha Mangaka ni tegemeo pekee kwa Jimbo la Nanyumbu. Kituo hiki kinakabiliwa na matatizo mengi ambayo yanaathiri utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kwanza ni ukosefu wa Majengo ya Ofisi na nyumba za Askari. Jengo ambalo zimo Ofisi na vyumba vya mahabusu ni dogo sana na halikidhi haja hiyo. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza Jengo la Ofisi na kujenga nyumba za Askari za kutosha.



Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie juu ya Vituo vidogo vya Polisi ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu. Vituo hivyo ni vichache sana kipo kimoja Mikangaula. Kituo cha Mikangaula hakina jengo imara na wananchi wamejenga jengo lingine lakini bado halijamalizika. Naomba Serikali isaidie katika umaliziaji wa Jengo la Kituo cha Polisi cha Mikangaula. Naomba ujenzi wa Vituo vidogo vya Polisi upanuliwe katika vijiji vya Michiga, Nanyumbu na Masuguru. Sehemu hizi ni muhimu kuwepo vituo vya Polisi ili kusaidia kulinda usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri Mapuri, Mheshimiwa Naibu Waziri John Chiligati, na Watendaji wote wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani kwa jitihada zao za wazi kabisa za Utendaji kazi ndani ya Wizara hii ngumu.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nichangie sehemu tatu (3) muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, wizi wa pesa za Serikali.

Pili, operesheni muhimu kuhusu ujambazi.

Tatu, pongezi kwa *RPC* wa Mkoa wa Arusha na pongezi kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya jinai.

Mheshimiwa Spika, nchi jirani Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, Zambia, Malawi na kadhalika. zimeshafahamu ubovu uliopo ndani ya nchi yetu ambao ni lazima sisi wenyewe tuwe makini kwani wanafanya mambo mengi mno ndani ya nchi yetu ambayo yanatishia usalama wa nchi na utulivu kwa ujumla

Mheshimiwa Spika, wananchi au raia wasio wema waishio nchi jirani wanavuka mipaka na kuingia nchini mwetu na kufanya wizi/ujambazi mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza sana kuona raia wabaya toka Kenya wanaingia nchini mwetu na kuiba fedha nyingi sana za Serikali. Niombe Serikali itafute kila mbinu ya kuzuia vitendo hivi ambavyo vinaonyesha udhaifu wetu.

Mheshimiwa Spika, ujambazi umeshamiri sana nchini. Pia silaha za Kijeshi zimezagaa sana mikononi mwa raia.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali ifanye Operesheni maalum na nzito na kukamata silaha zote zilizomo mikononi mwa raia waovu. Operesheni hii iwapo itapangwa vizuri na kuwahusisha wananchi, Jeshi la Wananchi, Jeshi la Polisi, Usalama wa Taifa na Mgambo/Sungusungu nina uhakika kabisa silaha zote zitakupwa barabarani au zitasalimishwa. Naomba Serikali ilichukulie hili maanani.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia basi nimpongeze sana sana Ndugu Rajabu Adadi Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai - *Department* yake ya Upelelezi imefanya kazi nzuri sana sana mpaka ikatuwezesha kuwakamata majambazi waliohusika na wizi wa fedha za Benki Kuu zilizoibiwa kupitia *NBC*.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza sana *RPC* wa Mkoa wa Arusha kwa kazi nzuri sana sana ambayo wote wananchi na Viongozi tunaiona. Naunga mkono hoja.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Omar Ramadhani Mapuri. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake Mheshimiwa John Chiligati, Katibu Mkuu, *IGP* Ndugu Mahita na watendaji wengine wote wa Wizara yake kwa kutuletea hapa Bungeni hotuba nzuri ambayo mimi naiunga mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, jeshi la Polisi mara nyingi sana linapewa lawama za uonevu, udhalilishwaji na kadhalika. Kwa wananchi wake, lakini mimi na wananchi tulio wengi tunajua kwamba wahalifu ndani ya jeshi hilo ni wachache wao uhalifu wao ni mkubwa na ni lazima udhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana wengi tunafarijika pale tunaposikia *IGP* amefanya mabadiliko kadhaa ili kurekebisha mambo jeshini na kuleta ufanisi na uwajibikaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo mimi natoa msisitizo au ushauri au maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba viongozi wa ngazi ya juu Jeshi la Polisi waendeleo kuwaelimisha maafisa wa Jeshi hilo kwamba:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, waache mara moja ile misako au kamata kamata ya vijana wetu wasio na hatia yoyote kwa visingizio kwamba ni wazururaji au wavuta bangi au wahalifu. Vijana hao mara nyingi sio wahalifu, ni vile tu hawana kazi. Sote tunajua tatizo la uhaba wa ajira. Sasa Polisi wasi "*compound*" tatizo la Serikali la kukabiliana na ajira ya vijana huku polisi wakiwa *harass* vijana wetu bure. Kamata kamata hiyo iachwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, Pili, imedhihirika kwamba Polisi wakikaa kwenye vituo kwa muda mrefu sana wachache wao wanaingia mitaani na kuwa wahalifu wakishirikiana na wakazi wachache wahalifu wa maeneo hayo, na kula njama na kujiingiza kwenye uvunjaji wa sheria, na kuwa tishio kwa raia wema.

Mheshimiwa Spika, naomba uwepo utaratibu wa kuwahamisha hamisha hawa Maofisa wa Polisi kila baada ya kati ya miezi 9 na miezi 12. Hii ni kuhakikisha hawakai sana kwenye kituo kimoja na kujiingiza kwenye uhalifu na uvunjaji wa Sheria. Hii kwa

mfano inaweza kufanywa kwa mzunguko wa Wilaya kama vile Kinondoni, Temeke Ilala, Pwani na kadhalika. Naomba sana hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi kwa hotuba yake nzuri na ya kina inayoainisha Utendaji kazi mzuri wa vikosi vyetu vya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto. Kwa kweli kazi zao ambazo ni nyeti sana zinaonekana nchini na kwenye Majimbo yetu. Moyo huo uendelee ili taifa letu liweze kusonga mbele kwa Maendeleo tunayotarajia kuyapata.

Mheshimiwa Spika, kwa leo mchango wangu nauuelekeza kwenye Jeshi la Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani. Kitengo hiki kinafanya kazi nzuri sana ya kusaidia Mwenendo mzima wa Usalama wa Polisi, magari na wananchi wanayoyatumia katika barabara zetu kuu ingawa ajali zipo lakini zimepungua kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa ushauri mdogo kwa barabara za mijini hasa miji yenye barabara mbili kila upande wa mwelekeo *Dual Carriage*. Katika hali ya kawaida, Barabara za aina hii huwa ile ya kulia inaitwa *Fast Lane* na maana yake ni kwamba yeyote ambaye ana mwendo wa kasi zaidi ya aliye mbele yake ndiye anayepaswa kuitumia hasa kwa *Overtaking* lakini walio wengi hupata *zig zag* upande wowote wa kushoto au kulia kwa kadri anavyoona ipo nafasi.

Hii haiendani na Madhumuni yaliyotarajiwa kwa barabara zenye mtazamo huo wa *Dual Carriage*, nadhani uelewa wa watumiaji haujawekwa wazi. Naomba wiki ya nenda kwa usalama barabarani ambayo huwa ipo kila mwaka, itumike kutoa elimu ya matumizi hayo kwa watumiaji barabara ili kuepusha ajali. Baada ya hilo naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. DR. ABDULKADER A. M. SHAREEF:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri na wafanyakazi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya chini ya mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti na uhaba wa vifaa hasa magari ya doria. Napenda kusema kwamba naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nina mapendekezo machache:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Upotevu ovyo - holela wa Pasi. Wimbi la upotevu wa pasi linaongezeka siku hadi siku na kutokana na urahisi wa kupata Pasi nyingine kwa utaratibu uliopo sasa ni dhahiri kwamba Wimbi hili litazidi kuwa kubwa. Matokeo yake ni kwamba wenye Pasi hawachukui tahadhari sahihi ya kutunza Pasi zao ipasavyo; wakiamini ikipotea watapata nyingine kwa; kutoa Ripoti kituo cha Polisi, kutangaza gazetini, baadaye kulipa ada ya Pasi mpya. Aidha utaratibu huu dhifu unawapa mwanya baadhi ya watu hata kuuza Pasi zao.

Mheshimiwa Spika, ndiyo linafanyika hilo! Nashauri uanzishwe utaratibu mpya ambao mbali ya hatua za kutoa Ripoti kwa polisi na kutangaza gazetini, hatua ya ada ibadilishwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upotevu wa mara ya kwanza ada ya pasi mpya iwe maradufu, na mwenye Pasi aelewe kumbukumbu kwamba amepoteza mara ya kwanza. Aidha asipewe Pasi mpya ila baada ya miezi mitatu (3) tangu kukamilisha utaratibu huu. Wale wanaoishi ugenini wapewe *Emergency Certificate* kuonesha kwamba pasi mpya inatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upotevu wa mara ya pili, ada iwe mara tatu (3) na pasi mpya asipewe ila baada ya miezi 3 hadi 6.

Mheshimiwa Spika, kwa upotevu wa mara ya tatu ada ni mara nne (4) na Pasi mpya isitolewe ila baada ya mwaka mmoja: Maana mwenye Pasi anaonyesha hana dhamana ya kuhifadhi hati ya taifa. Naamini utaratibu huu ikitangazwa, utapunguza upoteaji ovyo wa Pasi za Tanzania. Huu ndiyo utaratibu unaofuatwa na Mataifa mengi duniani na ambao umesaidia kupunguza wimbi la kupotea Pasi. Tuujaribu.

Mheshimiwa Spika, pili kupunguza ajali za barabarani. Ongezeko kubwa la ajali za barabarani unachangiwa sana na mambo matatu makuu.

Madereva kutofuata taratibu, Magari kutokuwa na breki madhubuti, Magari kutokuwa na taa zinazofanya kazi kikamilifu hasa taa za breki na taa za nyuma, Mipira au *tyre* kutokuwa na kashata za kutosha na hivyo kushindwa gari kusimama baada ya kupigwa breki gari linateleza sana barabarani.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwe na udhibiti mkali zaidi wa madereva, Magari yenye umri wa zaidi ya miaka mitatu (3) tangu upya wake, yafanyiwe uchunguzi wa kila mwaka kuhusu mambo manne na kutoruhusiwa barabarani hadi kupata *certificate*. Mambo hayo ni:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Breki ziwe zinafanya kazi sawasawa kwa mujibu wa taratibu za *Speed*. Pili, Taa zote hasa za breki sehemu ya nyuma ziwe zinafanya kazi sawasawa.

Tatu, Mipira iwe ina kashata za kutosha kuiwezesha gari kusimama inapopigwa breki na si kuteleza tu barabarani. Nne, vianzishwe vituo binafsi chini ya leseni ya Serikali ambavyo vitapewa Mamlaka ya kuifanya kazi hiyo na ambavyo vitakuwa na vifaa vyote vya kutekeleza kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri atembelee *UK* akajionee mwenyewe jinsi ya utaratibu huu unavyofanya kazi na unavyosaidia kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iko tayari kusaidia upangaji wa ziara hiyo na wahusika wa *UK*.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Polisi kwa kupambana na ujambazi, pongezi maalum kwa Kamanda Chiko kwa kukamata waliovunja na kunyang'anya Benki ya huko Moshi. Polisi wana *risk* maisha yao. Je, wale wanaokwenda kwenye Operesheni wana vifaa kama *night vision? Bullet proof vests, silencers etc.* Ni vema jibu mbaki nalo wenyewe. Wala sitegemei kuwa mtanijibu kwa maandishi kama vifaa hivyo mnavyo. Huu ni ushauri kikosi/vikundi vya polisi vinavyojitosa kupambana na majambazi wawe na *modern guns* na *gadgets* za kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, *Prisons*: Kamishna Mkuu Magereza azingatie na kufikiria barua niliyompelekea.

Mheshimiwa Spika, hili la pili ninaomba niletewe majibu kwa maandishi. Je maombi ya uraia kutoka kwa wananchi wa vijiji vilivyoomba uraia kwenye Jimbo langu yamefikia hatua gani. Vijiji husika huko Jimboni Nachingwea ni Matekwe, Majonanga, Songambebe *etc.* Naomba suala hili tulifikishe ukingoni.

Mheshimiwa Spika, Tatu, namwuliza Waziri akipata fedha gari la Polisi Nachingwea litaletwa lini?

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Eneo la machimbo la Nyamtukuza kuna machimbo ambapo wastani wa idadi ya watu ni kama 250,000. Hii huleteleza matukio mengi ya uhalifu kutokea. Askari abebaye silaha kwenda kutuliza au kupeleleza matukio hutembea kwa mguu kutoka kituo cha Polisi Nyabibuye na Muhange. Pia kuwe na gari katika kituo cha Kakonko ambacho itahudumia kata za Kakonko, Kasanda, Kasuga na Rugenge na pia maeneo ya machimbo ya Kelenge.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Wizara ilipe malipo - madai ya muda mrefu wazee wafuatao:- Mzee Alhaj Abdallah Sambiro ambaye anadai kwa muda mrefu Shs.240,000/= kama pango la nyumba yake iliyotumika kama kituo cha Polisi Kijiji cha Mahange kabla ya kujenga kituo; na Mzee Yusuf Bwotonde Shs.135,000/= kama madai ya kulisha Mahabusu Mahakama ndogo ya Kakonko;

Mheshimiwa Spika, serikali iangalie upya kiwango cha ada ya Pasi ya mfuasi \$100 ambaye mwanamume Mtanzania anayetaka kuhalalisha ukaaji wa mke ambaye si Mtanzania. Kiwango hiki ni kikubwa kwa mwananchi wa kawaida, kitazamwe upya hasa kwa nchi zinazoizunguka Tanzania.

Serikali pia izingatie haki za watoto pale ambapo akina mama wageni walioolewa na Watanzania hupelekwa makambi ya Wakimbizi au kufukuzwa nchi na kuachwa bila walezi. Utaratibu uwe unafanywa ili kuona uwezekano wa kukomesha tabia hii ikiwemo na elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, shukrani nyingi sana kwa Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Wamefanya kazi kubwa sana vitengo vyote *Police, Traffic, FFU, CID*, Uhamiaji, Magereza, wanastahili pongezi.

Mheshimiwa Spika, serikali iwapatie Polisi magari ya Kisasa yanayoweza kupambana na kufukuza majambazi. Kituo cha Mkuyuni pia kisaidiwe gari na ulinzi vijiji 37 vya Tarafa za jirani.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iwasaidie wananchi wa Mkuyuni ambao wamejenga jengo la Polisi wao wenyewe, wanahitaji Samani na Simu ya Upepo - *Radio call*.

Mheshimiwa Spika, serikali iwapatie Mikopo nafuu Polisi wa ngazi ya chini ili wajenge nyumba, wasaidie familia zao kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa hali ikoje. Jee kuna Kitengo chochote pale Makao Makuu kinachoshughulikia maswala ya Sungusungu? Kama kipo kitengo hicho naomba kiimarishwe.

Mheshimiwa Spika, ipo haja, ya kufanya ukarabati wa majengo ya zamani ya Polisi Matombo, Turiani, Ngerengere na kwingineko nchini.

Mheshimiwa Spika, viongozi hawa ni Ma-*Comrade* hasa hasa *PR* zao ni nzuri wanazoeleweka haraka sana. Watu hawa ni viongozi wanaokubalika na wako karibu sana na watu wa marika yote na watu wa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, kazi hii inabidi ifanyike kwa makini sana. Siyo jambo la haraka haraka tukawaingiza watu wasiostahili. Serikali isifanye kazi kama baadhi ya watu wanavyotaka iwe, bali Serikali ifanye kazi zake kwa utaratibu ambao imepanga.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana watoto au watu wa umri mdogo wasichangaywe na watu Wazima Mahabusu. Kisheria siyo vizuri na inavunja haki za Binaadamu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya vitambulisho vya Taifa itabidi tuone hali ilivyo ya Uraia. Kuna Raia hapa hapa nchini wana Uraia wa mara mbili wa Uingereza na Tanzania. Kama wapo Msako ufanywe. Kuna baadhi ya watu hawajijui ni raia wa nchi gani - ili watambuliwe ili wasitambuliwe.

Mheshimiwa Spika, kuna matumizi mabaya ya Jeshi letu la *FFU*. Kuna baadhi ya Wakuu wa Mikoa hutumia *FFU* kwenda kukabiliana na Mama Lishe au kina Mama wa *TES*. Huu si uungwana; kama yupo Mkuu wa Mkoa yeyote mwenye nia ya mapigano nawaambia kuwa nchi hii Tanzania ni ya utulivu. Tusitumie vibaya vijana

wetu *FFU* nchini, Mkuu wa Mkoa anayefanya hivyo apate kibali kwa Waziri mwenye dhamana.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naipongeza Wizara kwa ahadi yake ya kusaidia umaliziaji wa ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Mchinga Wilaya ya Lindi, Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Spika, ahadi hii ilitolewa na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mohammed Seif Khatibu alipotembelea Kijiji cha Mchinga. Kwa bahati mbaya hadi hii leo uwezo wa fedha yaelekea haujapatikana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara sasa iwatamkie wananchi wa Mchinga juu ya utekelezwaji wa ahadi hii ili wafahamu kuwa mimi Mbunge wao nimekuwa nikifuatilia juu ya ahadi hii. Nisingekuwa Waziri ningetamka humu Bungeni ili wanisikie.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie juu ya hali ya ugumu ya maisha katika gereza la Kingurungundwa lililopo Jimboni Mchinga Wilayani Lindi.

Mheshimiwa Spika, gereza hili lipo kilometa 70 kutoka Lindi mjini lakini halina njia za mawasiliano kama vile simu au radio ya mawasiliano hivyo kuwaweka Askari na wafungwa katika mazingira ya hatari pindi balaa likizuka.

Mheshimiwa Spika, gereza hili ambalo limezungukwa na vijiji vya Mjimwema, Mbwenkoo na Mkwajuni linalo Shule ya Msingi ambayo watoto wa Mji mwema na wa Askari wanasoma hapo.

Mheshimiwa Spika, kila ninapotoa maombi haya hujibiwa kuwa gereza hili linatakiwa kufungwa kwa sababu eneo hili lipo mbali na mji na linao simba wengi wala watu. Basi Wizara iamue moja kati ya kulifunga gereza hilo au kuwapatia radio ya mawasiliano na *generator* la umeme. Ni miaka tisa sasa tangu nilipoanza kupokea habari za kufungwa kwa gereza hili huku Askari na wafungwa wakiendelea kuishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa Wizara itakapoamua kulifunga gereza hili haitatoa sababu za umbali na simba wengi kwa sababu wapo wananchi wa Mjimwema wanaoishi eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naupongeza uongozi wa Magereza Mkoani Lindi kwa kuruhusu wenyeji wa eneo hili kupata huduma ya matibabu katika Zahanati ya gereza. Halmashauri ya Wilaya huchangia *kit* moja kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga hoja mkono asilimia mia moja kabla ya kuanza maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa hongera na pole kwa jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini palipo na mazuri mabaya hayakosekani hata yakiwa madogo madogo lakini kibaya kinaonekana kuliko kizuri.

Mheshimiwa Spika, mimi najielekeza zaidi katika Wilaya yangu ya Geita ya watu kuliko zote ukiondoa Kinondoni na Temeke. Kwa mantiki hiyo matukio yaliyoko Geita ni sawa kabisa na yale yanayotokea katika Wilaya hizi za mjini kama ilivyo Kinondoni na Temeke. Kwa maana hiyo yafuatayo naomba Wizara itupatie haya:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Gereza la Geita ni dogo sana watu waliomo ndani wengi na huduma ya maji katika gereza hili hakuna lakini wanajitolea na kujenga tanki la maji limekamilika kinachohitajika ni pampu ya kupeleka maji gerezani, ukichukulia maanani kuwa Geita haina maji ya bomba. Wafungwa wanabeba maji kichwani ni aibu tupu.

Mheshimiwa Spika, pili, Tupewe magari mawili ya kukabiliana na wimbi kubwa la majambazi ambalo linajitokeza mara kwa mara katika Wilaya yetu ya Geita.

Mheshimiwa Spika, tuna majengo mengi ya vituo vidogo vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi tunaomba Serikali iwasaidie kumalizia vituo hivi ili kuwapa huduma karibu nao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wingi wa watu na ukubwa wa Wilaya, tunaomba tupewe au tuongezewe maaskari wengine ili tuweze kukabiliana na ujambazi. Pia naomba idadi ya Askari wapelekwe kulingana na idadi ya watu.

Mheshimiwa Spika, naomba Gereza la Butundwe pamoja na Wizara hii kuipatia trekta katika mwaka wa fedha uliopita tunashukuru kwa hilo, lakini wananchi wa maeneo hayo baada ya kusikia kuwa trekta limepatikana, nao wamelipa Gereza zaidi ya hekta mia mbili (200). Kwa mantiki hiyo tunaomba gereza hilo liongezewe trekta jingine katika mwaka huu wa fedha.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napongeza kwa kazi nzuri zinazoendelea kufanywa na Wizara chini ya Uongozi wa Mheshimiwa O. R. Mapuri akisaidiwa na Mheshimiwa Cap. J. Chiligati. Kazi wanayofanya inastahili pongezi hizi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa leo ni katika Idara ya Magereza. Ninaamini kabisa kwamba Idara ya Magereza ni eneo ambalo sisi kama Taifa hatujaitumia kabisa katika kuleta Maendeleo ya nchi yetu. Magereza ikitumiwa vizuri ina uwezo wa kujitosheleza kwa mahitaji yake lakini pia inao uwezo wa kuzisaidia idara dada za Polisi na Uhamiaji. Idara ya Magereza inayo nguvukazi ambayo utilization yake sina hakika kama inafikia hata 20%. Idara ya Magereza inayo mashamba makubwa yanayoendelea kugeuka mapori na vichaka vya wanyama Waharibifu. Katika Magereza



kuna *Ma-engineer*, mafundi mchundo, Wahasibu, Waganga, Waalimu, *etc* ambao ni rasilimali isiyotumika.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kushauri hapa ni Serikali iangalie uwezekano wa kuiwezesha Idara ya Magereza kuwa engine of production, na hili linawezekana kwa kupeleka nyenzo za kazi za kutosha. Hivi sasa Magereza mengi yaliyobahatika kupata matrekta huko nyuma, matrekta hayo ama yako juu ya mawe au yanatembea spana mkononi na hivyo hayawezi kufanya uzalishaji wowote.

Mheshimiwa Spika, ni vema tuangalie uwezekano wa kuigeuza Idara ya Magereza kuwa kama “Jeshi la Kujenga Taifa/Uchumi na pengine Kanuni iliyotumiwa kuendesha J.K.T. kabla haijafutwa itumike ili Magereza ijenge na iweze kuchangia katika mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo mzuri Idara ya Magereza kwenye maonyesho ya saba saba (*DITF*) kila mwaka hufanya vizuri sana. Bidhaa zao katika *sector* mbalimbali, useremala, ushonaji, kilimo, na kadhalika. Vimekuwa vikionyesha ubora wa hali ya juu sana. Mafanikio hayo ya kwenye maonyesho ni bora yakawa mafanikio ya nchi nzima na siyo kwa lengo la maonyesho ya saba saba tu.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa dhati, Magereza iwezeshe. Ipewe *ma-tractor, planters, magari, harvesters, irrigation pumps*, wataalamu zaidi waongezwe ili jeshi la Magereza liweze kujiendesha na vile vile libebe gharama za uendeshaji wa Polisi na Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, naishia kusema *Prisons Department is an unutilized economic potential which if properly used, is able to sustain itself and us all.*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nami naungana na wachangiaji wenzangu wote kuunga mkono hoja hii. Kwanza kabisa napongeza jitihada zote zinazofanywa na Makamanda wetu wa Polisi, Magereza na Uhamiaji nchini. Kwa kweli kuna mabadiliko makubwa ambayo yameonekana ndani ya Jeshi la Polisi. Hata hivyo mimi nilikuwa nashauri kuwa muundo wa ajira ndani ya Majeshi yetu hususan Magereza na Polisi uboreshwe na ubadilishwe ili uweze kuvutia na kukidhi mahitaji ya sasa. Kwa mfano vijana wanaomaliza kidato cha sita wanaojiunga na Polisi hawaendelezwi ki-elimu kwa muda mrefu na hata utaratibu wa kupanda vyeo haueleweki vyema kama ilivyo kwa Jeshi letu la Wananchi (JWTZ) ambako vijana wote wa kidato cha sita hupelekwa kuchukua mafunzo ya u-Afisa Kadeti pale Monduli - nashauri na Jeshi la Polisi na Magereza liwe na utaratibu wa kuwaendeleza vijana hawa wenye elimu ya Kidato cha nne na cha sita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhamisho wa maafisa ndani ya Jeshi la Polisi uangaliwe ili iwe ni utaratibu wa kuwaondoa katika maeneo ambayo wamekaa kwa muda mrefu na kufanya mahusiano hata na wahalifu, si lazima wawe wale tu wanaotumia silaha! Wapo wa aina nyingi. Maafisa wa-rotate.

Mheshimiwa Spika, jambo la vivutio kwa maaskari ni la muhimu sana. Maslahi duni hayavutii kwa ajira ya namna yoyote. Ni vyema Serikali ikaboresha maslahi ya maaskari wetu na pia kuandaa mazingira mazuri ya kufanyia kazi katika maeneo yao. Ukipita kwenye ofisi zetu za Polisi/Magereza na Uhamiaji bado ofisi zipo katika hali mbaya na mabadiliko makubwa yanahitajika kufanyika kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, makazi mengi ya maaskari wetu yako katika hali mbaya sana na kweli inasikitisha ukifika kwenye makazi yao. Baadhi ya nyumba ni za tope na baadhi za mabati au maarufu kama *full suit*. Nina hakika ukifanyika utaratibu wa kufanya tathmini (*evaluation*) nina hakika nyumba nyingi zitakuwa *condemned* kwa makazi ya binadamu. Suala hili linaweza kusubiri Bajeti ya mwaka ya Serikali badala yake yafanyike mazungumzo na Taasisi kama *PPF, NSSF*. Na pia Idara ya Makazi (*habitant*) ya *UN* yenye makao yake Nairobi.

Mheshimiwa Spika, vyombo hivi vinaweza kusaidia, na ukatumika utaratibu wa kuwalipa kidogo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uhamiaji, napenda kuipongeza Idara kwa kusimamia kidete suala la Wahamiaji haramu nchini. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana. Kwa Idara kama hii suala la kufanya kazi *Manually* limepitwa na wakati. Kumbukumbu zinahitaji kuhifadhiwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa yaani Kompyuta. Huu siyo wakati wa kujadiliana kuhusu umuhimu wa kutumia teknolojia ya kisasa katika karne hii ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, idara ya Magereza inafanya kazi nzuri na hasa kwa ukweli kwamba nyingi ya maabusu zetu ziko *over crowded* kwa maana kwamba zina mzungu mkubwa wa kubeba. Magereza ziwezeshe na kwa kweli waendelezwe kitaaluma na ikiwezekana baadhi ya Magereza ziweze kutumika kama Vituo vya Utafiti wa Kilimo, ambako majaribio mbalimbali yangefanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba nilipongeze jeshi la Polisi kwa mapambano thabiti dhidi ya ugaidi/ujambazi ambao unaongezeka kwa kasi kubwa. Ni vyema Serikali ikiwapatia askari wetu nyenzo/vifaa vya kisasa ili waweze kukabiliana na matukio mbalimbali ambayo yamehatarisha maisha na mali za raia wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kuchukua nafasi fupi kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanya. Kazi ya ulinzi wa Wananchi na mali zao inazidi kuwa ngumu kila tunapoendelea mbele, hivyo kazi hiyo inahitaji juhudi na uhodari mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ofisi za Polisi Lushoto, Kwa kuwa sasa bajeti ya Wizara hii inaongezeka kila mwaka ni vema Wizara hii ikaangalia na kuboresha ofisi na majengo mbalimbali chini ya Idara zake Mikoani na Wilayani.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Ofisi ya Polisi Wilaya ya Lushoto ni mazee, mabovu kiasi kwamba Ofisi ya *OCD* Lushoto ni karibu sawa na choo cha kienyeji. Sina hakika kama Waziri au Naibu Waziri amewahi kutembelea Lushoto na kuona haya.

Mheshimiwa Spika, kama bado naomba viongozi hao wafike na kujionea wenyewe. Ni aibu kubwa kuwa na majengo kama yale kwa Wilaya kongwe kama Lushoto. Hata hivyo pamoja na hayo niwapongeze Polisi wa Lushoto kwamba hali ya usalama katika Wilaya yetu ambayo ilitoweka huko nyuma sasa ni shwari. Majengo ya Makao Makuu ya Polisi Wilaya ya Lushoto hayafai kukarabatiwa bali kujengwa upya, naomba.

Mheshimiwa Spika, kituo kidogo cha Polisi Mnazi, Kituo hicho nimekizungumzia sana hapa Bungeni. Kituo kidogo cha Mnazi kina Askari lakini hakina silaha hata moja, hakina usafiri hata pikipiki hakuna, *Radio call* ya zamani sana na nadhani kwa sasa haifanyi kazi kabisa. Kituo hicho kiko umbali kwa kilometa zaidi ya 100 kutoka Wilayani na pia kina mpaka mrefu sana na nchi jirani pamoja na mbuga ya wanyama ya Mkonazi/Umba. Naomba sana sana kituo hiki kiangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, gereza la Mng'aro katika Jimbo langu lina matatizo mengi. Majengo yake mengi kwa kweli ni ya muda. Yanahitaji ukarabati mkubwa. Naomba pia vyoo vya mtondoo viondolewe kabisa. Vinavunja hadhi ya Binadamu. Pamoja na hayo uko mgogoro wa mpaka kati ya Gereza hilo na Kijiji. Naomba Wizara hii ikisaidiana na vyombo vingine swala hilo la mgogoro wa mpaka litatuliwe haraka.

Mheshimiwa Spika, *Yono Company*: Kwa bahati mbaya sana iko Kampuni moja mjini Dar es Salaam jina nimelitaja hapo juu ambayo kwa mara ya kwanza nimewasumbua sana Waheshimiwa Wabunge wakati wa mikutano ya Kamati za Bunge.

Kampuni hiyo imekamata magari ya Wabunge likiwemo langu mara na wengine. Wafanyakazi wa Kampuni hiyo wana lugha chafu na kiburi sana sana.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo, hawa Yono ni watu gani, wanafanya kazi gani, nani au ni sheria gani iliyowapa haki ya kunyanyasa watu wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wakiwa kazini. Namshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa John Chiligati kwa msaada wake wa kuikomboa gari yangu.

Mheshimiwa Spika, kampuni hii kama inafanya kazi halali basi imeajiri wahuni ambao hawana hata heshima na watu, hivyo Kampuni inaifanya kazi kihuni haifai, naomba uamuzi wa kuipatia kazi uangaliwe upya. Madaraka ya Kipolisi haya wamepewa na nani?

Mheshimiwa Spika, niseme kweli kweli ninashangaa sana kwa matamshi ya baadhi ya viongozi wa kisiasa. Matamshi kama siyo CCM wala jeshi la kunizuia kungia Ikulu. Mtanzania leo tarehe 12-02-2004. Kauli kama hizi zinaashiria mzozo mkubwa. Serikali isinyamaze kimya lazima itoe tamko. Bila hivyo Watanzania wanaanza kupata hofu waondoeni wasi wasi wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukuwe nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Omar Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Kapteni Chiligati, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wao kwa maandalizi mazuri ya hotuba yao ambayo imewasilishwa leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nigusie kidogo juu ya suala la Wajibu wa Jeshi la Polisi hapa Tanzania. Wajibu Mkuu wa Jeshi hili ni kulinda usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, lakini tujiulize jee kazi hii Polisi wanaifanya ipasavyo? Je, kwa upande wa pili haki zao nao zinatimizwa ipasavyo?

Mheshimiwa Spika, ili jeshi la Polisi liweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa kuna mambo muhimu ni lazima yazingatiwe. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na mafunzo, zana za kutosha, makazi mazuri, mshahara wa kutosha, marupurupu mengineyo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika napenda nizungumzie mambo mawili muhimu sana. Nayo ni mafunzo na makazi.

Kwa kawaida vijana hupata ajira ya Polisi baada ya kupata mafunzo ya awali. Baadaye, na ili fursa ya kupanda cheo ipatikane basi hapana budi lazima mafunzo ya ziada yatolewe kwa Askari hao.

Mheshimiwa Spika, la kushangaza ni kwamba kuna baadhi ya Mikoa na hasa ile iliyo mbali na Makao Makuu ya Polisi kukosa fursa za kutosha kuwapatia mafunzo Askari wao, hii inavunja moyo na kupoteza ari ya utendaji kwa baadhi ya Askari.

Mheshimiwa Spika, hapana budi ni lazima maandalizi ya kutosha yafanywe kuhakikisha kwamba fursa za masomo na upandishaji wa vyeo zinakuwa sawia katika Mikoa yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Suala la Makazi bora kwa Askari ni jambo la muhimu sana ingawaje haitakuwa rahisi kwa Serikali kujenga makambi yatakayoweza kutosheleza makazi kwa askari wetu wote. Lakini la msingi ni kuhakikisha kwamba zile kambi zilizoanzishwa basi ujenzi unamalizika kabla ya kuanzisha kambi mpya.

Mheshimiwa Spika, kuna Kambi ya *FFU* iliyoko Finya Pemba. Kambi hii ilianza kujengwa miaka ya tisini. Na kwa mara ya mwisho fedha za ujenzi zilipatikana 1999 baadaye ujenzi ukasimama mpaka hii leo.

Mheshimiwa Spika, ni banda moja tu ambalo mpaka wakati huo ndio lilikuwa limemalizika kujengwa, matatu yalianzishwa lakini hayakuendelea. Kwa bahati mbaya

vyoo havikuwahi kujengwa, hakuna umeme ingawaje *line* ya umeme imepita ndani ya kambi hiyo. Askari wanajisaidia msituni. Hali hii ni ya kutisha. Hata lile banda ambalo Ujenzi wake ulimalizika nalo sasa linabomoka.

Mheshimiwa Spika, Ninamwomba Mheshimiwa Waziri afanye juu chini ahakikishe kwamba ujenzi wa kambi ya *FFU Finya* unamalizika na askari wanapata mahali pazuri pa kuishi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nigusie utendaji wa Polisi hususan kule Zanzibar. Kwa kiasi fulani Jeshi la Polisi Zanzibar wanajitahidi kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Lakini hivi karibuni kumejitokeza vitendo visivyo vya kimaadili vinavyofanywa na baadhi ya Polisi. Kule Zanzibar kumetokea hivi karibuni Vitendo vya kupigwa risasi na kuuwawa watuhumiwa. Kwa mfano pale Mtaa wa Miembeni, kadhalika kijana mmoja wa Bumbwini na mmoja alikuwa mwenye akili taahira aliyepigwa risasi na kufa Kituo cha Polisi Chake Chake.

Mheshimiwa Spika, hii ni baadhi ya mifano tu, sina hakika ni hatua gani Wizara imechukuwa ama kuchunguza na kuchukuwa hatua zinazostahili kukomesha vitendo hivi viovu vinavyofanywa na baadhi ya Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia kwako ninamwomba Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo yatakayoweza kuniridhisha juu ya namna ambavyo Wizara imeshughulikia matendo niliyoyataja hapo juu wakati anatoa majumuisho mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie hali ilivyo katika Jeshi la Magereza. Jeshi la Magereza kazi yake muhimu ni pamoja na kuchunga wafungwa wanaotekeleza adhabu zao kama zilivyoamuliwa na Mahakama. Aidha hushughulikia Mahabusu ambao kesi zao bado zinaendelea au uchunguzi juu ya tuhuma zao unaendelea. Ni dhahiri basi Jeshi la Magereza linapaswa kuhakikisha kwamba wafungwa wote wanapomaliza kutumikia adhabu zao basi warudi uraiani wakiwa na tabia chafu walizokuwanazo wameziacha na kwamba tabia zao sasa zinawawezesha kujumuika na jamii katika kuendesha shughuli zao za kimaisha bila bughudha yoyote.

Mheshimiwa Spika, mimi lalamiko langu katika mfumo mzima wa kudhibiti tabia za wafungwa unanitia mashaka. Dalili zinaonyesha kwamba badala ya wafungwa kubadilika kuwa na tabia njema mambo sivyo yalivyo huko magerezani. Licha ya kwamba gonjwa la Ukimwi ni hatari kwa wanadamu, vitendo vya ulawiti katika Magereza umeongezeka. Hali hii ikiachwa kuendelea itatufikisha pabaya. Katika Magereza kuna wale wanaofanyiwa ulawiti kutokana na kufanyiwa huruma katika kazi nzito, kupata chakula kingi/bora kuliko wengine. Lakini pia kuna wale ambao wanafanyiwa vitendo hivyo kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, tukidharau hali hii ikaendelea katika Magereza yetu basi ni dhahiri kwamba badala ya kunyosha tabia za wafungwa tutaendelea kuziharibu.

Pia kitendo cha kuwaweka pamoja majambazi sugu na wale waliofungwa kwa makosa madogo madogo, uwezekano upo wa hawa majambazi sugu kuwafundisha ujambazi hawa wengine na hatimaye Magereza yetu yakageuka kuwa vyuo vya kuzalisha majambazi. Ninaishauri Wizara hii kufanya kila juhudi kuwatenganisha majambazi sugu na wale waliofungwa kwa makosa madogo ndani ya Magereza kuepusha kurithishana tabia za uhalifu na baadaye kuiletea jamii usumbufu baada ya wafungwa hao kumaliza kutumikia vifungo vyao.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho lakini la muhimu sana, ninaishauri Wizara kuunda *Research Unit* itakayojumuisha wataalamu wa *Socialogy, politics, economy*, dini mbali mbali na kadhalika. *Research Unit* hii iwe inafanya kazi ya kutafiti mambo mbali mbali kama uhalifu ndani ya Magereza, tatizo la rushwa kwa watendaji, namna ya kuboresha utendaji ndani ya Taasisi za Wizara hii na kadhalika. Kwa kufanya hivyo itakuwa ni kazi nyepesi kwa Wizara kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, kama tunavyoona, humu Bungeni na nje ya Bunge kuwa pamoja na ukweli kwamba polisi hawana kabisa na wala hawapaswi kuwa na uanachama wa chama cha siasa au kukishabikia chama chochote cha siasa hata kama kimoja wapo kiko madarakani, bado Chama Tawala wanaonekana kujikomba sana kwa polisi.

Wapinzani tukiwemo sisi wa *CUF*, tunaliona jeshi la polisi kama chombo cha wananchi wote kinachopaswa kufanya kazi zao kwa kufuata sheria na kuheshimu maadili ya kazi zao kwa maslahi na usalama wa nchi yetu. Wenzetu wa Chama Cha Mapinduzi wanalitegemea jeshi la polisi kama chombo cha kuwahami waweze kudumu katika madaraka. Katika kuitegemea kwao polisi huwa wanachoma picha kuwa wapinzani hawana imani na jeshi hili na kuwatisha kuwa wapinzani wakipata Serikali watawafukuza kazi askari.

Mheshimiwa Spika, tusingekuwa na wasiwasi wowote sisi Wapinzani kama jeshi la polisi lenyewe hawaibebi CCM katika chaguzi hapa nchini. Mifano ipo mingi, uvurugaji wa mikutano ya wapinzani (*CUF*) mwaka 1995 wakati wa maandalizi ya Mkutano wa hadhara wa kampeni ya uchaguzi pale Mkoani Pemba askari polisi walifika katika uwanja wa mkutano halali uliopata kibali cha polisi pamoja na kupitishwa ratiba yake kwenye Tume ya Uchaguzi na kutoa amri ya kuwatawanya wananchi waliokwisha kuwepo uwanjani. Wananchi walishangazwa sana na amri hio na kwa kweli hawakuamini masikio yao.

Mheshimiwa Spika, wananchi walikataa kutii amri hiyo na wakaendelea kubaki na wengine kuongezeka. Baada ya muda askari polisi wakawa wamejitayarisha kivita wakiwa na mabomu ya kutoa machozi, bunduki mpaka za rashasha, virungu na kadhalika.

**MHE. RAMADHANI NYONJE PANDU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa asilimia mia moja na naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote watuunge mkono na waipitishe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua nini haki ya mtu aliyewekwa mahabusu katika kituo cha polisi. Baadhi ya vituo vya Polisi Zanzibar nahisi haviwatendei haki watuhumiwa waliowekwa chini ya ulinzi (mahabusu). Mahabusu wananyimwa chakula na kuwekwa na njaa hata kama chakula hicho kimetoka kwa familia zao. Tarehe 22 Aprili, 2004 mtoto wa miaka 14 (kijana wa kiume) aliwekwa mahabusu kituo cha Polisi Paje na hakupewa chakula kwa siku nzima (saa 24).

Mheshimiwa Spika, ni sheria gani ya nchi inayompa uwezo au haki ya askari polisi anapomkamata mtuhumiwa wa kosa lolote kumhoji au kuchukua maelezo mbele ya mlalamikaji nyumbani kwake kujieleza anapokuwa na kosa mbele ya vituo vya polisi. Kwa nini askari wa Kituo cha Polisi Paje wanatumia nafasi yao ya kazi kwa kufuata maelekezo ya watu binafsi (raia).

Tendo hili Mheshimiwa Waziri limetendeka. Askari wa Paje walielekezwa na Bi Naila Jidawi wamkamata mtuhumiwa mmoja (fulani) halafu wampeleke kwake akahojiwe na kuchukuliwa maelezo. Huu ndio utaratibu wa jeshi la Polisi au ni mpango wa kujitafutia chochote kutoka kwa mwekezaji huyo?

Mheshimiwa Spika, askari anapofariki muda gani familia yake inapaswa kusubiri malipo ya marehemu (mirathi). Mheshimiwa Waziri, askari CPL Hassan Vuai, alifariki kwa ajali ya gari Morogoro wakati akitoka kazini mwaka 2001 hadi leo bado familia ya marehemu haijalipwa kiasi cha kwamba familia yake imefuatilia malipo hayo hadi sasa wamechoka na kukata tamaa.

Kuhusu ajira za polisi, naomba pamoja na sita zilizohitajika katika uajiri wa Polisi suala la cheti cha kumaliza skuli (*national certificate*) lizingatiwe lakini kwa sababu vyeti vinachelewa kutoka kiasi cha kwamba inafika mwaka mmoja vyeti havijapatikana, basi nashauri *statement of results* zichukuliwe kuwa ni uthibitisho mahsusi na mtu kama akifanikiwa katika *interview* basi ukosefu wa *national certificate* isiwe kikwazo kikubwa na ikawa ndio sababu ya kutokuwaajiri vijana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa katika uajiri wa polisi ipo ni vyema polisi hasa Makamanda wakawa waadilifu mno katika suala la uajiri kwani kuna malalamiko vijana wengi huombwa chochote au huambiwa njoo baadae unione mimi saa fulani.

Mheshimiwa Spika, kipimo cha urefu katika uajiri ni muhimu lakini ni lazima kuwe na upendeleo maalum wa hata kama mtu atapungua nchi moja basi naomba isichukuliwe kuwa ni sababu ya kukosa ajira.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuongoza Bajeti kidogo kwa lengo la kunyanyua hali za askari kiuwezo wa kazi na kimapato.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kweli ni tulivu na ipo amani lakini ndani ya nyoyo za watu ipo hofu juu ya vitendo ingawa siyo vingi lakini vipo ambapo askari hutumia mwanya wa kutuliza ghasia baadhi ya nyakati na kutumia nguvu za ziada ambazo huwaumiza sana raia. Hali hii hujenga chuki za ndani kati ya raia na askari. Hivyo basi ni bora maelekezo yatolewe zaidi na zaidi juu ya wajibu wa polisi kwa raia, ambao ni kuwalinda na siyo kuwaumiza.

Mheshimiwa Spika, katika suala la uajiri wa askari lipo tatizo la wale askari wanaotia mkataba maalum mfano miaka 12 hawa wanapomaliza muda hudhalilika sana. Kwani hupata kiinua mgongo kidogo sana na hawapati pensheni. Hali hii huwafanya wakaribie kuwa omba omba na wale wanaoamua kusaini mkataba mrefu wao hupata kiinua mgongo kikubwa na pia hupokea pensheni nzuri. Ushauri wangu ni kuwa masuala haya yaangaliwe upya ili makundi haya mawili ya waajiriwa wa Polisi waache kazi na wasitirike wote katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, suala la mahabusu magerezani bado ni tatizo kubwa ambalo msingi wake mkubwa ni tabia ya askari wa upelelezi kutoa hoja ya kutokamilisha kwa lushahidi hata kwa makosa madogo tu. Hali hii inaitia gharama Serikali kwa kuwahudumia mahabusu na pia inasababisha msongamano wa watu magerezani usio kuwa wa lazima. Nashauri uwepo mpango wa kutenga muda maalum wa kukamilisha ushahidi wa makosa mbalimbali ili kuongeza uwajibikaji kwa askari wetu wa upelelezi.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa askari, mara nyingi wanakuwa na hamasa katika kukabiliana na matatizo mbalimbali hali ambayo huwafanya watoe amri za kukamatwa watu ovyo na kuswekwa mahabusu pasipo hatia. Nashauri Makamanda wetu wawe na uvumilivu mbele ya matatizo ili kupunguza uonevu wa raia na lawama kwa jeshi letu la polisi.

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi kabla sijachangia mada hii nitoe pole kwa familia na wananchi kwa ujumla wa jimbo la Mbeya Vijijini, kwa msiba wa Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, kilichotokea 24 Juni, 2004 Mwenyezi Mungu ailaze roho yake peponi, *amin*.

Kwanza, kabla ya kuchangia mada hii naona nisisahau kuwapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri wa Wizara hii na Katibu Mkuu na Maofisa wote wa Wizara hii pia nisisahau kuwapongeza *IGP* na Makamishna wote wa polisi kwa utaratibu mzuri wa kuliongoza Jeshi la Polisi na kufanikiwa vizuri katika kazi zao na pia kwa uamuzi mzuri wa kuwapandisha vyeo maaskari wa zamani ambao walikuwa wamesahauliwa katika utaratibu wa vyeo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusu Uhamiaji ukurasa wa 43. Kifungu 78 utowaji wa *passport*. Napenda kueleza na kuwakanya vijana wetu ambao ni raia wema tu kutokana na tatizo la maisha waliondoka hapa nchini kwa kutumia mbinu za kuzamia meli sio kama walitaka kufanya hivyo kwa raha lakini ni tabu ya maisha, vijana hao wako nje ya nchi na wanaleta misaada kwa



familia zao lakini wanashindwa kuingia nchini kwa sababu hawana *passport* za Tanzania na wanaipenda nchi yao. Je, hatuoni busara ya kutaka kuwafanyia mpango wa kuwapatia *passport* za nchi hii kwa kutumia Ofisi zao za ubalozi kwa wale wenye tabia na maadili mema kama raia wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la pensheni na kiinua mgongo ukweli ni kwamba jambo hili tumelisemea sana lakini jibu lake ni kwamba, sheria iliyopo inakidhi na inafaa sana lakini wahusika ambao ni askari polisi wanaokuwa wako karibu kustaafu wana maoni kuwa yana maana tena imepitwa na wakati na tunahisi hii ni kweli, wazo langu nakuomba kwamba uweke mikutano na askari polisi kwa ujumla na upate mawazo yao, pamoja na kuwa kuna utaratibu wa kuulizana askari anapofikia umri wa miaka 12 ya kazi, sheria hii inawafanya wapate malipo madogo mno, kwa hiyo, napendekeza, tunaomba sheria ibadilishwe askari wote wakifikia umri wa miaka 21 ya kazi waingie mojakwa moja kwenye mpango wa pensheni.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie makazi ya askari polisi ukweli Wizara imejitahidi kujenga nyumba lakini naomba watilie mkazo nyumba za askari waliopo kwenye makao ya mkoa kwa mfano Mkoa wa Kaskazini Unguja hapo Mkokotoni kituo hicho ni makao makuu ya mkoa, haina majengo yanayoweza kukidhi makazi ya askari wa mkoa huo pia kuna jengo la hapo Polisi Ufundi Dar es Salaam jengo la polisi halifai kukaa askari wanaweza kupata ajali ya kuangukiwa na jengo hilo wakati wowote, jengo hilo lote nusu yake limeshaanguka na linahatarisha maisha ya askari na familia zao na pia ipo mifano mingi ya mikono tofauti.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichangie vitendea kazi kwa askari polisi, ukweli ni kwamba wana upungufu mkubwa wa magari, polisi na vifaa vinginevyo, una upungufu mkubwa sana pia wa mafuta wanayotengewa ni machache mno hayakidhi haja hasa kwa vikosi vya *FFU* Ziwani Zanzibar ambapo kikosi hiyo kicho kinahudumia na Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa askari viongozi na pia wana kazi zao za kawaida za ulinzi, kuna vurugu ambazo hutokea wakati wowote ambazo hazimo ndani ya mpango hasa ikikaribia wakati wa kampeni za uchaguzi. Kwa hiyo, tunaomba wafikiriwe hali ya matumizi ya mafuta na huduma nyingine ili hali ya utendaji wao uzidi kuboreka zaidi

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuchangia hali ya malipo ya askari polisi ambao wamepandishwa vyeo lakini hawalipwi malipo mapya naomba hali hii irekebishwe na pia wakilipwa walipwe na malipo yaliyoanzia kuanzia muda walipopandishwa cheo, pia posho zao huwa hawalipwi kikamilifu, hili nalo litiliwe maanani.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie utendaji wa kazi za polisi pamoja na kuwa yapo mambo mazuri waliyoyatenda lakini kuna baadhi ya vitendo ni vya kuonyesha uzembe mno, kuna hali ya kuharibika kwa hali ya kisiasa, kuna baadhi ya raia wasiokuwa wema walikuwa wana mtindo wa kutega mabomu iko siku limegundulika bomu huko Kisiwani Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja, raia wema wametoa taarifa kituo cha Mkokotoni, matokeo yake askari kwa wakati ule hawakwenda na ilipofika muda walipofuatwa tena waliwajibu raia hao kuwa waende wakahakikishe kuwa kweli hilo ni bomu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama kuna mashaka huweza ukamwambia raia kuwa nenda ukahakikishe kama kweli ni bomu, inaonekana askari kiti yao kuna baadhi waoga wa kazi yao, ni kitendo cha aibu, hali hii imeshawahi kutokea pia ilikutwa silaha huko Kisiwani Tumbatu. Naomba tutupie macho sana baadhi ya maeneo kama haya ambayo yameonyesha dalili mbaya.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze na mchango wangu kwa kuunga hoja mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, imekaa vizuri, ombi langu ni matatizo ya mishahara kwa askari, nyumba za watumishi kama katika kambi za Mikumi, kituo cha Polisi na nyumba zao, ni mbaya sana, zinahitaji ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yangu ya Mikumi nina upungufu wa askari katika kituo cha Mikumi na Kituo cha Ruembe.

Mheshimiwa Spika, tuliomba toka mwaka 2003 kupata askari na kufungua kituo kipya. Katika Kata ya Malolo niliomba mabati 100 na Wizara ione uwezekano wa kuwezesha mpango huo wa kufungua kituo Malolo na ikawezeka kwa sababu kuna mradi mkubwa sana wa umwagiiaji.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kujibiwa barua yangu ya kuomba gari ya kuwasaidia kupambana na majambazi wa maeneo ya Kata ya Kidodi Ruaha, Mikumi. Naomba nikumbushe katika mchango wangu, barua yenye *Kumb. Na. MHA/BG/DOM/NW/17* imeonyesha matumaini.

Mheshimiwa Spika, naomba ikiwezekana nijibiwe katika hoja hii ya Wizara, tunayojadili. Barua nimepokea na nimeshukuru sana kujibiwa. Sasa ombi utekelezaji bado. Naamini nitapata jibu zuri. Ahsante.

**MHE. JUMANNE H. NGULI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Nawapongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo naomba nichangie katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ulinzi wa raia na mali zao. Pamoja na kazi nzuri mnayofanya tafadhali juhudi zaidi ifanyike ili kugundua mbinu zinazotumiwa na majambazi na vibaka katika ujambazi na wizi. Matukio mengi ya ujambazi na wizi mdogo mdogo katika miji na vijiji hali si shwari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira, nashukuru sana kuwa jeshi la polisi, liliajiri vijana 2,000. Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuajiri vijana toka Jeshi la Kujenga Taifa, mimi naona kuwa uwiano wa vijana kutoka kila Mkoa utazingatiwaje? Nafasi hizi zilikuwa zinapelekwa Mikoani kwa uwiano. Hii angalau ilikuwa inatoa uwakilishi wa makabila katika mikoa mbalimbali ambayo inaleta jeshi la sura ya Kitaifa. Naomba nipate maelezo jinsi gani tutakuwa na uwiano.

Mheshimiwa Spika, polisi wachache wanaoibisha jeshi. Tarehe 4 Oktoba, 2001 usiku wa kuamkia 5 Oktoba, 2001, Daudi Isack Mtinda mkazi wa Unyankindi, Singida Mjini alivamiwa na polisi wawili wenye silaha nyumbani kwake akiwa amelala na mke wake. Polisi hawa walipiga mlango na kuingia ndani ghafla, walimtoa kitandani akiwa uchi na kuanza kumpiga. Mke wake alipiga kelele pamoja naye mpaka mke wake (mama yake) akatoka na kuja kumwoko. Mama alimwangukia mtoto wake aliyekuwa uchi ili amwokoe na kipigo cha polisi. Baada ya hapo kijana huyo kwa mfadhaiko baada ya kuachiwa alitoka nje mbio kumbe na askari nao walitoka nje, ghafla walifyatua risasi na kumvunja mguu kwa risasi bila huruma.

Mheshimiwa Spika, sababu ya tukio hilo ni huyu kijana kumgombeza mdogo wake wa kike ambaye kumbe alikuwa ni rafiki wa mmoja ya askari hao. Msichana huyo alikuwa anamwingiza askari huyo bila heshima na kumlaza kwao. Askari hao baadaye ilifahamika kuwa walitoroka na silaha na kwenda kutekeleza matakwa yao hayo. Lakini linalonitia tabu ni wale askari kutochukuliwa hatua, pili, kijana Daudi bila kutendewa haki kwa kutibiwa na kupewa fidia. Kijana huyu walimsihi asishitaki na akakubali lakini baadaye kaachwa bila huduma. Kwanza haki za binadamu zimevunjwa kwa kijana huyu. Kama ana makosa kwa nini pia hakushtakiwa?

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya taarifa hii kumpatia Naibu Waziri, sasa ni mwaka mmoja nataka kujua, askari hao kwa nini hawajafukuzwa kazi na kushtakiwa? Huyu bwana atibiwe na mpaka sasa mguu wake umepinda na unahitaji *operation* tena. Sitishii kutoa shilingi lakini bila kupata majibu mazuri itanibidi nisumbue sana. Ahsante sana.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote katika vitengo vyote vya Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya Wizara na utekelezaji wa kufana kwa miaka iliyopita. Kwa sababu hiyo, naunga mkono hoja iliyoletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri na maombi mbalimbali hasa kwa Mikoa ya mipakani hususan Wilaya za mipaka ya Magharibi ya Taifa letu. Ngara, Aprili, 2004 Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama ya Bunge ilitembelea Mkoa wa Kagera. Ilipofika Ngara ilipewa taarifa ya ulinzi na usalama na ilizunguka Wilaya nzima, magereza, vituo vya polisi na uhamiaji. Kamati ilijionea, baada ya kusikia, matatizo ya

wakimbizi kwa miaka kumi na moja sasa ya wizi, mauaji, utekaji nyara magari, uharibifu wa mazingira, uuaji wa wanyamapori hakika mapori ya Akila na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia ilitambua upungufu wa askari polisi kukabiliana na hali yenyewe licha ya ukosefu na siyo upungufu wa vyombo vya usafiri. Ushuhuda huu anao Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maana ndiye alikuwa kiongozi. Naomba sasa kwa niaba ya uongozi wa Wilaya kilio cha wakazi wa Ngara hufanyiwa yafuatayo:-

Kwanza, tupewe usafiri wa magari kwa vituo vya Rulenge ambacho ni kituo cha pili kwa ukubwa cha Wilaya, Kabanga, Murusagamba, Kasulo na Mugoma ili kukabili ujambazi ambao unafanyika katika maeneo yote hasa ya misitu, mapori ya Tarafa za Rulenge na Marusagamba zenye Kata 7, vijiji 28 bila usafiri wowote.

Mheshimiwa Spika, pili, Makao Makuu ya Wilaya, *OCD* hana usafiri, *Landrover* iliyopo imezeeka na mbovu sana. Mara nyingi hutumia muda mrefu kufuata matukio maana hakuna magari magumu ya kuendesha hapa Wilayani.

Tatu, kujenga nyumba za polisi katika vitu vya Kasulo na Magoma. Hizi ni sehemu nyeti mipakani, njia kuu za kwenda Rwanda, Burundi na *DRC* ni vituo vya zamani. Wizara itoe *generators* Murusagamba, Rulenge, Kabanga ni sehemu zinazopata wageni wengi kila saa, mipakani na njia kuu kwa mataifa na wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali iongeze juhudi, wakimbizi warudi kwao mapema ili wananchi wapumue na kutulia kujijengea maendeleo kama Wilaya nyingine nchini. Magereza yamejaa, hasa wakimbizi. Wengi wao huwatupa mashahidi baada ya wenzao na wengineo kutoroka, kurudi makwao na hata kufa. Waondolewe magerezani na kukabidhiwa nchini kwao. Serikali inaingia hasara kubwa kuwatunza.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri azionee huruma Wilaya za Ngara, Karagwe, Biharamulo, Kibondo, Kasulu na Kigoma kuhusu usafiri kwa kuwa kwa mwaka wa 2004/2005 Wizara itanunua magari 174 kumbuka katika Ibara ya 35 (vii) Wilaya za umuhimu wa kwanza ziwe hizo zilizo katika matatizo ya kuvunjika amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhamiaji, kitengo hiki kina matatizo mengi hasa pale Maafisa wake wanapokuwa hawawashirikishi wakazi na viongozi katika kuwabaini wahamiaji haramu. Pia watendaji wawe katika vituo kwa muda usio mrefu sana ili kusiwe na nafasi za wao na kuingizwa katika vishawishi.

Mheshimiwa Spika, kwa siku na miaka ya hivi karibuni kumejitokeza mahusiano kazini yanayochanganya kati ya Mahakama na Polisi. Mara nyingine hutokea kubishana kwa ukali badala ya kubishia sheria mahakamani na umma wa sasa uliojaa wasomi na hata wanasheria wasio wazi kila mahali wakashangaa. Kuna hoja ya kuangalia hayo maana anayehujumiwa katika hali hiyo huwa ni mlalamikaji au mlalamikiwa kutokea kwa maelewano ya watafasiri wa sheria.

Mheshimiwa Spika, nyumba za askari wetu wa polisi na magereza ni chache. Kubwa zaidi ni ndogo sana kukidhi matakwa ya *occupants*. Imefikia nafasi askari wanaishi bila viti wala meza nyumbani mwao. Mengine ni ya kijamaa pale watumishi wanapokuwa na familia kubwa zenye watoto wenye umri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina umuhimu wa kulinda raia, mali zao, kusimamia amani na utulivu hautatekelezwa bila mazingira yanayofaa. Hivyo inabidi Serikali itoe haki kujenga wajibu wa jeshi la polisi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja tena.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Nampongeza DC kwa kazi nzuri sana na ngumu anayoifanya katika makabiliano na vitendo mbalimbali vya uhalifu hapa nchini. Kutokana na upelelezi huo ndio umewezesha kupatikana kwa fedha zilizoibiwa kule Moshi. Naomba asaidiwe kupata vifaa vya kisasa ili kazi yake iwe rahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hapa nakuambatishia tarehe zilizotokea utekaji wa magari kama kiambatisho kinachojieleza. Naomba maeneo hayo yapate magari, Kanena, Ikola, Mtowisa, Kasaza, Kipili na kadhalika ili iwe rahisi kupambana na watekaji hao. Aidha, wapewe pia vifaa vya kisasa vya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kuna matukio ya ujambazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya makosa ya ujambazi yaliyoripotiwa mwambao wa Ziwa Tanganyika kwa mwaka 2000 hadi Mei, 2004. Polisi katika kituo cha Karema matukio yaliyoripotiwa ni 14, watu waloitekwa ni 46, watu waliorudi salama ni 32, watu waliouwawa kwa kupigwa risasi ni 4, watu 10 hawajulikani walipo hadi sasa, mali ziliporwa ni nyavu 11, karabai zaidi ya 4 na bidhaa za dukani mbalimbali. Jumla ya thamani ya mali zote zilizoporwa 87,235,500/=.

Mheshimiwa Spika, matukio yaliripotiwa kama ifuatavyo, tarehe 4 Mei, 2000 majambazi manne, wenye silaha ya *SMG* walipora nyavu moja bila kuuwa, yenye thamani ya shilingi 145,000/= tarehe 4 Mei, 2000 majambazi hao hao nyavu moja na vitu mbalimbali majambazi kwa watu bila kuuwa vyenye thamani ya shilingi 717,000/= tarehe 19 Mei, 2000 majambazi walipora mali za duka bila kuuwa wala kuteka na thamani ya vitu haikujulikana, tarehe 30 Oktoba, 2000 majambazi wenye silaha ya aina ya *SMG* walipora fedha shilingi 66,000/= bila kuuwa tarehe 30 Novemba, 2000 majambazi hao hao walipora shilingi 15,000/= bila kuteka wala kuuwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Machi, 2003 majambazi wasiojulikana idadi yao wakiwa na *SMG* walipora wavu mmoja, karabai 4, kamba za uvuzi nne, vyote vikiwa na thamani ya shilingi 705,000/=, tarehe 7 Machi, 2003 huko Kasangantongwe majambazi yalipora mali za duka na pesa taslimu kiasi cha shilingi 1,536,000/= na kuteka watu watano ambao hadi sasa hawajulikani walipo.

Tarehe 27 Machi, 2003, majambazi hao wakiwa na silaha ya *SMG* walijaribu kuteka boti, waliposhindwa walimua mwanamke mmoja kwa risasi na kumjeruhi mwanamme mmoja na kutoweka. Tarehe 3 Agosti, 2003 majambazi kadhaa walipora mabegi ya nguo, redio moja, mtumbwi mmoja, bila kuteka, wala kuua, vyote vikiwa na thamani ya shilingi 129,000/=, tarehe 16 Desemba, 2003, majambazi wanne wenye silaha ya *SMG* walipora nyavu mbili, mtumbwi mmoja kuteka watu sita na kuua mtu mmoja, mateka watano walirudi salama. Thamani ya mali hizo haikufahamika.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Desemba, 2003, majambazi walipora nyavu moja na vifaa vya nyumbani na mali za dukani vyote vikiwa na thamani ya shilingi 1,500,000/=, watu sita walitekwa na baadaye kurudi (walirudi) wote salama. Tarehe 14 Februari, 2004, huko Rwega Ikola, majambazi wasiofahamika idadi yao walipora wavu mmoja na vifaa mbalimbali, vyote vyenye thamani ya shilingi 1,715,000/= na kuteka watu watano na hadi sasa haifahamiki walipo.

Tarehe 1 Machi, 2004 majambazi wasiofahamika idadi yao walipora nyavu mbili, mitumbwi miwili, vyote vikiwa na thamani ya shilingi 1,500,000 na kuteka watu 11 na kuua mmoja kati ya mateka hao walirudi 10 wakiwa salama. Tarehe 11 Mei, 2004, majambazi watano yenye silaha ya *SMG 2* walipora nyavu mbili na bidhaa zenye thamani mbalimbali zenye thamani ya shilingi 600,000/= na kuteka watu 12 na kumuua mmoja kati ya hao 12 na kurudi mateka 11 salama. Baada ya kuokolewa na askari wa JWTZ, Polisi, pamoja na wananchi na kufanikiwa kuuawa kwa hayo majambazi manne na kukamata silaha za *SMG* zikiwa na *magazine* nne bila risasi.

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo kwa kusema pia Kituo cha Polisi cha Longalombego ambacho kilikuwa kinajengwa kwa nguvu za wananchi lakini kilikwama. Je, Serikali itaweka bajeti ili tumalize ujenzi huo? Askari hawa wanasaidia pia kuzuia wizi wa Mifugo.

Je, katika magereza yetu wafungwa ni wangapi? Mahabusu ni wangapi? Je, gereza la Bariadi lina eneo kiasi gani? Mradi wa kupanda miti uhamishwe uende gereza la Matongo, ndilo gereza la Wilaya. Upinzani siyo kuvunja sheria au kuwa juu ya Sheria za nchi. Kesi za nyara za Serikali zisikilizwe na Mahakimu wa Mahakama za Wilaya, isilazimu Mahakama Kuu.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Kwanza naomba nitoe pongezi kwa Wizara hii kwa kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara hii, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa jeshi la polisi ningependa kuwapongeza kwa jinsi wanavyopambana na uhalifu hasa ujambazi wa kutumia silaha. Kazi hii inahitaji ujuzi, uzoefu na ujasiri mkubwa. Majambazi wanaiba fedha nyingi kwenye mabengi na sehemu zingine. Lakini wanajikuta wanakamatwa, fedha nyingi sana zinakamatwa, mali wanazonunua za gharama kubwa zinakamatwa na kadhalika. Majambazi wanakatishwa tamaa na ujasiri huu wa jeshi la Polisi. Wakikimbilia nchi jirani wanakamatwa. Safi sana.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuzagaa silaha nchini linahitaji juhudi za ziada kwa jeshi la polisi, Serikali kwa ujumla na wananchi. Silaha hizi zinahatarisha kweli usalama na amani ya wananchi. Pamoja na kuongeza ajira ya askari, mgambo na kadhalika ni muhimu sana kuwa na fungu kubwa la fedha za kuwalipa *informers*. Wananchi wanawajua majambazi wanaohodhi silaha mijini na vijijini. Wananchi wakijua kuwa wakitoa taarifa kwa kiwango fulani wananufaika watawaumbua majambazi hao karibu wote.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulisisitiza sana ni kuongeza upana na kina cha mafunzo ya jeshi la polisi katika zama hizi za utandawazi, mafunzo ya mbinu za mapambano lazima daima ziwe *upgraded* kwa kiwango cha Kimataifa. Mafunzo yaongezwe pia katika taaluma ya upelelezi (*CID*). Sasa hivi maarifa ya wizi wa kalamu kwa kutumia taaluma ya *Information and Communication Technology (ICT)* ambayo ni *highly advanced*, yameongezeka sana.

Kuhusu uhalifu wa Kimataifa wa mihadarati (*Drug Trafficking*) unazidi kuongezeka kwa viwango vya kutisha. Vile vile tatizo la *money laundering* limezidi kuwa kubwa sana. Hivyo Idara ya Upelelezi chini ya *DCI* inatakiwa uzidi kuajiri wasomi wa taaluma mbalimbali na kuwafunza taaluma ya upelelezi kwa kiwango cha kimataifa. Mafunzo ya aina hii yawe ni ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kupambana na uhalifu ni lazima pia kuimarisha taaluma ya kuendesha mashitaka Mahakamani (*Prosecution*). Pamoja na kwamba kuna Idara ya *DPP* katika Ofisi ya Mwanasheria Mku wa Serikali, lakini kesi zilizo nyingi sana zitaendelea kuendeshwa Mahakamani na *Police Public Prosecutors*. Hawa *PPs* hata kama hawana shahada za sheria ni muhimu sana kujua namna bora na ifaayo ya kuendesha mashtaka Mahakamani. *PP* ajue kweli namna ya kubaini *Primafaci'e case* ni nini, ajue namna ya ku-*plan* kesi yake, ajue namna ya kumwongoza shahidi wake kutoa ushahidi (*Examination in chief*), ajue kweli namna ya kuvunja ushahidi wa uwongo wa utetezi (*the art of cross examination*) pamoja na *re-examination*.

Mheshimiwa Spika, Mawakili wa utetezi (*Advocates*) wanazidi kuongezeka. Hivyo *PPs* vile vile wajue namna bora ya kuandaa na kuwasilisha Mahakamani *Submissions* za kesi zao. *PPs* wa aina hii wawe wengi iwezekanavyo ili waweze kupangwa *workload* ya kesi nyingi za jinai.

Mheshimiwa Spika, jeshi la magereza linafanya kazi nzuri sana yenye maadili yafaayo (*Professionalism*). Lakini matatizo yaliyoko ndani ya Magereza yamevukia sana viwango vya uwezo uliopo wa jeshi la Magereza. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imetoa taarifa ambayo tunahitaji uamuzi mzito wa Kitaifa kutafuta namna ya kuongeza uwezo wa jeshi la Magereza ku-*handle* hali iliyopo. Ni muhimu sana tutenge fedha nyingi sana kujenga magereza mengi iwezekanavyo. Hii itatuwezesha kupunguza tatizo kubwa la wafungwa na mahabusu kujaa magerezani (*congestion*).

Mheshimiwa Spika, njia nyingine ya kuongeza magereza ni kujenga magereza ya kilimo. Tutumie uwezo wa kilimo cha umwagiliaji na mifugo. Faida inayopatikana ibakie ndani ya magereza ili kuwa na *revolving fund* ya kujiimarisha kwa vifaa vya kilimo na kufungua magereza mengine.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Mkuu wa Polisi, Mheshimiwa Omari Mahita na uongozi wote wa polisi na Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo nianze kwa kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu usalama barabarani. Kwa kuwa kitengo hicho kinalalamikiwa mara kwa mara na wananchi walio wengi, suala zima la rushwa ni vema Serikali ikaunda sheria mpya itakayowawezesha askari wa usalama barabarani kuwatia hatiani wale wote wanaovunja sheria kwa kuzidisha idadi ya abiria kwenye basi au chombo chochote cha usafiri, hususan raia wenyewe. Kujaza abiria kupita kiasi kumesababisha ajali, kwa mfano, magari yanayokwenda minadani au wale wanaopakia abiria kwenye magari ya mizigo na kadhalika.

Kwa sheria hiyo pia itawezesha kukamatwa kwa wale wanaoruhusu wanafunzi kusimamishwa kwenye daladala kwa kuwatoza karibuni wote wanaosimamama ikiwezekana kwenda Mahakamani kwani mara nyingi wanaokufa kwenye ajali ni wale wanaosimama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi, kuna majengo mengi ya Polisi na Magereza, ni ya zaidi ya miaka 40 ni vema kabla ya ujenzi mpya zikakarabatiwa hizo zilizopo ili ujenzi mwingine ujengwe kwa awamu. Kwa kuwa Magereza wana kazi ngumu pia ni vema Idara hii iangaliwe upya kama Idara zingine za Wizara hii, kwani wafungwa wanaowahudumia ni watu wahalifu wa makosa mbalimbali yakiwemo ya mauaji, pia wapewe vifaa na nyenzo za uhakiki ili kukabiliana nao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahabusu, kwa kuwa Wilaya ya Igunga haina jengo la mahabusu na kusababisha usumbufu kwa watuhumiwa kuchukuliwa kutoka Nzega kuja kusikiliza kesi Igunga na kurudishwa Nzega na wakati mwingine kusababisha kubaki Igunga kwa kukosa usafiri, je, Serikali ina mpango gani na ina makusudi kuhakikisha kwamba jengo hili linakamilika mwaka huu 2004/2005 ili kutoa haki za kibinadamu kwa wananchi hao, ambao wanateseka kwa kuweka *lock up* ambayo ilistahili kukaa kwa muda wa zaidi ya siku mbili. Pamoja na hayo hata usafiri nina uhakika hakuna, mara kwa mara gari bovu au waombe kwa watu wenye magari.



**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwa kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yao nzuri ya bajeti yenye kuchambua nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kuchangia kwa kuipongeza Serikali na kwa kuipongeza Bajeti ya Wizara hii kwa sababu ni Wizara yenye majukumu mazito sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulipongeza jeshi la Polisi Zanzibar kwa kuwakamata watu 29 kufuatia ghasia zilizosababishwa na maandamano haramu Zanzibar. Ningeomba Serikali ya Zanzibar wafanye uchunguzi wa hali ya juu na ikithibitika wapewe adhabu inayofaa.

Nimefurahishwa na kusikia kwamba tumeshapata magari mawili ya Zimamoto kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam lakini ningeomba Serikali ikafanye juhudi kubwa sana iwapatie vyombo kama hivi mikoa mingine pamoja na Zanzibar tukizingatia kwamba ajali hizi zinatokea kila mahali.

Mheshimiwa Spika, lingine la kusikitisha sana ukizingatia kazi ngumu walizonazo askari wetu na kuwa hawana usafiri hata *Vespa* katika vituo vyao, naiomba Serikali iwaone askari wetu hawa kwa jicho la huruma angalau kwa gari japo moja kwa kila kituo, vinginevyo watakuwa kwenye hali ngumu hasa ukizingatia mwaka kesho wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongelee kuhusu mafao ya askari wetu, mimi naomba niungane na wenzangu kusema kwamba wasicheleweshewe sana mafao yao ukizingatia kwamba askari atakapokuwa nje ni sawa na kuwa kwenye mapumziko, anastahili kuwa na maisha mazuri kama atabakia kama raia si kutukuzwa sana kwa sababu atakuwa ameitumikia Serikali yetu sana ni vema kumuacha kwenye hali iliyokuwa hairidhishi.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie kuhusu usalama wa barabara, kwa kweli kama ilivyozungumzwa kwenye kitabu hiki kuwa ajali za barabarani ni nyingi sana hii inasababishwa na uendeshaji wa madreva hawafuati alama za barabarani vizuri na nyembamba wanavyojitakia wao wenyewe wanavyotaka tu kwa hiyo, ningeomba askari wa barabarani wasilifumbie macho na walichukulie hatua za kufaa kama iwezekanavyo ili zipungue ajali hizi nyingi za barabarani.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Waziri ambayo imegusa sehemu zote zinazohusu usalama wa raia na mali zao. Pili, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Mkuu wa Jeshi la Polisi (*IGP*) kwa kazi ngumu wanazofanya katika mazingira magumu ya ufinyu wa Bajeti na vifaa vichache.

Mheshimiwa Spika, tatu, pamoja na hali hiyo, naomba kumpongeza *IGP* kwa kuhakikisha kuwa Mkoa wa Manyara unapata *RPC* na kujenga nyumba 3 za maofisa wa Mkoa, Mjini Babati na sasa maandalizi ya Ofisi ya *RPC*. Hata hivyo, hali ya Wizara ni tofauti kwani *OCD* hadi sasa anaishi kwenye nyumba iliyoachwa na *DC*, hivyo sioni kwa nini Serikali ijenge nyumba ya *DC* na ile ambayo haimfai apewe *OCD* badala ya kujenga na nyumba ya *OCD*. Nashauri kuwa *OCD* wa Wilaya ya Babati ajengewe nyumba ya hadhi yake. Nitaomba kupata maelezo kuhusu ushauri huu.

Nne, mara zote nilipochangia Wizara hii nimekuwa nikiomba Wizara hii itoe gari la Polisi kwa kituo cha Magugu, Babati ambacho kinahudumia maeneo yenye ujambazi, mauaji na wizi wa mifugo na nina hakika Makao Makuu ya Polisi inazo taarifa za kutosha kuhusu ujambazi na wizi unaofanyika mara nyingi maeneo ya Mbugwe na Mdori karibu kabisa na Kituo kidogo cha Minjingu ambacho hakina uwezo wowote wa doria.

Aidha, nimekuwa nikieleza umuhimu wa kuimarisha kituo hiki cha Minjingu. Nitapenda kupata maelezo ya maombi haya ya gari kwa kituo cha Magugu na uimarishaji wa ulinzi na usalama katika maeneo hayo. Pamoja na Wilaya kuwa na gari bovu la *OCD* kwa muda mrefu na *OCD* kutembea kwa miguu na wakati mwingine kuwa omba omba kwa ajili ya kuhudumia matukio mengi ya Wilaya, naomba sasa *OCD* wa Babati apatiwe gari jipya na Idara ya *CID* nayo ipatiwe gari kwa kuzingatia kuwa Babati sasa ni Makao Makuu ya Mkoa na imepewa hadhi ya Halmashauri ya Mji, (*Referununuzi* wa magari 174 katika hotuba, ukurasa 19).

Mheshimiwa Spika, tano, mara nyingi nimefuatilia sana ufunguzi wa kituo cha Polisi cha Gallapo baada ya wananchi kukarabati sehemu ya majengo yanayohitajika. Naomba kufahamu ni nini kimebaki kwa ajili ya ufunguzi wa kituo hicho cha Gallapo ambacho ni makao makuu ya wananchi wa eneo hilo kwa miaka mingi? Nitapenda kupata maelezo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ifanye maandalizi ya kupanua gereza la Babati na ianze utaratibu wa kujenga gereza la Mkoa. Nakutaia kazi njema na kama nilivyoshauri nitaomba kupata maelezo ya ushauri wangu.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu pamoja na Watendaji kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuhimili usalama wa raia na mali zao. Ninasema wanajitahidi mno licha ya mazingira yetu ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na kwa jinsi ya pekee *IGP* Ndugu Omar Mahita, kwa kuunga mkono juhudi za wananchi wa Same katika ujenzi wa kituo cha Polisi cha kisasa Wilayani Same. Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Same nashukuru mno. Napenda pia niwashukuru kwa Wizara kukubali kutuchimbia kisima cha maji cha Same. Mwaka 2003 nilipotembelea pale shida ya maji ilikuwa inaashiria mlipuko wa magonjwa kwa wafungwa na askari. Miundombinu ya maji taka pia ni mibovu na maji taka yamesambaa kuzunguka gereza la Same. Pamoja na kushukuru na kupongeza viongozi kwa juhudi zao nzuri, naomba sasa

ili kazi yao hii ya kituo cha polisi cha kisasa na msaada wa maji kwa gereza na kuonekana imefaulu (*impact*) mambo matatu yafanyike:-

- (a) Askari wajengewe nyumba za kuishi za kisasa pia;
- (b) Idadi ya askari ya Same haikidhi mahitaji hasa Idara ya Upelelezi, nimelisemea kila mwaka halipati majibu; na
- (c) Miundombinu ya maji ikamilishwe. Kisima kilichochimbwa bado hakijakamilika. Kikamilishwe na kujengewa tanki la kuhifadhi maji kwa ajili ya askari Polisi na Magereza, pia na mahitaji ya wafungwa na kukarabati mifumo ya maji taka katika gereza la Same.

Jambo la tatu nataka nichangie kuhusu mazingira ya kazi ya askari ya nyumba za kuishi, afya zao, na majengo ya Ofisi (vituo vya Polisi) pia magari ya kazi kwa askari. Mimi nilipata ajali Oktoba, 2002. Nilipata huduma ya askari Polisi katika kituo cha Polisi cha Kibaha na tiba katika hospitali ya Tumbi, Kibaha. Mazingira ya hospitali ya Tumbi ni mazuri lakini yale ya kituo cha Polisi hayaridhishi, ni mabaya sana.

Kituo hiki kipo katika majengo ya *full suit* ya kuta za bati na paa la bati. Askari nao huishi pia katika majengo hayo ya *full suit* ukifika kituo cha Mkuza nyumba za askari zinasikitisha. Naiomba Serikali ijenge kituo cha Polisi cha kisasa Kibaha ikiwa ni pamoja na nyumba za askari badala ya nyumba za kisasa na askari kuishi uraiani, ujenzi wa kituo kipya Kibaha utaliondolea Taifa letu aibu tunayopata, ajali za barabara zinapotokea katika barabara kuu na kuhusisha wageni wa mataifa mengine. Naiomba Serikali ilianganalie hili sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wa mwisho unahusu matibabu ya askari pale wanapoumia wakiwa kazini. Imetokea askari wanajilipia wenyewe na hawana bima ya matibabu. Hivi ni kwa nini tunawadhalilisha askari wetu? Huduma ya afya kwa askari Polisi tunaiomba iangaliwe iwe na mfumo kama ule wa JWTZ. Je, ni kwa nini jeshi la Polisi halina hospitali kubwa ya jeshi lake kama ilivyo Lugalo kwa JWTZ? Kwa nini huduma ya afya kwa jeshi la Polisi imeishia ngazi ya kituo cha afya cha Kilwa? Hii haikidhi mahitaji ya jeshi letu hili la Polisi.

Mwisho naunga mkono hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kumpongeza.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote napenda kutoa rambirambi zangu kwa wafiwa wote na kuwapa pole wale waliopata ajali wakiwa safarini kuelekea Dodoma katika kazi za shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni sehemu muhimu ya dola yenye majukumu ya kushirikiana na raia kuendeleza amani na utulivu nchini na kuweka mazingira ya kuvutia wawekezaji wa humu nchini na wale wa kutoka nje na wananchi wanaamini hivyo.

Mheshimiwa Spika, dola ni sehemu katika jamii. Ni matumaini kwa wananchi wote inategemewa waletewe na wasimamie kupata haki. Lakini eneo hili likiwa litakimbiwa, badala ya kukimbiliwa heshima ya nchi itapungua kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mazingira wanayoishi askari hawa makambini inatisha hususan kituo kilichopo Mkokotoni na Mahonda, Mkoa wa Kaskazini Unguja ambapo katika Bajeti yako matarajio ya shughuli za Polisi katika mwaka 204/2005 sikuona sehemu yoyote ile ambayo bajeti yako imeeleza kuwa nyumba za Polisi katika vituo nilivyovitaja zitafanyiwa ukarabati au zitajengwa.

Mheshimiwa Spika, utakuta askari polisi anafamilia ya watoto zaidi ya watano na wana rika tofauti. Nyumba anayokaa ina chumba kimoja. Mtu kama huyu tunategemea afanye nini, kama hakufanya kila jitihada ili apate fedha za ziada? Utakuta baadhi ya Polisi walio wengi wanashawishika kuwa na nyumba ndogo kwa sababu kama hizo na polisi wengine kwa sababu hawapati muda wa mazungumzo na mkewe, anakodi nyumba ya kulala wageni au anangoja giza liingie ili aende vichakani na mkewe, ambavyo siyo lengo.

Kwa hiyo, tulilaumu jeshi la Polisi kuwa ndiyo chanzo cha matatizo yote hayo kwa askari wetu watiifu. Suala la nyumba kwa Polisi walioko Mkoa wa Kaskazini Unguja litafutiwe ufumbuzi wa haraka ili vijana hawa waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. Kuna kiwanja kimetengewa makusudi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za polisi kilichopo Mahonda. Je, tatizo ni nini kwani ni zaidi ya miaka 8 sasa hata dalili ya ujenzi haipo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Makamishna na Makamanda wote wa Majeshi ya Polisi, magereza na Uhamiaji.

Napenda kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuimarisha Polisi Korogwe, kwa bahati mbaya Wilaya hiyo imekumbwa na mikasa ya vitendo vya majambazi sana kiasi cha kuitishia maisha ya jamii. Matukio hayo yameongezeka sana kiasi cha kuleta wasiwasi kwamba hivi Polisi wako wapi na wanafanya nini?

Mheshimiwa Spika, Korogwe ni katikati ya Dar es Salaam na Arusha, kuna milango na njia nyingi sana zinazoweza kuwafikisha majambazi Arusha na Dar es Salaam. Kwa hiyo, nashauri kuipatia Korogwe vifaa madhubuti kama vile magari safi na imara, askari wazoefu wa silaha imara. Ujambazi wa kuvamia magari ya abiria pia umezidi sana. Jitihada ya kuwa na doria katika barabara kuu ifanyike mara kwa mara ili

kuwaogopesha majambazi. Kifo cha Katibu Kata wa Mombo, juzi kimesikitisha watu wengi sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kituo cha Polisi Mashewa. Kituo hiki kila mwaka nimekiomba kiboshwe na kipatiwe usafiri na polisi wa kutosha. Lakini hadi leo hii hakuna lolote lililofanyika. Kituo cha Mashewa ni tegemeo la Tarafa ya Magila na Daluni hadi Kalalani kwenye machimbo ya vito vya thamani Kalalani. Kuna makampuni makubwa ya machimbo kama vile *AAPs*. Matukio ya uhalifu ni mengi na Polisi hakuna. Naomba sana wapewe usafiri na polisi waongezwe na kituo kiboshwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upelelezi unachukua muda mrefu sana. Matokeo yake wananchi wanakosa haki zao. Kesi hizo hadi leo hivi kuna Korogwe yupo mzee mmoja wa kijiji cha Maurini ambaye kesi yake imechukua zaidi ya miaka mitano sasa bila kushughulikiwa. Nashauri sana upelelezi uchukue muda mfupi ili kesi zipelekwe Mahakamani mapema. Aidha, naomba yule mzee wa Maurini, Korogwe kama upelelezi umeshindikana Mzee Abdallah aachiliwe huru.

Mheshimiwa Spika, nyumba za askari za Polisi na Magereza, nyumba za askari Korogwe ni aibu tupu. Naomba nyumba zile zikamilishwe na wajengewe mpya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gereza la Kwamngumi. Gereza hili naomba lipatiwe umeme. Ni gereza muhimu la uchumi na tulikwishaomba umeme muda mrefu, ikawepo ahadi lakini hadi leo hii mradi huo haujatekelezwa. Naomba sana mradi huo sasa utekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maslahi ya askari, kwa kuzingatia kazi ngumu ya askari wetu naomba maslahi ya askari yalipwe haraka. Madai ya askari wetu yanachukua muda mrefu sana kulipwa. Aidha, nashauri sana askari wetu wapatiwe kipaumbele katika malipo. Pia nashauri sana Serikali ione uwezekano wa kuwaongeza askari polisi na magereza kuongezwa mishahara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kikosi cha zimamoto, hali ya kikosi chetu cha zimamoto sio nzuri, hairidhishi, magari ni machache, yaongezwe ili yawawezeshe kufanya kazi kwa ufanisi. Aidha, jeshi hili kwa kutokana na ajali za moto zilivyozidi ni vizuri sana wakapatiwa vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, napenda kuwapongeza sana jeshi la Polisi na Magereza kwa kutekeleza sera ya maendeleo nchini kwa vitendo. Majeshi haya yanatia fora kwa kuwa na timu nyingi katika ligi za Taifa katika michezo mbalimbali, inashauriwa sasa mpaka timu moja nzuri ya polisi na magereza ili iweze kuwa na uwezo wa kushindana Kimataifa katika kulifikisha Taifa hasa katika *football*. Naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu yaani Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nampongeza sana Waziri Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Naibu wake na

Watendaji wote na Wizara hii kwa hotuba nzuri. Mchango wangu utakuwa katika sehemu chache tu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri anisaidie kwa kunieleza ni nani kwa askari polisi anatakiwa kuwapigia *salute* Wabunge? Nauliza hili maana *RPC* wangu wote katika Mkoa wa Tabora na ma-*OCD* wote wamekuwa wananipigia *salute*, walio chini yao wamekuwa na kigugumizi!

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze askari polisi wa Mjini Tabora wamefikia hatua gani katika suala la mauaji ya Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Kanyenye, Marehemu Ibrahim Daudi Mkuiloh aliyefariki tarehe 1 Mei, 2003, baada ya kupigwa risasi nyumbani kwake usiku wa tarehe 30 Aprili, 2003 na majambazi? Nauliza swali hili maana muda mrefu sasa umepita bila kuwa na ufumbuzi wowote. Nitafurahi kupata majibu ili na mimi niweze kuwaleeza wapiga kura wangu wa Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kusikia kilio chetu na kuanza kujenga ofisi ya *RPC* Mkoani kwetu, napenda kupitia Bunge hili, kuwapongeza askari polisi wa Mjini Tabora kwa kazi nzuri wanayofanya kukabiliana na majambazi. Naomba waendelee na kazi hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na viongozi wote wa ngazi mbalimbali wakiongozwa na Katibu Mkuu na Wizara hii kwa hotuba nzuri.

Napenda niwapongeze watumishi wa Wizara kwa ujumla na mmoja mmoja, kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu katika idara zao kwa dhati, kila mmoja anatambua ugumu wa kufanya kazi katika Wizara hii. Hii ni Wizara moja wapo ya Wizara mabaya watumishi wake wana nafasi kubwa ya kuvutika katika rushwa hususan kupokea rushwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni dhahiri kuwa watumishi wa Wizara hii kuliko hata katika Wizara nyingine kwa vile ni Wizara hii ndiyo inayotakiwa kusimamia haki katika nchi, uangalifu mkubwa uendeleo kutumika katika zoezi la kuajiri watumishi wa Wizara hii hata kama njia ndefu itahitajika kutumika katika zoezi hili wanatakiwa kuwa wenye uzalendo wa hali ya juu. Ni vyema Serikali iangalie maslahi na uwezo wao ili watumishi wasije wakaingia katika vishawishi vya rushwa ambavyo ndivyo sumu kubwa ya utendaji bora na ufanisi wa kazi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Kwimba, Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba ni Ngudu. Makao Makuu ya Polisi ni ya zamani na ni ya kizamani, Polisi hawana nyumba za kutosha na wanaishi uraiani mbali ya ukweli kuwa wanakaa muda mrefu mno hali inayowaondolea hata hadhi yao ya uaskari kwa kuzoeana mno na raia hata wanashindwa hata kufanya kazi zao.

*OCD* Kwimba ndiye vile vile anayeshughulikia masuala ya usalama Wilayani Misungwi. Kituo kina gari moja tu nalo ni bovu kwa kipindi kirefu sasa kuzifanya Wilaya hizi mbili Kwimba na Misungwi kukosa misaada ya polisi. Wananchi wema ni vizuri wakaelezwa mara kwa mara ugumu wa kazi za Jeshi la Polisi. Jeshi hili linahitaji kuwezesha, hivyo ushauri wangu ni kuwa pindi Serikali itakapopata uwezo ingenunua hata pikipiki kwa ajili ya vituo vya nje kama Malya na Hungumalwa ili matatizo yanayoweza kutatuliwa na Polisi moja au mawili wawezeshe kuyafikia maeneo ya matukio mapema. Vile vile ili kazi iwe rahisi kuwapata mapema kila mara uwezo unapopatikana, nyumba za askari zijengwe. Hii itawasaidia askari wetu waendele kuwa na nidhamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama mipakani, nchi nyingi zinazotuzunguka haziko shwari sana na kwa ujumla dunia ina zidi kuharibika. Ni vizuri iwapo tunapenda kuendelea na ama tuimarisha ulinzi wa mipaka yetu. Hivyo ni vyema sheria zetu zikapitiwa mara kwa mara ili tujipatia uwezo wa kudhibiti waingiao na watokao nchini mwetu. Idara ya uhamiaji iimarishwe. Naendelea kuiomba Wizara hii kuendelea kupata uwezo ili utendaji wa kazi uendele kuwa bora. Mwenyezi Mungu aendele kuwapa nguvu. Ninaunga mkono hoja.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuelezea masikitiko yangu kutokana na utendaji wa jeshi hilo licha ya kwamba kuiongeza bajeti ya jeshi la Polisi kutoka shilingi bilioni 70 hadi shilingi bilioni 100.

Mheshimiwa Spika, ujambazi umeongezeka, wizi wa mabanki umeongezeka, kuna nini katika hili? Pia namwomba Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho anieleze maendeleo ya wizi uliotokea *CRDB*, Tawi la Azikiwe ambapo hajautolea maelezo kwenye hoja yake.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe pongezi zangu za dhata kwa Kamanda Mbinga wa Mkoa wa Kagera, kwa kazi anayoifanya kama ninavyoona kwenye vyombo vya habari. Pongezi zingine zimwendee Kamanda wa Polisi wa Mikoa ya Dar es Salaam na Lindi kwa kazi nzuri anayoifanya. Lakini nina masikitiko makubwa Mkoa wa Lindi umekuwa unabadilisha makamanda kila miezi mitatu. Alikuwa Kamanda Kombe, akahamishwa katika kipindi cha miezi mitatu, akaletwa Kamanda mwingine akahamishwa kwa kipindi kifupi wala jina silikumbuki. Sasa Kamanda wa Dar es Salaam mwacheni afanye kazi.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la usafiri Wilaya ya Kilwa, Kamanda tumempata ni mchapakazi wa hali ya juu, kiboko ya wapinzani. Wilaya ya Kilwa ni sawa na Mkoa wa Kilimanjaro kiukubwa, hivyo, gari moja halitoshi. Tunaomba ama tuongezewe gari au gari ambalo limeharibika litengenezwe.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la kutomwona Mkuu wa Jeshi la Polisi Kilwa. Tangu niwe Mbunge mwaka 2000, Mkuu wa Jeshi la Polisi hajatembelea Kilwa. Tunamwomba aje aone maendeleo ya Kilwa na pia aone jinsi wafanyakazi walio chini ya Wizara yake wanavyoishi.

Tuna kikundi cha UWT Kilwa kinasubiri zawadi kama zile alizomwaga Morogoro. Asiishie Morogoro kwani yeye ni kiongozi wa Taifa lazima afanye mambo Kitaifa. Ujio wake utahamasisha kampeni ya ujenzi wa nyumba bora za Polisi. Mwisho namkaribisha *IGP* Kilwa mwezi Septemba, 2004. Naunga mkono hoja.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini bado ni ya wasiwasi hasa kwa watu wanaosafiri kati ya Mkoa na Mkoa. Naishauri Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kubuni utaratibu wa kusindikiza magari kwa kufuambatana na polisi wenye silaha hasa kwa mabasi ya abiria kwa zile sehemu ambazo zimekithiri kwa ujambazi. Hili likitendeka litapunguza kwa kiasi kikubwa wimbi la kuvamiwa na kuporwa abiria wanaosafiri katika mabasi hayo. Pili, napendekeza kwa jeshi la polisi kuanzisha mpango kamambe na wa kudumu wa kufanya *patrol* hasa wakati wa usiku katika barabara kuu kupunguza uwezekano wa magari ya mizigo kuvamiwa na majambazi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kulitokea ulipuaji wa mabomu huko Zanzibar. Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilifuatilia suala hili na tumesikia watu kadhaa walikamatwa wakishukiwa kwa namna moja ama nyingine kuhusika na milipuko hiyo. La kusikitisha ni kwamba hadi leo hakuna tarifa yoyote iliyotolewa kwa Bunge hili ikieleza ni nani walihusika na kashfa hiyo. Tunaomba Serikali kupitia Jeshi la Polisi litoe taarifa kamili ya matukio ya mabomu Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia ya ardhi Wawi. Eneo la ardhi lililojengwa nyumba za kisasa za Polisi lilikuwa ni mali ya wananchi wa eneo la Mfikiwa Chake Chake Pemba. Mwaka 2003 nilipochangia katika Bajeti ya Wizara hii, niliuliza hatma ya watu waliokuwa na ardhi iliyojengwa nyumba za polisi Mfikiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu kuwa mipango iko mbioni kuwalipa fidia wananchi hao. Je, fidia hiyo tayari imeshatolewa kwa wahusika na kama bado, Serikali inasemaje juu ya wananchi hao na hatma yao itakuwa nini?

Mheshimiwa Spika, tunashauri Wizara iangalie uwezekano wa haraka wa kukipatia kituo cha polisi Chake Chake Pemba gari moja kwa ajili ya kufuatilia matukio mbalimbali ya maafa na majanga yanayotokea Wilayani huko ili polisi waweze kutekeleza kazi zao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, rushwa imekithiri sana hasa katika kitengo cha *Traffic*, ni kawaida kwa magari yote ya mizigo kulipa kila kituo cha *traffic* shilingi 1,000/= kutoka Dar es Salaam-Morogoro-Dodoma. Namwomba Mheshimiwa Waziri au Naibu wake siku moja aingie kwenye gari la mizigo kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma ajionee hali halisi ya rushwa humo njiani. Naipongeza Wizara kwa uamuzi wake wa kuajiri askari wapya 2,000 katika mwaka huu. Nashauri uajiri wa askari hawa ufanyike bila kujali ni chama gani mwombaji anatoka. La kuzingatia ni sifa zinazohitajika tu akiwa nazo.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko ya kijana mmoja kwa jina anaitwa Masoud Hamad (Kibeberu) ambaye alikuwa askari wa Kitengo cha *FFU* Matangatuwani, Wete



Pemba. Ameleta malalamiko yake kwenye Wizara na hata kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama juu ya namna ambavyo hakutendewa haki na Jeshi la Polisi. Je, Mheshimiwa Waziri anazo taarifa za kijana huyo ambaye ametumikia Jeshi hili kwa muda wa miaka kadhaa? Namwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wafuatilie suala hili ili kijana Masoud Hamad aweze kupata haki zake anazostahili.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ipunguze urasimu katika utaratibu wa kupata *passport book* kwa Watanzania ili kuondoa usumbufu kwa watu wanaohitaji huduma hii.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, naomba niwasilishe machache juu ya hoja iliyo hapo juu, kwamba sasa Bunge lipitishie Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2004/2005.

Mimi sina tatizo na fedha hizi ila nitapenda kukumbushia wajibu wa Wizara pamoja na mapungufu yaliyopo ndani ya Wizara hii. Jambo la kwanza ni juu ya ujambazi ambao unatishia maisha ya Watanzania pamoja na wageni ambao wengi wao ni watalii na wengine ni wawekezaji. Jambo hili kama Serikali haitakuwa *serious* na kujaribu kukomesha, uchumi tunaongumzia pamoja na amani na utulivu tunaojivunia vitatoweka na itakuwa aibu kubwa, kwani mambo haya yanaonekana wazi.

Mheshimiwa Spika, cha ajabu ni kwamba polisi wetu wamekuwa wakishirikiana nao kama ushahidi ulivyojidhihirisha maeneo mbalimbali kama vile wizi wa fedha kituo cha polisi Msimbazi, Dar es Salaam aidha, wizi uliotokea huko Moshi katika benki ya *NBC* na fedha chungu nzima kukutwa nyumbani kwa mapolisi. Hatua ninayopendekeza ni kura za maoni na kwa kuwa tunajua kwamba kuna kusingiziana basi kura hizo za siri zifanywe mara kwa mara mpaka Tume ya Uchunguzi huo iridhike na baada ya hapo wafungwe maisha chini ya kifungu cha wahujumu uchumi ambacho Rais pekee ndie atakuwa na madaraka ya kusamehe mtu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, hivyo nashauri Wizara imshauri Rais juu ya wazo hili. Tukitoa mfano wa wizi uliotokea Moshi *NBC*, ni zaidi ya shilingi bilioni tano! Je, sio hujuma? Roho za wasio na hatia zinatolewa na majambazi hawa juu ya watu wanaostahili kuwa katika jamii ya Kitanzania na kama hawastahili kwa nini wasiwekwe mahali ili wawe kando na jamii ili na wengine wajifunze?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nashauri juu ya silaha zilizopo mikononi mwa raia wema, silaha hizi zifanyiwe uhakiki kila mara walau kwa mwaka mara mbili na pia itolewe adhabu kubwa kwa mtu asiyelipia leseni ya silaha yake. Jambo hili litasaidia uhakiki na pia gharama ya leseni iongezeke kwani sheria ya zamani inafa ifanyiwe marekebisho ili malipo yafanane na silaha yenyewe, pia polisi wawaandikie wenye silaha barua ya ukumbusho wa kulipia ada kila mwaka ili mwenye silaha aendelee akikumbuka kuwa kumbe polisi wanaikumbuka silaha yangu? Kwani baadhi ya wananchi wenye silaha siyo waaminifu kwani huanzisha silaha zao kufanyia uhalifu na kama hatufanyi usahili kama nilivyoshauri hali itakuwa mbaya. Ni lazima kuhakiki silaha zote.

Jambo la pili, ni juu ya polisi kuwa kwenye makambi wote, hili ni jambo la busara sana japo hali ya uchumi ni mbaya, tujaribu kidogo kidogo ili kufanikisha kwa kufanya hivyo, mahusiano kati ya polisi na raia wema washio, yanahatarisha kwani silaha nyingi zimo katika jeshi na haziuzwi kwa raia wa kawaida ila hawa polisi huazimisha silaha kwa nia mbaya ya kuangamiza raia wema na kuwachukulia mali zao. Polisi wa aina hiyo apate adhabu mara mbili hata tatu na ikibidi wapatiwe adhabu ya kifo maana nia yao ilikuwa kuua, basi nao wauawe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu takrima. Takrima ni rushwa tena kubwa sana maana ukiangalia Mahakimu wengi wamekamatwa na rushwa ya shilingi 20,000/= au shilingi 50,000/= ambao ndio wengi! Lakini mbege yaani pombe ya kienyeji huko Moshi, kwenye kampeni ilitumia zaidi ya shilingi milioni tano kwa kipindi cha miezi miwili maana kila mkutano ni zaidi ya shilingi 300,000/=, je, hiyo nini nini? Maana mwingine anasema: “Mimi sinywi mbege ila nipe soda au nipe bia au nipe hiyo pesa nikanunue sukari au kilo ya nyama,” mipaka ni nini? Kwa nini Wizara hii isipige vita jambo hili la takrima? Tunaomba jibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala ndani ya jeshi la polisi kuna malalamiko makubwa juu ya vikosi vyenyewe pamoja na watumishi hao utakuta Polisi ana mhonga kiongozi ili apangiwe kwenye kikosi fulani na si kingine ni kitengo cha *traffic* au upelelezi, kwenye *Field Force Unit* hawataki kwa sababu nafikiri hakuna namna ya kupata kipato cha ziada kama wewe ni mwajiriwa ndani ya kikosi hiki cha *field force* inakuwa kama ni adhabu.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kikosi hiki kipewe posho zaidi ya wengine ili ku-*balance* na vile vile kuwe na *rotation* ya mara kwa mara kwamba askari asikae mahali pamoja kwa muda mrefu, wazungushwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nasema tena kuwa ni aibu msafara wa Mbunge pamoja na Madiwani watatu Moshi kuvamiwa na kuporwa na kuumizwa sana. Polisi kutokuwa *serious* kwa viongozi wake wakubwa kiasi hicho bila kusikia chochote hadi leo? Magari niliyosema na watu wanafahamika, Diwani Kiwelu alishonwa mgongoni kwa kipigo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya hata funguo za gari sina *PF 3* iko *KCMC* hadi leo juu ya jicho langu. Pongezi nyingi *OCD* Moshi. Naomba majibu.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kazi nzuri anayoifanya kusimamia vizuri sera za CCM. Nampongeza pia kamanda mwenzangu Kepteni John Chiligati, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na naunga mkono kazi nzuri anayofanya *IGP* na Maafisa na Wakuu wa Idara, Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kushukuru Wizara kwa kutupatia gari kwa Wilaya ya Ulanga kule Mahenge. Nashauri magizo yatolewe kutenga pesa sasa kwa

ujenzi wa nyumba. Wanaishi katika nyumba mbovu na baahdi yao wanaishi katika uwanja wa mpira pale Mahenge. Wizara iwe na mpango wa makusudi juu ya ujenzi wa nyumba za askari polisi na askari magereza. Naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR JUMA OMAR:** Mheshimiwa Spika, suala la ujambazi bado linatishia amani ya nchi yetu kwani pamoja na juhudi kubwa ya askari wetu wa jeshi la Polisi kutambua na wahalifu ipo haja ya kuongeza juhudi na ufanisi zaidi kwani inaonekana wazi kwamba kila siku ujambazi unaongezeka kila pembe ya nchi yetu na wananchi huuawa na wengine kuporwa mali zao kwa hiyo, tunaishauri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi walifanyie kazi na suala la ujambazi kwani askari hufanya kazi ya ziada pale ambapo amevamiwa kiongozi na sio kwa kila mtu. Kwani raia wa kawaida wanaonekana sio muhimu ila kiongozi.

Mheshimiwa Spika, kubwa uvunjwaji wa ama hapa nchini unaangaliwa upande mmoja tu kwani Serikali inaonyesha dhahiri kwamba matukio ya ulipuaji wa mabomu Zanzibar kwa ufahamu lakini haitaki kueleza ukweli mpaka sasa hivi na hakuna taarifa yoyote kuhusu matukio hayo je ni kitu gani ambacho kinafichwa nashauri kwamba wale wote ambao wanahusika na matukio hayo wapelekwe mahakamani bila kujali ili hali ya kisiasa akiwa raia au askari au kama ni kiongozi kwani kila yanapotokea matukio hayo hushutumiwa vyama vya upinzani tu.

Mheshimiwa Spika, kwa Zanzibar matukio kama hayo ni mambo ya kawaida kila inapokaribia uchaguzi na mara zote hushutumiwa viongozi na wafuasi wa upinzani tu kama kwamba upinzani ni uadui Tanzania hususan Zanzibar na wafuasi hao huwekwa rumande kwa muda mrefu na baadae huambiwa hakuna ushahidi. Je, hii ndio nchi yenye amani na utawala bora, je, vitendo hutokea na siku zote hukosekana ushahidi na watu wasio na hatia baada ya kudhalilishwa magerezani?

Mheshimiwa Spika, Waziri amesema hatua maalum zitachuliwa ili kuwawezesha jeshi la polisi kujiandaa na kutekeleza na kufanikisha vyema majukumu yake wakati wa uchaguzi mkuu mwaka 2005 hii inatia wasiwasi kwani kila unapofika wakati wa uchaguzi polisi ndio wahusika wakati wa kupora visanduku vya kura kwa kutumia uwezo wao waliopewa na Serikali ya CCM na mtutu wa bunduki mwaka 2000 ilitokea, je, hii ndio kujiandaa kwa uchaguzi mkuu ujao. Tunamwomba Waziri atufafanulie zaidi maandalizi zaidi ya jeshi la polisi katika uchaguzi wa 2005.

Mheshimiwa Spika, sasa uraia wa Tanzania una utata kwa kukosa vitambulisho vya uraia, sasa hivi tunaieleka katika uchaguzi wa 2005, je, kutokana na kukosekana kwa vitambulisho uandikishwaji wa daftari unaweza ukaingiliwa na wasiohusika hususan maeneo ya mipakani watu ambao sio Watanzania wanaweza wakaingia katika daftari hilo?

Mheshimiwa Spika, kuna vigezo gani kuhusu uhamisho wa askari polisi kwani kuna malalamiko kwa baadhi ya askari hao kwamba wasio wahi kupewa uhamisho katika vituo ambavyo wanfanyia kazi zaidi ya mara moja bila kulipwa chochote kwa mfano

Askari No. B 4998 PC Ali, aliamishwa tarehe 12 Februari, 2002 kutoka Pemba kwenda Unguja yeye na familia yake bila kulipwa.

Vile vile aliamishwa tena katoka Unguja kwenda Pemba tarehe 26 Februari, 2004 vile vile bila malipo sasa hivi anaishi Pemba na watoto wake wako Unguja je, hii ndio kawaida ya askari wote au ni yeye huyo tu?

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri haoni ni kuwavunja moyo askari wetu tena askari huyo ametumia pesa yake kwa ajili ya kusoma na kuchukua *Diploma* ya Uhasibu kiasi ya shilingi 1,276,000/= alitumia mwaka 2001 hadi 2003 bila pesa hizo kurudishiwa mwenyewe na walimuahidi kumrudishia.

Mheshimiwa Spika, hali ya magereza yetu sio nzuri ukilinganisha na uwezo wa kubeba wafungwa na mahabusu. Kwa hiyo, Wizara iangalie vyema hali hii kwani wafungwa ni kama binadamu wengine, kwani kufanya kosa sio sababu ya kudhalilishwa kwenye magereza kwani wengine ni washutumiwa tu wala sio kwamba wameshafanya makosa kwa hiyo sio vyema kuwaadhibu watu ambao bado hajathibitishwa na Mahakama kuwa wana makosa vile vile Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, ili kesi za walio mahabusu wasicheleweshewe kesi zao, ili waweze kujulikana kuwa wana hatia au hana ili waweze kutolewa mahesabu.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kuunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa kazi nzuri ambayo ameifanya na anaendelea kuifanya kwa ufanisi mkubwa ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nachangia upande wa Magereza. Katika Mkoa wa Tabora, Wilaya za Nzega na Igunga, tunapata shida sana kwa kutumia Gereza moja tu ambalo liko Nzega. Je, Serikali haioni umuhimu wa Igunga kujengewa Gereza lao ambalo litapunguza usumbufu wa kupeleka Wafungwa hao huko Nzega?

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza zaidi, hata gari ya kuwatoa Igunga haipo na husafiri kwa kupewa *lift* na watu binafsi. Hamwoni hapo hata hao Polisi wanaowapeleka Nzega wana *risk* maisha yao? Ni muhimu kwa maslahi ya wananchi wetu, Igunga wajengewe Gereza lao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Polisi Tabora. Katika Wilaya ya Sikonge, kuna Kituo kimoja tu cha Polisi, ambacho ni vigumu sana kwa wananchi wa Kipili, inakuwa vigumu sana kufika maeneo hayo kutoa shida zao. Tunaomba kuongezewa vitu hata viwili katika Wilaya hiyo ili wananchi wawe karibu na vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *OCD* Sikonge. Wilaya ya Sikonge inakua siku baada ya siku kulingana na Serikali kupeleka mahitaji ya wananchi kama barabara, umeme, maji na panaongezeka kwa kasi zaidi. Umefika wasa wakati wa kumpeleka *OCD* katika Wilaya hiyo, hasa ukizingatia kuwa Kituo chenyewe ni kimoja tu. Tunaelewa kuwa

kumpeleka *OCD*, inahitaji gharama. Lakini muhimu kwa bajeti ya sasa ni kutenga kiasi cha fedha ili kumpeleka *OCD* Sikonge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta kwa Vituo vya Polisi. Kuna utaratibu wa kupeleka mafuta katika vituo na mafuta hayo ni madogo. Je, Serikali haioni sasa wakati wa kuongeza bajeti ya Wizara hii ili mafuta yaweze kupatikana na hata wanapopata taarifa ya tukio, waweze kufika kiurahisi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELEII:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Je, Wizara hii ina mpango gani wa kujenga Gereza la Wilaya ya Igunga ili kupunguza msongamano katika Gereza la Nzega?

Mheshimiwa Spika, yapo madai ya muda mrefu ya wazabuni, hasa Magereza. Je, kuna utaratibu gani wa kuyapunguza? Jeshi la Sungusungu limesaidia katika kuondoa wezi wa mifugo. Je, Wizara haiwezi kuwaomba Sungusungu washiriki katika vita na majambazi?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003, Wizara iliahidi kutoa gari kwa ajili ya kusaidia wafungwa na mahabusu kusafirishwa toka Igunga kuja Nzega. Je, katika mgao huu, Wilaya hizi zitapewa ziada ya magari na mafuta?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ninawatakia kazi njema.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu wa maandishi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jengo la Polisi la Wilaya ya Nkansi, ninatoa shukrani zangu za kutoka moyoni kwa Wizara na Jeshi la Polisi na hasa *IGP* na Wasaidizi wake wote na Kamanda wa Mkoa wa Rukwa, SACP - Salum Ramadhanani Mkwama, kwa kuhangaikia ujenzi huo kwa nguvu zake zote.

Mheshimiwa Spika, jengo hili limechukua miaka 22 mpaka hivi sasa linapokamilika. Hata wakandarasi waliopewa kujenga jengo hili nao walichangia sana kufuja fedha zilizokuwa zikitolewa. Hivyo, nachukua nafasi hii kumpongeza Ndugu Kiluswa, Mkandarasi anayemalizia jengo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoani Rukwa, Ndugu Anyosisye Thomas Kiluswa (*Kiluswa Building Contractors and Civil Engineering*) ni mmoja wa wakandarasi anayefanya kazi zake kwa makini sana, vizuri zaidi na kwa uaminifu wa hali ya juu na gharama zake ni rahisi. Akipewa mradi kwa mfano, barabara, huifanya kazi hiyo kwa ubora wa kiwango cha juu na barabara hudumu muda mrefu. Aidha, humaliza kazi zake kwa wakati au hata kabla ya wakati wa makubaliano yenu. Namhimiza sana aendelee na ujasiri huo.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuona kuwa jengo hili limechukua muda marefu sana kukamilika. Lakini baya zaidi ni kwamba, Serikali imeusahau Mkoa wa Rukwa kwa mambo mengi. Mfano, kwa kupitia Wizara hii, hakuna jengo la Polisi la Wilaya ya Sumbawanga na hata Mpanda pia. Hakuna jengo la mahabusu pale Wilayani Nkansi (Namanyere). Nkansi hakuna hata gari la *OC-CID* wakati wengine walishapewa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali ni kuona uwezekano wa kuyakamilisha hayo hapo juu. Pia kwa wakati huo, ninaomba samani (*furniture*) za jengo la Polisi, Wilaya ya Nkansi, maana hawana samani bora. Ni mambo ya kushangaza kabisa jamani.

Mheshimiwa Spika, kwa furaha na matumaini makubwa, ninampongeza *OCD* wangu mpya, Kamanda *SSP* Matata, ambaye aliporipoti tu alisema yeye hatakaa zile ofisi mbovu na zisizo na hadhi ya Jeshi la Polisi na akasema anahamia hata chumba kimoja kilichokamilika katika ofisi mpya. Hii ni changamoto sana kwetu na jambo la kufurahisha kwa upendo wake huo kwetu sisi wana Nkansi. Hata kabla hajakaa Wilayani mwetu, ameonyesha moyo wa kutupenda na kutusaidia. Hii inaonyesha ni jinsi gani anavyoingana na sisi katika majonzi yetu kuwa sasa jengo liishe haraka na kufunguliwa. Ninamtakia kazi njema katika wilaya yetu. Namshukuru sana na kumkaribisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu wake, Mheshimiwa Chiligati, Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (UTUMISHI), pamoja na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, kwa kunikubalia kutoa Fungu (*Vote*) ya Uhamiaji. Nawashukuru sana sana kwa uhamiaji kupewa *Vote* yao, ni ukombozi mkubwa mno kwao, kwani mambo mengi waliyokuwa wanakwama, sasa watayatekeleza.

Mheshimiwa Spika, namshauri Mkurugenzi wa Uhamiaji (*DIS*), awe makini sana katika kusimamia matumizi mazuri ya pesa katika *Vote* yake mpya. Nampa hongera kwa mafanikio hayo ambayo yalionekana kama kitendawili.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kulishauri Jeshi la Polisi kupitia *IGP*, waige mfano kwa nchi jirani ambazo katika mageti ya barabarani, kwenye vyuma huwa kuna karatasi zinazowaka wakati wa usiku (*Luminous Papers*) au rangi ziwakazo gizani (*Luminous Paint*). Lengo kubwa ni kuondokana na ajali zembe ambazo zimekuwa zikitokea katika mageti yetu ya Polisi Tanzania na nyingine kutokana na kukosekana kwa ming'aro kutokuwepo. Ni vizuri *IGP* atume Maafisa wake wakaangelie haya ninayoyasema kule Zambia au Malawi na kwingineko. Maana mimi ni shahidi, kwani nimekuwa nikiendesha gari katika nchi hizo nilizozitaja, ikiwemo Kenya na Zimbabwe. Kama hilo haliwezekani, basi mageti hayo yaondolewe wakati wa usiku.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nazidi kutoa pongezi kwa Wizara hii na ninaunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningaunga mkono hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia kwa mia. Aidha, naomba kutoa maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kituo cha Polisi Wilayani Namtumbo, huko nyuma, *IGP* Mahita aliahidi kutoa fedha ili kukarabati majengo ya zamani ya Polisi kwa Sh. 1,500,000/= ili *OCD* awepo pale Namtumbo ambako uhalafu ungeluweza kushughulikiwa kwa urahisi. Wilaya ya Namtumbo ina ukumbwa wa mara mbili wa Wilaya ya Songea, ingawa *population* zinalingana.

Vile vile, upo uhalafu mkubwa sana hasa kuhusu ujangili *kule Selous Game Reserve*. Je, kwa nini alipofika Kamishna, *CP* Mwanzansu alifuta mpango huo? Je, wakati wa 2004/2005, tutapata fedha za kujenga Ofisi mpya ya *OCD* na makazi yake kule kwenye *site* mpya ya Ofisi za Wilaya? Kama jibu ni hapana, kwa nini tusipewe hizo Sh. 1,500,000/= tukarabati majengo ya Polisi ya zamani kusudi *OCD* na *CID* watumie ofisi hiyo ya muda?

Mheshimiwa Spika, majengo mazuri ya kupanga *OCD* na *CID* yapo tayari. Tafadhali turejee uamuzi wa *IPG* wa awali. Pango la Namtumbo halitakuwa kubwa, maana Namtumbo kwa sasa bado ni kijiji kikubwa cha watu wapatao 100,000 hivi, majengo mazuri yana pango la nafuu sana. Vinginevyo, tutakarabati kwa bei nafuu na tutumie majengo ya Namtumbo *NAFCO Farm* ambayo hayatumiki kwa sasa. Ukarabati ukifanywa na *Namabengo Rural Trade School*, ambayo ni Shule ya Serikali, utafanyika kwa bei poa. Mbunge atarahisisha suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Namabengo Police Post*, kituo cha *OCS* ni kamili kulingana na ramani za Jeshi la Polisi, lakini hapakuwepo *provision* ya chumba cha silaha. Wananchi wapo tayari kufanya *extension* ya jengo la chumba cha silaha. Tayari matofali ya kuchoma yapo. Tunachomba ni bati, kitasa, bawabu, rangi na saruji ya kupigia lipu. Saruji hiyo haizidi mifuko 10. Vile vile tunahitaji mlingoti wa Bendera ya Polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kituo cha Polisi Mkongo, nyumba ya Ofisi ipo, bado kupiga lipu sehemu za ndani na kugawa vyumba mfano, mapokezi, *OCS*, Wahasibu, Wanawake na Wanaume, silaha na kadhalika. Aidha, ujenzi wa nyumba za Askari, tayari yapo matofali ya kuchoma. Msaada unaombwa ni saruji, vitasa, bawabu, rangi na bati za nyumba za kuishi *OCS* na Askari wake. Tunaomba msaada huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kituo cha Polisi Kitanda, matofali ya kuchoma ni tayari kulingana na ramani ya Jeshi la Polisi. Tafadhali msaada wa bati, rangi, saruji, mbao za kenchi, madirisha na milango, zinapatikana sasa. Vitatengenezwa vifaa *bure on self help basis*. Tukipewa misaada hiyo yote, tutaweza kukamilisha ujenzi huo. Ahsante sana.

**MHE. MIZENGO K. P. PINDA:** Mheshimiwa Spika, hali ya magari ya Polisi Wilayani Mpanda inatisha. Tarehe 8 Julai, 2004 wakati wa kukimbiza mwenge, gari la Polisi aina ya *Landrover 110 (Station Wagon)* ilitia aibu, magurudumu yake yote yalikuwa kipara cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Wakimbizi ya Katumba ni kubwa mno. Polisi wanastahili usafiri. Vivyo hivyo, kwa Kambi ya Wakimbizi ya Mishamo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kituo cha Polisi cha Tarafa ya Usenya. Kituo hiki kinahudumia wakazi wapatao 80,000, lakini jengo lake liko katika hali mbaya sana. Ninaomba angalau likarabatiwe. Aidha, kituo hiki kinastahili kupata gari.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, Mbulu ni Wilaya kubwa kwa eneo na ni ya zamani sana. Ina Tarafa tano na wakazi wanaokaribia 300,000, lakini Wilaya hii ina Kituo cha Polisi kimoja tu, yaani Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Miji Midogo inayokua haraka kama vile Haydom na Dongobesh, imekuwa na matukio ya uhalifu ya mara kwa mara. Wilaya za jirani zote zina Vituo vya Polisi, hata pale ambapo inajulikana hakuna uhalifu wa kutosha kama ilivyo katika miji yetu ya Haydom na Dongobesh.

Mheshimiwa Spika, Mkuu mpya wa Polisi wa Mkoa mpya wa Manyara aagizwe kufanya tathmini ili ama Mbulu kujengwe vituo vipya viwili vya Polisi au kuhamisha mojawapo ya Vituo vya Polisi kutoka katika maeneo ambayo inajulikana hakuna matukio makubwa ya uhalifu na kuna kituo (Vituo) vya Polisi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Pia Nampongeza Naibu Waziri kwa kazi nzuri. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Ili Askari Polisi waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu, ipo haja kwa Serikali kuvipatia Vituo vyote vya Polisi, kikiwepo Kituo cha Polisi cha Mpwapwa, magari mapya. Pia *OCDs* wote, Wakuu wa Upelelezi Wilaya wote, wakiwemo wa Wilaya ya Mpwapwa, wapatiwe magari mapya ili kupambana na suala zima la uhalifu hapa nchini. Uhalifu unaongezeka siku hadi siku. Hata hivyo, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya kupambana na uhalifu hapa nchini. Ushauri wangu ni kwamba, Serikali iwapatie vitendea kazi vya kisasa ili kupambana na uhalifu huo na pia wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara ili kujifunza mbinu mbalimbali za kupambana na uhalifu, ndani na nje ya nchi. Usafiri uboreshwe katika Magereza yote nchini na mawasiliano ya simu ni muhimu.



Mheshimiwa Spika, je, tangu Bodi za *Parole* kuundwa ni wafungwa wangapi wameachiwa kwa utaratibu wa *Parole*? Je, utaratibu huo umesaidia vipi kupunguza msongamano wa wafungwa katika Magereza yetu hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Upandaji wa Vyeo katika Jeshi la Polisi na Magereza. Kwa kuwa kupanda cheo ni haki ya mtumishi kama hana dosari yoyote na ametekeleza majukumu yake kufuatana na Sheria za Jeshi la Polisi na Magereza. Je, ni sababu gani zinazofanya Askari hao wakae muda mrefu bila kupandishwa vyeo kama sifa nilizozitaja wanazo?

Mheshimiwa Spika, pia napenda kulishukuru Jeshi la Magereza na Serikali kwa ujumla, kwa kazi nzuri iliyofanywa ya kupeleka umeme katika Gereza la Mpwapwa. Nampongeza sana Kamishna Mkuu wa Magereza na Wasaidizi wake kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa nyumba za Askari Polisi. Kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2003/2004, zilitengwa fedha na Bunge hili lilipitisha bajeti ya fedha za maendeleo, je, ni nyumba ngapi za Askari Polisi zilikarabatiwa ili Polisi wetu waweze kukaa katika mazingira mazuri na kutekeleza majukumu yao vizuri? Je, katika Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla, ni nyumba ngapi zimefanyiwa ukarabati?

Hata hivyo, nampongeza sana Mkuu wa Jeshi la Polisi na Wasaidizi wake na Askari wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya, kusimamia usalama wa raia na mali zao. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mikono kwa hoja asilimia 100.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba kukumbushia msaada nilioahidiwa wa kusaidia gati katika Kituo cha Polisi Igalula.

Mheshimiwa Spika, nilieleza matatizo wanayoyapata Askari walioko kikazi katika Jimbo langu la Uchaguzi. Kieneo ni kubwa na kesi zenye kero ni za mauaji hasa Kabila la Wasukuma waliohamia kwa wingi Igalula. Mila na desturi zao wanaziendeleza, kuwaua wazee na kudhulumiana na kuuana kwa ajili ya mali, wizi wa baiskeli na maeneo mengi ni ya msitu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru kama kumbukumbu ya kupata hiyo gari ya zamani iliyokuwa inarekebishwa bado tu *spare* zinachongwa huko Japan. Askari wanapta tabu kufuatilia na baadaye kuambiwa wanaleta kero. Nina hakika Waziri unafahamu mazingira ya kuishi vijijini. Umbali na maeneo, uduni wa elimu na shida ya Askari kupanda baiskeli ili akakamate mshitakiwa. Je, akimpakia kwenye baiskeli ili amlete kituoni, akikatwa kichwa au akinyongwa? Ahadi ni deni hasa kwa Jimbo langu lenye matatizo ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, naomba jibu wakati Waziri atakapokuwa anajibu hoja za mjadala wa Wizara yake. Nawasilisha.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninaomba kuunga mkono hoja hii.

Aidha, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Viongozi mbalimbali na Watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa yote mazuri waliyoyafanya katika mwaka 2003/2004. Hata hivyo, nitashukuru endapo yafuatayo yatazingatiwa:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitambulisho vya Utaifa. Suala la wananchi kupewa vitambulisho, limechukua muda mrefu sasa na Serikali haisemi tatizo hasa ni nini. Ukosefu wa vitambulisho unasumbua zaidi katika maeneo ya mipakani, hasa Mkoani Kigoma ambapo wananchi wanasumbuliwa sana na kuitwa kwamba ni wakimbizi kutoka nchi jirani za Rwanda, Burundi, Kongo na Zambia. Ninaomba Serikali ilivalie njuga suala hili ili liishe na wananchi wapewe vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la Wakimbizi (*Refugees*), Mkoa wa Kigoma kwa muda mrefu sasa umewahifadhi wakimbizi kutoka nchi za Burundi na Congo na hao wakimbizi wamekuwa ni chanzo kikubwa cha ujambazi, uharibifu wa mazingira na uzagaaji wa silaha Mkoani Kigoma. Wananchi au wakazi wa Mkoa huu wameumia sana kwa niaba ya Taifa zima, lakini hakuna hata kifuta machozi ambacho Serikali au/na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi (*UNHCR*) wamewapatia wakazi hao. Ni vyema sasa Serikali ikasimamia ili kasi ya kuwaondoa wakimbizi kuwarudisha kwao iongezeke.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha kwa mawasiliano ya vituo vilivyoko mpakani hasa Mkoani Kigoma, bado vinahitaji kuboreshwa kimawasiliano kwa kuvipatia vifaa vya mawasiliano hasa radio na magari. Aidha, idadi ya Askari iongezwe ili kuweza kukabiliana na matukio mbalimbali kutokea nchi jirani na vile vile kuimarisha usalama katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba yafuatayo yazingatiwe na Wizara:-

Mheshimiwa Spika, naomba *OCD* Kongwa na Afisa Upelelezi wa Wilaya ya Kongwa, wapewe kila mmoja gari jipya kati ya magari 174 yatakayonunuliwa mwaka huu. Ombi letu hili ni la siku nyingi. Tunaomba mwaka huu tukumbukwe.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mji Mdogo wa Kibaigwa wamejenga Kituo cha Polisi tayari. Tunaomba kituo hicho kianze kufanya kazi haraka kwa vile hali ya usalama pale ni tete na tayari lipo Soko la Kimataifa ambalo kiulinzi hutegemea Polisi kutoka Kongwa. Pia nashauri gari moja la Polisi liwe pale Kibaigwa ili wafanye *highway patrol* badala ya kutegemea gari na Askari kutoka Dodoma. Hoja hii naomba Waziri na Naibu Waziri, waiseme wakati wa kufunga hoja yao. Wananchi wangependa kusikia.

Mheshimiwa Spika, Gereza la Kongwa linahitaji trekta jipya kwa miradi ya kilimo. Pia nilitembelea Gereza hili na kulikagua. Uongozi wa pale ni mzuri, wenye bidii ya kazi na usafi wa Gereza na chakula unaridhisha. Tatizo ni kwamba, vyoo karibu vyote ndani ya Gereza vimeharibika. Inawezekana kabisa kuvikarabati na vikawa ni *flashing toilets*. Hii itaboresha sana usafi na kuepukana na maradhi. Ukarabati huu wa vyoo unahitaji si zaidi ya shilingi milioni mbili. Ni kiasi kidogo sana. Gereza limechakaa sana, lilijengwa kwenye miaka 1940 na lina *cracks* nyingi sana, linaweza kukarabatiwa. Kwa hiyo, siku zijazo litengewe fungu.

Mheshimiwa Spika, Polisi kwa ujumla wanafanya kazi nzuri Wilayani Kongwa. Tatizo kubwa ni ukosefu wa gari zima, lipo *110 Land Rover* bovu sana. Wananchi wanaomba Jeshi la Polisi kufanya kazi zao kwa taratibu za Kipolisi na si vinginevyo. Kwa vile hivi sasa imekuwa ni kawaida kwa wananchi, watumishi wa Serikali, viongozi wa ngazi za vijiji wa Serikali na Chama kutiwa ndani (mahabusu) kwa amri za baadhi ya viongozi ambao siyo Mapolisi kwa siku kadhaa, bila kufunguliwa jalada lolote wala mashtaka yoyote.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Polisi wasikubali kulaza watu ndani ili kuwafurahisha baadhi ya viongozi wa Serikali. Huu ni uvunjwaji mkubwa wa haki za binadamu. Narudia kusema, kwa kuwa Askari Polisi ni safi kule Kongwa, ila tu wafanye kazi zao *professionally* na wasitumiwe ku-*harass* wananchi bure.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara hii kupitia Waziri wake, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara kwa juhudi na maarifa wanayotumia katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Wizara hii inayo majukumu magumu na mazito kuyatekeleza, hasa ikizingatiwa kuwa suala la amani na usalama wa wananchi, bado unakabiliwa na mapambano mazito ya araa wasio wema, wakiwemo majambazi, wezi na wahalifu mbalimbali wanavyobadili mbinu zao mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kujenga mazingira mazuri yenye uhusiano kati ya Askari wa Polisi na Walinzi wa Jadi (Sungusungu). Hii ni kwa kuzingatia uzito wa kazi yao ya ulinzi wa raia na mali zao, kwani idadi ya Askari ni ndogo sana, pamoja na vifaa vya kutendea kazi kutotosha. Bado Polisi hawajatambua kazi nzuri inayofanywa na Sungusungu. Badala yake ukiacha viongozi ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa, Askari wa ngazi ya chini wanageuza Walinzi wa Jadi kama miradi yao ya kiuchumi, wakitumia udhaifu wao wa kutojua sheria, aidha uonevu wa dhahiri kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu, naomba Wizara/Serikali iruhusu na kuanzisha Vituo Vidogo vya Polisi katika Kata za Salawe, Mwakitovyo na Lyabukande ili kusaidia wananchi wa maeneo hayo kukabiliana na wimbi la maovu mbalimbali

yanayojitokeza, yakiwemo ukataji mapanga vikongwe na wizi wa kutumia silaha na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyenzo za kazi. Aidha, Kituo cha Polisi cha Iselamagazi, kipatiwe gari ili kuratibu vyema kazi ya ulinzi na usalama katika maeneo husika katika ukanda huo wa Magharibi mwa wilaya yetu, ambao ni eneo kubwa sana, yatokeapo mauaji au matukio maovu, inachukua muda mrefu kupeleka taarifa Wilayani, na Askari kutoka huko kufika katika maeneo ya tukio.

Kuhusu mafunzo ya Askari, kama nilivyoshauri katika bajeti ya Wizara hii mwaka 2003/2004, mafunzo ya Askari wa Polisi yaongezewe muda badala ya utumikao sasa. Hii ni kwa kuwa uhalifu unazidi kuongezeka na mbinu zao kubadilika kuwa za hali ya juu kwa utumiaji silaha kubwa na kadhalika. Aidha, utaratibu wa upatikanaji wa wanaojiunga na Polisi, uanzie ngazi ya kijiji badala ya Wilayani, ili kupata taarifa sahihi za mhusika juu ya tabia na mwenendo wake, badala ya kutumia elimu na vigezo vingine tu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, narudia kuipongeza sana Serikali kupitia Wizara hii, kwa juhudi wanazofanya. Nawatakia mafanikio katika mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri ya udhibiti wa uhalifu nchini na hasa mtandao wake unaoiwezesha kupata wahalifu mara baada ya matukio. Haya ni mabadiliko makubwa, ukilinganisha na hali ya miaka iliyopita, ambapo wahalifu waliweza kupotea na kujificha bila kuonekana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Katibu Mkuu, Ndugu Bakari Mahiza na Mkuu wa Polisi, Kamanda Omar Mahita, kwa uadifu na umahiri wao wa utendaji.

Mheshimiwa Spika, mimi nina mchango mdogo kuhusiana na Wilaya yangu mpya ya Kilulindi, Mkoani Tanga. Nina maoni yafuatayo:-

Kwanza, naomba idadi ya Askari Polisi katika Kituo cha Polisi cha Songe ambacho kina jukumu la kuhudumia Wilaya mpya ya Kilindi, iongezwe kutoka watatu wa sasa hadi angalau 15. Kituo cha Songe kinahudumia Wilaya nyingi zinazoizunguka za Kiteto, Simanjiro, Kilosa na Mvomero, ambazo Makao yao Makuu yako mbali.

Pili, naomba Wizara irudishe huduma za kituo kilichokuwa Kambi ya Mkuyu kwa kuwa majengo ya Ofisi na Nyumba za Askari zipo. Huduma hii iliamishwa baada ya Kambi kuhama. Eneo la tarafa zinazozunguka kituo, zilikuwa zinategemea sana kituo hiki kwa usalama, maana Vituo vya Handeni na Songe, viko mbali sana.

Tatu, Kituo cha Songe kilikuwa na gari, lakini ilibidi lipelekwe Makao Makuu ya Wilaya kule Handeni kuziba pengo la usafiri. Naomba Kituo cha Songe kipatiwe gari kama hatua ya kukiimarisha kama Kituo cha Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kwa kuwa wananchi wa Kata ya Kikunde, Tarafa ya Kwekivu, wamekamilisha jengo la Kituo cha Polisi kufikia ngazi ya renta, naomba Wizara isaidie kuezeka jengo hili ambalo ni kubwa na zuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya hii mpya, Makao yake Makuu Songe, yanahudumia maeneo mengi ya Wilaya jirani, naomba Wizara ijenge Gereza Songe ili wafungwa wasisafirishwe masafa marefu hadi Handeni au Kibaya (Kiteto) au Kilosa. Uongozi wa Wilaya ya Kilindi na wananchi wako tayari kushiriki na kuwezesha ujenzi wa Gereza endapo Wizara itaamua Gereza lijengwe Songe au sehemu yoyote muafaka Wilayani Kilindi. Tunapendekeza Gereza hili liwe la kilimo, maana Gereza la Mkoa la Kilimo lilikuwa Kilindi, katika Kijiji cha Tamota hadi lilipohamishwa kwa sababu zisizoeleweka.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuridhia maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu muhimu ya ulinzi wa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Katibu Mkuu wa Wizara hii na Wataalam wote kwa jinsi walivyoandaa bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkoani, yamechakaa mno. Ni ya zamani sana, sambamba na lile la Kituo cha Polisi cha Kengeja, nalo ni bovu, linavuja na linahatarisha maisha ya Askari wetu. Hivyo, ninaishauri Serikali iyafanyie ukarabati wa hali ya juu majengo haya haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kujenga kambi za kuishi Askari, majengo ya kutosha, ili kuwawezesha Askari kuepukana na usumbufu wa kuishi uraiiani na kutapelekea kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali iangalie upya viwango vya mishahara ya Askari kulingana na vyeo vyao, kwani mara nyingine Askari anapanda cheo, lakini mishahara wake unabakia ule ule kabla ya kupanda cheo na hata kama ataandika barua kadhaa, basi huwa hakuna majibu. Ni vyema hili likapewa umuhimu mkubwa katika harakati za kukabiliana na rushwa ndani ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ikaboreshe mikopo kwa Askari wake katika hali ya kupambana na umaskini. Ni vyema wakakopeshwa fedha za kutosha kulingana na mishahara yao na kukopeshwa vyombo vya usafiri kulingana na vyeo vyao.

Kwani kuna vyeo ambavyo havistahili Askari kupanda pikipiki. Hivyo, hili liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuwapatia fedha za uhamisho Askari wake mara tu baada ya kuwahamisha kama ilivyo sheria. Inasikitisha kuona kuwa Askari kadhaa wamepewa uhamisho kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine na haki hiyo hadi lao haijatolewa. Hii ni kero kubwa sana na inafaa ipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, uajiri katika Jeshi la Polisi Tanzania Zanzibar, bado umetawaliwa na upendeleo wa itikadi za kisiasa, bila kuangalia uwezo wa mtu na mwombaji sifa alizo nazo. Huu ni udhaifu mkubwa. Hivyo, ninaishauri Serikali iachane na tabia hii mbaya, kwani wote ni Watanzania na wana haki sawa bila ubaguzi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ikafafanue na kulipatia ufumbuzi wa haraka suala la ujazaji mkataba wa kujisajili katika makundi yanayotambulika Askari wa Pensheni na wale wa Kiinua Mgongo, ambapo imepelekea manung'uniko makubwa ya kudhihirika mapishano makubwa ya fedha pale Askari wanapostaafu, hata kama wote wawili walikuwa na cheo cha aina moja.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ikaangalie upya kiwango cha urefu wa futi 5 na inchi 11 kama kigezo kinachotakiwa kuwa sifa ya kumwajiri mwombaji kuwa Askari. Ni vyema kiwango cha urefu huu kikapunguzwa, kwani ukuaji wa watu wengi unapungua nchini Tanzania. Ninapendekeza urefu wa futi 5 tu unatosha kumwajiri Askari, zaidi tuangalie elimu yake.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kutenga fungu maalum la fedha kwa ajili ya Madiwani wa Masheha, ili kuwapatia semina na mafunzo maalum katika kufanikisha Elimu ya Uhamiaji na kuweza kupambana na wahamiaji haramu nchini. Sambamba na hili, ni vyema Serikali ikawapatia mafunzo kazini wafanyakazi wa Uhamiaji kwa kuboresha ufanisi kazini.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali iwapatie mshahara mnono/mzuri wafanyakazi wa Uhamiaji, ili kuwawezesha kuepukana na rushwa kazini. Ninaishauri Serikali kuwajengea nyumba za kuishi karibu na vituo vyao vya kazi, ili kukabiliana na usumbufu wa kuishi mbali kwa wafanyakazi wa Uhamiaji, jambo ambalo linapunguza ufanisi kazini.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza kazi inayoendelea kuboreka, inayofanywa na Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Idara ya Uhamiaji, chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, akisaidiwa na Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, Ndugu Bakari Mahinza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nilipokuwa nachangia hoja ya Wizara hii, nilitoa hoja ya kutokuridhika kwangu na Wizara hii kwa kutokuitambua Wilaya ya

Ruangwa, ambayo ilianzishwa mwaka 1995 kama Wilaya kamili. Kwa mshangao, Wizara imeendelea na inaendelea kuishughulikia Wilaya hii kama Kituo Kidogo cha Polisi mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kama ilivyobainisha katika hotuba ya Waziri, haina mipango yoyote ya sasa na wala baadaye ya kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya, ukiachilia mbali suala la ujenzi wa majengo ya Kituo cha Polisi, mpaka leo Idara ya Polisi haijateua Mkuu wa Polisi wa Wilaya (*OCD*) ya Ruangwa. Hakuna maelezo yoyote yanayotolewa na Wizara ni kwa nini hali hii inaendelea. Wananchi wa Ruangwa wamechoshwa na kuendelea kuwa tegemezi na Wilaya jirani ya Lindi kwa huduma ya Polisi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupata usumbufu unaotokana na hali hii, wananchi wa Ruangwa wanasikitishwa sana na kuendelea kwa kero hii sugu bila kutatuliwa na wameniagiza kufuatilia suala hili ili kupata maelezo kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa nini Serikali inaendelea kuruhusu kuendelea kwa hali hiyo. Kwa niaba yao, namwomba Waziri atoe maelezo ya kina wakati anatoa majumuisho ya mjadala wa hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utumiaji wa simu za mkononi (*Mobile Telephones*), Wizara itafakari kwa undani zaidi matumizi ya simu za mkononi kwa madereva wakati wanaendesha gari. Hii ni hatari kwa watumiaji wengine wa barabara, kwa vile wakati dereva anatumia simu, anakosa umaskini katika uendeshaji na utumiaji salama wa barabara. Ninatoa rai kwa dhati kabisa kuwa, utumiaji wa simu za mkononi wakati dereva anaendesha gari, upigwe marufuku mara moja. Endapo dereva yeyote yule anataka kutumia simu ya mkononi, basi aegeshe gari lake pembezoni mwa barabara, ndipo aendelee na shughuli hizo. Hili linawezekana kwa kutumia sheria na kanuni za utumiaji barabara kuu (*Highway Code*), ili kunusuru maisha ya watumiaji wa barabara.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingi, alama za barabarani hazikuwekwa bayana. Aidha, ukubwa wa alama hizo ni mdogo mno (*microscopic*), kiasi kuwa haukidhi madhumuni yake ya kutoa tahadhari kwa watumiaji barabara. Wizara ilitazame upya suala hili, ili kuongeza ukubwa wa alama hizo. Tufuate au kuiga mitindo inayotumiwa na nchi zilizoendelea kama vile Ulaya au Marekani. Nchi hii haina upungufu wa mbao, tuna utajiri mkubwa wa mbao. Hivyo basi, tututumie utajiri wetu huo wa mbao katika kunusuru maisha ya Watanzania na watumiaji wengine wa barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mia kwa mia na kumhakikishia ushirikiano wa wananchi wa Ruangwa katika kutekeleza mipango yake kama ilivyoainishwa katika hotuba yake.

**MHE. DR. MILITON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, wakati Naibu Waziri akijibu swali langu kuhusu wananchi wanaojichukulia sheria mikononi na kuua wahalifu, hata wale vibaka wadogo wadogo wasio na silaha, alisema wananchi hao huwa kweli wana hasira na si kwamba wauaji hao ni vibaka, wengine ni wasio na ajira.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea na mazungumzo na wananchi kuhusu suala hili, wamesema wananchi wengine hushiriki katika mauaji hayo kwa kuwa wakiwakamata vibaka na wahalifu hao na kuwapeleka Polisi, huachiwa na kurudi kuendelea kuwaibia na kufanya uhalifu mwingine. Ningeshauri Jeshi la Polisi liwe makini na kuwashughulikia kisheria na kuwapeleka Mahakamani badala ya kuwaachia.

Aidha, Polisi wawe macho kuingilia haraka pale wananchi wanapojichukulia sheria mikononi, kuwapiga na kuwaua wezi na wahalifu wengine kabla mauaji hayajatokea. Hii pia itaondoa uwezekano wa watu wengine wasio na hatia kuuawa kwa makosa, kama kijana aliyefanya makosa ya kuchanganya baiskeli yake, akachukua nyingine na kuacha ya kwake, kijana huyo aliuawa kikatili, kumbe hakuwa mwizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi nasema Polisi Mkaoni Dar es Salaam hawajapambana kwa dhati na wahalifu na matapeli wa Kimataifa watokao nje ya nchi yetu. Watu hao wako wengi sana Jijini Dar es Salaam na wanawaibia Watanzania na wafanyabiashara kwa kuwatapeli. Jeshi la Polisi wanalijua hilo. Naamini Askari wengine wanawajua hawa matapeli na hata wanapoishi vijijini. Mazingira pia yanaonyesha kuwa Polisi wanawalinda matapeli hawa kwa maslahi yao. Matapeli hawa wanaoishi nchini bila vibali sahihi au vya bandia (vya wakimbizi), wametapakaa na wanatembea kwa uhuru kabisa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni mimi na Mheshimiwa Hadija Kusaga, tuliweza kuwatega matapeli wawili waliotaka kumwibia/kumtapeli Mheshimiwa Hadija Kusaga, kwa kushirikiana na Askari Wapelelezi. Lakini pamoja na kufanikiwa kuwafikisha wahalifu hao Polisi na kuomba angalau matapeli hao wafukuzwe nchini kwa Polisi kuwafikisha *Immigration*, hilo halikufanyika na matapeli hao waliachiwa huru na wapo mitaani Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, habari ambazo nimezipata hivi karibuni, tapeli mmojawapo kati ya hao, aitwaye Chilombo/Kalombo na anayetoka Congo, ameahidi kufanya kila awezavyo na kutumia fedha ili mimi na Mheshimiwa Hadija Kusaga tuuawe au tumizwe kwa kumfanya alale mahabusu kwa siku mbili. Kwa hiyo, hapa tulipo, maisha yetu yako hatarini, licha ya sisi kufikisha suala la matapeli hao kwa *IGP* na *RPC* wa Dar es Salaam. Sasa ni zaidi ya miezi miwili, Polisi wako kimya na wala matapeli hawa hawajafikishwa *Immigration* ili wafukuzwe nchini.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu za dhati napenda kuwapongeza Jeshi la Polisi kwa mapambano makali na makubwa wanayopambana na maadui majambazi. Vita vya majambazi ni milipuko inayotokea usiku na mchana. Lakini Jeshi letu liko tayari kupambana kila mara ujambazi unapotokea. Napenda kuwapongeza na kuwashukuru.



Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi zetu hata za Viongozi Wakuu wa Jeshi, bado haitoshi, naomba Jeshi la Polisi wanapofanya mambo makubwa ya vita vya majambazi ambayo tunafahamu kwamba wamekubali kutoa maisha yao, wapambanaji hao wapewe motisha tena kubwa ili wawe na moyo zaidi.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawapongeza Jeshi la Polisi wale ambao wamefuatilia majambazi waliovamia Benki ya *NBC* Moshi na kuwakamata majambazi na fedha nyingi ambazo hakuna aliyetarajia kwamba zitapatikana tena. Jeshi letu limenipa moyo kwamba tuna Jeshi imara. Napenda kuwapongeza kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri mambo matatu. La kwanza, kwenye bajeti ya mwaka 2003/2004, niliomba hapa Bungeni kuwa Kituo kilichoko *Lake Natron*, ambacho kilijengwa na wananchi, wasaidiwe kumaliza. Bado naomba kwenye bajeti hii kwamba kimaliziwe, kwani wananchi huko hawana eneo la kukimbilia. Ndiyo maana wananchi wamechangia jengo hilo

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kukumbusha gari la Kituo cha Polisi Longido, kwani wananchi hawajui Kituo kingine. Matukio yanayotokea mpakani ni mengi sana, kituo hicho kinahitaji kupata gari.

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda malalamiko ya wananchi wa Jimbo langu la Longido, Serikali na Chama cha Mapinduzi, imejaribu kumaliza kero ndogo ndogo zinazowasumbua wananchi. Lakini mpaka wa Namanga bado kuna kero nyingi za wafanyabiashara wadogo wadogo kukamatwa vitu vyao. Mpaka huo umekuwa kero kwa wananchi wafanyabiashara, wameanza kuhamia maeneo mengine ya mipakani kama Holili na Sirari. Kwa nini vituo vya mpakani viwe tofauti huku wote wanatumia sheria moja?

Mheshimiwa Spika, wananchi wanahoji, kwa nini wananyanyaswa huku biashara kati ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki imeruhusiwa? Wakenya wanafanya biashara mpakani wakilindwa na Serikali yao, huku wao wanabanwa na Serikali yao! Naomba uongozi wa Polisi uangalie kero iliyoko mpakani Namanga. Kuna vibali ambavyo vinatolewa kwa baadhi ya wafanyabiashara, ambavyo hata Bungeni hatujapitisha. Kila mwananchi mwenye uwezo anaruhusiwa kufanya biashara halali. Kwa nini wabanwe tena?

Mheshimiwa Spika, mwisho, nazidi kueleza kuwa Jeshi letu wanapofanya vizuri, wapewe motisha zaidi na zaidi. Kwani wamejitoa kulinda wananchi na mali zao. Kwa mfano, walifanya kazi mpaka fedha za Benki ya *NBC* zikarudishwa na kuwaweka mikononi wezi zaidi ya 28, hao wanaostahili wapandishwe vyeo na kupewa motisha kubwa.

Mheshimiwa Spika, kupitia hotuba hii, napenda kuwapongeza Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha kupitia *RPC* wa Arusha, kwa kazi nzuri wanayofanya kupambana na majambazi waliozidi huko Arusha. Kweli tuna Jeshi zuri.

Mheshimiwa Spika, malalamiko yanayolalamikiwa Polisi ni ubinadamu tu, hakuna binadamu anayefanya kazi ya Malaika, hasa kazi ya hatari kama hii. Hongera sana, endeleeni na juhudi zenu. Tunawashukuru sana.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, hotuba ya bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ni nzuri sana. Ninajiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza sana Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hotuba yake nzuri. Ninawapongeza sana Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Viongozi Wakuu wa Polisi, Magereza na Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, jana asubuhi nilihabatika kumwona na kumsikia *IGP* Mahita, Mkuu wa Jeshi la Polisi, akiwahutubia Askari wa *Traffic* katika Luninga ya *ITV*. Nilimsikia akilalamika juu ya tabia ya Askari wa Usalama wa Barabarani, ya kupokea rushwa kutoka kwa madereva wahalifu na pia tabia yao mbaya ya kudai fedha kutoka kwa madereva hata pasipo kuwepo makosa yoyote.

Mheshimiwa Spika, nilifurahishwa kumsikia Mkuu wa Jeshi la Polisi akikubali hadharani kuwa rushwa ndani ya Jeshi la Polisi ipo na hasa katika Kikosi cha Polisi wa Usalama Barabarani. Kilichonisikitisha ni kwamba, wakati *IGP* akisikitika kwamba rushwa inanuka katika kikosi hicho cha Usalama Barabarani, Askari aliokuwa akiwahutubia, walikuwa wakicheka, wakionyesha dhahiri kwamba, maneno ya *IGP* yalikuwa hayana maana.

Mheshimiwa Spika, nidhamu katika Jeshi la Polisi imepungua sana. Je, Jeshi la Polisi lina mkakati gani wa kurudisha nidhamu katika Jeshi hilo? Ninakubali kuwa kwa ujumla Jeshi la Polisi nchini Tanzania, linafanya kazi nzuri sana, lakini lazima tukubali vile vile kuwa wapo Askari wakorofi, hasa katika Vikosi vya Upelelezi na Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Spika, ningependa nitoe shukrani kwa Viongozi wa Jeshi la Polisi kwa uamuzi wao mzuri wa kujenga kituo kipyaa cha Polisi Mjini Kyela. Wananchi wa Kyela wamefurahishwa sana na ujenzi wa kituo hicho na kwa niaba yao, ninatoa shukrani kubwa kwa Serikali. Wananchi wako tayari kushirikiana na Serikali kwa hali na mali katika kazi ya kulinda usalama wa Wilaya ya Kyela na nchi nzima kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kyela wana maombi yafuatayo: Kwanza, wanaomba *OCD* wa Kyela asiondolewe Kyela. Kama muda wake wa kustaafu umefika, basi tunaomba apewe mkataba wa kazi kwa miaka mingine miwili ili aendelee kuitumikia Kyela. *OCD* huyu ni mchapa kazi, mstaarabu, mwenye hekima na busara nyingi, mchukia rushwa mkubwa, asiyekubali hongo, muungwana, asiyekuwa na hasikii majungu na mwenye huruma, lakini makini. Ni mfano mzuri wa askari safi.

Mheshimiwa Spika, ombi la pili, wananchi wa Kyela wanaomba mahabusu inayojengwa katika Gereza la Kyela, ikamilike haraka ili kuondoa kero kubwa inayowakabili watu wa Kyela na ambayo ni bughudha kubwa sana kwao. Hivi sasa watuhumiwa wa makosa mbalimbali Wilayani Kyela, wanapopelekwa Mahakamani na

kukosa wadhamini, hupelekwa Wilaya jirani ya Tukuyu (km. 52) na kutupwa ndani ya rumande huko. Ndugu na marafiki wa watuhumiwa, inabidi wawafuate huko kuwapa chakula na mahitaji mengine. Ni gharama kubwa kwao.

Mheshimiwa Spika, kwa wananchi wa Kyela, kero hii ni kubwa na inawanyanyasa sana. Pia ni gharama kubwa kwa Serikali, kwani lazima gari la Serikali liwapeleke Tukuyu na kurudi Kyela. Halafu siku ifuatayo, gari iwafuate Tukuyu na kuwarudisha tena baada ya Mahakama. *This is a routine business, very costly.* Mwaka 2003 niliahidiwa na Naibu Waziri kwamba, Serikali ingetoa kiasi cha fedha kukamilisha jengo la mahabusu, ambalo wananchi walianza kulijenga. Sijui kama ahadi hiyo ilitolewa.

Mheshimiwa Spika, ningependa nipate maelezo juu ya jinsi gani Serikali inashughulikia tatizo hili. Serikali isilipuuze tatizo hili hata kidogo. Mahabusu wengi wa Kyela wakipelekwa Tukuyu, wanakufa na wengi wanapata magonjwa ya vichomi kwa sababu ya tofauti ya hali ya hewa. Kyela ni joto na Tukuyu ni baridi. Mimi kama Mbunge, sitaki ugomvi na Serikali yangu, lakini vile vile sitavumilia kuona watu wangu wanadhalilishwa na kunyanyaswa kama vile bado wanaishi enzi za ukoloni.

Mheshimiwa Spika, ombi la tatu la wananchi wa Kyela, hususan wakazi wa Ipinda, ni ukamilishaji wa Kituo cha Polisi cha Ipinda. Kituo kimekamiliwa, lakini kwa mujibu wa taratibu za Jeshi la Polisi, kituo hakiwezi kufunguliwa kwa sababu hakuna nyumba ya kukaa Askari. Hivi sasa tunakarabati nyumba moja tuliyopewa na Chama cha Ushirika. Serikali itusaidie fedha za kumaliza nyumba hiyo. Mji Mdogo wa Ipinda ni kituo muhimu cha biashara, kikikutanisha watu wa Wilaya za Kyela, Rungwe, Ludewa na Makete. Matukio mengi ya uhalifu yanahitaji Kituo cha Polisi kuwepo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaomba katika mgao wa magari, Kyela ipewe kipaumbele. Kyela ni Wilaya ya mpakani. Wilaya ina miji midogo mine ya Kasumulu, Ipinda, Matema na Mji wa Kyela wenyewe. Lazima liwepo gari na ku-*patrol* sehemu zote hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya Wizara hii. Nampongeza pia *IGP*, Kamishna Mkuu wa Magereza pamoja na Mkurugenzi wa Uhamiaji, kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao ipasavyo. “Tusione vinaelea, vimeundwa”. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa spika, mwaka 2003 niliomba Wisara itazame uwezekano wa mambo yafuatayo kwenye Jimbo langu na Mkoa kwa ujumla. Kwanza, ni ujenzi wa Ofisi ya Polisi Wilaya ya Sumbawanga Mjini, ambayo ni pamoja na Wilaya ya Vijijini. *OCD* bado anatumia kiofisi kidogo cha *OCS* kilichojengwa wakati wa Uhuru mwaka 1961. Kwa nini mpaka sasa ombi hili halijafikiwa, pamoja na kwamba mwaka huu, Ofisi na

Vituo vya Polisi vipya katika wilaya kadhaa vitajengwa? Naomba maelezo. *OCD* wa Sumbawanga anahudumia mjini na vijijini?

Mheshimiwa Spika, la pili, mwaka 2003 niliomba na nikauliza swali Bungeni kuhusu Gereza la Mahabusu Mjini Sumbawanga, ambalo nalo licha ya kufurika kwa wingi wa wafungwa, bado hata hali yake siyo nzuri. Nalo lilijengwa wakati wa Uhuru mwaka 1961. Ningependa pia nipate maelezo ya ziada baada ya Wizara kuahidi mara nyingi kuwa itaishughulikia suala hili, bila mafanikio. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, ajitahidi kufuatilia mwenyewe maelekezo na ahadi za Wizara ili tusionekane nasi tunajiingiza katika kutoa ahadi hewa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, la tatu, nilishauri pia jitihada za makusudi zitumike katika kujenga nyumba za Askari na kuboresha maslahi yao. Pamoja na jitihada hizo, bado kuna haja ya kuliangalia suala hili kwa mikoa na wilaya ambazo ziko pembezoni na wengi wakipelekwa wanaona ni adhabu. Kuna hisia kuwa baadhi ya wananchi wanadhani Askari wanaopelekwa Mkoa wa Rukwa, wanakomolewa na kudhani ni adhabu kwao. Namwomba Mheshimiwa Waziri, asaidie kusahihisha mawazo kama hayo ili askari nao wasivunjike moyo. Maana Askari wengi wanaokwenda Rukwa hufurahia maisha ya huko baada ya kukaa kwa muda.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri kwa ahadi yake ya kupeleka trekta katika Gereza la Kilimo Mollo (Sumbawanga). Pamoja na pongezi hizo, bado naomba uwezekano wa kupeleka wafungwa zaidi katika Gereza hilo ili uzalishaji wa mazao ya kilimo na hasa mahindi, uongezeke. Naelewa baadhi ya Magereza yana wafungwa ambao hawana kazi. Nguvukazi hii ihamishiwe kwenye shughuli ili kweli Magereza yetu yajitegemee angalau kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa unao wageni na wakimbizi wengi. Tunashauri kuanzia sasa, Idara ya Uhamiaji iongeze watumishi ili kudhibiti hali hii kwa ajili ya usalama wa mkoa na kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ujao wa 2005. Tusifanye makosa ya kuingiliwa na wageni wakati wa uchaguzi. Hatari ya kuvurugika uchaguzi inawezekana katika mikoa kama hiyo.

Mheshimiwa spika, jengo lililokuwa la Benki ya Taifa ya *Biashara NBC (1997) Limited*, lilinunuliwa na Mahakama Kuu ili litumike kurahisisha kesi zisiwe zinapelekwa Mbeya. Leo ni zaidi ya miaka miwili tangu linunuliwe. Naomba Waziri ashirikiane na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba ili jengo hili lianze kutumika kwa ajili ya Mkoa mzima wa Rukwa badala ya kupeleka kesi zote Mbeya.

Mheshimiwa Spika, naomba nipatiwe majibu kuhusiana na hoja zangu hizi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naomba kutoa mchango wangu kwenye hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama

ilivyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani kwenye Bunge lako la Bajeti 2004/2005 kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, kwa hotuba nzuri. Pongezi hizi pia nazitoa kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Katibu Mkuu wa Wizara, Bwana Bakari A. Mahiza, Makamanda wote na Watendaji wote wa Wizara, kwa kushiriki kwenye shughuli nzito ambayo imefanikisha uzuri wa hotuba hii. Kwa namna ya pekee, naomba sana kumpongeza sana *IGP* Ndugu Omari Mahita, kwa ushiriki wake kwenye maandalizi ya hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, ningependa nitoe maoni yangu kwenye hotuba hii kufuatana na hali ya matatizo kwenye Jimbo la Mwanza Mjini. Kuna jengo la muda mrefu kwenye Kambi ya Askari ya Mabatini, ambalo mpaka sasa halijakamilika. Kwenye bajeti ya mwaka 2003/2004, maombi ya kukamilisha jengo hili, niliyaleta kwenye Wizara. Nitafurahi sana kama Waziri atakapokuwa anajibu hizi hoja, basi anihakikishie kwamba mwaka huu wa fedha, jengo hili litakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya majengo ya Kambi za Askari Mwanza, sasa ni chakavu sana. Hali ya uchakavu mkubwa wa majengo haya ni maeneo ya mabafu, vyoo na majiko. Ni vizuri kufikiria namna ya kufanya matengenezo (*repair*) ya nyumba hizi. Kwa hiyo, kwa Mwanza pamoja na mapungufu ya nyumba za Askari, ni vizuri kwa zile zilizopo zikafanyiwe matengenezo (*repair*).

Mheshimiwa Spika, tunalo eneo moja ambako Askari Mwanza wanaishi liitwalo Kigoto, ambako hali ya makazi hayo ni mbaya na haistahili kutumika kama makazi ya binadamu. Eneo hili lilikuwa Kiwanda cha Kukamua Mafuta. Kwa hiyo, kutokana na matatizo ya nyumba, Askari wanaishi maeneo hayo kwa shida sana.

Mheshimiwa Spika, nyumba ambazo Askari wanaishi eneo hili, zilikuwa mabohari ya kuwekea mbegu za kukamua mafuta. Kwa hiyo, kwenye mabohari hayo, hapakufanyiwa mgawanyo wa kukatwa vyumba (*partitioning*). Kwa hiyo, Askari wanaoishi humo wanakata vyumba kwa kutumia majamvi na khanga na vitenge. Kwa hiyo, hakuna usalama wa mali wala siri. Hali hii ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ifanye kila linalowezezana kupata ufumbuzi wa tatizo la makazi kwa Askari wa eneo la Kigoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL E. Ntwina:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuyapongeza Majeshi ya Wizara hii kwa kuweza kufanya kazi nzuri sana. Pamoja na shukrani hizi, nina matatizo ya kimsingi kule Jimboni Songwe.

Mheshimiwa Spika, bado tunahitaji kujengwa kwa Kituo cha Polisi pale Mkwajuni. Ingawa wananchi wa Kijiji cha Galula wamejenga Kituo Kidogo cha Polisi kwa kujitolea, ilikuwepo ahadi ya fedha katika *budget* iliyopita na ya zamani ya Amiri na

Ndugu Mahita kuwa, tungesaidiwa kupata *cement* kumalizia suala la ujenzi. Naomba ahadi hiyo itekelezwe. Si mingi, itamalizia kama mifuko 50 ya *cement*. Naomba Waziri mwenyewe aje au kama *IGP* Mahita anaweza kuja kulifungua jengo lile la Polisi, bila shaka safari hii itawatia nguvu kama ikifanywa ziara huko.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri aangalie uwezekano wa kupewa usafiri na trekta, ambavyo nimekuwa naviomba hapa mara kwa mara. Vifaa hivyo naviomba kwa ajili ya Gereza la Ngwara, ambako kilimo kinastawi na hakuna usafiri wa kuaminika. Yapo magari ya *KIA* ambayo hayakidhi kabisa hali yenyewe. Naomba *Land Rover* au *Lorry* kusaidia eneo hili la Ngwara.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Waziri asaidie Kituo cha Galula usafiri, walau wapewe pikipiki (Honda). Kwani kumekuwa na matatizo mengi ambayo yanahitajika kufikiwa kwa mara moja haraka haraka. Pikipiki/Honda hiyo itasaidia sana. Kama ni vigumu, basi naomba angalau Polisi wa Kituo kile wapewe mkopo wa vitendea kazi hivi.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la nyumba za Polisi pale Jimboni kwangu kwa maana ya Galula na Mkwajuni Polisi. Wananchi wangu wanaweza kujenga ikiwa nayo Ofisi ya Polisi itasaidia kutoa vifaa kama vile mabati na saruji.

Mheshimiwa Spika, miaka yote nimekuwa nikiomba sana trekta pale Gereza la Ngwara, angalau lile za zamani basi litengenezwe. Kila nifanyapo ziara huko, naulizwa juu ya uwezekano wa kupatikana kwa trekta. Kwa sababu kama vifaa vya kilimo vingekuwa vingi, basi wangeongeza nguvu ya kulima.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Idara ya Polisi Makao Makuu, kwa kuboresha sana vituo hivi viwili kwa kupewa *Radio Calls* na Gari pale Mkwajuni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kudumisha amani.

Mheshimiwa Spika, kule Jimboni Nkenge, Kata ya Kanyigo, eneo la Kigarama, kuna kizuizi cha Polisi (*barrier*). Ukipita kwenye hiyo *barrier*, unaenda Kata nyingine ya Kashenye ambayo iko Tanzania na ni kati ya Kata 17 za Jimbo la Nkenge. Hivi karibuni nilipokuwa kwenye ziara kabla ya kuja kwenye Kikao cha Bajeti, nilipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa Kata ya Kanyigo na Kata ya Kashenye kuhusu wananchi pamoja na magari kuzuiliwa kupita kwenye hiyo *barrier* kuanzia saa 12.00 za jioni.

Mheshimiwa Spika, ndiyo tuseme kwamba, inapofika saa 12.00 za jioni, magari hayaruhusiwi kwenda Kata ya Kashenye na mengine yanazuiliwa hata kwenda kwenye Kituo cha Afya kilichopo Kata ya Kanyigo, eneo la Kigarama. Kwa hiyo, naomba wananchi wangu wasizuiliwe kutembea au kutumia magari ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, naunga miono hoja mia kwa mia.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza hotuba ya Waziri na kwa ujumla na Wataalam wote walioshirikiana kuiandaa taarifa. Mimi sina tatizo, naitakia kheri Wizara katika utekelezaji. Ila ninachoshauri ni kwamba, mipango ili iende vizuri, ni ufuatiliaji na kusimamia kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri inayofanywa. Polisi inauza maisha kwa kujitoa kukabiliana na wahalifu, majambazi wenye silaha, bila kuwa na uhakika na maisha yao. Lakini wanajitoa kwa ajili ya Taifa letu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi tangu tupate uhuru, halijapewa kipaumbele. Bajeti yao iongezwe na mambo muhimu nashauri yatiliwe maanani. Askari wapatiwe nyumba za kisasa, wapatiwe silaha za kiasasa, wapatiwe mikopo kwa ajili ya vifaa vya nyumbani, pikipiki, motisha na kadhalika na Askari asikae kituo kimoja zaidi ya miaka 10, kwa sababu kazi yake ni ngumu na anashughulika na watu wa aina mbalimbali, wema na wabaya. Akikaa muda mrefu, tunahatarisha maisha yake. Pia Askari apatiwe mafunzo ya ndani na nje na anapohitaji likizo, apewe mara moja.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara, Askari wana tatizo la nyumba. Lakini katika mipango ya kuboresha, sijaona taratibu za ujenzi wa nyumba za Askari. Nashauri mtumie hekima ya kuona nyumba katika bajeti hii, hata chache zianze kujengwa ili kuwapa motisha na itafuta fikra zilizotawala kwamba watumishi wanaofanya kazi Mikoa ya Kusini ni sehemu ya adhabu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa, kipindi cha juma sasa, madereva wamehojiwa Dar es Salaam na *Television ya Channel Ten* kwamba, wanaionaje rushwa. Wamekiri kuwa ipo na kwamba, kama hawatoi chochote kwa *Traffic Police*, Madereva wanakosa kazi, watakuwa wanasumbuliwa njoo kesho na kadhalika. Pia walitamka kuwa labda Bunge watusaidie, ila wao tatizo liko nje ya uwezo.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa jambo hili kwamba siyo vyema kunyamaza. Kwa sababu yaliyoongelewa ni mazito na tusi yapuuzwa. Serikali iseme lolote katika kukemea, bila kutoa maelezo. Raia walioona *TV*, watakuwa hawaiielewi Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya bajeti mia kwa mia.

**MHE. ROBERT K. MASHALLA:** Mheshimiwa Spika, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kusimamia ulinzi wa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi hili, bado Jeshi hili linafanya kazi katika mazingira magumu. Mfano hai ni Polisi walioko Wilaya ya Bukombe. Kwanza, Askari hawa ni wachache sana kulingana na ukubwa wa eneo, lakini vile vile matukio ya ujambazi wa mara kwa mara ni mengi kwa vile Wilaya hii iko jirani na Kambi za Wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchache wa Askari hawa, hata vitendea kazi vyao havikidhi mahitaji kwa Wilaya ya Bukombe yenye matukio mengi ya ujambazi na idadi ya watu laki nane kwa mujibu wa sensa ya 2002. Wilaya ina gari moja tu la Polisi, hali ambayo inachangia sana kuzorotesha ulinzi wa Jeshi hili. Serikali iliahidi kutoa gari kwa ajili ya *patrol*, lakini mpaka sasa gari hili halijaja. Tunaomba gari hili litolewe ili lisaidie kuimarisha ulinzi. Tatizo lingine ambalo linadhoofisha ulinzi ni mgao wa lita 200 za mafuta kwa mwezi. Utaratibu huu umekuwa kero kwa wananchi. Kwani kufuatana na matukio mengi yanayohitaji matumizi ya gari, mafuta haya huisha kabla ya mwisho wa mwezi na matokeo yake ni kwamba, tukio likitokea wananchi huambiwa kuchangia gharama za mafuta ili Askari waende kwenye tukio. Hivyo, tunaomba mgao wa mafuta uongezwe na hasa kwenye maeneo muhimu kama Bukombe.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri huu, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa vile wanasimamia kwa karibu sana ufanisi wa Jeshi hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kukupongeza wewe binafsi kwa kuendesha Bunge letu hili kwa ufanisi wa hali ya juu kabisa.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wao wote, kwa kuwasilisha bajeti yao kwenye Bunge hili na kuonyesha matumaini mazuri ya utendaji wao kwenye kipindi kilichopita na kupata imani zaidi kuwa kipindi hiki cha mwaka 2004/2005, utendaji utakuwa wa juu zaidi hasa ukizingatia ongezeko la fedha lililopatikana hivi sasa, kuwa na ziada ya kuweza kufanikisha malengo yote yaliyopangwa ili yafanikiwe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utendaji mzuri wa Kamishna wa Polisi Zanzibar, hasa ukizingatia hali ya siasa ya Zanzibar, ambayo ina tofauti sana na sehemu nyingi hapa nchini, kwa kiasi kikubwa, Kamishna wa Zanzibar anastahili kila aina ya pongezi kwa vile anavyoweza kupambana nao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wastaafu, ni vyema kwa sasa likapewa kipaumbele suala la wastaafu, kwani wanasumbuka sana mara tu baada ya kumaliza utumishi wao na ni jambo ambalo linafahamika wazi kwa kila mmoja muda wake wa kustaafu. Lakini jambo linalofanyika ni usumbufu ambao si wa lazima kwa kuhangaika kwenye maboti na kulipa pango za Hoteli kwa siku kadhaa na kurudi bila ya mafanikio. Je, kuna ugumu gani kuwekwa Ofisi Ndogo ya Mambo ya Ndani ya Nchi Zanzibar ili wale wote wenye madai yao wakahudumiwa pale pale Zanzibar? Majengo mengi ya Askari wa Polisi Zanzibar, yako katika hali mbaya sana hasa ukizingatia kuwa ni majengo ya zamani sana na yanachukua muda mrefu kufanyiwa matengenezo, ambayo ni hatari kwa Maaskari wetu kwa kaisha yao.



Mheshimiwa Spika, mwezi wa Machi, 2004, Zanzibar kulikuwa na vitendo vya hujuma vingi tu. Ni jambo la kumpongeza Mkuu wa Jeshi la Polisi, alichukua jitihada zote kwa kuongeza ulinzi katika Kisiwa chetu na kupatiwa magari, redio za mawasiliano na kuwawezesha Askari kutembea usiku kucha mpaka vitendo hivyo vyote vikamalizika. Lakini jambo la kusikitikitisha ni kwamba, mara tu baada ya kumalizika vitendo hivyo, zoezi lile lote limekatika. Sijui Mheshimiwa Waziri, anasubiri vitokee vitendo vingine ndiyo atarudisha ile nguvu ambayo ilikuwepo wakati wa hujuma?

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Ahsante.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuchangia, ninachukua fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muyuni, kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Katibu Mkuu wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu Bakari Mahiza, *IGP* Ndugu Omar Mahita na Kamishna wa Polisi Zanzibar, Ndugu Khalidi Iddi Nuizan, kwa juhudi zao za kuimarisha Ulinzi wa ndani wa nchi zetu zote za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Jeshi la Polisi zinaonekana na kila mtu mwenye macho yake. Amani inaonekana, ingawa bado wapo wanaoyabeza maendeleo haya. Ninawaomba sana, juhudi hizi ziendelezwe hivyo hivyo, mbali na bajeti yenye uchache wa fedha na Mwenyezi Mungu atatusidishia kheri na baraka. Mbali na pongezi hizi kwa Jeshi letu la Polisi, ninaomba kuwakumbusha kuwa kutokana na kuongezeka kwa kudhalilishwa kwa Askari Polisi na raia, umefika wakati hivi sasa kuliangalia kwa makini suala la udhalilishaji wa Jeshi la Polisi, la kupigwa pigwa ovyo na raia wakati wanapokuwa kazini. Ni jambo la aibu kwa Askari kupigwa na raia ambaye anamlinda usiku na mchana. Hivi sasa kumejitokeza mtindo huu mbaya. Kwa hiyo, wale ambao wanaohusika, ni lazima wachukuliwe hatua kali, tena kali ili iwe ni fundisho. Jeshi la Polisi liache ushuba na urafiki usiokuwa na msingi na wasiookuwa na imani na Jeshi letu la Polisi, kiwango cha kuwa na kiburi kama hiki cha kuwafanyia utovu wa nidhamu kama huu hasa kwa Askari wa Kike. Ambapo kama nilivyochangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika mkutano huu huu juu ya kesi ya Askari aliyepigwa mbele ya raia na Kondakta wa Daladala kule Zanzibar. Kesi hiyo ipo Polisi au Mahakamani. Lakini hapana kinachoendelea zaidi ya majisifu na majigambo ya mtuhumiwa huyo kuwa hakuna chochote cha ziada kitakachotokea, imepita. Cha ziada ni kuhamishwa Askari huyo katika sehemu hiyo ya kazi na kupelekwa sehemu nyingine. Uhamisho wa kazi ni jambo la kawaida, lakini likiambatana na dhana ya uhalifu, linaleta sura mbaya na kuwapa kiburi watuhumiwa na kulidhalilisha Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, labda imekuwa sasa baadhi ya raia wabovu wamejenga imani mbovu juu ya Jeshi la Polisi na kuona kama ni sawa na wao. Hii siyo imani nzuri, kwani vitendo kama hivi vinazidi kuongezeka kama tulivyosikia katika vyombo vya habari, yaliyotokea kule Shinyanga kwa Askari wa Usalama Barabarani kupigwa makofi na mtoto wa Tajiri/Mmiliki wa magari ya biashara (Taarifa ya Kipindi cha Kutoka Mikoani na *Radio Tanzania One* cha tarehe 12 Julai, 2004). Tumesikia ameshikwa na kupelekwa

Mahamani kesho yake 13 Julai, 2004. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wakuu wa Polisi wote wa Tanzania Bara na Zanzibar, kuyafuatilia masuala haya ipasavyo. Tunaona aibu kwa Jeshi letu la Polisi kutendewa hivi na sisi kama viongozi hatujui tufanye nini kwa lengo la kuheshimu taratibu za Mamlaka za Vyombo vya Dola.

Jambo lingine la msingi ni kuwa, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, jambo kubwa ambalo limezungumzwa sana ni suala la kuliimarisha Jeshi la Polisi kama chombo. Lakini sikuona zaidi sehemu ambayo imewapendelea Askari wenyewe kimaslahi. Askari wetu wana kazi ngumu na majukumu makubwa kwa juhudi zao zote. Ipo kila haja ya kuwatazama Askari wetu kwa kuwapatia maslahi bora zaidi, ikiwa ni pamoja na kuwapatia mikopo nafuu ya nyumba zao ili wakimaliza muda wao, wasizurure zurure mitaani na kuonekana kama maadui wakati walipokuwa kazini.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napenda kutoa ushauri ufuatao, kuhusu majengo ya Polisi hapo Shinyanga Mjini, mwaka 2003/2004, mliahidi kuweka matumizi hayo kwa mwaka 2004/2005, yaani *budget* ya mwaka huu. Sikuona fedha yoyote kwa ajili ya ukarabati ama kuwajengea Polisi wa Shinyanga. Naomba sana wakati Waziri anajumuisha, nipatiwe majibu ya ahadi. Nyumba mbovu za Mkoani Shinyanga na Wilaya zake, nazo zikumbukwe kwa kutatua tatizo hili. Katika suala la usalama kwa mkoa wetu, napenda sana kumpongeza *RPC* na Viongozi wote wa Polisi Wilayani pale Mkoani, kwa kazi nzuri ya kupambana na ujambazi na kupunguza madhara ya ujambazi. Lakini tatizo bado lipo. Pia nazidi kuwapongeza kwa kazi nzuri hasa kwa sasa wakati wa msimu wa pamba, ambapo fedha nyingi za pamba zinasambazwa kununulia pamba. Hili nalipongeza sana.

Suala la ujambazi Kitaifa, linatakiwa liwekewe mkakati wa nguvu na kuuangamiza kabisa ujambazi. Maana ukikomaa ujambazi, ndiyo utaanza kupambana na Serikali na hasa Jeshi la Polisi. Yanayotokea kwa sura ya ujambazi huko Liberia, Siera Leone, Somalia na kadhalika, yameanza makundi ya ujambazi na baadaye kuweka mtandao wa ujambazi. Ni vyema nguvu ya ziada itumike kuangamiza ujambazi nchini kote. Kwa sasa nchi yote ya Tanzania, watu wanafanya kazi nusu siku (saa 12) badala ya saa 24 kama ilivyo katika nchi jirani. Suala la usalama litaturudisha nyuma kiuchumi, ni vyema suala hili likapewa nguvu ya fedha. Nashauri pia wanunue bunduki za kisasa ili kupambana kikweli kweli na tatizo hili. Penye amani na utulivu, ndipo panapatikana maendeleo. Pia magari na vitendea kazi vipatikane. Pia ni vyema *helicopter* mpya ikanunuliwa. Kwanza, *helicopter* hiyo ndiyo inasaidia Viongozi wa Kitaifa kwenda haraka katika mahali wanapotakiwa. Kwenye *budget* ya 2003/2004, nilishauri kuhusu suala hili. Nilidhani katika mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, suala la *helicopter* mpya na kubwa ingelifaa sana.

Mheshimiwa Spika, motisha ya Askari kuhusu maslahi yao ya kuhama, ya kutembea wakiwa kazini pamoja mishahara yao iboreshwe. Suala la utendaji mzuri si la

magari, bunduki na vifaa vingine. Vitu hivi viendane na maslahi ya Askari kulipwa kwa wakati. Katika Jimbo la Shinyanga Mjini, Kituo cha Polisi ni kidogo sana na baadhi ya watumishi hupokezana katika kuandika hata ripoti zao. Naomba sana Kituo cha Polisi Shinyanga Mjini (Manispaa), hakina hadhi ya Manispaa. Naiomba Wizara hii iweke mipango ya kujenga Ofisi yenye hadhi Mkoani petu. Suala la wafungwa, yaani Magereza, napongeza kwa chakula kinachotolewa na pia napongeza uboreshaji wa *drainage system* ya Gereza la Shinyanga Mjini (Manispaa).

Pia suala la nguo limewekewa mikakati mizuri. Pamoja na kwamba, wananchi tunapotetea wafungwa wanadhani tunayo tabia ya ujambazi, la hasha. Jela ni mahali pa wote, hata Wabunge, Mawaziri na hata Rais huenda Jela. Kwa hiyo, ni vyema Mahakama zikaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kulipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kuwanasa wachunaji ngozi wa Mbeya na wezi wa fedha kwenye Benki zetu na majambazi sugu yote yaliyoshikwa na Jeshi la Polisi. Ni vyema sana kuwa na ushirikiano wa Mahakama na Jeshi la Polisi, maana ndiyo Serikali yenyewe. Palipo na udhia penyeza rupia. Rushwa haiwezi kwisha pasipo kutoa udhia wa Polisi, hasa kuhusu maslahi yao. Suala la rushwa husababishwa na udhia walio nao watendaji wa Polisi. Tuletewe mkakati wa kuboresha maslahi ya Polisi. Huu ni udhia mkubwa na ndiyo unaosababisha rushwa. Naunga mkono hoja kwa mare nyingine.

**MHE. EDWARD N. LOWASSA:** Mheshimiwa Spika, napongeza kwa hotuba nzuri. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *IGP*, Mkurugenzi wa Uhamiaji na Mkuu wa Magereza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 niliahidiwa nyumba (*Police Line*) pale Monduli na mimi tukishirikiana na *OCD* Monduli, tumeshapata kiwanja. Ahadi hii itatekelezwa?

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Hotuba ni nzuri, miradi pia ni safi. Tatizo ni fedha alizogawiwa Mheshimiwa Waziri ni kidogo, ukilinganisha na matatizo ya Wizara. Mimi nina ombi, Madaba ni Mji Mdogo uliopo katikati ya Miji ya Songea na Njombe. Tunacho Kituo cha Polisi kipo km. 130 toka Songea na km. 130 toka Njombe. Barabara inayounganisha Njombe na Songea ni ya lami, kuna ajali kila siku. Naomba nipatiwe gari la Polisi, *Defender* siyo *Hyundai*.

**SPIKA:** Ahsante. Kama nilivyokwisha kueleza Waheshimiwa Wabunge, Wizara zenye siku mbili kama hii mjadala wa jumla unamalizika saa 7.00 kipindi cha asubuhi, halafu mchana watoa hoja wanapewa nafasi ya kujibu hoja zilizotolewa. Kwa uzoefu tulionao kwenye Wizara ya Elimu na Utamaduni, kumbe Waheshimiwa Wabunge, wanapenda kuuliza maswali wakati wa Kamati. Kwa hiyo, ni vizuri tukawapa muda mrefu wa kuweza kujibu hayo maswali wakati wa Kamati. Kwa hiyo, tutakaporudi mchana watoa hoja mjiandae kuanza kuhitimisha hoja yenu saa 11.00 jioni.

Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Kabla sijaanza kuchangia, naomba kwa niaba ya wapigakura wangu wa Jimbo la Manyoni Mashariki, nitoe salaam za rambirambi kwa wananchi wa Mbeya Vijijini kwa kumpoteza Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitoe salaam za rambirambi kwa ndugu zetu Wabunge wote ambao wamepata msiba katika kipindi hiki cha Bunge hili. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wabunge wote kabisa. Kwa siku mbili wametupa ushauri mwingi sana ambao utatuwezesha mimi na Mheshimiwa Waziri wetu kuendesha vizuri kazi hii mliyotukabidhi. Hoja hii ni nzito kama alivyosema Mheshimiwa Dr. William Shija na uzito wake umeonekana kutokana na jinsi watu walivyochangia. Hoja hii imechangiwa kwa maandishi na watu 103, waliochangia kwa kusema ni 25, waliochangia wakati ule wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni 14 kwa hiyo jumla hoja hii imechangiwa na watu 142, haijapata kutokea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kweli kujibu hoja za watu 142 kwa muda wa saa moja sio jambo rahisi.

**MBUNGE FULANI:** Sio rahisi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sio rahisi. Kwa hiyo, naomba kabisa wale ambao hatutawagusa kwenye majibu yetu muelewe tu hivyo kwamba muda wa saa moja hatuwezi kujibu hoja za watu 142 waliozungumza kwa siku mbili. Naomba mtusamehe lakini hoja zote tumezichukua na tutazijibu kwa maandishi na baadaye tutatoa kakitabu ambacho kitakuwa na majibu ya kila hoja. Kwa hiyo, hakuna hoja hata moja ya Mbunge ambayo tumeipuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, katika kuchangia kwangu nitapenda kujibu hoja za waliochangia wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na waliochangia Idara ya Magereza, hoja za wengine, Mheshimiwa Waziri mtoa hoja atakuja kuzijibu na kuwatambua rasmi wale waliochangia.

Sasa waliochangia wakati wa hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Venance Mwamoto, wao waliuliza wale wazima moto walioshughulika kuzima moto wa *TANESCO* pale Ubungo na hasa

wale waliojitosa kwenda kufunga ile *valve* ambayo ilikuwa inapitisha mafuta na walipofunga ile *valve* ndio moto ukazimika, wanasema vipi wamefanya kazi kubwa kama hivyo mmewapa motisha ya shilingi 200,000 tu?

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba wale waliofanya kitendo kile cha kijasiri ambao ni Mratibu wa Zimamoto, Mpemba Magogo na mwenzake Sajini Fadhili Matola, hawa walipewa motisha ya ahsante ya shilingi 1,200,000 kila mmoja wao. *(Makofi)*

Lakini vile vile wale walioshughulika na lile zoezi la kuzima moto wamepandishwa vyeo maana ule moto hawakushiriki watu wawili tu ilikuwa ni timu kubwa. Kwa hiyo, kuna watu wamepandishwa vyeo kutoka u-*Private* kwenda u-*Corporal* askari 11, kutoka *Corporal - Sergeant* askari 5, *Sergeant - Staff Sergeant* askari 15, *Staff Sergeant - Major* wawili na wale Maofisa wanashughulikiwa sasa na Tume zinazohusika.

Kwa hiyo, kwa kweli wale vijana walioshughulika na zoezi la kuzima moto tumewaenzi kiasi kikubwa tu sio jinsi ambavyo Wabunge walikuwa wanafikiri kwamba tuliwapa shilingi 200,000 tu lakini tumewapa fedha za kutosha na kupandishwa vyeo wao na wenzao. *(Makofi)*

Vile vile Mheshimiwa Salum aliulizia matukio ya Januari 27 kule Zanzibar, anasema ahadi ya Serikali ya kutoa kifuta machozi kwa walioathirika imefikia wapi?

Jibu ni kwamba suala hili halishughulikiwi na Wizara ya Mambo ya Ndani, linashughulikiwa na Tume ya Muafaka na naamini kwamba wanalishughulikia hata kwenye magazeti tumeona jinsi wanavyowasiliana na Mataifa ya Nje. Kwa hiyo, tuiachie hiyo mamlaka inayohusika sisi Wizara ya Mambo ya Ndani hatuhusiki moja kwa moja na hilo.

Mheshimiwa Mohamed Ali Said, alikuwa na hoja kwamba Serikali iimarishe ulinzi wa Rais, nataka kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba ulinzi wa Rais na viongozi wakuu wa Kitaifa unashughulikiwa vizuri kabisa baina ya Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kanali Mstaafu Feteah Saad Mgeni, Mheshimiwa Sumri Abdallah Mohammed na Mheshimiwa Faustine Rwilomba katika kuchangia kwao walisema kwamba tuongeze kasi na vita dhidi ya majambazi. Kazi hiyo tunaifanya kupitia Jeshi la Polisi na kwenye magazeti mnasikia jinsi majambazi yanavyokamatwa kila siku hata wale waliokimbilia Kenya, wale wa Moshi lakini kwa kazi nzuri wamefuatwa mpaka kule Kenya na bwana mmoja akakutwa kajificha chooni, huko huko chooni amefuatwa na amekutwa na maburungutu ya fedha za Kitanzania, dola za Marekani na ameletwa hapa na yale maburungutu yameletwa hapa. Huo ni mfano tu kwamba kuna kazi inafanyika na itaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyotoa kauli juzi hapa ndani ya Bunge kwamba majambazi huko yaliyoko sasa yaanze kujisalimisha kwa sababu tumeshachoka, wananchi wamechoka. Sasa hivi majambazi wamebadilisha mtindo, wanarusha risasi kwa Polisi tunasema wakome kwa sababu kama ni bunduki Polisi wanazo bunduki nyingi

kuliko wao majambazi, kama ni risasi Polisi wana risasi nyingi kuliko wao majambazi kwa hiyo wajue hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Henry Shekiffu, alitoa rai kwamba Serikali idhibiti njia kuu ya lami kati ya Mombo na Lushoto. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Henry Shekiffu na wananchi wa eneo hilo kwamba tayari Polisi Mkoa wa Tanga wamepeva maelekezo maalum ya kuongeza udhibiti wa ulinzi katika eneo hilo ili kukabiliana na matukio ya ujambazi katika eneo hilo vile vile na kuongeza *highway patrol* katika eneo hilo.

Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Venance Mwamoto, walizungumzia habari ya kuongeza magari ya Polisi na hoja hiyo tena imejirudia sana katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hili Mheshimiwa Waziri atalifafanua lakini inatosha kusema kwamba katika kitabu chetu cha hotuba ya Bajeti, tumeonyesha kwamba mwaka huu yatanunuliwa magari 174 ya Polisi, kwa kweli ni machache kulingana na mahitaji halisi. Lengo letu sisi ni katika kila Wilaya kuwe na magari angalau matatu la *OCD*, *OC-CID* na lingine la Mkuu wa Kituo (*OCS*). Tukifikia magari matatu, mtaona hali ya mabadiliko ya ufanisi wa Polisi. Kwa hiyo, haya magari 174 yanapunguza tu kwamba katika baadhi ya Wilaya walikuwa hawana magari kabisa wengine walikuwa na gari la *OCD* lakini liko juu ya mawe, haya magari yanakuja tu kupunguza makali ya tatizo lakini tusiwe na matumaini kwamba sasa kila mtu atapata magari mawili, mawili, matatu matatu hilo lengo hatualikamilisha mwaka huu, lakini *inshallah* mwakani tena tukipata fungu kama hili tunaweza kukamilisha lengo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, alitoa hoja kwamba wanawake ndani ya Jeshi la Polisi wananyanyaswa kijinsia kwa maana kwamba hatuwatazami kuwapa vyeo. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Bunge lako Tukufu kwamba kwa kweli katika Wizara ya Mambo ya Ndani hatuna ubaguzi katika Majeshi yetu yote iwe ni katika Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji, wote wanatendewa sawa. Akinamama ndani ya Jeshi la Polisi wako ma-*RPC* na wanafanya kazi nzuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mheshimiwa Diana Chilolo, aliwataja hapa baadhi ya ma-*RPC* akinamama yule wa Tanga na yule wa Mtwara na *inshallah* watazidi kuongezeka. Ma-*OCD* vile vile wako wengi na hata tunapokuwa Dodoma hapa wakati wa Bunge anayetulinda sisi Wabunge mwanzo wa Bunge mpaka mwisho ni *OCD* mwanamke na anafanya kazi vizuri. Hatujasema kwamba wanatosha, tunasema kwamba tutaendelea kuwaongeza kwa sababu uwezo wanao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Samwel Chitalilo, yeye alitoa hoja kuhusu kutokuwepo kwa amani katika Jimbo lake la Buchosa hasa tatizo la ujambazi kwenye Kisiwa cha Masome kule Ziwani. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Samwel Chitalilo, kwamba hali hiyo ya ujambazi iliwahi kutokea mwaka 2003, Polisi wakaidhibiti, mwaka 2004 imejitokeza tena Polisi wataidhibiti. Nadhani akiwa hapa hapa katika kikao hiki cha Bunge atapata habari moto utakaowaka huko katika Jimbo lake katika vita kupambana na majambazi, ndio kazi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile labda nitumie nafasi hii kujibu hoja zake nyingine mpya alizozitoa katika hotuba yetu. Alitoa malalamiko kwamba kule kuna Polisi ambao hawana silaha. Malalamiko yake ni ya kweli, kwa sasa Polisi wameshindwa kupeleka silaha kwa sababu hakuna mahali pa kutunza silaha (*armoury*). Silaha ina taratibu zake huwezi kuitundika silaha kwenye dari, upo utaratibu wake.

Kwa hiyo, sasa hivi kwa kuzingatia kilio cha Mheshimiwa Mbunge, kwanza tunaandaa mazingira tupate kwanza armory. Sasa hivi uko mpango na *IGP* ametuhakikishia katika vituo vyake vitatu kimoja kilicho katikati kitateuliwa pajengwe *armoury* ili silaha hizo zikipelekwa basi kuwe na mahali salama pa kuziweka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, naomba uwe na subira tuandae mazingira hayo kwanza ndipo tupeleke silaha tukizipeleka tu kienyeji kwa kweli inakuwa tunakiuka maadili ya utaratibu wa kutunza silaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kituo chake kimoja ambacho alitualika kikafunguliwe, Mheshimiwa Waziri amesema atapata nafasi aende akakifungue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, yeye aliomba Serikali iimarisha kituo cha Polisi cha Mlandege na kujenga vituo vipya vya Darajani na Vikokotoni ili kuimarisha usalama. Hoja yake tumeipokea na tutaifanyia kazi. Kwa kweli ndio lengo letu la kuimarisha ulinzi. Kwa hiyo, kituo cha Mlandege tutatizama uwezekano wa kukiimarisha na *inshallah* Bajeti ikikubali siku zijazo tujenge vituo vipya pale Darajani na Vikokotoni.

Mheshimiwa Remidius Kissassi, alisema Polisi, Tume ya Uchaguzi na Msajili wa Vyama vya Siasa wawashughulikie wanasiasa wanaotoa lugha za matusi. Hii hoja ilitolewa na Mheshimiwa Remidius Kissassi na Mheshimiwa Ali Said Salim. Tunakubaliana nao kabisa, kwanza kutoa lugha ya matusi mtu wa kawaida, mwanasiasa, ama kiongozi ni kosa la jinai. Kwa hiyo, naomba viongozi wenzangu tuelewe hivyo na Jeshi la Polisi halitasita kumkamata mtu yeyote bila kujali ni wa chama gani, ni kiongozi, mwananchi wa kawaida, ili mradi tu ni yule anayetumia matusi. Kwa hiyo, wale wenye midomo ambayo haina itifaki wakae chonjo hasa tunapokwenda kwenye uchaguzi lazima maneno yetu yawe yanayojenga amani, mshikamano na umoja wa Taifa ndio kiongozi barabara lakini kiongozi wa matusi huyo anaonekana kwamba amefilisika tu kisiasa ndio maana sasa anaingia kwenye matusi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ali Said Salim, alisema Serikali itoe taarifa nani alihusika na ulipuaji wa mabomu kule Zanzibar. Kama tulivyoeleza katika hotuba yetu ya Bajeti kwamba baada ya matukio yale Polisi walikamatwa watu wapatao 49, watu hawa wamepelekwa Mahakamani sasa hivi kesi iko Mahakamani, tsubiri maamuzi ya Mahakama. Kwa kawaida mambo yakiwa Mahakamani hatutakiwi tena tuyazungumze sana hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa John Singo, alisema fedha zaidi zilizotolewa kwa Jeshi la Polisi zitumike kusimamia Uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka 2005, tunakubaliana naye na kwamba fedha hizi kwa kweli kwa sehemu kubwa zimeongezwa ili kulipa Jeshi la Polisi

uwezo wa kukabiliana na hali ya uhalifu nchini, ndio madhumuni yake makubwa. Bajeti ya uchaguzi kwa sababu uchaguzi ni Oktoba mwaka 2005, itakuja kwenye Bunge lijalo lakini ongezeko hili tunapambana na hali ya majambazi.

Hata ndugu zangu wa upande wa Upinzani, Mheshimiwa Frank Maghoba, alisema sasa sisi tuna wasiwasi kwa nini Jeshi la Polisi limeongezwa, nguvu zinaelekezwa wapi, nguvu zinaelekezwa kwa wahalifu. Wale raia wema wale wafurahi tu kwamba sasa chombo chao kimeongezewa nguvu ila wale wahalifu ndio wakae mkao wa kukamatwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, alisema kwamba utaratibu wa kustaafisha Polisi wakiwa vijana uangaliwe upya. Ni kweli katika Jeshi hasa Jeshi la Polisi watu wanastaafu kwa umri mbalimbali. Wale wa vyeo vya chini wanastaafu mapema zaidi, wale wa vyeo vya juu (*senior officers*) wanakwenda mpaka miaka 60 kwa sababu kazi zao ni kazi za kupanga, kutoa amri, lakini wale ambao kazi zao ni za doria, za kupambana na majambazi, kufukuzana na majambazi wakifikia umri fulani kama hajapanda cheo kwenda juu lazima astaafu kwa sababu sasa mazingira ya kazi yake havitaendana na umri wake. Ndio maana ya utaratibu uliopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie katika hoja za Jeshi la Magereza, Mheshimiwa Lucas Seleli na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, waliuliza kwamba Wizara ina mpango gani kujenga Gereza katika Wilaya ya Igunga ili kupunguza msongamano katika Gereza hilo, nafikiri jibu limepatikana kwenye hotuba yetu ya Bajeti kwamba sasa katika mwaka huu wa fedha tuna mpango wa kujenga Gereza kule Igunga.

Mheshimiwa Lucas Seleli, aliuliza vile vile kuna utaratibu gani wa kupunguza madeni ya muda mrefu ya Wazabuni katika Magereza, jibu ni kwamba madeni yote ya Wazabuni wanaoidai Magereza yamesharatibiwa na yamewasilishwa katika Wizara ya Fedha kule Hazina ili utaratibu wa kuyalipa ufanyike.

Mheshimiwa Job Ndugai, ameulizia habari za Gereza la Kongwa linahitaji trekta jipya. Mheshimiwa Job Ndugai, kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti hatukuweza kusambaza matrekta kila mahali. Mwaka uliopita tulipata matrekta 10 tu, Magereza mengi yalikosa, mwaka huu tunanunua mengine vile vile sio mengi tutaendelea kuyasambaza huu ni utaratibu wa kudumu. Kwa hiyo, kama hatujafika kwenye Gereza la Kongwa na Magereza mengine muwe na subira lakini nia yetu Magereza yote ya kilimo yapate matrekta turudishe utaratibu wa Magereza kuzalisha chakula cha kutosha na kujitegemea kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kwenye ushauri aliotupatia.

Mheshimiwa Job Ndugai vile vile ameulizia tatizo la maji taka Gereza la Kongwa, Serikali tumeshaanza kurekebisha mifumo ya maji taka katika Magereza mbalimbali na Gereza la Kongwa na mengine tutayafikia kwa awamu. Kwa hiyo, naomba awe na subira.



Vile vile ameuliza kuhusu uchakavu wa Gereza la Kongwa, sasa hivi tumeanza kukarabati Magereza lakini tumeanza kukarabati yale Magereza Makuu (*Central Prisons*) tukishamaliza tutaanza kuteremka Magereza haya ya kawaida kwa hiyo tutafika.

Mheshimiwa George Lubeleje, yeye ameulizia habari ya utaratibu wa Bodi za *Parole* kwamba je, tangu Bodi za *Parole* kuandwa, wafungwa wangapi wameachiwa kwa utaratibu huo? Tumemjibu kwamba tangu utaratibu wa *Parole* uanze, imeshafungulia wafungwa 728 na haya ni matokeo ya yale marekebisho tuliyoifanya mwaka jana. Ie sheria ilikaa miaka minne ikafungulia wafungwa watatu tu, mwaka jana Bunge hili hili mkaifanyia marekebisho matokeo ya marekebisho hayo sasa katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu tumeshafungulia 728. Kwa hiyo, ni utaratibu ambao unatusaidia kupunguza msongamano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Juma Kidunda, ameulizia kuhusu ujenzi wa Gereza la mahabusu Kilindi, ukweli ni kwamba tunazo Wilaya hasa hizi mpya 32 ambazo hazina Magereza kabisa ikiwemo pamoja na Wilaya ya Kilindi. Kwa hiyo, tumeshaanza kujenga taratibu kwa awamu, tungekuwa na fedha tungejenga yote 32 kwa mwaka mmoja, fedha zipo kidogo, kwa hiyo, tunajenga kwa awamu. Tunaomba Mheshimiwa Juma Kidunda asubiri zamu ya Wilaya yake.

Mheshimiwa Janeth Mashele, ameulizia habari ya kurudisha Mabaraza ya Vijiji na Kata ili kupunguza msongamano kwenye Magereza. Ni kweli tunao utaratibu wa Mabaraza ya Kata (*Ward Tribunals*) ambayo kwa mujibu wa sheria ya nchi yameruhusiwa kusikiliza kesi na kutoa adhabu huko huko vijijini. Lakini katika Wilaya nyingi hizi *Ward Tribunals* hazifanyi kazi, baadhi ya Wilaya zinafanya kazi na zinasaidia kupunguza msongamano Mahakamani kwa sababu kesi ndogo ndogo hazifiki Mahakamani zinaishia kwenye hili Baraza la Kata. Kwa hiyo, ni ushauri mzuri na tutashirikiana na wenzetu wa Idara ya Sheria na Katiba kwa sababu ndio walezi wa haya Mabaraza ili yaene katika Wilaya zote, yasaidie kupunguza msongamano kule kwenye Mahakama zetu.

Mheshimiwa Janethh Mashele, vile vile ametoa ushauri kwamba wanaofungwa muda mrefu wakishamaliza vifungo vyao tuwape zana za kazi ili wakaanze maisha mapya. Ni wazo zuri lakini kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti tunashindwa kutekeleza.

Mheshimiwa Edson Halinga, ameulizia Gereza la Mbozi amesema litamalizika lini? Mheshimiwa Edson Halinga, Gereza la Mbozi limo kwenye mpango wetu, mwaka 2003 tulitoa shilingi milioni 20 kwa ajili ya kujenga Gereza hilo na mwaka huu vile vile tumetenga fedha kwa ajili ya Gereza hilo. Lengo letu likamilike mwaka huu wa fedha na lianze kutumika.

Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, ameulizia habari ya upanuzi wa Gereza kule kwake, tunasema kwamba upanuzi wa Magereza unaenda sambamba na ujenzi wa Magereza mapya kwenye Wilaya ambazo hazina Magereza kufuatana na upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini. Kwa hiyo, kuna mahali tunajenga Magereza

mapya kuna mahali tunafanya ukarabati na upanuzi kwa hiyo na Kilombero inshallah tutafika.

Mheshimiwa Abu Kiwanga, vile vile alisema kwa nini tunawachanganya watoto wadogo na watu wazima kwenye Magereza? Ukweli ni kwamba kwenye Magereza watoto na watu wazima wanatenganishwa na ndio utaratibu na ndivyo sheria ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Frank Maghoba, aliuliza Serikali inafanya mikakati gani kupunguza msongamano Magerezani. Tunapunguza msongamano kwanza hatua kwa hatua kupanua Magereza yaliyopo, lakini pia tunajenga mapya kwa mfano mwaka huu tunajenga mabweni kule Kyela, tunajenga mabweni mapya ya wafungwa kule Mbarali, Igunga na Mbozi. Vile vile Sheria ya *Parole* nayo tunaitumia kupunguza msongamano wa wafungwa. Vile vile tunayo Sheria ya Kifungo cha Nje (*extra mural labour*), wale wanaofungwa mwaka mmoja kwenda chini iko sheria kuruhusu kwamba wafungwe nje nayo tunaitumia hata jana Mheshimiwa Waziri ametoa mpaka takwimu, wangapi wameachiwa na huu utaratibu wa *extra mural labour*. Iko misamaha ya Rais na jana zilitolewa hapa takwimu Rais kasamehe wangapi na sasa tunaanza kutumia sheria ya *Community Service* watu wenye makosa madogo madogo, wanaofungwa kifungo cha miaka mitatu kwenda chini, tulipitisha sheria hii hapa. Mwaka huu inaanza kufanya kazi lakini kwa Mikoa sita ya majaribio kama alivyovitaja jana Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake.

Kwa hiyo, hawa wenye makosa madogo madogo kwa utaratibu wa sheria hii hawatafika jela, hawatakanyaga Gereza hawa, atafika Mahakamani atahukumwa, anarudishwa kwenye kijiji chake aende akatumikie umma mpaka amalize miaka yake ya adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ameulizia habari za ujenzi wa vyoo ndani ya Magereza, hili nalo vile vile limo katika mipango yetu ya kuboresha mifumo ya maji safi na taka katika Magereza yote nchini lakini tunakwenda kwa awamu.

Kamati ya Ulinzi na Usalama nayo ilitushauri mambo mengi, moja wametushauri kwamba tufufue ile Kamati iliyoundwa mwaka 1991 ile ya kusukuma kesi ambayo wajumbe wake walikuwa ni *DPP, IGP, PCP* yaani Kamishna wa Magereza na Msajili wa Mahakama Kuu. Hili jambo tumeshalizingumza kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na ile Kamati nyingine ya Katiba na tunashauriana na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ili Kamati hii tuifufue ipite tena kama ilivyopita ule mwaka 1991 ili iweze kupunguza msongamano. Vile vile tunawasiliana na Wizara ya Sheria na Mambi ya Katiba ili zile Kamati za kusukuma kesi kwenye Wilaya na Mikoa, *Case Flow Management Committees* nazo zifanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wametushauri kwamba Mabaraza ya Kata na Vijiji yafufuliwe, nimeshalijibu kwamba tutawasiliana na Wizara ya wenzetu ili Mabaraza haya yafufuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wametushauri kwamba Serikali iongeze Mahakimu na Mahakama za Mwanzo ili kesi ziweze kutembea huko, tumelipokea na tutaliwasilisha kwa Wizara ya wenzetu.

Mheshimiwa John Mwakipesile, ametukumbusha habari ya kujenga mabweni ya wafungwa kule Kyela, kwenye hotuba yetu ya Bajeti tumesema kwamba tumetenga fedha kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Paul Ntwina, ameomba Wizara iangalie uwezekano wa Gereza Ngwala kupewa usafiri na trekta. Kama nilivyosema matrekta tunayanunua kwa awamu, Gereza la Ngwala lina uzalishaji mzuri kwa hiyo, safiri ijayo tukipata matrekta litakuwa ni miongoni mwa Magereza ambayo yatapatiwa matrekta.

Mheshimiwa Charles Kagonji, ameulizia ukarabati wa Gereza la Mngaro na hasa kuondoa mitondoo. Tunayo programu ya kuondoa mitondoo, mitondoo ni jambo ambalo limepitwa na wakati yaani watu wajisaidie pale halafu tena asubuhi wabebe kutoa nje, ni jambo ambalo limepitwa na wakati, ni kinyume cha ustaarabu wetu. Kwa kweli sasa tumeshaanza programu kamili ya kupambana na mitondoo na kuiondoa kabisa katika Magereza yetu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ernest Mabina, ameulizia ununuzi wa pampu ya maji Gereza la Geita, nataka kumhakikishia kwamba mradi huo tunao na tayari zimetengwa shilingi milioni 10 kwa ajili ya shughuli hiyo kwa hiyo kazi itafanyika na Mheshimiwa Leonard Shango, yeye anaomba tufufue trekta katika Magereza yake, tutatizama hilo trekta je, linaweza kufufuliwa je, kwa shilingi ngapi kama liko ndani ya uwezo kazi hiyo itafanyika.

Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Gereza lake la Kingurungurundwa, jina gumu kweli, ameomba tumpatie mawasiliano ya *radio call* na *generator* ya umeme. Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, tunaweza tu kuahidi *radio call* lakini *generator* hatuwezi kuahidi moja kwa moja ngoja tuifanyie kazi lakini *radio call* itakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Paul Kimiti, amehoji kama Gereza la Sumbawanga ni chakavu, limefurika wafungwa, hilo tatizo tunalifahamu. Mwaka 2003 tulitenga fedha kidogo shilingi 3,200,000 kuanza kazi na kazi hiyo tutaendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, anasema vitendo vya kulawiti Magerezani vimezidi mno, sijui alifanya utafiti wapi kwa sababu jambo hilo sisi Wizara hatuna habari. Kwanza kupata ile faragha ndani ya Gereza, kupata faragha ufanye mambo hayo sio rahisi ndugu zangu, faragha mpaka ufanye hivyo sio rahisi jinsi unavyofikiria. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Tutoe mifano.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Kwa hiyo, ni dhana tu inadhaniwa lakini *on practice*, sio rahisi kiasi hicho mnachofikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Paul Kimiti, anashukuru Gereza la Mollo tumepeleka trekta. Tunashukuru kwa shukrani hizo na anaomba tuongeze wafungwa ili wapate nguvu kazi katika gereza hilo. Sasa tunaowatumia katika kazi hizi ni wale wafungwa wa muda mrefu na wafungwa wa muda mrefu wapo katika *central prisons* zenye ngome. Sasa pale Mollo siyo *central prison*, lakini sisi tunataka Magereza haya ya kilimo yatumie zana zaidi kuliko nguvu kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Joel Bendera, ametushauri kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani tuunde timu moja ya mpira tukitaka kuwa mabingwa, Polisi, Magereza, Uhamiaji tuunde timu moja ili tupate ubingwa mpaka wa Afrika. Tumepokea ushauri wake. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Semindu Pawa, amesema tunachanganya watu wenye umri mdogo na watu wazima Gerezani. Mheshimiwa Semindu Pawa, sisi tunawatenganisha wala hatuwaweki pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, anasema Gereza liwezeshe kwa kupewa matrekta na *planters*. Tumesikia lakini vile vile tunakabiliwa na hali ya ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hoja ni nyingi sana, naomba mimi niishie hapa ili Mheshimiwa Waziri naye aweze kujibu. Kwa hiyo, nashukuru tena kwa muda ulionipa na nasema naunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa tena fursa hii ya kufanya majumuisho ya mjadala huu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao kwa kweli kwa tathmini yangu nauona ulikuwa mzuri sana sana kwenye kujenga na kutusaidia katika majukumu yetu. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tumepata jumla wa wachangiaji waliosema 26, halafu 103 walioandika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu kwa haraka kabisa niwatambue wote hao. Waliochangia kwa kusema ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Frank Maghoba, Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mohammed Abdully Ally, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz, Mheshimiwa Martha Wejja, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Danhi Makanga,

Mheshimiwa James Musalika na Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Abdulkader Shareef, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Masoud Salim, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Janeth Mashelle, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Ali Sheha Mussa, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Edgar Maokola Majogo na Mheshimiwa Paul Ntwina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Mudhihir Mohammed Mudhihir, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Mohammed Ali Said, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid na Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine vile vile ni Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Ali Ameir Mohammed, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Kepteni Theodos Kasapira, Mheshimiwa Jumanne Hamisi Nguli,

Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Danhi Makanga na Mheshimiwa Mohammed Khatib, wote hao nawashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wingi wa michango hiyo bila shaka Waheshimiwa Wabunge watatuvumilia kwamba hatutaweza kujibu kila swali au hoja iliyotolewa katika majumuisho haya, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba majibu ya kimaandishi tutayaandaa na yatawafikia baada ya kuyahariri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kutoa shukrani kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa taarifa yao ambayo imetoa maelekezo mengi na mapendekezo mengi ambayo yote tunayapokea, tunayakubali na tutayafanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Frank Maghoba, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa maelezo aliyoyatoa kuhusu Wizara hii, kapongeza palipostahili kupongeza, kakosoa alipohisi akosoe na kutaka ufafanuzi baadhi ya sehemu ambazo alipenda ufafanuzi na aliwasilisha si kwa jazba. Kwa hiyo, nampongeza na namshukuru kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kuelezea kwa mambo ya jumla. Kwanza nitaanza na hili moja ambalo limesemewa na wengi wakati mwingine kwa jazba. Mimi napenda nichuje jazba zote niziweke upande. Sasa nitazame hoja tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yenyewe ilihusu hii nyongeza ya Jeshi la Polisi, Mheshimiwa Naibu Waziri amelizungumzia. Mimi kwa kifupi kabisa napenda nitaje vipengele vitano ambavyo hasa ndivyo tulivyoelekeza nguvu zetu katika nyongeza ya Bajeti ya Jeshi la Polisi. Kwanza ni ununuzi wa magari kama tulivyosema yale pamoja na ukarabati wa boti saba za maziwani, *Lake Tanganyika, Lake Victoria* na *Lake Nyasa*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgao wa magari napenda kuchukua fursa hii kuwahakikishia Wabunge kwamba kila Wilaya tunaihakikishia gari imara. Kilio cha mwaka jana ilikuwa kila mmoja anaomba gari la *OCD*. Kila *OCD* atapata gari baada ya bajeti hii. Waheshimiwa Wabunge baada ya kuona kwamba idadi ile ya magari ni kubwa na wakawa wanajua kwamba ma-*OCD* watapata magari, sasa hivi wamechangia hasa vituo, wamekuja *down* kwenye vituo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sitoahidi kwamba kila kituo tutakipatia gari. Tupeni fursa nyingine tukalifanyie kazi tena kwa ajili ya Bajeti ya mwakani. Lakini kwa magari yale ambayo *OCD* alikuwa nalo, baada ya kupata jipya yatafanyiwa *reallocation*. Sasa katika kufanya kazi hiyo tutazingatia vilio vya Waheshimiwa Wabunge, maeneo ambayo yana unyeti wa aina yake ili magari kama hayo yapelekwe huko kuhakikisha usalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni kuimarisha mawasiliano ya Jeshi la Polisi nchi nzima. Hilo ndilo eneo la pili ambalo tumeelekeza matumizi makubwa.

Kwenye hotuba yangu nimetaja mtambo wa Dar es Salaam, ule mtambo una *component* moja ya huduma ya 999 Dar es Salaam, lakini *component* nyingine ni ya kuunganisha Makao Makuu na Mikoa yote. Kwa hiyo, kutakuwa na mawasiliano ya nchi nzima pamoja na *network* ya *radio calls* kwa nchi nzima. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni kuongeza Bajeti ya *operations* za Polisi. Ni kilio cha Waheshimiwa Wabunge muda mrefu mpaka wakati mwingine wanatwambia mfanye *joint operations* na Jeshi la Wananchi na nani. Kwa hiyo, tunaongeza Bajeti ili kufanikisha *operations*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nne, tumeomba fedha kwa ajili ya posho za askari wanapokwenda katika *operations* na kazi maalum kwenye vituo vya uchaguzi, kwenda kusimamia usalama katika vituo vya uchaguzi. Tulikuwa na utata huko nyuma ambao mwaka huu tunataka tuondoe. Tulipokuwa tukipeleka askari wetu kwenye vituo vya uandikishaji au vya kupigia kura, tulikuwa tunatarajia Tume za Uchaguzi ndio ziwalipe wale askari na wakati mwingine tulizungumza nao walituhidi hivyo. Ukifika wakati wa utekelezaji hali inakuwa ngumu kibajeti, matokeo yake askari wanakosa huku na huku. Tunaondoa utata, safari hii posho tunawalipa wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tano, tunaongeza mafuta kwa kiwango kikubwa kwa ajili ya matumizi ya gari la Jeshi la Polisi. Mimi nadhani baada ya ufafanuzi huo sioni haja ya Mheshimiwa yeyote kuwa na wasiwasi wa nyongeza hii. Nia ni njema ya kuhakikisha kwamba Jeshi letu la Polisi linafanya kazi nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni Jeshi la Polisi kutofungamana na upande wowote wa kisiasa au Jeshi la Polisi kutojihusisha na siasa.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba jitihada zetu zote ni kujenga Jeshi ambalo halina mwelekeo wowote wa kisiasa. Wapo Waheshimiwa ambao walitaja kesi ambazo walihisi zimeshughulikiwa kwa haraka kama kesi ya Mheshimiwa Anne Kilango kwamba imeshughulikiwa haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie kwamba na ile *incident* ya Bukoba kule nayo tumeishughulikia vizuri na wale wote tuliowatumu tumewashika. Sasa kule imemhusu kiongozi wa Chama cha Upinzani na waliowakamata ni Polisi hawa hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bariadi kulikuwa na *incident*, Polisi kwa kweli waliingilia kati. Watu wa pande mbili wamejaa mishawasha ya kisiasa mpaka wanarushiana mawe, wameingia Polisi kusuluhisha na waliowatumu kwamba wanahusika waliwashika wote bila kujali ni *UDP*, *CUF* au *CCM*, wote walikwenda ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya mwenyewe amekiri Bungeni humu kwamba Jeshi la Polisi lilikwenda na anaamini kwamba lilikwenda

kumwoko. Kwa hiyo, hilo ndilo Jeshi la Polisi tunalolijenga. Lakini tunataka tusaaidiane wote viongozi wa kisiasa, kwa sababu tunaposema lisijihusishe na siasa sasa na sisi wanasiasa tusilihusishe hata kidogo. Wakati mwingine tunalionyesha vidole kwamba Polisi wamefanya hivi, wamesaidia Chama hiki na ndugu zangu wa Upinzani nataka niwahakikishie hizo shutuma hata huku CCM zinatoka, huwa nazipata huku, maana huwa mnafikiri ni ninyi tu. Huwa tunapata, Polisi wako hapa bwana wanashabikia Upinzani, ukija huku mnasema ahaa, Polisi wanasaidia CCM. Polisi huwa wanafanya kazi zao, sasa wakimshika mtu asikimbilie kwenye itikadi ya Chama.

Kwa hiyo, wote naomba tuzingatie sheria, tuongozwe na sheria katika utendaji wetu wa kazi za kisiasa. Majibizano ya jazba hayasaidii hata kidogo na wala hayaashirii mema kwa usalama wa nchi yetu. Kwa sababu ukimchokoza mwenzio na yeye atajibu kwa jazba vile vile. Matokeo yake mtajikuta mnachokozana, mnachokozana, mwisho kweli moto unawaka na hii si kwa manufaa ya mtu yeyote. Kwa hiyo, hilo ndilo ombi langu, tusaaidiane kulisaidia Jeshi la Polisi lifanye kazi zake. Sisi tufanye siasa zetu lakini nani atashinda uchaguzi, uamuzi tuwaachie wapiga kura wenyewe. (*Makofi*)

Nigusie lingine la jumla juu ya *Dual Nationality*. Mheshimiwa Bernard Membe, alipokuwa akichangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, alipendekeza kwamba tuondokane na utaratibu wa kutazama wazazi, mradi mtu akishazaliwa Tanzania tu awe ni raia bila kutazama baba yake au mama yake ni Mtanzania au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ya mjadala, mimi nadhani tuendelee kuyajadili Kitaifa, kila mmoja anapopata fursa atoe maoni yake. Lakini kwa sasa hivi kwa hali ya sasa hivi, mimi naona si wakati muafaka kutekeleza lolote kati ya haya. Nadhani moja, tuhakikishe kwamba hili tatizo la wakimbizi tunalimaliza maana ukianza kuzungumzia juu ya *Dual Nationality* hata wakimbizi wale waliopo mipakani tunaowapigia kelele kila siku wataanza kusubiri kwanza. Halafu mipakani tutazame mwananchi yupo mpakani baina ya Kenya na Tanzania ni raia wa nchi zote mbili. Ukifika wakati wa uchaguzi Kenya ana haki ya kupiga kura na ukifika wakati wa uchaguzi Tanzania ana haki ya kuja kupiga kura Tanzania.

Sasa yote hayo tuyazingatie. Halafu ukisema kwamba kila anayezaliwa Tanzania kwa *at least* kwa wakati huu unaweza kugundua karibu nusu ya wale wakimbizi ambao tunapiga kelele waondoke, tunaweza kujikuta kwamba wameshakuwa Watanzania *overnight*. Kwa hiyo, ndiyo maana nikasema tuendelee kulijadili, ukifika wakati pengine tutalitazama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili suala la mtu kuzaliwa tu akapata uraia, Mheshimiwa Bernard Membe amesema limepitwa na wakati na akasema nchi nyingi zina mwelekeo huo.

Mimi nilikwenda kulifanyia *research* kidogo, nikaenda kwenye *internet* nikatazama Katiba za nchi zote nilizoweza kuzipata, zilizoandikwa Kiingereza maana nyingine za Kifaransa na nini sikuweza kuzisoma. Lakini katika nchi kumi na nne za Afrika hasa majirani wetu, kwanza *East Africa* yote bado sheria yetu ni ya namna moja,



*SADC Region* wote bado tuna utaratibu huu. Nikaenda kwenye *Commonwealth* nikakuta nchi nyingi bado zinakwenda na utaratibu huu.

Katika nchi kumi na nne nilizoweza kuzitazama, kumi na moja zote zinakwenda na utaratibu huo na ni tatu tu ambazo mtu ukizaliwa tu moja kwa moja, ukiondoa wale wakubwa bila shaka natazama nchi za aina yetu, nikaona Jamaica, *Saint Vincent and in Grenadines* na India. Sasa wengi bado tunakwenda hivyo labda hilo niliweke hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la rushwa na ubambikizaji wa kesi. Hili ni tatizo moja na ubambikizaji wa kesi unatokana na rushwa na hili tunalielewa kule Wizarani na tunalifanyia kazi. Hata mimi kila ninapokwenda kutembelea Magereza mengi, kilio kikubwa ni hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata sisi Wizarani tunalizingatia na tunalifanyia kazi tukishirikiana na *PCB*. Tunajitahidi kuelekeza mbinu pamoja na hii ya kuwakamata ambao tunawashika tukiwapata na ushahidi kwamba wamejihusisha na rushwa kama nilivyoieleza kwenye hotuba, lakini tunajitahidi kutazama maeneo ya kuziba mianya ya rushwa.

Kwa hiyo, tumo katika kutazama upya taratibu zetu nyingi tu, miongoni mwa hizo ni utaratibu ambao upo sasa hivi wa askari wetu hasa wale wa barabarani kwamba wanapokamata magari halafu wanaingia humo humo ili afuatane nalo kwenda kituoni. Sisi huo tunauona ni mwanya wa rushwa tunautafutia njia ya kuuziba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuzidi kulegeza masharti ya dhamana ili kupunguza huo ubambikizaji, kuboresha mazingira ya kazi, halafu tutajitahidi kupunguza urasimu katika utendaji wa kazi zetu mbalimbali pamoja na suala moja ambalo limetajwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa walipokuwa wakichangia la utoaji wa *passport*.

Ni kweli ukisema *passport* zitolewe Zanzibar tu na Dar es Salaam tu umeweka mwanya wa rushwa. Huu ni mwanya ambao nao tunataka tuutazame, tunatazama njia nzuri za ku-*decentralize* ili kupunguza huu uwezekano wa rushwa na kurahisisha utaratibu. Miongoni mwa mambo hasa katika utoaji wa *passport* yanachangia hasa pale tulipopungukiwa na *passport*. Zilipunguka kidogo ikabidi utaratibu uwe mgumu. Wakajitokeza mawakala ambao wanamwambia mtu bwana nipe mimi hii kazi nikakufanyie, mimi kule nina uenyeji mkubwa, lakini mle unipe na shilingi ishirini, kama hujatoa ishirini inakuwa kazi ngumu. Sasa ishirini anakaa nazo yeye, lakini wewe mwananchi wa kawaida utaona kumbe tatizo lipo Uhamiaji. Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo tunayashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu eneo la kusaidia nguvu za wananchi. Katika maandiko yale na michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi kila mmoja ametaja eneo moja au mawili ambapo wanahitaji msaada wa Serikali, wananchi wamefanya, wamejitahidi, kwa hiyo, Serikali iwasaidie. Nataka niwahakikishie wale wote ambao

mpaka leo nimewapa ahadi, ahadi za nyuma na nilizozitoa mpaka leo nawahakikishia kwamba ahadi hizo tutazitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Natron kule ya Mheshimiwa Lekule Laizer, kuna Simanjiro, Mchinga, Ikola na Karema ya Mheshimiwa Margareth Bwana, kuna vituo viwili kule Nyumba ya Mungu vya Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kuna Siha na vingine. Kama sikukitaja atakuja kuniambia tu.

Mheshimiwa Samwel Chitalilo, aliomba tukamfungulie kule kituo chake cha Nyakariri tutakwenda, kuna kituo cha Kibaigwa hakijafunguliwa, tutakifungua na kukipatia askari. Mheshimiwa Anatory Choya, ameniambia kule wananchi kule Biharamulo wamejenga jengo la matumizi ya kijamii *(Police Welfare Building)*. Tutamchangia nguvu na wengine waliotaja vituo vingine kama vile Bumbwini na Chwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kuhusu ukarabati *Mbamba Bay*, nadhani ni ahadi yangu hiyo tokea mwaka jana, Makambano, Mabatini- Mwanza, nyumba za askari, *Ng'ambo Station* kwenda kuitembelea na vingine, ahadi ambazo mpaka sasa hivi tutakuwa nazo na nilikwishawahakikishia Waheshimiwa Wabunge tutazitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujambazi lilizungumziwa sana tena kwa hamasa na uchungu. Ni kweli wote linatumiza na tunajua ni kubwa kama nilivyokiri kwenye hotuba yangu. Lakini na jitihada Waheshimiwa Wabunge wanazona kwamba panapotokea tukio tunawakamata na siku hizi ukamataji ni mzuri, hatuchukui muda mrefu, kwa kweli tunawashika na kesi karibu zote zipo Mahakamani. Tunachukua himizo la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kwamba nchi isilale usiku, nchi iwe macho mchana na usiku, ndiyo hizi juhudi ambazo tunakwenda nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, aliuliza nini maana ya amani na utulivu tuliyoizungumza pale? Tunasema katika kipindi hiki tunashukuru Mungu hatukukumbana na tatizo la ugaidi. Hicho kingekuwa ni kitu cha kuhatarisha amani ya nchi na wala hatujafika mahali tukawa tuna mapigano ya wenyewe kwa wenyewe. Hayo ni mambo ambayo ungesema kwamba yamehatarisha usalama wa nchi. Matukio yanatokea, lakini mengi ni *local*, litatokea kama Morogoro, Mwanza lakini tunayakabili, hayajafikia kiwango hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wanaonyemelea Majimbo aliyosema Mheshimiwa Samwel Chitalilo, ile si kuhatarisha amani ya nchi. Kama anayenyemelea Jimbo lako ni mwanachama mwenzio wa Chama chako anahatarisha usalama na amani yako. Kama ni mwanachama wa Chama tofauti, pengine anahatarisha Chama chako.

Kwa hiyo, tulitazame hivyo si kwa maana ya kutazama vinginevyo, lakini dawa yake ni nzuri, dawa yake ni *delivery* tu ambayo Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani mmeifanya katika kipindi cha miaka minne hii iliyopita na mwaka unaokuja. Naamini kabisa juhudi zenu wananchi wanazona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba pamoja na juhudi hizi tulizozieleza humu, tuna mpango wa maendeleo wa miaka kumi ambao umo katika maandalizi na hili ninajibu lile swali ambalo Mheshimiwa mmoja alilizungumzia kuhusu matatizo ya nyumba. Tunataka tuyamalize, hili ndilo lengo letu, tulimalize tatizo la nyumba za askari, majengo ya vituo mbalimbali vya Polisi, Magereza na vyote.

Tuna mpango wa miaka kumi ambao una-*cover* Polisi, Magereza, Zimamoto, Uhamiaji na Chuo cha Mafunzo Zanzibar ambao gharama yake ni trilioni 1.3. Maana kama tunazipata hizo ndiyo unaweza ukasema kwamba matatizo yote yatamalizika na si katika mwaka mmoja, ni katika kipindi cha miaka kumi. Kwa hiyo, miongoni mwa mambo ambayo tayari tunayafanya sasa hivi tunayamegua kutoka kwenye huo mpango wa miaka kumi na utakapomaliza tutautoa rasmi na utakuwa *incorporated* katika Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge walizungumza kuhusu matatizo ya kuchelewa kutolewa kwa mafao. Haya tunayafanyia kazi, wamo Waheshimiwa Wabunge walituletea, wamekiri kwamba tumeyashughulikia, lakini tulipoyashughulikia yale ya watu wao, tuliwashughulikia na wengine wote.

Kwa hiyo, ukiona kwamba mtu wako alikwamuka, kwa kweli limekwamuka kundi zima lililofanana naye. Tatizo lenyewe ni kwamba sisi siyo tunamaliza huo mchakato, sisi tunaanza tu pale ambapo inabidi tumalizie Hazina. Nadhani tungekuwa ni wenyewe tu tungekuwa hatuchukui muda mrefu. (*Kicheko*)

Kumezungumziwa kuchelewa kwa vyeo. Mwaka huu tuliwapeleka kwenye *training* askari wote ambao walikuwa na zaidi ya miaka 20 hawajapandishwa vyeo. Kwa hiyo, tunafanya *mass promotion*, tukienda mwaka huu tutatizama wa miaka 15 kidogo kidogo mpaka tutawamaliza na wakati Jeshi letu linakua na nafasi hizo za vyeo zitazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda unanikimbia, sikuweza kuingia kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge mmoja mmoja, lakini kama nilivyosema yote tumeyachukua, ahadi zote tulizozitoa tumezitoa kwa uhakika tutazitekeleza. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote watuungane mkono katika kuhakikisha tunafanikisha majukumu yetu ya kuhakikisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

#### FUNGU 28 - WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI - *POLICE FORCE*

Kifungu 2001 - *Police Mainforce* ... .. 57,830,842,800/=

**MWENYEKITI:** Naomba msimame hivyo hivyo tutaanza na upande huu. Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nataka tu kupata maelezo. Mheshimiwa Waziri amesisitiza na kujibu kwa ufasaha kuhusu vipengele vitano vya maendeleo. Kifungu 2001 Mshahara wa Waziri.

Kuhusu ambavyo Serikali itatoa mafuta, magari ya *OCD* na vitu vingine, lakini katika michango ya jumla kulikuwa na kilio cha Waheshimiwa Wabunge kuhusu Polisi wanavyokaa na familia zao na kwamba Serikali lazima wengine iwajengee nyumba kwa sababu mambo mengine yanaabisha jinsi wanavyolala. Sasa nakumbuka tu kidogo amegusia Mheshimiwa Waziri, kwamba kuna mpango wa miaka kumi ambao unahitaji trilioni moja na bilioni mia tatu.

Sasa ninachotaka kujua kwa kifupi tu tunataka atuhakikishe kwa sababu Jeshi la Polisi lina nguvu sana, lina watu wa magereza, tunaomba washirikiane na JKT wako watu wanashinda pale wanapiga miguu, Magereza wenyewe wanashinda pale eti wanalinda ng'ombe. Jinsi ambavyo Serikali kwa miaka mitatu, minne inaweza ikaleta programu ya muda mfupi ya kuwajengea askari nyumba za kudumu za kukaa hao Polisi, badala ya kukaa kwenye vibanda wakati wa baridi ni baridi na wakati wa jua kama yale mabati yanapata joto kweli kweli. Sasa hiyo ndiyo tunataka atwambie mpango wa muda mfupi ambao Serikali itawahakikishia kwamba mtu analala na mke wake wanajisikia vizuri siyo kuwaacha kwenye vibanda vile kama vya watoto wadogo. Ndiyo tunataka kujua hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, naomba usubiri kwenye kitabu cha maendeleo. Kwenye *aspect* ya maendeleo ujenzi na mipango ya ujenzi itakuwa kwenye maendeleo au huko mbele kuna *Police Building* ya 6001 utacheiki pale.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake ila tu nilikuwa nimeomba mambo matatu. Lakini katika hayo nitaomba mawili ambayo nilikuwa nimesisitiza kuhusu ujambazi.

**MWENYEKITI:** Unazungumzia kifungu gani?

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Ninazungumzia *Sub Vote 2001*.

**MWENYEKITI:** Kifungu 2001 sawasawa.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, kwa kweli bado kilio changu kiko pale pale na kama nilivyosema kwamba ninawaamini sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa utendaji. Sasa nilichokuwa nategemea ni kwamba Mheshimiwa Waziri ange-*declare* katika Bunge hili kwamba vilio vya Waheshimiwa Wabunge amevisikia na ana-*declare*. Kwa hiyo, ninachokisubiri nataka a-*declare* kuhusiana na majambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tumezuiwa kusafiri usiku, mama mmoja alikuwa anatoa kilio anawahi kwenye msiba, alifikia kutoa maneno ambayo yalinichoma sana mimi kama Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kama hivyo unavyotaka Mheshimiwa Waziri amefanya *declaration* amesikia, usiendee kuhutubia maana siyo nafasi ya hotuba, maana unapomtaja huyo mama unaendelea na hotuba tena.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, namuahirisha huyo mama. Sasa ninachoomba Mheshimiwa Waziri atoe *declaration* kwamba kuanzia leo na kwa vile tumepata mafuta ya kutosha tutafanya *patrol* kuhakikisha kwamba sasa wananchi wanasafiri usiku bila tatizo. Tunaomba a-*declare*.

Halafu la pili, nilikuwa nimemwomba Mheshimiwa Waziri kwamba kweli kuna tatizo kule Jimboni vijana wawili waliuawa. Sasa namwomba pia kwa vile hawezi kuwa na jibu hapa na haliwezi kulipata kama Mheshimiwa Waziri. Naomba iundwe Tume ndogo ya kwenda kupata ukweli halisi wa hili jambo ili angalau tuwape wananchi ukweli halisi ni nini kilitokea badala ya kuwa kila kukicha wanaendelea kulia na kuuliza. Kwa hiyo, naomba hayo mambo mawili.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu la kwanza mimi nadhani tumeshatoa *declaration* ya mapambano dhidi ya ujambazi. Aliitoa kauli hiyo Naibu Waziri na mimi katika maeneo ambayo nimeweka wazi hapa ni kwamba tumeelekeza fedha nyingi ni katika *operations*. *Operations* ndizo hizo za kuhakikisha usalama katika maeneo mle kote ambako kuna matatizo ya usalama ni kuhakikisha kwamba tunarejsha usalama kama kulikuwa na ujambazi. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi tutalitekeleza hili katika sehemu mbalimbali ambazo sasa hivi hazisafiriki kwa urahisi usiku zitasafirika tu.

Halafu hilo la pili, ningepomba maadam ameisha-*declare* mwenyewe kwamba ametuamini, mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri wangu hapa kwamba anatuamini, basi naomba atuamini kwamba hili suala kwa kweli tumelichukua na tumekubaliana kwamba tutalichunguza wenyewe sisi Mawaziri kujua kweli wake na tutamuarifu Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *programme 20, Sub-vote 2001*. Jana nilipochangia nilimwomba Mheshimiwa Waziri aone utofauti wa uzito wa kazi miongoni mwa watendaji katika Wizara yake kwa maana ya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto, na nikaeleza kwamba nadhani haikuwa sawasawa kwa vyombo vinne vyote mishahara yao kuwa kwenye scale moja. Nikapendekeza kwamba Polisi watazamwe zaidi kutokana na ugumu na uzito wa kazi zao. Lakini alipo-*wind up* hapa sikupata maelezo yoyote. Jana nilimwambia kwamba asilimia 10 naisubiri leo atakaponipa maelezo. Naomba tu Mheshimiwa Waziri aniambie anafikiria nini kuhusu ushauri wangu ule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, unaweza kusubiri mpaka *General*. Fungu namba 51 ulingoje kwenye *general* ambako maelezo yote utayapata.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Programme 20, Police Operations, Sub Vote 2001*, katika mchango wangu wa maandishi nilipenda nijue kule Jimboni kwangu kuna Kata nyingi ziko karibu na mpaka wa Uganda. Kwa hiyo, natambua umuhimu wa kuwa na vizuizi mbalimbali, lakini upande wa Kashenyi na Kanyingo kabla ya kufika Kata ya Kashenyi kuna Kata ya Kanyingo sasa pale kwenye Kata ya Kanyingo kimewekwa kizuizi na ikifika saa mbili za jioni magari kutoka Kata ya Kanyingo hayaruhusiwi kwenda Kata ya Kashenyi, lakini ukipita kwenye hicho kizuizi unafika kuna Kituo cha Afya.

Kwa hiyo, hata kama mtu anaumwa ni mahututi, haruhusiwi kupita kwenye kizuizi ikafika saa mbili usiku. Sasa wananchi wamenituma niulizie ni kwa nini wanazuiliwa kutembea ndani ya nchi yao mara tu inapofika saa mbili usiku?

Mimi ningependa Mheshimiwa Waziri atoe maelezo, je, anaruhusu Watanzania waendele kuzuiliwa ndani ya nchi yao kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine ukizingatia hasa pale Kata ya Kanyingo kwenda Kata ya Kashenyi maana Kata ya Kashenyi ni sehemu ya Tanzania na walinipigia kura naendelea kuwatambua kama watu walio sehemu ya Tanzania. Kwa hiyo, kuwazuia kwamba wasiende kule mimi kama Mbunge sikubaliani nalo naomba Mheshimiwa Waziri aeleze kwa nini wanaweka kizuizi kama Polisi wanahitaji kizuizi hicho basi wakae pale masaa 24 wasizuie mtu yeyote kwenda Kashenyi au kutoka Kashenyi kuja Kata ya Kanyingo au kwenda kwingineko.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge aturuhusu ili na sisi tupate nafasi ya kuyaelewa kwa undani zaidi hayo mazingira yalivyo huko. Kwa sababu katika hali ya kawaida hatuzui mienendo ya kawaida hasa kama ziko katika mazingira ya usalama.

Sasa naomba atupate muda ili na sisi tujue kama sababu hasa nini na kama ni yetu Polisi maana pengine hata siyo Polisi pengine wanatumiwa na mamlaka nyingine. Kwa hapa sitoweza kujibu mara moja ametuandikia kweli, lakini ni taarifa ambayo ndiyo

kwanza tumeipata na hatujaweza kuwasiliana na wenzetu katika kipindi hiki kifupi tukajua ukweli.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilifikiri tunapokuwa kwenye Bajeti ndiyo maana Maafisa wote katika Wizara wanakuja hapa Dodoma wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara. Nilifikiri maana yake ni kuja hapa ili Waheshimiwa Wabunge wakihoji chochote basi waweze kupata majibu haraka. Lakini ndiyo maana nilichangia kwa maandishi mapema ili Wizara iweze kufuatilia. Sipendi kusema kwamba wamezembea kutolizingatia hilo na kufuatilia na sina sababu ya kutompata muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wasiwasi wangu isije ikawa hapa anachohitaji ni fedha maana tatizo tukishapitisha Bajeti huwa nasikia Wizara mbalimbali zinafanya sherehe ingawa sijui umuhimu wa sherehe hizo kwa sababu kama fedha si zao. Kwa hiyo, isije ikawa kwamba sasa tukishapitisha basi baada ya hapo wafanye sherehe. Sasa aeleze ni muda gani nimpe na yeye atakuwa tayari lini kupata taarifa hizo na mimi sina wasiwasi akishatamka hivyo basi nitajua atalifanyia kazi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani asiondoke kwanza na mawazo kwamba hapa tunaomba fedha tu tukimaliza tunakwenda kufanya sherehe. Nadhani amewasikia Waheshimiwa Wabunge wengi walipokuwa wakichangia hapa wakikiri tulivyoyashughulikia masuala yao waliyotupa. Kwa hiyo na yeye napenda nimhakikishie tatalishughulikia, namkaribisha na yeye awe karibu na sisi. Mimi kujiweka *on safe side* namhakikishia ndani ya kipindi cha miezi miwili tutampatia jibu, lakini nina uhakika kabla ya hapo tutaweza kupata jawabu. (*Makofi*)

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mawazo yangu nitayatoa kwenye hoja inayokuja. Ahsante.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko kwenye *Sub Vote 2001 - Police Mainforce* kifungu kidogo cha 270300 *Vehicles and Mobile equipments*.

Mimi natoka Wilaya ya Nzega ambayo inapakana na Wilaya ya Igunga nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo amesema Wilaya ya Igunga watajengewa gereza. Lakini kwa sasa na mwaka 2003 Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba angeweza kutupa gari kwa ajili ya kusafirisha mahabusu kutoka Igunga ambako huwa wanakuja kwenye mahabusu ya Nzega. Sasa hivi amesema watoa magari kwa ajili ya *Ma-OCD*. Je, lile ombi la gari ambalo aliahidi toka mwaka jana la Mobile la kuwasafirisha Mahabusu wanaokuja kutoka Igunga kuja Nzega na kuwarudisha kwenye kesi ili kupunguza mlundikano kwenye gereza la Nzega analionaje?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye bajeti hii kuna *provision*

ya magari ya kusafirisha mahabusu na wakati tunaipanga hiyo na Nzega tulikuwa nayo kichwani, kwa hiyo, asiwe na wasiwasi katika hili. (*Makofi*)

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yangu nitayatoa kwenye *General Vote*, namba 51.

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye programu hiyo hiyo 20, *Police Mainforce*. Nataka tu suala la utawala nina maelezo kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumekuwa tukiomba Kituo cha Polisi kwenye Mji mdogo unaoitwa Gallapo na wananchi wameshafanya shughuli za ukarabati kama nilivyomwandikia Mheshimiwa Waziri, lakini sasa imechukua muda mrefu kidogo na mahitaji ya Kituo hiki sasa ni muhimu kwa sababu sasa barabara kubwa itajengwa kati ya Babati na Makao Makuu ya Wilaya za Simanjiro na Kiteto. Sasa nataka anihakikishie tu kwamba Kituo hiki cha Gallapo kitafunguliwa lini? Maana imeshapita miaka ya kutosha na nimekuwa nikifuatilia kwa muda tangu tulipokuwa kwenye Mkoa wa mmoja wa Arusha. Sasa ningependa kupata maelezo hapo.

Lakini la pili, vile vile ni suala la utawala. Kwanza, nipongeze kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kila Wilaya sasa itapata gari ya *OCD* tunashukuru kwa hilo. Lakini akasema najua mkimaliza hapo tunakwenda kwenye Vituo. Sasa kuna Kituo ambacho hata mwaka jana nilikichangia Kituo cha Magugu ambacho nacho ni kikubwa. Sasa aniambie katika utaratibu huu wa sasa kama Kituo hicho sasa kitafikiriwa kupata gari au namna gani? Ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu ufunguzi wa Kituo cha Gallapo tutatuma Maofisa wetu waende wakakigie kuona ni kwa kadri gani kinakidhi haja kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunakifungua ndani ya kipindi cha mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimuahidi hivyo Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto mwaka 2003 naye tumemtekelezea, kwa hiyo, na yeye tutafanya hivyo hivyo. (*Makofi*)

Kuhusu suala la magari ya vituo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengine wote kwamba wametupa maombi waliokwisha tupa na waliokuwa hawajatupa watupe, lakini naomba watupe nafasi ili na sisi tuyachambue hali kwa upeo wa nchi nzima. Kwa sababu kama nilivyosema hatuna magari ya kupeleka kwenye vituo vyote. Kwa hiyo, katika kugawa tutazingatia hali ilivyo ya kiusalama katika kila eneo, ombi la Mheshimiwa Mbunge, lakini nikianza kusema hapa wewe nitakupa na mwengine nitakupa mwisho nitajikuta sina magari yamekwisha yote. Sasa naomba wanipe hiyo fursa ili tuya-*study* kwa upeo mpana zaidi.

**MHE. JUMANNE H. NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Programme 20 Sub Vote 2001.*



Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu ambalo nataka nifahamu na nililichangia kwa maandishi ni kwamba kuna tatizo lililotokea kwa mwananchi wangu mmoja kule Jimboni. Alipigwa risasi na kuvunjwa mguu na Askari Polisi wawili ambao walikwenda kumingilia usiku. Sasa tatizo hilo nilishamweleza Naibu Waziri, nikampelekea kwa maandishi na yule kijana alifika hapa Dodoma wakati tukiwa Bungeni akaonana na Naibu Waziri, akamwambia kwamba angemshughulikia kwa muda mfupi na ukweli ni kwamba aliandika barua na akanipa nakala kwa *IGP*.

Sasa mpaka wakati huu hakuna jibu lolote ambalo limepatikana na yule bwana amelemaa na mguu wake sasa hivi unahitaji matibabu alikuwa ameahidiwa kutibiwa, lakini hawakumshughulikia kumtibu alikwenda Hydrom hospitali mpaka bili ikafika shilingi 600,000/=, lakini hakuna mtu ambaye alijishughulisha kwenda kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maafikiano ni kwamba Polisi walikuwa wamemwombwa yule kijana asishitaki kwa sababu kwa kweli walikuwa wamemkosea. Kisa cha kufanya hivyo ni kwamba yule alipigana na mdogo wake kwa sababu mdogo wake alikuwa anavunja maadili analeta kijana huyo wa Polisi mle ndani ya nyumba. Sasa yule kijana akaona si vizuri akamgombeza, baada ya kumgombeza nafikiri alipokwenda kumwambia yule rafiki yake ambaye ni kijana wa Polisi ndiyo wakaondoka usiku kuja kupiga yule kijana tena walimfanyia vitu ambavyo si vya kawaida. Kumwamsha usiku uchi na mke wake na kuanza kumshambulia. Sasa katika purukushani akatoka mbio kukimbia wakashuti na bunduki wakamvunja mguu. Nimeomba nielezwe hayo kwa sababu imeshakuwa muda mrefu. Sasa sijaelezwa hilo. Naomba nipate jibu ni vipi huyu kijana atashughulikiwa ambaye mpaka sasa hivi mguu wake amelemaa na mfupa karibu uko nje. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge alileta hilo tatizo na huyo bwana ni kweli alimleta mpaka hapa Bungeni tulionana naye akaeleza tukio lenyewe. Baadaye tuliwasiliana na *IGP* uchunguzi ulifanywa hadithi yenyewe ni ndefu, lakini kwa kifupi ni kweli kulikuwa kuna ugomvi hapo nyumbani. Huyo aliyepigwa alikwenda Kituo cha Polisi kuripoti kwamba nimepigwa na nimeumizwa.

Kwa hiyo, ukimpiga mtu ni kosa la jinai, Polisi walikwenda kum-*arrest*, katika kum-*arrest* yule bwana alifanya fujo. Kwanza, alikuwa amelewa sana akataka kuwapiga kwa chupa, lakini baadaye akaanza kukimbia. Sasa mhalifu anapokimbia kwa tatizo la Polisi katika kumfanya asikimbie unampiga miguuni. Ndiyo taratibu zenyewe na ndivyo walivyofanya wale Polisi, kwa hiyo walimpiga miguuni risasi wakam-*arrest*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya hapo kilichotokea ndiyo hayo malalamiko ambayo mpaka yakatufikia. Alipopigwa akaenda kutibiwa hospitali karibu miezi sita alikuwa yuko hospitali anatibiwa. Alipomaliza kutibiwa ndiyo yakatufikia sisi. *IGP* akaagiza uchunguzi ufanywe, ukafanywa. Sasa hoja pale ikawa je, Polisi katika kum-*arrest* walitumia nguvu sawasawa, ama walitumia nguvu za ziada? Hilo ndiyo lilikuwa suala ambalo lilikuwepo. Wale Polisi wakafikishwa kwenye Mahakama ya

Kijeshi kule Singida ile Mahakama imeishakamilisha tunapozungumza sasa hivi na mapendekezo yapo Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Makao Makuu ya Jeshi la Polisi watatoa uamuzi haraka iwezekanavyo kuhusiana na hatma ya hilo tukio lipo na uchunguzi umekamilika kesi ya Kijeshi kule kwa *RPC* ameshamaliza. Kwa hiyo, sasa suala liko Makao Makuu ya Polisi na *IGP* ametuahidi kwamba atalimaliza mapema iwezekanavyo.

**MHE. JUMANNE H. NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kubishana na ndugu yangu, lakini ninalotaka kuliweka wazi ni kwamba huyu bwana kama angekuwa na makosa yanavyosemekana kwa kweli alikuwa anatakiwa kushitakiwa, tangu wakati ule huyu bwana hajashitakiwa na wala hajaambiwa lolote lile. Lakini licha ya hivyo ni kwamba huyu bwana sasa hivi yaani ninavyoongea sasa hivi ni mbovu kilema.

Halafu mguu wake katika kushughulikiwa haufungwa vizuri mfupa karibu uko nje hana msaada wowote alipo pale anahitaji matibabu na hawezi kwenda hospitali tena kwa sababu bili ya kwanza haijalipwa na kwa mapatano na *RPC* alivyokuwa amemuahidi ni kwamba wangeweza kutekeleza haya yote. Halafu na bado baada ya kufuatilia ni kwamba wale vijana hawakutoka kwa amri au hawakutoka kwa ruksa pale Polisi waliondoka tu kwa amri yao kwenda kushambulia huyu kijana. Haya yote yalijulikana pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema sitaki niendeleo kubishana na ndugu yangu. Lakini ningependa kujua kwa kweli ni vipi wataweza kumshughulikia kwa sasa hivi maana ninavyoongea juzi hapa Waziri Mkuu alipokuwa kule alikuja kutaka kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu kama siyo mimi kumwambia bwana Waziri Mkuu sasa hivi ana shughuli maalum, naomba ukae nitaendelea kulishughulikia suala lako. Ni kilema mpaka sasa hivi na yuko ndani, ndogo wake sasa hivi ndiyo huyu anayekimbiza mwenge ambaye ni Mkuu wa msafara wa Mwenge sasa hivi. Sasa naomba nielezwe kwa kweli ni vipi atashughulikiwa haraka ili aweze kuona huyu bwana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumpiga mtu na kumjeruhi ni kosa la jinai, yule bwana alikuwa na kosa ambalo alitakiwa apelekwe Mahakamani kwa sababu ni kosa la jinai. Alitumia muda muda mrefu kukaa hospitali. Alipotoka yule ndugu yake aliyepigwa na kuumizwa akaenda kufuta shauri lile kwamba mimi sitaki ndugu yangu aendeleo kushitakiwa na hili kosa. Kwa hiyo, mlalamikaji akafuta, kwa hiyo, sisi kwa upande wa kumpeleka huyu Mahakamani tukaishia hapo yule aliyekimiza alisema sitaki ndugu yangu aendeleo kushitakiwa Mahakamani futeni. Tunachoshughulikia sisi sasa hivi ni wale askari kujiridhisha je, kile kitendo kilikuwa sawasawa au siyo sawasawa, ndiyo jambo sasa hivi limeishamalizika katika ngazi ya Mkoa lipo Ofisini kwa *IGP*.

**MHE. JUMANNE H. NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tiba, namna ya kushughulikiwa huyo mtu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kulikuwa na mambo mawili ambayo alisema pamoja na huo utaratibu wa kipolisi unaoendelea anaulizia tiba ya yule mtu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anasema walikuwa na makubaliano na *RPC* huko, mimi nitayafuatilia haya makubaliano na nitaagiza yatekelezwe kama yalivyokuwa. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Kifungu 2001. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kila Wilaya na kila *OCD* atapewa gari sasa. Lakini kwa kuwa Wilaya ya Ruangwa Mkoa wa Lindi imekuwa Wilaya kamili toka mwaka 1995 na toka imekuwa Wilaya haijapata *OCD* na haijapata hata Ofisi na kwa kuwa ile ni Wilaya kamili ina *DC*, ina Halmashauri, ina Viongozi wote kasoro *OCD*, je, ni lini Wizara ya Mambo ya Ndani itamleta *OCD* wa Wilaya ya Ruangwa na gari lake liweze kufika pale kama ni haki ambayo ya kila Wilaya inatakiwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza ahadi yangu kwamba kila Wilaya itapatiwa gari *whether* yupo *OCD* au hayupo.

Suala la *OCD* tunalifuatilia si Wilaya hii peke yake ambayo haijapata *OCD*. Huwa tuna viwango vya mahitaji ambavyo tunapenda vifikiwe kwanza kabla hatujapeleka *OCD*. Lakini sasa maadam Mheshimiwa Mbunge ananiambia kwamba ni muda mrefu hatujapeleka *OCD*, basi hilo tutalisimamia kuhakikisha kwamba hivyo viwango vinatimizwa ili tumpeleke katika kipindi hiki hiki cha mwaka huu. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Je Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufafanua viwango hivyo ni vipi kama vinapaswa kutekelezwa kule au ni Serikali inayopaswa kutekeleza ili tuhakikishe kwamba sasa isitimie miaka 10 kabla Ruangwa haijapata *OCD*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, viwango hivyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni kweli tunazo Wilaya nyingi hasa hizi Wilaya mpya ambazo hazina Ma-*OCD* wala isichukuliwe kwamba ni Ruangwa peke yake. Hazina Ma-*OCD* kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kuna mazingira ambayo lazima yawekwe kwanza ndipo tupeleke *OCD*. Hizi Wilaya mpya zingine hazina hata ofisi ukipeleka *OCD* leo hata mahali pa kufanyia kazi yeye na *OC CID* na wengine wowote wale wanaomsaidia ofisi hakuna. Mahali pa kumweka akakaa na familia yake hakuna. Kwanza sasa hivi tunajaribu kujenga mazingira hayo yakishakamilika ndipo tuanze kupeleka Ma-*OCD* katika hizo Wilaya ambazo hazina Ma-*OCD*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ili tusiwe na maswali mengi. Swali lilikuwa kwa kifupi tu ni viwango gani hivyo? Kwa hiyo, ni kiwango cha nyumba ndiyo maana yake? Nyumba ya Polisi. Kwa hiyo, mkijibu mkaacha vizuri na ikaeleweka itatupunguzia muda.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba ametuambia kinachotakiwa ni Ofisi. Je, nani anatakiwa kujenga ofisi na narudia ni miaka 10 sasa, huu ni mwaka wa 9 toka Ruangwa kuwa Wilaya kamili.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaoeleweka huwa tunahimizana hapa miaka yote kwamba wananchi waanze hizi shughuli halafu Serikali inachangia. Mwaka huu tumefungua jengo kule Kiteto zuri tu walianza wananchi wenyewe, Same na Simanjiro iko katika hatua za mwisho ni wananchi wenyewe tu wamefika hatua kubwa. Kwa hiyo, kadri ambavyo wananchi watajitokeza na kuanza zile shughuli ndiyo nayo inasaidia kufikiwa yale malengo mapema.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Police Marine* ... .. 442,890,800/=

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Nilitaka maelezo kwa upande wa Bahari ya Hindi. Waziri hakuzungumza chochote kuhusu mashua za Polisi. Sina uhakika lakini hivi sasa sioni kama tuna vyombo vya Polisi kwenye bahari ya Hindi. Je, Wizara ina mpango gani wa kuimarisha ulinzi wa Polisi katika bahari ya Hindi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna tatizo katika bahari ya Hindi kama tulivyokuwa nayo kwenye Maziwa.

Mipango ya kukabiliana au kuondoa tatizo hilo tunayo. Lakini kwa Bajeti ya mwaka huu haikuwezekana kuyakabili yote kwenye Maziwa na bahari ya Hindi. Kwa hiyo, mwaka huu tunaanzia Maziwani mwaka kesho tukijaliwa tutakuja baharini.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nahitaji ufafanuzi tu. Wakati Mheshimiwa Waziri akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge alitamka kuwa Wizara imekarabati boti 7 zinazotoa huduma kwenye Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Ninavyofahamu Ziwa Nyasa hatuna boti yoyote ya Polisi. Labda pengine kauli hii ilitoka kwa ajili ya ununuzi wa boti mpya kwa ajili ya Ziwa Nyasa ama vipi? Nilitaka kupata ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sio sahihi kwamba Ziwa Nyasa hakuna boti kabisa. Ziko mbili ila kwa muda mrefu zimekuwa mbovu zilikuwa hazionekani lakini ni katika hizo saba tunazo

karabati mbili ziko kule. Kwa sasa hivi ziko *grounded* pale *Itungi Port* tutazikarabati na tukishakamilika ataanza kuziona.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 2002 ningepata nipate ufafanuzi kuhusu hii *sub vote*. Kwa kweli kuna tatizo kubwa sana katika Ziwa Victoria kwa upande wa Kisorya katika jimbo langu la Mwibara kutokea Kisorya mpaka eneo la Guta kuna majambazi ambayo yanawavamia wavuvi usiku wakati wanavua yanawanyang'anya samaki na hivi karibuni kumetokea matukio ya vifo.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anawahakikishiaje hawa katika hizi *sub marine* zinazokuja kuhakikisha kwamba watakuwa na usalama?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ziwa la Victoria upande wa Musoma anakotoka Mheshimiwa Mbunge iko boti moja na miongoni mwa hizo ambazo tunazikarabati na ataiona vile vile inaanza kufanya kazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2003 - *Railway Police Division* ... .. 278,210,100/=  
Kifungu 2004 - *Police Signals Branch* ... .. 2,855,828,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2005 - *Police Zanzibar*... .. 4,582,499,600/=

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie ufafanuzi katika hili fungu la Mafuta (*Fuel and Oil*).

Mwaka 2003 fedha zilizokisiwa zilikuwa shilingi 211,000,000 na mwaka huu ni kiwango kile kile. Wakati mwaka 2003 miongoni mwa kilio kikubwa kilikuwa ni tatizo la upungufu wa hizi fedha katika kuliwezesha Jeshi la Polisi kufuatilia matukio mbalimbali yanayotokea kule Zanzibar. Hivi karibuni kama unavyoona hali yenyewe *Ma-terrorist* walifanya vitu vyao pale. Wakalipua mabomu, kuna maeneo ya utalii imekuwa matokeo mara kwa mara yanatokea kuvamiwa na majambazi. Lakini tatizo kubwa linakuja kwamba au hata katika matokeo yanayowakuta wananchi unapowasiliana wakati mwingine unakuta tatizo kwa upande wa Jeshi la Polisi mafuta linakuwa ni tatizo kuwawezesha kufuatilia kwa ukamilifu.

Sasa Mheshimiwa Waziri, nataka anisaidie na anieleweshe ni kigezo kipi alikitumia makisio ya mwaka 2003 na mwaka 2004 kuwa ni yale yale wakati haya matatizo yanaongezeka?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lilichangiwa pia nakumbuka Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi, nadhani. Katika maandalizi ya Bajeti huwa tunakwenda katika hatua mbili. Hatua ya mwanzo tunaletewa *ceilings* halafu tunazipanga wenyewe kama vile ambavyo tunaona ziwe na kila Idara huwa imepewa *ceilings* zake apange mwenyewe mafungu yake, *priority* atapeleka wapi. Kwa hiyo, Zanzibar wakapanga *priorities* zao zikawa vile.

Hatua ya pili inakuja sasa kujadili ziada (*above the ceiling*). Sasa nilisema mapema kuna maeneo ambayo tuliyajadili kwa kuyaombea Bajeti ya ziada kwa kiasi kikubwa na mawili ikawa ni *Police Operations* pamoja na *fuels*. Hizi fedha zote zimewekwa pale kwenye *Police Operations* kifungu 2001 kifungu ambacho wameshapitisha Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, zile fedha zilizoko kule ni za nchi nzima zitakwenda mpaka Zanzibar. Kwa hiyo, zaidi ya hizo zilizopo hapo ziada ya kule Makao Makuu itafika wakati wa *operations* na wakati kazi za ziada.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2006 - *Police Airwing* ..... 779,969,300/=  
Kifungu 2007 - *Tazara Police* ..... 118,819,600/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2008 - *Field Force Unit* ..... 2,179,648,700/=

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu kinachohusu *Field Force*, nilikuwa nimechangia nikitaka ufafanuzi kwamba kumekuwa na malalamiko kwenye Kitengo hicho Polisi wanapopeleka *Field Force* wanaona ni shida kwenda *Field Force* na wanaona kama ni adhabu kwenda *Field Force*.

Sasa nilikuwa nimeangalia hapa katika hii *vote* hakuna mabadiliko ya fedha ukiangalia hizi za kipindi kilichopita na hizi za safari hii nyongeza ni kidogo sana ukilinganisha na labda *Traffic* hapa zinaonekana kama nyongeza ni mara mbili.

Sasa nilikuwa nimetaka ufafanuzi kwa nini hicho kitengo ambao wanapata shida sana katika vitengo vyote vya Polisi, kwa nini wasiangaliwe zaidi aidha, kwa posho au kwa kuhamishwa mara kwa mara wasikae mahali pamoja? Kwa sababu malalamiko yalikuwa ni mengi na wamewahi kuja kwetu sisi hapa Bungeni wakitulalamikia bwana ebu tusaidie tuweze kuhamishwa, tuweze kufanya nini? Sasa nilikuwa nataka kupata ufafanuzi kuhusu hali hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama atazitazama vizuri kasma zilizopo hapo zote zinahusu zaidi mishahara na posho katika hali ya kawaida. Masuala mengine hapo yametawanywa kwenye vifungu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia *operations* sehemu kubwa ni *FFU* ndio wanaotumika katika *operations*. Maadam liko eneo ambalo tumeliongeza fedha nyingi kwa kutaka kufaidika kwa kiasi kikubwa ni wao *FFU*. Kwa hiyo, asitazame hapo tu akafikiria mambo yote yamekwisha.

Maombi ya uhamisho yako mengi tu si *FFU* peke yake na askari wengine wa kawaida. Humu ndani karibu kila Mbunge ameniletea maombi ya askari wao kutaka wapewe uhamisho. Lakini hayo si rahisi kuyatekeleza hasa kwa vile yanaambatana na maslahi na Waheshimiwa Wabunge wamo waliolalamika humu kwamba kuna Polisi wamepewa uhamisho bado wana madai yao. Kwa hiyo, wakati mwingine inabidi tutazame kwanza tushughulikie madai ya nyuma, tuyamalize hayo kabla ya kuanza kutoa uhamisho mwingine isipokuwa pale ambapo inabidi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2009 - *Traffic Police*... .. 1,158,565,900/=

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote 2009 Traffic Police*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipomsikia Mheshimiwa Waziri wakati ana *wind-up* amezungumzia tu kwamba fedha zinazoombwa zitakuwa ni kwa sababu ya kuimarisha *operations*. Lakini juu ya matatizo ambayo yanatukuta ya hawa jamaa wa Usalama Barabarani. Dawa hajatuambia kwa sababu hii ni kero wale hawajui kama wewe Mbunge au nani. Weka gari pembeni, washa taa, wanatoa *sticker* wanaondoka.

Sasa mimi nadhani *its high time* kwamba namshukuru *IGP* juzi amefoka pale kwamba kuna *Traffic* amepewa rushwa ya nyama kidogo inatia matumaini kama Mkuu wa Jeshi. Lakini bado kuna mambo ya ovyo ovyo yanafanyika pale tunaomba tuelezwe.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nikifanya majumuisho nimetoa ahadi kwamba mapambano dhidi ya rushwa katika Wizara yetu kwa upeo wake wote tutayaongeza kwa kasi na nikasema kwamba zaidi ya kuwaandama wale ambao tunawashika na wakathibitika kwa rushwa wakachukuliwa hatua, tunatazama eneo la kuziba mianya. Nikatoa mfano mmojawapo uliohusiana na hawa hawa *Traffic* anaosema Mheshimiwa Omar Chubi. Kwa mfano huo wa kukamata gari halafu ukaingia humo ukafuatana na uliyemkamata na mianya mingine yote tunaitafuta ili kuiziba. Kwa hiyo, mimi nataka nimhakikishie tu kwamba hayo mapambano yanaendelea na wao tutaendelea kujitahidi kuwaongezea uwezo wa kazi kama ambavyo tunafanya kwa wengine.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia kifungu hiki hiki cha *sub vote 2009 Traffic Police*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuja hapa mara zote huwa tunalalamika kwa shughuli za *Traffic* kwamba wanafanya hivi, hivi, wanachukua rushwa, wanafanya hivi. Lakini nilipokuwa nikichangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na leo kwa maandishi nilizungumzia suala la unyanyaswaji wa askari kwa kupigwa. Je, Mheshimiwa Waziri atatuambia nini kwa kesi kama hizi ambayo kwa ushahidi hii imetokea Zanzibar na jana nimeisikia tena Shinyanga wanaofanyiwa *Traffic* na watu hawa wamiliki wa magari. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Wanaopigwa ni *Traffic*?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anayepiga askari, anayepiga raia wa kawaida ni mkosaji. Kila tunaowashika wanakamatwa tunawashughulikia kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. Sisi tunawahimiza askari wetu vile vile kwamba wasijenge sana mazoea na watu maana wakati mwingine yanakuwa katika mazingira na mazoea yaliyozidi pengine anaona wepesi wepesi tu na ndiyo maana na hii miradi mikubwa mikubwa ambayo tunayafanyia kazi kuhakikisha kwamba wanaishi katika nyumba mbali na uraiiani ili nidhamu iongezeke. Lakini yeyote ambaye anachezea askari wetu anachukuliwa hatua za kisheria na tutaendelea kufanya hivyo.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote* hiyo hiyo 2009 - *Traffic Police*.

Wakati nachangia muda ulioniishia lakini nilikuwa nimependekeza na Waziri alinielewa kwamba tofauti iliyopo kati ya *Traffic Police* na *FFU* ni kubwa na kwamba *Traffic* wanalalamikiwa na kila mtu hata *IGP* analalamika, Wabunge wanalalamika. Nilikuwa nimependekeza kwa nini utaratibu wa zamani wa kuwahamisha askari hawa vikosi kila baada ya miaka mitatu usifanywe ili *Traffic* asijue kwamba kazi hiyo ya neema mpaka viepo kwa hiyo aendelee kututesa. Nataka majibu ya Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hili.

Niunganishe na swali lililoulizwa mapema kuhusu *FFU* nadhani na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya ambao nao wanaomba sana uhamisho. Nalo unapoletewa ombi la uhamisho kama hivyo aghalabu anakuwa anaomba aende *Traffic*. Sasa nilijibu wakati ule na najibu hivi sasa vile vile kwamba hapo nyuma tulirejeshwa nyuma kidogo na tatizo la posho na ndiyo maana tumejitahidi hata katika Bajeti ya mwaka huu kuongeza kiwango cha posho ambacho tutaweza kukitumia kwa kuhamisha askari. Nadhani safari hii tutakuwa na uwezo mzuri zaidi wa kufanya uhamisho sio baina ya vikosi tu bali hata aina ya maeneo. (*Makofi*)



**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Waziri hajasema, mimi nasema *Traffic* ahame aende kwenye Kikosi cha Mbwa, aende *FFU* na yule *FFU* aende kule *Traffic*, ili tatizo ni rushwa huyu usimhamishe kumtoa Kagera unamleta Nyang’wale nataka aende *FFU* kikosi kizima. Nataka majibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, pale pale kumtoa Dar es salaam kumpeleka huku. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mimi nadhani Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimjibu Mheshimiwa James Musalika kwamba hiyo kazi tutaifanya, uhamisho baina ya vikosi. Ila yeye anataka uhamisho wa *Traffic* tu. Sasa ukimhamisha *Traffic* bila shaka itabidi umhamishe na mwingine aje pale. Ndiyo maana ni *both ways*.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2010 - *Police Airport* ... .. 253,346,900/=  
Kifungu 2011 - *Police Dog and Horses* ... .. 412,314,600/=  
Kifungu 3001 - *Police College - Moshi* ... .. 1,741,500,200/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3002 - *Police College* ... .. 632,914,100/=

**MHE. REMIDIUS E. KISSASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kifungu 3002 - *Police College* hii ya 3001 tunajua ni *Police College Moshi* nilitaka kujua hii *Police College* ni ipi? Ipo ya Zanzibar ya Dar es Salaam, ni ipi sasa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni *Police Colleges* zote. Labda imeachwa “s” tu.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni zote ziko ngapi kwani? Na kwa nini hii ya Moshi ikawa tofauti na hizi zingine?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Ya Moshi inabidi iwe tofauti kwa sababu kwanza ndiyo kubwa yenye kuchukua *recruits* kwa ajili ya mafunzo ya awali. Hizi nyingine moja Dar es Salaam na nyingine ya Zanzibar ni kwa ajili ya *NCO*’s wale Makoplo na maofisa wengine.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu 4001.

**MWENYEKITI:** Aah, tuko kwenye *Police College - Moshi*. Una mashaka na *Police College* au una kifungu cha mbele zaidi?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 - *Police Vehicle Maintenance Unit* ... .. 120,238,900/=

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nimezungumzia Wilaya ya Ngara kutokuwa na magari wakati kuna matatizo mengi. Hivi karibuni nilipokuwa nikijibiwa swali kuhusu kuwa na magari kwa sababu ya Sekondari za Ngara nilizungumzia kwamba jana yake alikuwa ameuawa jambazi mmoja kwa sababu uvamizi umezidi Wilayani Ngara.

Napenda pia niseme kwamba jana amekufa mwingine kwa sababu hiyo hiyo. Sasa katika maombi yangu niliomba kwamba Wizara hii iongeze magari kwa Polisi Wilayani Ngara. Kuna gari moja tu zee ambalo linatumika na *OCD* Wilayani Ngara. Kwa hiyo, naomba nijue kwamba Mheshimiwa Waziri yuko tayari kupeleka magari kwa vituo viwili hasa vikubwa kituo cha Lulenge ambacho ni cha pili kwa ukubwa Wilayani Ngara na kituo cha Murusagamba kwa sababu haya ndio maingilio hasa ya majambazi wanaochangamana na wakimbizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri endelea kujibu hili la magari naona linajitokeza mara kwa mara.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimeshajibu kuhusiana na hili suala la magari. Nimewaomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mheshimiwa Gwassa Sebabili, naye namwomba kwamba namhakikishia atapata gari jipya la Wilaya. Halafu mengine maombi mmeshatuletea na mnaendelea kutupa tutayapokea tutayazingatia kwa mujibu wa uzito wa pahali. Kwa hiyo, namwomba anikubalie hilo Mheshimiwa Mbunge na hili ombi amelileta kwenye *maintenance of vehicle*. Mimi nilifikiri labda kama gari lake ni bovu tutalichukua pale tukalitengeneze likawe imara baada ya kupata lile lingine lile litumike kwenye eneo lingine.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Police Medical Unit* ... .. 741,274,900/=

Kifungu 6001 - *Police Building Brigade* ... .. 949,741,100/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 7001 - *Criminal Investigation Division* ... .. 6,174,184,900/=

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Fungu 250300, *Employment Allowances*, moja katika tatizo la upelelezi wa kesi za jinai

ni Askari kukosa hizi *allowances* na matokeo yake huwa wanachelewesha sana upelelezi wa kesi. Ukiangalia mafungu yote ya Wizara nyingine zote *Employment Allowances* zinashinda hata mishahara. Ni kwa nini Askari wakapewa *Employment Allowance* ndogo kuliko mafungu mengine na hasa hili?

Moja ya sababu kubwa ya Askari kutopeleleza kesi ni kwa sababu hawana *allowances* na utakapokwenda kupeleka shauri lako mara nyingi wanakuomba angalau pesa ya chakula uwasaidie wakati wanafanya upelelezi. hili ni tatizo moja.

Lakini la pili, katika kuchelewesha kesi mwaka 2003 Mheshimiwa Waziri tulimshauri kwamba kwa kuwa sasa vipo vyombo vya ulinzi vya *private*, tulimshauri kwamba kuanzishwe na *Private Investigation* kama vile ambavyo nchi nyingine wanafanya na akaahidi katika Bunge hili kwamba watalifanyia kazi na watalitolea majibu. Naomba atupatie majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijibu swali hasa nilipoulizwa kuhusu mafuta Zanzibar na nikajibu kwamba kuna Bajeti ya ziada ambayo imewekwa kule Makao Makuu, matumizi yake ni upeo wa nchi nzima. Hii ni pamoja na jitihada hizo za *Criminal Investigation*. Zitakuwa ni *allowances* zote ambazo zitatolewa kwa ajili ya kazi maalum zikiwepo pamoja na za upelelezi. Hata *operation* zina sehemu kubwa ya upelelezi ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kutumia wapelelezi binafsi, nadhani hili si jambo rahisi ni la *policy* ambalo huwezi ukaliambia mara moja. Sasa hivi tuko tunatazama mambo mengi ya kisheria pamoja na ya kisera. Pia, kuna suala la *prosecution* kwamba Polisi wanaendelea kufanya *prosecution*. Haya tunayajadili kwa pamoja ili baadaye tuone kwamba tunaweza tukafikia uamuzi gani. Kwa mfano, kule Zanzibar tayari walishaanza kutoka kwenye *prosecution*, wanapeleka kwa *DPP* na huku wazo hilo tunalifanyia kazi pamoja na suala hilo kutazama kama tunaweza kutumia wapelelezi binafsi. (*Makofi*)

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *sub vote* hiyo ya 7001 nina mpango wa kuzuia mishahara ya wapelelezi kifungu 250100 mpaka nipate maelezo.

Wakati nichangia kwa maandishi nilieleza mambo mawili, kwamba sasa hivi kumekuwepo na wimbi kubwa sana la watu kutoka nje ya nchi hii wanaingia Dar es Salaam, wanakaa na wanafanya uhalifu na utapeli na nikatoa wasiwasi wangu kwamba polisi na hasa wapelelezi inawezekana wanashirikiana nao na wanawaficha *actually* na nikataka kujua ni hatua gani Wizara itafanya kuzuia wimbi hili na kuwakamata?

Lakini pili, nilisema kwamba mimi na Mheshimiwa Hadija Kusaga, kwa kusaidiana na wapelelezi tuliweza kuwanasa matapeli wawili kutoka nchi za nje waliotaka kumtapeli Mheshimiwa Hadija Kusaga na wakafikishwa Polisi. Lakini

kinyume cha matumaini yetu kwamba matapeli wale watafikishwa *Immigration* ili wapewe *repatriation*, waliachiwa kwa dhamana na bado wako pale jijini na wanatutishia kwamba mimi na Mheshimiwa Hadija Kusaga, kwa sababu wameshatutambua, watatua. Nataka kujua kwamba yule tapeli anayeitwa Chilombo aliyeachiwa kwa dhamana bila kupelekwa *Immigration* ili apate *repatriation* atakamatwa lini? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza kwenye hotuba yangu kwamba tunazo *operations* za kusaka wahamiaji haramu na hizo zinaendeshwa kwa ushirikiano baina ya Polisi na Uhamiaji. Kwa hiyo, si suala la kwamba tuna mpango au hatuna, mpango huo upo na tunautekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopata *cases* ambazo tunazona ni *obvious* ambaye hatuna shaka kwamba ni mhamiaji haramu anaondoshwa. Lakini kutenda kosa la jinai haitoshi, kama yumo ndani kihalali kaja kwa mujibu wa taratibu za nchi na amefanya kosa, inabidi zitafutwe taratibu za kawaida za makosa kama raia wa nchi. Humpigi *PI* kwa sababu tu ameiba au amefanya nini, inabidi aingizwe kwenye mkondo wa upelelezi na mkondo wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, anawatuhumu kwa sababu ya utapeli na kesi amesema inaendelea. Wameachiwa kwa dhamana, lakini kesi inaendelea. Nadhani atupe fursa tuiachie hiyo kesi tuiendeleze kwa mujibu wa taratibu za nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, je, hii kesi iko Mahakamani ili tuache hili jambo tusizungumze? Kama bado liko katika mikono ya Polisi tunaweza kuzungumza, lakini kama liko Mahakamani tayari hatuwezi.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba liko Mahakamani huyu Chilombo yuko nje na anatishia maisha ya Wabunge wawili. Ndiyo maana nasema *it is a serious case*, arudishwe ndani, ni kwa nini yuko nje na anatishia maisha ya Wabunge wawili? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nilisisitize kwamba, jambo hili kama kweli liko Mahakamani basi tusilizungumze. Isipokuwa hoja yako kwamba mnatishiwa, basi muandike hiyo barua kutoa taarifa iwe *administration* badala ya kulijadili hapa, kwa sababu kama kweli liko Mahakamani nadhani Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, unaelewa kwamba hatuwezi kulizungumza. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**MWENYEKITI:** Hilo tuachie hapo, tuachie *administration* kama kweli lipo Mahakamani, *unless* unakataa halipo Mahakamani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo Mahakamani.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme mapema kwamba siko katika suala la kituo wala nini, nimekubaliana na ahadi aliyotoa Waziri na kwa kweli kuna ahadi aliwahi kutupa *IGP* na ametekeleza. Kwa hiyo, naamini hilo litatekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, ninyi nyote mnaosoma magazeti, mmesoma mara nyingi matukio yanayotokea Mererani. Kuna wakati mwezi wa tatu ama wa nne, Watumishi wa Kampuni ya *AFGEM* waliwakuta Watanzania huko chini ardhini wakichimba madini na wao walivuka mpaka wao, vijana hawa wa Kitanzania walipowaona kwa sababu walikuwa na silaha na vijana hawakuwa na silaha wakakimbia, lakini wamewapiga risasi na ilionyeshwa kwenye gazeti migongo ya hao vijana ilivyochakazwa kwa risasi. Hiyo kesi mpaka sasa haijashughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miezi hiyo hiyo, kijana alipigwa risasi karibu na *fence* ya *AFGEM* na wakatoa sababu kwamba alidandia lori lililokuwa linabeba mawe ya kuchambua na kupata *Tanzanite*. Wiki mbili zilizopita kijana amepigwa risasi ambaye mpaka leo bado yuko hospitalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anijibu yafuatayo, je, hawa wageni wakiwapiga Watanzania risasi wao wako juu ya sheria? Je, wageni kuwapiga Watanzania risasi ni sehemu ya uwekezaji? Je, hiyo Kampuni ya uwekezaji wako juu ya sheria? Je, wao wanaruhusiwa kuchukua sheria mikononi mwao?

Waziri amerudia hapa zaidi ya mara nne kwamba kutukana, kupiga, ni kosa la jinai. Kwa hiyo, kupiga ngumi, kupiga rungu, kukata sime ni kosa la jinai, lakini kupiga risasi siyo kosa la jinai? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na hao waliofanya hivyo wamepatikana na wanafikishwa Polisi, baada ya nusu saa ama dakika 45 wanaondoka na wenzao huko wakiona kwamba wamekamatwa wanawatorosha wanawapeleka kwao. Naomba nipate maelezo ya hayo. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mwekezaji ambaye yuko juu ya sheria na wala vitendo vya kupiga risasi au kuua, kuumiza Watanzania si sehemu ya uwekezaji. Hayo maswali mawili ninayajibu hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya sisi kusoma kwenye magazeti tukaliingilia kati hao wahusika wote wameshakamatwa, pamoja na huyo Meneja Mkuu anayesemekana. (*Makofi*)

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kusikitika hasa kwa jibu la Waziri kwamba baada ya kuona kwenye magazeti, lakini hao Wananchi waliripoti kwenye vituo vya polisi, haikuchukuliwa hatua yoyote mpaka ionekane kwenye magazeti! Kwa hiyo, usalama wa Watanzania tunawekeza kwenye magazeti? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu amesema wameshahughulikiwa, wameshakamatwa, lakini nasema si ajabu keshokutwa wakaachiwa na wakatoroshwa kupelekwa Afrika Kusini na walishakamatwa na wakaachiwa, labda kama leo wamekamatwa tena na watatoroshwa kupelekwa huko kwao Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kuweka usalama wa Watanzania kwenye magazeti? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiadharau magazeti, magazeti ni moja kati ya vyanzo vinavyofichua uhalifu. Unaweza ukajificha au ukawa umefichwa, gazeti likafichua. Sasa kama lilipofichua mkashughulikia nadhani ni katika sehemu ya wajibu na tunahimiza magazeti yaendelee kufichua tu. *(Makofi)*

**MHE. MUTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *sub vote 7001*, tuliwahi kutoa mapendekezo kwamba Wananchi wengi wanapata shida katika taratibu za kupelelezewa kesi zao na hivyo kukaa Magereza muda mrefu na tukapendekeza kuanzishwe chuo maalum kwa ajili ya upelelezi ili tuwe na wapelelezi wengi kuondokana na hili tatizo. Nitaomba maelezo hayo. Hilo moja.

La pili, nataka nipate maelezo ya kina kwani kumekuwa na matatizo, kesi inapokuwa inamuhusu polisi na mpelelezi wa kesi hiyo ni polisi, Mheshimiwa Waziri naomba unisaidie utaratibu utakuwaje kesi inamuhusu polisi na mpelelezi ni polisi na atakiwa atoe taarifa kwa ajili ya polisi? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimkumbushe Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, kwamba kwenye hotuba yangu nimezungumzia suala la Chuo cha Wapelelezi kwamba katika Bajeti ya mwaka 2004/2005, hii ambayo tunaizungumza sasa hivi ni miongoni mwa shughuli zitakazofanyika ni maandalizi ya ujenzi wa hicho chuo na kitakuwepo hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upelelezi, nilipokuwa nikijibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, niligusia hapa kwamba, tunatazama upya mfumo mzima wa upelelezi na *prosecution* yaani uendeshaji wa mashtaka. Upelelezi bila shaka kwa sasa hivi jukumu hilo limepewa Polisi. Sasa haina maana kwamba akifanya kosa polisi naye asipelelezwe, wanapelelezwa na wanaokutwa na kesi za kujibu wanafikishwa mahakamani na wapo wengi tu. Lakini tunatazama huko mbele kama baada ya upelelezi hatua za kuendesha mashtaka, je, bado tuendelee nazo polisi? Hayo ni miongoni mwa mambo ambayo tunayafanyia kazi ya kisera.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia nimeomba kwamba polisi waongezwe katika Wilaya ya Ngara pamoja na kusema kwamba, ni vizuri wakaongezwa katika Wilaya za mipakani hasa ile mipaka ambayo imejawa na tatizo la wakimbizi.

Hivi karibuni Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge lako Tukufu ilikuwa Ngara, imeona jinsi Magereza yalivyojaa wahalifu. Nimetoka kusema kwamba sasa hivi majambazi wanauawa kwa wingi, kuna kesi nyingi zimejaa mahakamani za miaka nenda miaka rudi. Lugha ni kwamba, kesi zinapelelezwa lakini upelelezi haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachokiomba ni kwamba, Mheshimiwa Waziri anisaidie kujua Askari Polisi wataongezwa lini na kiasi gani katika Wilaya ya Ngara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako polisi katika nchi hii ambao nafikiri kwamba wanazo kazi, lakini siyo nyingi sana. Polisi walioko katika Mikoa ya katikati ambako hakuna matatizo, kwa imani yangu nafikiri kwamba wanaweza wakasogezwa katika maeneo ya mipakani kuzunguka nchi yetu ambako kuna matatizo kuweza kulinda watu, mali zao na kurudisha amani na utulivu. Lakini sidhani kama Serikali inafanya hivyo ninavyojaribu kuomba kwamba ifanye. Naomba Mheshimiwa Waziri, aniambie atapeleka au ataongeza askari na askari wa upelelezi lini kwa Wilaya ya Ngara?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngara ni moja ya Wilaya ambazo tunapeleka Polisi wa ziada kwa sababu ya matatizo maalum. Kila baada ya miezi sita tunapeleka Polisi wa ziada wakirudi wanapelekwa wengine, ni *operation* maalum ikiwemo Wilaya ya Ngara. Hilo zoezi la kupeleka polisi wa ziada tunaendelea nalo mpaka hili tatizo la wakimbizi litakapomalizika.

Lakini vile vile, kwa sababu sasa hivi tuna-*train* kila mwaka, tunaajiri kila mwaka, hivi juzi tu tumemaliza zoezi la kuhoji na kuteua vijana kwenda Moshi, nadhani watakwenda baada ya bajeti hii. Wanapomaliza kipaumbele tunatoa kwa zile Wilaya zenye matatizo maalum kama Ngara na katika Bajeti ya sasa hivi mtakayopitisha kuna askari polisi 2000 wapya ambao vile mtatupa uwezo wa kuajiri. Wakimaliza masomo tunapowapangia vituo tunatazama maeneo yenye hali ngumu ya kiulinzi kama Ngara. Kwa hiyo, kwa utaratibu huo awe na hakika kwamba Polisi wataongezeka.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa jibu lake, lakini inapofikiriwa kwamba watu wanakwenda mafunzoni kesho halafu waje kurudi baada ya mwaka mmoja au miaka miwili ndiyo waweze kuwasaidia watu waliomo katika matatizo, sidhani kama hiyo inasaidia kitu au sidhani kama ni jibu sahihi.

Juzi nimempigia simu saa nane usiku Mheshimiwa Naibu Waziri, baada ya kuambiwa matatizo yaliyopo Wilayani Ngara. Kwa hiyo, naomba basi anisaidie kwamba atapeleka askari Ngara kwenda kuwasaidia wananchi wa Ngara wakati hao wanaofunzwa watakuja kushika nafasi za hao watakaokuwa wametumwa Ngara.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri alimwambia kwamba, tuna utaratibu wa kudumu mpaka hapo tutakapomaliza tatizo la wakimbizi, wa kupeleka askari wa ziada kwa kutambua hiyo hali

halisi ya Ngara na ni kwa mujibu wa mazingira yetu. Sasa Mheshimiwa Mbunge tayari Ngara wana ziada ambayo kwingine hawana, wangependa nao wapate hiyo fursa, lakini hawaipati, ila tumetoa mazingatio maalum kwa Ngara na maeneo ya mipakani kwa sababu hiyo maalum. Tunapenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika askari waliomaliza mafunzo, waliopita amepata, watakaokuja nao watakapomaliza mafunzo tutamwongeza. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 7002 - *Stock Theft Prevention Unit*... ..287,700,300/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tena nirudie nilivyosema juzi. Wizara hii ina vifungu vingi sana, bado kabisa. Sasa tunazo dakika 12 tu kwa ajili ya michango hii ya kawaida, tukifika hapo ni moja kwa moja. Kwa hiyo, naomba niwaambie mapema.

## **FUNGU 29 - MAGEREZA**

Kifungu 1001 - *Prisons Headquarters*... .. 2,018,869,400/=

Kifungu 2001 - *Parole Department* ... .. 248,195,500/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation* ... ..34,030,652,000/=

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia juu ya kifungu ambacho kinahusu *Maintenance - Physical Infrastructure 270100*. Mji wa Bukoba una kitu ambacho ni *special, Free Zone* iko katikati ya Mji na pale zile *septic sinks* za pale kwa muda mrefu sana hazijawa *maintained*, zimefurika, kinyesi kinazagaa, kinaingia, kwenye mitaro mpaka kwenye maji ambayo yanaelekea *Lake Victoria*.

Sasa nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri katika hiki kifungu kama jambo hili wamelifikiria kwa sababu wananchi wa Bukoba Mjini maisha yao yako hatarini. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyojibu wakati wa majumuisho kwamba tunayo programu ya kutengeneza *systems* za maji taka na maji safi.



Kwa hiyo, Gereza la Mkoa wa Kagera pale Bukoba tutalifikia katika mwaka huu wa fedha, tutalitengeneza lipendeze na kwa taarifa yako ni kwamba, lile gereza ndiyo la kwanza kupata mpaka na *television*. Kwa hiyo, ipo mipango mizuri tu ya kuboresha Magereza pamoja na Gereza la Bukoba. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2003 - <i>Resettlement of Offenders</i> .....	351,483,600/=
Kifungu 3001 - <i>Prisons Staff College</i> .....	677,430,700/=
Kifungu 3002 - <i>Prisons Driving School</i> .....	103,431,600/=
Kifungu 3003 - <i>Prisons Trade School</i> .....	247,489,300/=
Kifungu 3004 - <i>Prisons College Kiwila</i> .....	558,428,400/=
Kifungu 4001 - <i>Prisons Building Brigade</i> .....	857,720,300/=
Kifungu 4002 - <i>Prison Industries</i> .....	140,424,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4003 - <i>Prison Farms</i> .....	354,189,500/=
--	---------------

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia kwa maandishi nilikuwa nimeelezea tatizo la shamba la Magereza la Ushora ambapo trekta yao kwa miaka mitano imeharibika na sasa hawana kifaa chochote.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie kuwa aidha, hilo trekta lifafufuliwa au shamba hilo litapewa trekta mpya kwa sababu ni shamba muhimu sana kwa Magereza ya Wilaya ya Iramba. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa majumuisho tulitanka kwamba hoja ya Mheshimiwa Mbunge tumeipokea, lile trekta litachunguzwa tuone kwanza, je, linatengenezeka? Kama linatengenezeka ni kwa gharama ngapi? Kama linatengenezeka tunamuahidi kwamba tutalitengeneza.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **FUNGU 51 - WIZARA YA MAMBO YA NDANI**

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i> ... ..	1,071,223,400/=
---	-----------------

**MHE. FRANK G. MAGHOB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi nilizungumzia habari za vitambulisho, lakini katika majumuisho Waziri sikumsikia akizungumzia vitambulisho kwamba lini vitapatikana? Nataka maelezo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitambulisho tumelizungumza kwenye hotuba yangu ya Bajeti na nimeeleza kwamba katika Bajeti ya mwaka huu tunafanya upembuzi yakinifu.

**WABUNGE FULANI:** Eenh! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Ndiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya upembuzi yakinifu kwa sababu hili suala ni la muda mrefu na tulifika mahali tukapata mzabuni akapewa kazi, lakini sasa wakati wa utekelezaji akawa ana-raise mambo mapya, kila siku linakuja jipya na tukagundua kwamba tatizo kubwa ni kwamba kumbe tulikuwa hatuna *feasibility study*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mzabuni anajua hasa anaongozwa na kitu gani kinachotakiwa na sisi wenyewe tunajua tunaongozwa na kitu gani kinachotakiwa. Kwa hiyo, tumeamua hivyo na Serikali ilikuwa ni lazima ifanye uamuzi mmoja kutokana na uwezo wake wa kifedha. Tulikuwa na mawili, tulikuwa na daftari la kudumu la wapigakura na tuna suala la vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote mawili kwa pamoja kwa hali yetu ya kiuchumi tusingeweza kwenda nayo tukaamua tu- *pursue* daftari la wapiga kura kwa sababu kwanza ni hitaji kubwa la Kikatiba, lakini pili ndiyo uhakikisho mkubwa katika mazingira ya leo kwamba uchaguzi utakuwa huru na wa haki.

**MHE. FRANK G. MAGHOB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala kama alivyosema Waziri ni la muda mrefu na sasa hivi tunatayarisha daftari la wapiga kura wakati hatuna uhakika Watanzania waliomo ndani nchini ni wangapi kwa sababu pamoja na Sensa iliyopita hatuwezi kujua wakimbizi walioko nchini ni wangapi, ni vitambulisho vinaweza kutusaidia kujua Watanzania halisi ni wangapi ndiyo tuandike daftari la wapiga. Naomba maelezo ya kutosha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Frank Maghoba, ile Sensa haikusema sisi ni wangapi? (*Kicheko*)

**MHE. FRANK G. MAGHOB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia wakimbizi tulionao ni wangapi na vitambulisho jinsi ninavyofahamu ndivyo vinavyofanya kujua nani ni Mtanzania na nani ambaye siyo Mtanzania. Naomba nieleweke hivyo. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuwatambua Watanzania na wasiokuwa Watanzania si kwa kuwa ukishapata kitambulisho ndiyo ulishakuwa na uhakika. Ni lazima utakwenda kwenye zoezi la kuwatumia wananchi kule kule kijijini. Kazi ambayo inafanyika kwa ajili ya uchaguzi kwa sababu wakati wa uandikishaji hata kwenye daftari la kupiga kura wataandikishwa vijijini, vyama vitakuwa na mawakala kwa utaratibu ambao utahakikisha kwamba ni

mwenye haki tu ya kupiga kura ndiye anayepiga kura. Sasa kama anataka idadi ya wakimbizi tulionao, idadi ya wakimbizi tumeitaja kwenye hotuba yetu ni zaidi ya watu 672,000 na Sensa ya Mheshimiwa Mbunge atakumbuka tumeshafanya. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge bado unahitaji *clarification*?

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nahitaji maelezo. Ni lini sasa upembuzi huo utafanyika na utachukua muda gani ili kupata vitambulisho? Ndiyo swali nataka kujibiwa.

**MWENYEKITI:** Jamani tumlinde ana haki yake ya kuhoji.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi umeshaanza, tunatarajia utanza baada ya Bajeti hii, tunatarajia ndani ya kipindi cha miezi utakamilika. Lakini kwa bajeti hasa kwa ajili ya vitambulisho itakuwa mwaka kesho. (Makofi)

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, mimi swali langu tayari nilishauliza kwamba nini vigezo vya Wizara ya Mambo ya Ndani kuweka mishahara yao kwenye *scale* moja kwa watumishi wote wa magereza, polisi, uhamiaji na zimamoto wakati kazi zao ni tofauti na uzito? Kwa hiyo, naomba Waziri anipe maelezo wametumia vigezo gani kufanya maamuzi hayo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ametupa wazo ni zuri tu na ushauri na tulitoa kauli ya jumla kwamba mawazo na ushauri wote tunauchukua.

Sasa hili nitatoa *specifically* maadamu ameli- *raise* kwamba hilo wazi lake tumelichukua na tatalifanyia kwa sababu hili la Wizara ya Mambo ya Ndani peke yake. Nadhani hilo analijua ni la upeo wa Serikali nzima. Kwa hiyo, hilo tutalianza halafu tuone katika upeo wa Serikali nzima inafikia uamuzi gani. (Makofi)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i> ... ..	246,593,200/=
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i> ... ..	182,142,300/=
Kifungu 1004 - <i>Community Service Secretariat</i> ... ..	502,215,500/=
Kif. 3001 - <i>Fire and Rescue Services</i> ... ..	438,076,100/=
Kif. 3002 - <i>Fire and Resare Services Training Inst</i> ... ..	185,645,200/=
Kif. 4001 - <i>Refugees Unit</i> ... ..	363,194,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, ule muda wa kuhoji jumla umeshafikia mwisho, kwa hiyo, tutahoja jumla, jumla. *(Makofi)*

### **FUNGU 93 - UHAMIAJI**

Kifungu 2001 - *Immigration Zanzibar* ..... 513,980,800/=  
Kifungu 2002 - *Immigration Mainland* ..... 6,828,050,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **FUNGU 51 - POLICE FORCE**

Kifungu 2001 - *Police Mainforce* ..... 5,300,000/=

**MWENYEKITI:** Nilimuahidi Mheshimiwa Mbunge, ningekupa muda lakini unajua sasa haiwezekani tena.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yote)*

### **FUNGU 29 - MAGEREZA**

Kifungu 2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation* ..... 399,258,300/=  
Kifungu 4001 - *Prison Building Bridage* ..... 2,000,000/=  
Kifungu 4002 - *Prison Industries* ..... 4,000,000/=  
Kifungu 4003 - *Prison Farms* ..... 500,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa mwaka 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba taarifa ya Kamati sasa ipokelewe na makisio haya yapitishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2004/2005 ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi  
yalipitishwa na Bunge)

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

Mheshimiwa Naib Spika, wakati nachangia hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja tarehe 29 Juni, 2004 nilisema kuna mambo fulani ambayo hayaridhishi kwenye Benki ya *Exim*. Kilichofanyika ni kwamba tarehe 9 Julai, 2004 siku ya Ijumaa, Mkurugenzi Mtendaji wa *Exim Bank* ametoa *full page* kwenye *Daily News* na *The Guardian*, akisema kwamba yale mambo niliyoyazungumza ni ya uongo. Sasa ninavyojua humu ndani hatuzungumzi uongo. Sasa kabla sijafanya lolote naomba mwongozo wako. (Kicheko/Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaeleza lolote pengine niseme tu kama alichosema Mheshimiwa Omar Chubi, kwamba humu ndani watu hawapaswi kusema uongo, siyo hawasemi uongo, hawapaswi kusema uongo. (Makofi/Kicheko)

Sasa naomba nisome kifungu cha 50 (1) cha kanuni zetu kinasema hivi: “Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni, kwa sababu hiyo Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni atawajibika kuwa na hakika kwa maelezo anayoyatoa ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au kubahatisha tu. Spika au Mbunge mwingine yeyote aweze kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa usemi wake. Mbunge aliyetakiwa kufanya hivyo atawajibika kutoa uthibitisho huo katika muda atakaopewa na Spika kwa ajili hiyo.”

Waheshimiwa Wabunge, wakati anatoa maelezo yake Mheshimiwa Omar Chubi, katika hotuba yake humu ndani kama anavyosema mwenyewe hakusema uongo. Lakini mtu mwingine nje ya Bunge amesema kwamba haikuwa sahihi, kwa bahati mbaya mimi sijalisoma hilo gazeti sijui wameandika nini.

Lakini kama mnavyojua huu mkutano wetu ni wa hadhara ndiyo maana inatangazwa kila mtu anajua kila linaloendelea humu ndani. Sasa kama hilo ambalo Mheshimiwa Omar Chubi, alilisema ni la uongo kwa maana hiyo au si la uongo, hilo mimi siwezi kujua.

Sasa ni wajibu wa Mheshimiwa Omar Chubi, basi kuja humu ndani kusema hilo ambalo wanasema ni uongo kwamba si kweli ushahidi wake ni huu hapa. Mtu yeyote nje anayo haki kama limesemwa humu ndani analiona linamwelelea yeye, ana haki ya kujitetea. Lakini maadam kwako umeona kwamba hukutendewa haki na kwamba uliyoyasema yalikuwa sahihi basi pengine ni wewe sasa uje ulieleze Bunge humu kutoa ushahidi wa hayo yanayosemwa huko nje maana hakuna namna nyingine. (Makofi)

Sasa baada ya maelezo hayo tutakusubiri wewe mwenyewe ukiona sawa sawa utaendelea, ukiona una haki ya kueleza nafasi ipo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya ufafanuzi huo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.41 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano tarehe 14 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*